

**KUNGA ZA KIUANDISHI ZA KIMAJARIBIO KATIKA RIWAYA TEULE ZA  
KISASA ZA KYALLO WADI WAMITILA**

**MUTUA JANICE MWIKALI**


**Tasnifu imewasilishwa katika Shule ya Waliofuzu ili Kutimiza Baadhi ya Mahitaji ya  
Shahada ya Uzamifu katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Egerton**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**JUNI, 2023**

## UNGAMO NA IDHINI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kutahiniwa katika chuo kikuu chochote kwa mahitaji ya shahada yoyote ile.

Sahihi 

Tarehe 22/06/2023

**Janice Mwikali Mutua**  
AD12/30004/16


### **Idhini**

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi 

Tarehe 23/06/2023

**Dkt. AbdulRahim Hussein Taib Ali, PhD**  
Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu  
Chuo Kikuu cha Egerton

Sahihi 

Tarehe: 23/06/2023

**Prof. Issa Y. Mwamzandi, PhD**  
Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano  
Chuo Kikuu cha Kabianga

## **HATI LINZI**

©2023, **Janice Mwikali Mutua**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kutafsiri, kunakili au kuhifadhi tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

**TABARUKU**

Kwa Marehemu Babangu;

Francis Mwangi Mwai

**“laiti ungalisubiri kidogo tu”**

Na

Wanangu

Dennis Mutua na Rodgers Feddy

“Iwafae ninyi na kuwashajiisha, daima kulenga juu maishani.”

## SHUKRANI

Namshukuru Rabuka kwa kunipa afya nzuri na neema wakati wote wa masomo yangu ya uzamifu na hatimaye kuniwezesha kuikamilisha kazi hii. Ukamilifu wa kazi hii ni ukweli wa usemi, “Tone la Mungu ni bahari ya chungu.” Utukuzwe wewe uketiye juu sana! Mkono mmoja hauchinji ng’ombe; ufanisi wa kazi hii umeafikiwa kwa sababu ya juhudi za wengi ambao sina budi kuwataja na kuwashukuru. Nawashukuru sana wahadhiri wasimamizi wangu Profesa Issa Y. Mwamzandi na Daktari AbdulRahim Hussein Taib Ali. Ukarimu wenu katika kuisoma kazi hii bila kuchoka ulihakikisha kuwa kinolewacho sharti kipate.

Namshukuru Mheshimiwa Profesa Phyllis Bartoo kwa imani yako kwangu. Kutoka kwako nilijifunza kwamba hakuna refu lisilokuwa na ncha. Kwa kuwa mshikamano wa mikono daima hurahisisha kazi, siwezi kuwasahau wahadhiri wangu walionifunza katika viwango vya shahada na uzamili. Profesa Catherine Kitetu, Daktari Josephine Khaemba, Daktari Lucy Wathika, Daktari Joseph Walunywa, Daktari Dishon Kweya na Daktari Raphael Gacheiya. Kwa pamoja himizo lenu lilikuwa, “yote yawezekana.” Kwenu nyote nasema, asanteni sana! Wanafunzi wenzangu tuliyoabiri gari hili la Uzamifu pamoja, Bwana Mathew Kwambai, Daktari Melvine Auma na Marehemu Judy Gakii; asanteni sana kwa kujitolea kuhariri kazi hii ili kuondoa makosa ya tahajia. Hakika mlikuwa wahisani wenye kutegemewa.

Shukrani za dhati zimwendee mume wangu mpenzi Prof. Dr.-Ing. Benedict M. Mutua. Asante kwa kuufadhili usomi huu kwa hali na mali. Kwa wanangu ninaowaenzi; Dennis Mutua asante sana kwa kunisaidia kuipiga chapa tasnifu hii. Na kwako Rodgers Feddy asante kwa kuhakikisha kuwa kila nilipoketi mezani kusoma hapakukosa kinywaji mwafaka. Kwa mamangu mpenzi, asante kwa kunilea, kunipeleka shuleni na zaidi kunihimiza kwa maneno halisi kuwa, “ndoto hutimizwa na binadamu, nawe ni mmoja wao.” Kwako mama, nakuenzi kwa sababu kama si wewe nisingaliona milango ya darasa. Aidha, nawashukuru waumini wote wa kanisa la Nakuru Christian Centre kwa kunipa amani na utangamano. Shukrani za mwanya ziwaendee wachungaji wangu Sam Owenga, Fred Kamau, Sammy Watho, Josephine Mwangi na Mwinjilisti Nixon Osumba kwa kuniombea kila nilipoyahisi magumu katika safari hii. Ushauri wako uligonga ndipo! Dua yangu kwenu wote, “Mungu asiyesinzia awalinde na akutangulieni, Ameen!”

Asanteni sana!

## ABSTRACT

Experimental prose refers to written fictional works that use innovative techniques where the stylistic devices employed deviate and go beyond the realistic historical account of events. Through experimental writing, contemporary prose writers communicate pertinent issues that directly concern the society. Since authors have the freedom to use any technique that best represents their views, new strategies of writing have been used in today's "neo-realistic" Swahili novel. Wamitila is one of the writers who uses experimental methods as a means of writing in his contemporary fictional works. The main objective of this research was to establish the nature and extent of the author's use of the said methods. This research, therefore, sought to identify aspects of experimental methods used in selected Wamitila's Swahili novels. The research investigated how the author uses different experimental methods to convey his message to the audience. Three novels by the author were purposively selected. They include: *Musaleo*, *Msichana wa Mbalamwezi* and *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji*. The main view was to interrogate how the author employed different experimental methods as a writing strategy in the novels. The study was guided by postmodernism theory as proposed by Jean-Francois Lyotard, Jean Baudrillard, Jurgen Habermas and Fredric Jameson. The theory advocates for a complete deviation from realistic metanarrative to a fictional narrative that is characterized by use of multiple strategies. Data that was collected was qualitative in nature and was analysed by employing interpretive and descriptive approach where the researcher highlighted and explained the experimental methods that the author employed in the selected texts. The study established that the author successfully used experimental methods such as use of many short stories (fragmentation), intertextuality, symbolism, dialogue, magical realism and other literary techniques to portray his message to the audience. This study therefore underscores the radical shift in which modern Swahili authors represent societal issues in their works of fiction. These new findings have contributed knowledge on literary writing strategies and techniques. In addition, it is also believed that these findings will guide and assist upcoming writers and readers in understanding experimentalism as a tool of communicating intricate themes in today's Swahili prose.

## IKISIRI

Riwaya za kimajaribio ni kazi andishi za kibunifu zilizoandikwa kwa kufuata mitindo mipya ya uandishi wa riwaya za kisasa ambapo mbinu zinazotumiwa hukiuka uhalisia wa kihistoria wa kijadi hasa katika uwasilishaji wa vitushi. Kwa kuwa wasanii wana uhuru wa kuandika jinsi wapendavyo, matumizi ya mbinu za majaribio yamepelekea kuibuka kwa riwaya mpya ya Kiswahili inayoegemea mkondo wa “uhalisia-mpya.” Wamitila ni mmojawapo wa waandishi wa riwaya za Kiswahili anayetumia mbinu za kimajaribio kama kunga ya uandishi wa bunilizi zake za kisasa. Kiini cha utafiti huu kilikuwa kubainisha namna mwandishi anavyozitumia mbinu za kimajaribio kama msingi mkuu wa ubunifu katika riwaya anazozibuni. Vilevile, utafiti huu uliazimia kubainisha mbinu mahususi anazotumia Wamitila kuangazia maswala yanayoibuka katika jamii. Kuafikia haya, riwaya tatu za mwandishi zimeteuliwa kimaksudi. Ni pamoja na: *Musaleo, Msichana wa Mbalamwezi na Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji*. Mtafiti ameweka bayana mbinu za kimajaribio anazotumia Wamitila kwa kuzitambulisha na kufafanua vipengele mbalimbali vya mbinu husika katika riwaya teule. Aidha, utafiti ulichunguza jinsi mbinu hizo zilivyotumika kama kunga ya uandishi na kifaa cha kuwasilishia ujumbe katika riwaya za kisasa. Utafiti uliongozwa na nadharia ya usasaleo kama ilivyoasisiwa Jean-Francois Lyotard, Jean Baudrillard, Jurgen Habermas na Fredric Jameson. Kwa mujibu wa nadharia ya usasaleo utaratibu maalum wa kijamii uliozoeleka huyumbishwa. Nadharia hii inakiuka matumizi ya riwaya kuu ya kihalisia na kupendekeza kutumika kwa riwaya mpya iliyojawa na uradidi unaoleta maana pana kama njia ya kuelezea maswala muhimu ya jamii. Kwa kuwa data iliyokusanywa ilikuwa ya kithamano, mtafiti alisoma riwaya teule za mwandishi na kudondoa mbinu mbalimbali za kimajaribio zilizotumika katika bunilizi husika. Utafiti ulibaini kuwa Wamitila amewasilisha maswala mahususi yanayohusu jamii kwa kutumia mbinu za kimajaribio kama kunga yake ya ubunifu. Hatimaye, mtafiti alibaini kuwa simulizi fupi, urejeleomatini, taashira, dayolojia, uhalisiajabu, tamathali za lugha ndivyo vipengele vikuu vya kimajaribio vinavyokatiza usimulizi katika riwaya teule. Utafiti huu umesisitiza kuhusu jinsi waandishi wa riwaya ya kisasa ya Kiswahili wanavyoyasawiri maswala ya kijamii katika bunilizi zao. Matokeo ya utafiti ni nyongeza kwa taaluma ya ujuzi na ufahamu unaohusu kunga za uandishi wa kazi za fasihi. Aidha, ni mchango katika kuwaelekeza waandishi na wasomaji kuhusu uelewa wa mbinu za kimajaribio kama kunga ya kuwasilisha dhamira na maudhui katika riwaya ya Kiswahili.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO NA IDHINI</b> .....	<b>ii</b>
<b>HATI LINZI</b> .....	<b>iii</b>
<b>TABARUKU</b> .....	<b>iv</b>
<b>SHUKRANI</b> .....	<b>v</b>
<b>ABSTRACT</b> .....	<b>vi</b>
<b>IKISIRI</b> .....	<b>vii</b>
<b>ORODHA YA MAJEDWALI</b> .....	<b>xi</b>
<b>VIELELEZO</b> .....	<b>xii</b>
<b>VIFUPISHO VYA MANENO</b> .....	<b>xiii</b>
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	<b>1</b>
<b>UTANGULIZI</b> .....	<b>1</b>
1.1 Usuli wa Mada.....	1
1.2 Mada ya Utafiti.....	7
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	7
1.3.1 Madhumuni ya Jumla.....	7
1.3.2 Madhumuni Mahususi.....	7
1.4 Maswali ya Utafiti.....	7
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	8
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	8
1.7 Ufafanuzi wa Istilahi na Akronimu.....	10
<b>SURA YA PILI</b> .....	<b>12</b>
<b>YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA</b> .....	<b>12</b>
2.1 Utangulizi.....	12
2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Chanzo na Ukuaji wa Kunga za Kiuandishi za Kimajaribio.....	12
2.3 Kunga za Uandishi wa Riwaya.....	17
2.4 Umbo, Maendeleo na Mabadiliko Katika Riwaya ya Kiswahili.....	19
2.5 Sifa Bainifu za Riwaya ya Kiswahili ya Kimajaribio.....	21
2.6 Mitazamo ya Uandishi wa Riwaya Tangu Jadi hadi Sasa.....	22
2.7 Riwaya za Wamitila.....	27
2.8 Muhtasari wa Riwaya Teule.....	28



2.8.1 Riwaya ya <i>Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji</i> .....	28
2.8.2 Riwaya ya <i>Musaleo!</i> .....	29
2.8.3 Riwaya ya <i>Msichana wa Mbalamwezi</i> .....	32
2.9 Misingi ya Nadharia .....	33
2.9.1 Nadharia ya Usasaleo .....	33
2.9.2 Mihimili ya Usasaleo .....	34
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>38</b>
<b>MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>38</b>
3.1 Utangulizi .....	38
3.2 Muundo wa Utafiti .....	38
3.3 Uteuzi wa Sampuli .....	38
3.4 Mbinu za Ukusanyaji wa Data .....	39
3.4.1 Mpango Maalum wa Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data .....	39
3.5 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data .....	42
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>45</b>
<b>KUNGA ZA KIUANDISHI ZA KIMAJARIBIO KATIKA RIWAYA ZA KISASA ZA KYALLO WADI WAMITILA .....</b>	<b>45</b>
4.1 Utangulizi .....	45
4.2 Ukatazaji wa Usimulizi .....	45
4.2.1 Uhalisiajabu .....	46
4.2.2 Matumizi ya Majina ya Watu, Mahali au Vitu .....	50
4.2.3 Matumizi ya Dini, Mitholojia na Simulizi za Kiafrika .....	88
4.2.4 Matumizi ya Matini za Kitaaluma .....	94
4.3 Hitimisho .....	101
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>103</b>
<b>MCHANGO WA MBINU ZA KIMAJARIBIO KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI KATIKA RIWAYA ZA KISASA ZA KYALLO WADI WAMITILA .....</b>	<b>103</b>
5.1 Utangulizi .....	103
5.2 Uwasilishaji wa Maudhui kwa Njia Fiche .....	103
5.3 Taswira ya Jamii ya Kisasa .....	110
5.3.1 Changamoto za Uandishi Bunifu wa Kisasa .....	111

5.3.2 Mapendekezo Kuhusu Uandishi na Uchapishaji wa Riwaya Mpya .....	117
5.4 Hitimisho .....	119
<b>SURA YA SITA .....</b>	<b>121</b>
<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>121</b>
6.1 Utangulizi .....	121
6.2 Muhtasari wa Utafiti .....	121
6.3 Hitimisho .....	123
6.4 Mapendekezo .....	124
6.4.1 Tafiti za Baadaye .....	125
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>126</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>136</b>
A: Kibali kutoka NACOSTI .....	136
B: Nakala za Makala .....	137
C: Mbinu za Kimajaribio katika Riwaya ya <i>Musaleo!</i> .....	141
D: Simulizi Fupi zenye Taashira katika Riwaya ya <i>Msichana wa Mbalamwezi</i> .....	150
E: Simulizi Fupi zenye Taashira katika Riwaya ya <i>Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji</i> .....	156
F: Mbinu za Kimajaribio na Uwasilishaji wa Maudhui katika Riwaya Teule .....	162

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Sifa Bainifu za Kunga za Kimajaribio katika Riwaya Teule za Kisasa za K. W. Wamitila .....	42
Jedwali 3.2: Maswala Muhimu Yanayohodhi Kunga za Kiuandishi za Kimajaribio katika Riwaya za Kisasa za K.W. Wamitila .....	43
Jedwali 4.1: Matumizi ya Majina.....	50

## VIELELEZO

Kielelezo 3.1: Muundo wa Mpango Maalum wa Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data.....	41
Kielelezo 3.2: Muundo wa Uchanganuzi wa Data .....	44

## VIFUPISHO VYA MANENO

k.	-	kurasa
MMM	-	<i>Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji</i>
ML	-	<i>Musaleo!</i>
MWM	-	<i>Msichana wa Mbalamwezi</i>
uk.	-	ukurasa

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### **1.1 Usuli wa Mada**

Mbinu za kiuandishi za kimajaribio ni dhana katika utunzi wa kazi za fasihi ambapo waandishi hukiuka mipangilio ya kijadi iliyozingatia mfumo wa “mwanzo-kati-mwisho”. Katika mfumo wa mwanzo-kati-mwisho kazi ya fasihi huwasilishwa kwa njia ya moja kwa moja inayoegemea mtindo wa kihalisia. Mwamzandi (2013) anafafanua kwamba mtindo wa uandishi uliozingatia uhalisia ni mzuri ingawa kwa sasa unatiliwa shaka. Wasomaji wa fasihi ya sasa wako tayari kupokea kazi za kimajaribio kwa sababu hata wachapishaji wamezipa kazi hizo nafasi katika uchapishaji. Hapo awali wachapishaji hawangechapisha kazi zozote za kimajaribio kwa sababu hazingekuwa na manufaa kwa wanunuzi. Maoni haya yanaleta dhana kuwa huenda wachapishaji walidhani riwaya za majaribio hazingekuwa na manufaa kwao hasa ikichukuliwa kwamba uandishi pia ni kitegauchumi. Hata hivyo, uandishi wa kazi za Kiswahili hasa riwaya umebadilika pakubwa. Inakisiwa kwamba uhuru wa uchapishaji uliopo hivi leo umepelekea kuwepo kwa kazi nyingi mpya mpya za fasihi na pia zenye sifa mpya za mbinu mpya za kiuandishi za kimajaribio.

Mulokozi (1996) anafafanua kuwa riwaya za kimajaribio ni aina ya riwaya inayojitokeza katika mikondo miwili. Mkondo wa mjadala-nafsi na mkondo wa riwaya-kweli. Riwaya katika mikondo yote miwili hutungwa pasipo kuzingatia kanuni za kawaida za uandishi wa riwaya. Mtiririko wa visa na matukio uliozoeleka hukiukwa. Madai ya watunzi wa riwaya za majaribio ni kwamba umbo la kawaida la riwaya halitoshelezi mahitaji ya karne hii ya Ishirini na Moja yenye maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano. Hivyo, riwaya mpya hubuni mbinu za kuelezea mtiririko wa fikra, hisia na tajriba ya nafsi isiyofuata mfuatano sahili wa visa na matukio, ambao huwa nje ya urazini wa kawaida wa kibinadamu. Senkoro (2006) anaongeza kuwa riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio, kama ilivyo kwa fasihi yoyote ya kimajaribio, ni neno linalotumika kutaja kazi za riwaya zinazochanganya mbinu za kijadi na za kisasa katika uandishi wake. Majaribio yenyewe hulenga katika ukiukaji wa kaida zilizozeleka za kiutunzi wa riwaya na kutokeza mitindo mipya isiyofanana na ile ya kijadi. Riwaya hizi zikichunguzwa kwa umakini, sifa yake kubwa huonekana katika mparaganyiko wa matukio. Isitoshe riwaya hizi huwa na matumizi ya fantasia na uhalisia-mazingaombwe,

mwingilianomatini, uchanganyaji wa historia na ubunifu, matumizi ya wahusika na mandhari dhanaishi miongoni mwa sifa nyingine ambazo zitatarajiwa kubainika katika utafiti huu. Hata hivyo inaaminika kuwa utunzi huu wa kimajaribio ulioanza katika miaka ya 1990 umekita mizizi ulimwenguni kote. Riwaya zinazotungwa kwa kuegemea mbinu hizi hurejelewa kama riwaya za kimajaribio au riwaya za kisasa. Katika Kiswahili riwaya zinazotumia mbinu za kimajaribio kama kunga ya uandishi hurejelewa kama riwaya mpya, riwaya za kisasa, riwaya za kimajaribio au riwaya za Karne ya Ishirini na Moja (Mwamzandi, 2013).

Kunga za uandishi ni mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wasanii ili kuipa kazi fulani wasifu wa kisanaa (Wamitila, 2003 b). Mohamed (1995) anafafanua zaidi kwamba kwa kuwa fasihi ni sanaa ya lugha inahitaji vifaa kuikamilisha. Kunga za uandishi ni vifaa ambavyo hufanikisha kazi yoyote ya fasihi. Ni sawa na mbinu. Baadhi ya kunga zinazojenga kazi za fasihi ni pamoja na nyenzo, ubunaji, umbo na mtindo, bombwe, maana, upatanisho, mvuto, uzuri wa kisanaa na mtindo. Hivyo, kunga ni mbinu zinazotumika kuijenga kazi za fasihi. Kunga ni kiambajengo muhimu katika uandishi wa kazi za sanaa yoyote zikiwemo riwaya (Mohamed, 1995). Kawaida maswala ya jamii huwasilishwa na fasihi kwa kutumia kunga tofauti tofauti za uandishi. Kadri jamii inavyokua na kubadilika, vivyo hivyo mbinu za kuibuni fasihi inayoimulika jamii husika hukua na kubadilika.

Mbinu za kiuandishi za kimajaribio zimekuwepo tangu miaka ya 1990 na zimedhihirika ulimwenguni kote (Rettova, 2016). Ramen na Chaudbarry (2011) wakirejelea bunilizi ya *Stirrings Still* iliyoandikwa na Samuel Beckett wanaeleza kwamba kazi hii ilikiuka kaida zote za kijadi za utunzi. Hii ni kwa sababu ya matumizi mengi ya vipengele vingi vya mbinu za kiuandishi za kimajaribio kama vile uradidi uliokithiri, usimulizi uliokosa mantiki, ploti changamano na matumizi ya wahusika wa kifantasia. Barth (1984) anafafanua kuwa waandishi wa baadhi ya riwaya Marekani Kusini pia walitumia mbinu za majaribio. Kipengele cha kimajaribio kilichodhihirika zaidi katika riwaya zao kilikuwa uhalisia-mazingaombwe. Katika fasihi ya Marekani swala la uhalisia-mazingaombwe ni jambo linalosawiriwa kuwa la kawaida tu. Kwa mfano, barani humo, msanii Gabriel Garcia Marquez aliangazia taswira ya jamii yake kwa kutumia mbinu ya uhalisia-mazingaombwe katika fani ya uhusika ambapo alimsawiri mhusika mkuu kama mzee aliyemiliki mbawa kubwa. Kwa mujibu wa Barth (1984) wengine walioboba katika uandishi wa kimajaribio Marekani Kusini ni pamoja na David Markson (1927-2010)

aliyeandika kazi za kimajaribio kama vile *Readers Block* (1996), *Vanishing Point* (2004) na *The Last Novel* (2007) miongoni mwa nyingine.

Mwandishi chipukizi wa Marekani Marisha Pessl aidha alibobea katika uandishi wa kimajaribio. Alitumia kipengele cha hiponozi au kiini-macho katika riwaya ya *Night Film* (2014). Riwaya nyingine aliyoandika Pessl ambayo hata mada yake iliibua sifa ya uchangamano ni *Special Topics in Calamity Physics* (2007). Maelezo haya yanabaini kuwa uandishi wa kimajaribio ni jambo lililokita mizizi hasa baada ya usasa.

Bara la Afrika halikuachwa nyuma katika mabadiliko ya uandishi wa nathari za Kiswahili. Kama wanavyosema Njogu na Chimera (1999), kulikuwa na mabadiliko kadhaa katika uandishi wa nathari ambapo riwaya ya Kiswahili ilishuhudia umbo jipya ambalo halikuwa na nafasi ya kurejelea tabia za kijadi za kimiundo na kimaudhui. Wataalamu hawa wanaendelea kusema kuwa riwaya mpya iliyoibuka wakati huo ilikuwa na umbo jipya ambalo lilikuwa tofauti sana na riwaya ya kijadi. Quayson (1995) akirejelea mabadiliko ya uandishi nchini Nigeria anaeleza kwamba uandishi wa riwaya ya kisasa ni wa majaribio ya mitholojia ambapo riwaya halisia za jadi sasa zimekuwa riwaya za kimajaribio za visasili. Maoni ya Njogu na Chimera yanaafikiana na mawazo ya Gaylard (2005) na Quayson (1995) kwamba waandishi wengi wa riwaya za Kiafrika wanahama kutoka kwenye matumizi ya uhalisia na kuegemeza uandishi wao katika nyenzo za kimajaribio.

Khamis (2007) anadokeza kuwa chanzo cha uandishi wa kimajaribio katika riwaya za Kiswahili ni pale waandishi nchini Kenya na Tanzania walipoanza kukataa kuitikia “hewala” kwa kila kitu walichokiona na kusikia kutoka kwa waandishi wakoloni na vibaraka wao. Waandishi hawa walikataa kufuata kila kanuni ya ubunaji, uwasilishaji wa mawazo na uigaji wa sanaa walizozikuta au kuwekewa na watangulizi wao. Kwa hivyo, katika juhudi za kujikomboa kutokana na kasumba za kikoloni, waandishi wa riwaya za Kiswahili walianza kuirejelea jadi yao. Waandishi hao waliingiza katika kazi zao hali tofauti za kifasihi hasa zile zilizofungamana na fasihi simulizi kwa lengo la kujenga dhamira zilizojikita katika muktadha wa kiasili. Katika hoja hii, Khamis anaibua udhahiri wa maswala ya uingilianomatini na uingilianotanzu ambayo ni mojawapo wa nyenzo kuu katika uandishi wa kimajaribio. Waandishi Waafrika wanaorejelewa na Khamis walitumia mbinu hizi mpya za utunzi kuisawiri jamii ya wakati huo kikamilifu.



Khamis (2007) anaendelea kueleza kuwa mabadiliko katika nathari za Kiswahili yamepitia katika vipindi vitatu vikuu. Katika vipindi hivi vyote riwaya za Kiswahili zimepiga hatua tofauti tofauti na kupevuka zaidi kama anavyosema Mulokozi (1996:164). Kwa mfano, katika miaka ya tisini, riwaya zilizotungwa zilikuwa za kifalsafa na zilijadili zaidi maisha, utawala na ujenzi wa jamii mpya huku zikizingatia mtindo wa uhalisia. Riwaya hizi ziliisawiri jamii katika mikondo ya ubinadamu, usawa na ustawi. Kinyume na haya, riwaya za Kiswahili za kisasa zimeshuhudia mabadiliko mengi kifani na kimaudhui. Riwaya za sasa zinaangazia maswala ibuka hasa yale yanayotokana na maendeleo ya kisayansi, mawasiliano na utandawazi. Hivyo, mabadiliko yaliyoshuhudiwa yalisababishwa na mpito wa wakati kwani waandishi wameiona jamii ikibadilika katika mila, desturi na mienendo kutokana na nguvu mpya za kiuchumi na kiteknolojia.

Riwaya mpya za Kiswahili zimeandikwa kwa wingi katika Karne ya Ishirini na Moja huku zikiwa na mabadiliko ya kimuundo, kimaudhui na pia kifani. Walibora (2013) akirejelea riwaya mpya ya *Mbali na Nyumbani* ya Adam Shafi iliyoandikwa katika Karne ya Ishirini na Moja amedai kuwa uandishi wa kisasa umeenea kwa kasi katika mataifa ya Afrika Mashariki. Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita machapisho mengi ya bunilizi katika Kiswahili ambayo ni tofauti na yale ya kijadi hasa nchini Kenya yamekuwa mengi. Hivi ni kusema kwamba Karne ya Ishirini na Moja ni muhimu kwani waandishi wakongwe na chipukizi tumbi nzima wamechapishiwa kazi zao kwa wingi zaidi kuliko kipindi chochote kingine katika historia ya fasihi ya Kiswahili.

Walibora anasisitiza kuwepo kwa utunzi na uchapishaji mwingi wa riwaya za Kiswahili barani Afrika hali kadhalika katika ukanda wa Afrika Mashariki hususan nchini Kenya. Baadhi ya riwaya zilizotungwa wakati huu nyingi ni za kimajaribio. Wamitila ni mmojawapo wa waandishi wanaorejelewa na Walibora. Riwaya zilizoandikwa na kuchapishwa katika kipindi hiki zinahakiki jamii kwa undani huku zikiakisi matumizi ya mbinu za kiubunifu za kimajaribio zinazoasi kaida za utunzi wa kijadi wa riwaya (Khamis, 2012). Vipengele vya majaribio vilivyozingatiwa zaidi katika kipindi kinachorejelewa na Khamis ni uhalisia-ndoto na ubunaji wa visasili. Aidha, aina ya lugha inayotumiwa na waandishi wa riwaya wa wakati huu imeathiriwa na matukio mbalimbali katika jamii ya mtunzi. Hata hivyo, riwaya zinaendelea kuchukua dhima ya uchunguzi wa jamii huku zikibeba silaha mpya za utunzi na kushughulikia matatizo mapya

katika jamii ya kisasa. Kwa mujibu wa maoni haya, ni dhahiri kwamba utunzi au uandishi wa riwaya za Kiswahili umekuwa tofauti zaidi hasa katika Karne ya Ishirini na Moja. Khamis (2012) anasisitiza kwamba hili ni jambo tofauti likilinganishwa na utunzi wa hapo awali uliozingatia hadithi za uhalisia iliyowasilishwa kwa njia ya moja kwa moja.

Mintarafu ya haya, matumizi ya mbinu za kimajaribio ni dhana ibuka katika uwanda wa uandishi wa riwaya za kisasa za Kiswahili zinazoegemea mtazamo wa usasaleo ambapo waandishi hukwepa mtindo wa uandishi wa kihalisia na kukumbatia mkondo wa uhalisia-mpya. Mbinu mbalimbali za kimajaribio zikiwemo uhalisia-ndoto, ubunaji wa visasili na urejeleomatini hutumiwa na waandishi wa riwaya mpya za Kiswahili katika juhudi za kuwasilisha ujumbe muhimu kwa hadhira lengwa. Alomo (2016) amefafanua kuwa mbinu za kisasa za utunzi wa riwaya zinatumia vipengele vya usasaleo kama nyenzo ya kuwasilishia ujumbe ingawa ni jambo linalozua utata zaidi hasa katika msuko wa masimulizi. Mabadiliko katika mitindo ya uwasilishaji wa kazi za fasihi ndicho kiini cha riwaya mpya yaani riwaya za majaribio. Hata hivyo, utafiti wa Alomo ulikuwa linganishi na ulijishughulisha na uwakilishaji wa utandawazi katika riwaya teule. Utafiti huu ulijikita kwenye matumizi ya mbinu za kimajaribio katika uandishi mahususi wa riwaya za Wamitila.

Gromov (2004) anashikilia kuwa riwaya za kimajaribio zilianza kukita mizizi katika fasihi ya Kiswahili katika miaka ya 1990 kwa uandishi wa mwanya na wa pekee wa Euphrase Kezilahabi katika *Nagona* na *Mzingile*. Rettova (2016) katika makala yake, *Writing in the Swing? Neo-Realism in Post Experimental Swahili Fiction* anadai kwamba riwaya za Kiswahili zimeshuhudia maendeleo makubwa katika mbinu za kiuandishi. Riwaya za sasa zinaegemea mfumo mpya wa utunzi ambao umepelekea kuachwa kwa hali ya kijadi ya uhalisia. Rettova anaendelea kuufafanua mfumo huo mpya kwa jina la “uhalisia-mpya”. Baadhi ya waandishi wa kiafrika waliotajwa na Rettova kama wanamajaribio ni William Mkufya, Said Ahmed Mohamed na Wamitila.

Mwandishi Wamitila amebobea katika nyanja mbalimbali za utafiti, uhakiki na uandishi wa kazi tofauti tofauti za fasihi zikiwemo tamthilia, ushairi, hadithi fupi, fasihi ya watoto na riwaya. Wamitila alizaliwa mnamo 1966 mjini Machakos nchini Kenya. Walibora (2013) amemtaja Wamitila mwandishi wa vitabu vingi na mtaalamu aliyefanya tahakiki nyingi za fasihi ya

Kiswahili kwa jumla. Minajili ya haya mwandishi Wamitila anatambulika kama mwandishi mashuhuri wa maswala mbalimbali yanayochipuka na kuendelea katika jamii kila uchao. Inakisiwa kwamba kama katika riwaya nyingine za kimajaribio, uandishi wa Wamitila una uwezo wa kuwa changamano zaidi kiasi cha kutotimiza wajibu na dhima ya fasihi katika jamii. Bertoncini (2006) katika Mwamzandi (2013:48) anaeleza kuwa msomaji wa kazi za kimajaribio huenda akajipata ameghumiwa na kushangazwa na matumizi mapana ya mbinu za utunzi za kimajaribio. Mifano ya sifa bainifu ya mbinu za kimajaribio ni urejeleomatini, uhalisia-mazingaombwe na matumizi ya vipande vingi vidogo vidogo vya masimulizi vilivyotapakaa kote katika usimulizi. Vilevile, baadhi ya mbinu za kiuandishi wa kimajaribio zinazohusishwa zimesheheni istilahi na mijadala ya kigeni pamoja na dhana changamano za kifalsafa, utandawazi na teknolojia mpya.

Katika mahojiano ya moja kwa moja baina ya Wamitila na Lutz Diegner yaliyofanyika mnamo 3/11/2004 kuhusu riwaya ya *Bina-Adamu!*, mojawapo wa riwaya ya kisasa ya Wamitila, inabainika kwamba uandishi wake ni wa kipekee na unatumia mbinu za kipekee. Kwa mfano, Diegner anapomwuliza Wamitila sababu za kuandika kitabu kigumu kama *Bina –Adamu!* Anajibu;

Siamini kuwa hii ni riwaya ngumu. Nadhani inaeleweka na msomaji anaweza kuisoma”  
(Wamitila, 2005, uk. 95)

Maoni ya Diegner ni kuwa uandishi wa Wamitila ni mgumu na changamano hata ingawa mwandishi mwenyewe hakubaliani na wazo hilo. Hivyo, kuna umuhimu wa kutambulisha na kuweka bayana sifa bainifu za mbinu mahususi za kimajaribio anazotumia Wamitila na jinsi kila mbinu hizo zinavyomsaidia kuafikia majukumu yake ya kutoa taswira kamili ya jamii ya sasa kama mwandishi. Ili kuafikia malengo ya usomi huu, utafiti huu ulitambulisha, kufafanua na kuhakiki vipengele mbalimbali vya mbinu za kiuandishi za kimajaribio kama zilivyotumika katika utunzi wa riwaya tatu teule zilizoandikwa na Wamitila kati ya miaka 2004 – 2014. Aidha, utafiti ulifafanua jinsi mbinu za kimajaribio kwa jumla zinavyotumika kuwasilisha maudhui na kuiakisi jamii ya leo katika riwaya bunifu za Wamitila.

## **1.2 Mada ya Utafiti**

Baadhi ya waandishi wa riwaya za Kiswahili za kisasa wamekwepa uandishi wa kihalisia wa kijadi na kuukumbatia uandishi unaoegemea mkondo wa uhalisia-mpya. Uandishi huu mpya umedhalilisha mtindo wa kijadi wa uandishi wa riwaya wa mwanzo-kati-mwisho. Hii ni kwa sababu jamii imekumbwa na maswala mengi ambayo hayawezi kuwasilishwa kwa kutumia muundo na mtindo mmoja wa utunzi. Wamitila ni mmojawapo wa waandishi wa kisasa anayetumia mtindo mpya wa utunzi katika kuzungumzia maswala mbali mbali yanayoikumba jamii ya sasa. Kazi zake ni changamano na gumu kufuatilia katika usomaji. Hivyo basi utafiti huu umefafanua kunga za kiuandishi za kimajaribio anazotumia mwandishi teule, mchango wake katika uwasilishaji wa maudhui na uamilifu wake katika uchoraji wa taswira ya jamii ya kisasa.

## **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

### **1.3.1 Madhumuni ya Jumla**

Madhumuni ya jumla ya utafiti huu yalikuwa ni kutambulisha na kuweka bayana matumizi na sifa za mbinu za kimajaribio kama kunga ya ubunifu katika riwaya za kisasa kwa kuzingatia riwaya teule za Wamitila.

### **1.3.2 Madhumuni Mahususi**

- i. Kubainisha kunga za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya za kisasa za Wamitila;
- ii. Kujadili mchango wa kunga za kiuandishi za kimajaribio katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya za kisasa za Wamitila; na
- iii. Kufafanua jinsi kunga za kiuandishi za kimajaribio anazotumia Wamitila zinavyoiakisi jamii ya leo.

## **1.4 Maswali ya Utafiti**

- i. Mwandishi Wamitila anatumia kunga zipi zakiuandishi za kimajaribio katika riwaya zake za kisasa?
- ii. Kunga za kiuandishi za kimajaribio anazotumia Wamitila zina mchango gani katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya zake za kisasa?
- iii. Kunga za kiuandishi za kimajaribio anazotumia mwandishi Wamitila zinaiakisi vipi jamii ya leo?

## **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yataifaa taaluma ya fasihi ya Kiswahili katika nyanja za utafiti, utamaduni, historia, nadharia ya fasihi na elimu. Katika uwanda wa utafiti matokeo ya utafiti yatumika kama marejeleo muhimu katika tafiti za baadaye. Tafiti mahususi zitakazonufaika ni zile zinazohusiana na kunga za uandishi wa riwaya za kisasa zenye sura ya kimajaribio. Kama urejeleo, utafiti utawafaa wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili katika viwango vyote vya elimu kuanzia astashahada hadi uzamifu. Kwa kuweka bayana sifa bainifu, vipengele na mbinu mahususi za kimajaribio katika riwaya teule, wasomaji wa riwaya za kisasa watafaidika na ufahamu wa jinsi riwaya zenyewe zinavyofumwa. Kwa hivyo, itakuwa rahisi kung'amua ujumbe uliokusudiwa na mwandishi kwa wepesi. Katika uwanda wa utamadauni utafiti huu utawazindua wanajamii kwa kubainishia taswira mbalimbali za jamii ya kisasa. Mintarafu ya haya, waandishi chipukizi, watafiti, wahakiki na wasomi wengine wataielewa jamii ya kisasa kwa undani. Ufahamu na uelewa huu utakuwa msingi bora kwa yeyote ambaye angependa kutafiti au kuandika kazi bunifu katika mazingira ya kisasa. Kihistoria, utafiti huu ni sehemu mojawapo ya maendeleo ya historia ya utanzu mzima wa riwaya ya Kiswahili. Historia ya riwaya ya Kiswahili imebainika wazi nchini Kenya, Ukanda wa Afrika Mashariki, Afrika, na ulimwenguni kwa jumla tangu Karne ya Ishirini kufikia sasa. Aidha, utafiti huu ni mchango mkubwa katika ukuzaji na uimarishaji wa nadharia za fasihi hasa zile zinazohusu uandishi wa riwaya za kisasa. Hatimaye, katika uwanda wa elimu utafiti huu ni wa faida kubwa kwa wale wanaobuni sera hasa za fasihi inayofanywa shuleni. Umewapa mwanga kuhusu kuwepo kwa uandishi wa kimajaribio ambao ni hifadhi kwa wasomi wa kima cha juu. Hivyo, walimu, wanafunzi na washikadau wengine katika sekta ya elimu wamepewa mwanga kuhusu jinsi ya kusoma riwaya za kimajaribio zilizojawa na uchangamano.

## **1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umeshughulikia riwaya tatu za kimajaribio za mwandishi tajika wa fasihi; Kyalo Wadi Wamitila. Ni mwandishi wa tanzu mbali mbali za fasihi zikiwemo riwaya, tamthilia, hadithi fupi, mashairi, hadithi za watoto na pia tahakiki mbali mbali za kazi za fasihi. Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa riwaya pekee. Riwaya tatu teule za mwandishi zilizoangaziwa ni pamoja na *Musaleo!* (2004), *Msichana wa Mbalamwezi* (2011), na *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* (2014). Riwaya hizi ziliteuliwa kimaksudi kwa sababu zinatamalaki sifa tofauti

tofauti za riwaya za kimajaribio. Utafiti uliangazia sifa bainifu za mbinu za kimajaribio kama zinavyotumiwa na mwandishi katika riwaya ili kuwasilisha maudhui na kuiakisi taswira ya jamii ya leo. Sifa bainifu zilizoshughulikiwa ni pamoja na ukatizwaji wa usimulizi unaosababishwa na taashira, urejeleomatini, msuko changamano, lugha na fani nyinginezo za fasihi. Katika riwaya za kimajaribio hali zilizotajwa zinahusiana na kuingiliana.

## 1.7 Ufafanuzi wa Istilahi na Akronimu

- Dayolojia:** Mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi kuhusu jambo fulani. Yanaweza kuwasilishwa ana kwa ana au kwa njia ya simu. Katika utafiti huu, dayolojia zimewasilishwa katika njia ya maandishi.
- Jamii ya kisasa:** Sura ya jamii katika karne ya ishirini na moja. Pia imerejelewa kama jamii ya Karne ya Ishirini na Moja. Vilevile, katika utafiti istilahi hii inajumuisha mataifa ya Afrika yanayoendelea.
- Kunga za kiuandishi:** Vigezo vinavyoifanya kazi fulani ya fasihi ibainike na ikubalike kama sanaa. Katika utafiti huu kunga za uandishi ni sawa na mbinu za uandishi wa bunilizi. Aidha, kunga ni sawa na nyenzo.
- Mbinu za majaribio:** Nyenzo za uandishi wa kazi za fasihi zinazoipelekea kazi husika kukiuka kaida za kijadi za utunzi wa uhalisia. Katika utafiti huu mbinu hizi za kimaribio zimerejelewa kama za mtindo mpya. Mifano ya mbinu za kimajaribio ni kama vile taashira, uradidi, urejeleomatini, dayolojia, mwingilianotanzu miongoni mwa nyingine.
- Riwaya za kijadi:** Riwaya za mwanzo mwanzo zilizozingatia uhalisia wa kihistoria. Mtindo uliotumiwa kuandikia riwaya za kijadi ambao ni tofauti na ule wa riwaya za kisasa. Katika utafiti huu, riwaya za kijadi ni kinyume cha riwaya za kimajaribio. Vilevile, zimerejelewa kama riwaya asilia.
- Riwaya za kimajaribio:** Riwaya zilizoandikwa kwa kutumia mbinu za kimajaribio. Nyingi ya riwaya hizi zinaegemea mtazamo wa usasaleo. Aidha, ni riwaya zilizoandikwa baada ya usasa yaani baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Vilevile istilahi hii ilirejelea riwaya zilizoandikwa baada ya uvumbuzi wa teknolojia mpya. Katika utafiti huu pia zimerejelewa

kama riwaya za kisasa, riwaya za Karne ya Ishirini na Moja au riwaya mpya.

**Usasaleo:** Mtazamo wa uandishi wa riwaya mpya unaopinga na kuumbua maswala yaliyozingatiwa katika enzi za usasa. Katika utunzi wa kazi zinazoegemea mtazamo huu, watunzi wana uhuru wa kujaribu/kutumia mbinu mpya badala ya kujibana kwa mbinu moja. Vilevile, istilahi hii ilitumiwa kurejelea mwongozo wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data pamoja na uhakiki wa riwaya teule. Usasaleo ni kisawe cha usasabaadaye.

**Uhalisia mpya** Matumizi ya mbinu inayowasilisha mambo yaliyo katika hali halisi ya jamii kwa kutumia udhahania au uhalisiajabu.

**Uandishi wa bunilizi:** Hatua na mbinu zinazotumiwa na waandishi bunifu katika utunzi wa kazi za fasihi.



## SURA YA PILI

### YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

#### 2.1 Utangulizi

Sura hii imeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Imeonyesha maoni ya wasomi kuhusiana na kunga za kiuandishi za kimajaribio kwa jumla. Mtafiti amebainisha chanzo na historia ya mbinu za kiuandishi za kimajaribio kama kunga ya uandishi wa riwaya na nathari kwa jumla. Maswala ya umbo, maendeleo na mabadiliko katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili yameangaziwa ili kuibua taswira ya mahali riwaya ilipoanzia na pale ilipo sasa. Aidha, sura hii imeweka bayana maelezo mbalimbali kuhusu tofauti za kimuundo na msuko baina ya riwaya za kijadi na zile za kimajaribio. Isitoshe, ufafanuzi kuhusu sifa za riwaya za kijadi na za kimajaribio umefanywa. Vilevile, yaliyoandikwa kuhusu historia ya uandishi wa riwaya za Wamitila yameangaziwa. Mtafiti amezingatia yale yaliyosemwa na watafiti wengine kuhusu mtindo wa uandishi wa Wamitila. Hatimaye, misingi na mihimili ya nadharia ya usasaleo ambayo imeuongoza utafiti huu imefafanuliwa. Mtafiti ameeleza jinsi mihimili hiyo ilivyotumiwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Mapengo ya kiusomi yaliyopo yamebainishwa na kutathminiwa.

#### 2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Chanzo na Ukuaji wa Kunga za Kiuandishi za Kimajaribio

Kunga za kimajaribio zilikuwepo na zitaendelea kuwepo ila kwa mitindo na miundo tofauti. Barth (1984) anasema kwamba kitovu cha uandishi wa kimajaribio ni mabara Uropa na Marekani ambapo uandishi wa kimajaribio ulihusishwa na enzi za usasaleo na uzinduzi wa kitaaluma. Katika kitabu chake *Introduction to Literature of Exhaustion* Barth anaeleza kwamba uandishi wa kimajaribio ulipata umaarufu mkubwa katika miaka ya 1910. Waandishi wa kwanza wa kimajaribio ambao walikuwa ni Wazungu na Wamarekani walianza kwa kujaribu hali chache za uandishi wa kimajaribio. Hali zilizotumika sana katika utunzi wakati huo ni matumizi ya vijikaratasi-chapwa na vihadithi vidogo vidogo. Kwa misingi hii ni dhahiri kwamba kulitokea mabadiliko makubwa katika uandishi wa kazi za fasihi kwa jumla zikiwemo riwaya. Waandishi wa kazi za nathari zilizovuma wakati huo ni pamoja na Eliot na Stein, riwaya *Ulysses* ya mwandishi James Joyce iliandikwa na kuchapishwa wakati huo. Kutokana na mawazo haya ni dhahiri kuwa ingawa uandishi wa kimajaribio umekuwepo tangu jadi umekumbwa na mabadiliko kila uchao. Minajili ya haya utafiti huu uliungazia uandishi wa kimajaribio kwa

kuongozwa na riwaya za mwandishi Wamitila kama mwanamajaribio wa riwaya ya Kiswahili ya Karne ya Ishirini na Moja. Maoni ya Barth (1984) yameuwekea msingi huu hasa katika shughuli ya ubainishaji na uchanganuzi wa sifa bainifu za utunzi wa kimajaribio katika riwaya teule za Wamitila. Lengo kuu lilikuwa kubaini jinsi mwandishi alivyotumia mbinu za kimajaribio kama kunga ya uandishi ya uwasilishaji wa maudhui katika riwaya zake. Aidha, mtafiti amebainisha jinsi ubunifu wa Wamitila unavyoiakisi jamii ya leo.

Kneppert (2016) anadai kuwa kipindi cha historia cha *Avant-garde* kilitoa mchango mkubwa katika maendeleo na ukuaji wa riwaya za kimajaribio katika Karne ya Ishirini. Waandishi katika kipindi hiki walikuwa na sababu mbalimbali za kutumia mbinu za kimajaribio katika uandishi wa bunilizi walizotunga. Uandishi wa kimajaribio ulichochea na hali za kisiasa zilizokuwepo wakati huo. Wanajamii walitaka uhuru, haki na usawa katika nyanja zote za jamii zao, uandishi ukiwemo. Walitumia uandishi wa kimajaribio kufahamishana jinsi ya kujinasua kutoka kwa ukoloni. Vuguvugu jingine lililojiita *Dada* liliibuka na kusesitiza kuwepo kwa uandishi wenye uhuru wa kuwasilisha mawazo (Barth, 1984). Kwa hamasisho hili mwandishi Tristan Tzara alitumia uhuru wa utunzi kuandikia manifesto yake iliyosisimua. Kwa kutumia vijikaratasi vyenye matini tofauti tofauti alizokata kutoka kwenye magazeti na kuzifanya nyenzo za kuwasilishia manifesto hiyo, Tzara aliamsha ari mpya ya ubunifu ambao umeendelezwa katika Karne ya Ishirini na Moja na waandishi akiwemo Wamitila. Mbinu alizotumia Tzara kuandikia hadithi zake ni msingi maalumu wa uandishi wa kimajaribio kwa kuwa unaendeleza matumizi ya simulizi fupi fupi katika usimulizi mkuu. Mpito wa wakati uliibua matumizi na mitindo tofauti ya simulizi fupi. Tofauti na utafiti wa Kneppert (2016), utafiti huu umeangaliza ruwaza mbalimbali za simulizi fupi zinazotumika katika riwaya teule.

Kwa mujibu wa Barth (1984), katika miaka ya 1910-1920 kundi jingine la kimapinduzi, *The Surrealist Movement* lilitumia mbinu zilizokiuka kaida na utaalumu wa kijadi ili kuamsha hisia za jamii na kuihamasisha kwa uandishi bunifu. Riwaya moja iliyobobea wakati huu ni *LesChamps Magnetiques* ya waandishi Andre Breton na Philippe Soupalt. Msanii mwingine wa wakati huu alikuwa Robert Desnos wa riwaya ya kusesimua, *Sorrow of Sorrow* iliyoandikwa kwa kuzingatia mtindo wa hiponozizi. Mtindo huu unasisitiza uandishi unaojikita katika upumbazaji wa akili ya msomaji na kumweka katika hali ya kuwa kama katika usingizi mzito. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa uandishi wa kimajaribio hutokana na miundo au mitindo ya utunzi

inayohusika katika tungo zenyewe. Utafiti wa Kneppert unadhihirisha kuwa uandishi wa kimajaribio huchochewa na matukio mahsusi katika jamii. Mintarafu ya haya, utafiti huu haukujikita na vochochezi bali ulijadili sifa bainifu za mbinu za kiuandishi za kimajaribio kama zinavyoshuhudiwa katika riwaya teule. Ufafanuzi wa maudhui ulitumiwa kueleza jinsi mwandishi anavyoiakisi taswira ya jamii yake.

Hali ya kisiasa ilipobadilika barani Uropa mwishoni mwa miaka ya 1930 uongozi wa kifashti ulishika hatamu. Waandishi wa wakati huo walishikilia kuwa usasa haukutosheleza kueleza kikamilifu mabadiliko ya kisiasa yaliyokuwemo. Kwa sababu ya hofu ya maafa yaliyosababishwa kote ulimwenguni na uongozi wa kiimla wa ufashti, uandishi wa kimajaribio ulififia kwa muda (Barth, 1984). Baadaye, waandishi wachache kama vile Kenneth Patchen, Jack Kerouac na John Hawkes walifufua na kuendeleza ndoto ya uandishi wa kimajaribio kati ya 1940 – 1950. Barth (1984) anaendelea kueleza kuwa hali hii iliendelea hadi miaka ya 1960 ambapo ilibainika wazi kuwa utukufu wa usasa ulikuwa umekita mizizi na kudidimiza usasaleo katika maswala ya uandishi. Uandishi na uchapishaji wa bunilizi za kimajaribio ulipungua kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, ukakamavu wa mwandishi William Burrough katika riwaya *Naked Lunch* uliibua hisia nzito za hamu ya kuwa na uhuru katika uandishi. Katika uhuru huo, Burrough aliibua mbinu mpya iliyoitwa “*Cut-up*” ambapo matini zilizopigwa chapa zilikatwa kutoka magazetini na vitabu vingine na kutumika katika uandishi wa riwaya. Kufikia mwisho wa miaka ya 1960 uandishi wa kimajaribio ulishika kasi tena na ukawa maarufu. Umaarufu wa uandishi wa kimajaribio uliwafanya waandishi wa kihalisia kama Bernard Malamud na Norman Mailer kuukumbatia. Sifa bainifu ya kimajaribio iliyotumika zaidi katika uandishi ni matumizi ya bunilizi ndogo ndogo zilizotapakaa katika bunilizi kuu. Msanii aliyebobea wakati huo alikuwa Thomas Pynchon. Aliandika riwaya *Gravity’s Rainbow* iliyonunuliwa kwa wingi sana. Maelezo ya Barth yanabaini kuwa uandishi wa kimajaribio uliongeza elementi mpya za uandishi kulingana na mpito wa wakati. Hali hii imedhihirika katika kipindi cha historia ambapo Wamitila anaandikia. Katika msingi huu, utafiti huu ulibainisha sifa bainifu mbalimbali za kimajaribio zilizofanikisha matumizi ya mbinu za kimajaribio katika uwasilishaji wa maudhui pamoja na uakisi wa jamii ya kisasa katika riwaya teule za Wamitila katika kipindi cha historia alichandikia.

Martha (2008) ametafiti kuhusu riwaya za kimajaribio kati ya miaka ya 1970 – 1980. Kwa mujibu wa utafiti wake riwaya za nyakati hizo zilikuwa na sifa za kimajaribio zilizokuwa changamano zaidi. Akirejelea riwaya *If on a Winter's Night a Traveller* ya Italo Calvino anasema kuwa riwaya yenyewe ilikuwa changamano katika mpangilio wa sura. Baadaye katika mwaka 2005 uandishi wa kimajaribio ulipata mashiko (Barth, 1984). Riwaya zilizobobea katika kipindi hicho ni pamoja na *Pedro Paramo* ya Juan Rulfo wa Mexico, *One Hundred Years of Solitude* ya Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, *The War of the End of the World* ya Mario Vargas wa Peru, *Yo-Yo Boing* ya Giannina Braschi wa Puerto Rico na *Paradise* ya Lezanna Lima wa Cuba, Marekani Kusini. Waandishi wa kipindi hiki waliambatanisha mbinu za kimajaribio na hisia mbalimbali katika uandishi wa riwaya. Wengine waliongeza swala la futuhi katika usimulizi. Hatimaye, sanaa ya kimajaribio ilizaliwa upya na uandishi wa Mark Danielewski katika riwaya yake ya *House of Leaves*. Katika riwaya hii mwandishi alitumia simulizi fupi fupi kuifikia hadhira yake. Utafiti huu ulichanganua matumizi ya aina mbalimbali za simulizi fupi fupi na jinsi zinavyomwezesha mwandishi Wamitila kuwasilisha maswala muhimu yanayoihusu jamii katika riwaya teule.

Katika Karne ya Ishirini na Moja riwaya za kimajaribio zilihhusiana na kuibuka kwa matumizi ya tarakilishi na teknolojia za kidijitali. Elliot (2017) katika ufafanuzi wa riwaya *Z213:Exit* ya Dimitris Lyacos anafafanua kuwa ni hadithi iliyoandikwa kwa kurejelea simulizi nyingi fupi fupi. Riwaya ya Dimitris ni hadithi nzuri lakini uchangamano wa mtindo na msuko wake huweza kumchosha msomaji (Elliot, 2017). Kwa misingi hii utafiti huu ulizingatia jinsi mwandishi Wamitila anavyopanga na kutumia kipengele cha bunilizi nyingi fupi fupi katika riwaya kuu katika uwasilishaji wa ujumbe wake kwa jamii. Aidha, mtafiti amejadili athari za tendo la uchupaji wa vihadithi vidogo vidogo katika hadithi kuu na jinsi unavyoakisi jamii ya Karne ya Ishirini na Moja. Utafiti wa Elliot umetaja kwamba Dimitris alirejelea simulizi nyingi katika riwaya yake lakini haukutaja wala kueleza aina za simulizi zenyewe. Mintarafu ya haya, utafiti huu umeangazia aina mbalimbali za matini zilizorejelewa na mwandishi katika riwaya teule. Zaidi ya hayo, mtafiti ameeleza maana zilizoibuliwa na bunilizi hizo ili kuonyesha mchango wa mbinu za kimajaribio katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya teule.

Mbinu za kiuandishi za kimajaribio zilikita mizizi barani Afrika kwa mara ya kwanza kwa uandishi wa riwaya katika lugha ya Kiingereza (Zabus, 1997). Uandishi wa riwaya ya *Things*

*Fall Apart* ya Chinua Achebe mnamo mwaka 1958 ulisisimua ari ya waandishi wengine wa Kiafrika waliotumia mbinu za kiuandishi za kimajaribio. Katika mwaka wa 1973, Ayi Kwei Armah aliandika riwaya ya *Two Thousand Seasons*. Emecheta Buchi aliandika *The Slave Girl* mnamo mwaka 1977. Riwaya iliyokuwa na mabadiliko makubwa zaidi ya kimajaribio barani Afrika wakati huo ilikuwa *Sozaboy* ya Ken Saro-Wiwa. Mwandishi huyu alikiuka sheria ya kijadi ya utunzi kwa kutumia lugha yenye makosa mengi ya kisarufi ili kuonyesha uozo uliokuwa katika nchi ya Nigeria wakati huo. Maovu ya dhuluma na uufisadi yalikithiri nchini humo. Riwaya yenyewe ilifahamika kama, “*A Novel in Rotten English*” (Zabus, 1997). Kwa misingi hii utafiti huu ulifafanua matumizi ya lugha huru ambayo ni mojawapo ya sifa bainifu za kimajaribio. Mtafiti ameonyesha jinsi riwaya zilivyotumia lugha huru kuyafichua maswala mbalimbali ya kindani yaliyofichika katika jamii husika hivyo kubainisha mchango wa mbinu za kimajaribio katika uwasilishaji wa maudhui.

Wakirejelea uandishi wa kimajaribio barani Afrika, Deleuze na Guattari (1986:26) wanasema kuwa riwaya za Kiafrika zilifanyika kuwa “fasihi ya wachache iliyoandikwa kwa lugha ya wengi”. Katika utambuzi na ufafanuzi wa mbinu za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya teule za kisasa, utafiti huu ulichanganua matumizi ya uandishi huru na fiche kama kipengele cha uandishi wa kimajaribio kinachokatiza usimulizi katika riwaya husika. Uchanganuzi umethibitisha ukweli wa usemi kuwa “riwaya mpya ni fasihi ya wachache iliyoandikwa katika lugha ya wengi”.

Khamis (1991) anaeleza kuwa mabadiliko katika riwaya ya Kiswahili yalianza kushuhudiwa kuanzia miaka ya 1990. Vilevile, riwaya ya kimajaribio ilianza kubainika barani Afrika miaka hiyo hiyo ya 1990 na 1991 kwa uchapishaji wa riwaya za Euphrase Kezilahabi; *Nagona na Mzingile* mtawalia (Gromov, 1998). Gromov anaeleza kuwa riwaya za Kezilahabi zilikiuka kabisa kaida za utunzi wa bunilizi za kijadi za Kiswahili. Badala ya mtindo wa kijadi, ziliegemea mtindo wa uhalisia-mpya. Zilionyesha sifa bainifu za kimajaribio katika fani za muundo na mtindo. Tangu wakati huo riwaya za Kiswahili za kimajaribio zimeandikwa na kuchapishwa kwa wingi hasa nchini Kenya na hali kadhalika kwingineko katika Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa haya, utafiti huu ulichanganua mitindo na miundo ya kimajaribio iliyotumika katika riwaya za kisasa zikiwakishwa na riwaya zilizoandikwa na Wamitila.

### 2.3 Kunga za Uandishi wa Riwaya

Mikakati, maarifa au vifaa muhimu vinavyotumika kuandikia riwaya za kimajaribio huchangia katika kuujenga ubunifu wa mwandishi husika. Katika muktadha wa fasihi, kunga, mbinu au maarifa anayotumia mwandishi Wamitila katika ubunifu wa riwaya zake zimezipa sura tofauti na riwaya za kijadi. Kama anavyofafanua Mohammed (1995) vigezo vingi alivyotumia Wamitila vimezifanya riwaya zake kuwa na umbo na mtindo wenye uchangamano. Vigezo muhimu vinavyoikamilisha kazi yoyote ya sanaa ni nyenzo, ubunaji, umbo na muundo, maana, upatanisho, hisia, uzuri wa kisanaa na mtindo. Kunga zote hizi huingiliana na kutegemeana katika ubunaji wa kazi za fasihi. Utafiti huu ulichanganua jinsi riwaya za Wamitila zinavyofanikiwa kuwasilisha maswala muhimu yanayoikumba jamii kwa kutumia kunga za kiuandishi za kimajaribio. Maswala ambayo yameshughulikiwa katika kazi teule yanahusu nyanda za kisosholojia, kiuchumi, kisiasa, kisaikolojia miongoni mwa nyingine ila yamefichika kwa ustadi katika kunga za kimajaribio. Yametapakazwa kote riwayani kwa njia changamano. Mtafiti ameongozwa na ufahamu huu kuchanganua ujumbe uliofichwa katika kunga za kimajaribio zilizotumika katika riwaya za mwandishi teule.

Nyenzo hutumiwa kuundia na kuwasilishia kazi ya fasihi kwa hadhira lengwa. Ubunaji ni sawa na ubunifu (Mohammed, 1995). Katika ubunifu ambao ndicho kiini cha kazi ya fasihi msanii hupanga, hunakili na kuwasilisha kazi yake kwa namna inavyonata ili aeleweke na hadhira lengwa. Kazi ya fasihi lazima ibuniwe kwa kutumia lugha ya kisasa, uzoefu wa mtunzi na maarifa aliyopata kutokana na upelelezi wa mazingira na ulimwengu unaomzunguka (Gromov, 2009). Hivyo, mtaalamu Gromov anashikilia kuwa kazi ya mwandishi hufanywa kuwa ya kipekee kwa sababu ya kunga za uandishi anazotumika. Katika utafiti wake wa riwaya za *Nagona* na *Mzingile*, Gromov anadokeza kuwa utunzi wa Kezilahabi umeipa idara ya usomi data nyingi ya kutafitia zikiwemo data za uandishi wa kimajaribio. Kando na haya, riwaya za kisasa zikiwemo za mwandishi Wamitila zimeelezwa kuwa zenye uchangamano mwingi (Rettova, 2016). Uchangamano wa kazi zozote za fasihi huletwa na kunga zinazotumika. Mintarafu ya haya, utafiti huu umebainisha kwamba mbinu za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya za Wamitila zimezipa riwaya zenyewe upekee hasa kuhusu jinsi zinavyowasilisha maswala muhimu ya kijamii. Upekee huo ni kitambulisho kamili cha jinsi jamii ya kisasa ilivyo.

Mohammed (1995) anasisitiza kwamba kazi ya fasihi ni kama uchongaji. Kinachosababisha mvuto katika kazi ya fasihi ni muundo na mpango wa kunga zinazotumiwa na mwandishi. Mbinu zinazotumiwa na mwandishi ni sharti zivutie hadhira. Kukubalika au kupendwa kwa kazi ya fasihi kunategemea pakubwa ubunifu wa mtunzi. Umbo kama kigezo cha kunga za utunzi hurejelea matokeo ya kuunganishwa kwa vitu vya aina aina ambavyo huwekwa katika mfumo fulani kwa ubingwa na ufundi. Mfumo unaotumiwa na waandishi wa kazi za sanaa husababisha umbo la kazi husika. Nalo umbo na muundo huleta tofauti katika kazi za sanaa. Utafiti ulikuwa na jukumu la kuchunguza kwa makini vipengele vinavyovunjavunja muundo na mtindo wa kijadi katika riwaya teule na kufanya uwasilishaji wa maswala ya jamii kuwa na utofauti na upekee.

Mwandishi yeyote hutumia maneno katika kujenga umbo la sanaa katika mpangilio fulani. Bombwe huambatana na mpangilio huo ili kuleta hali ya uradidi katika kazi ya fasihi kwa kutumia sauti mbalimbali. Sauti katika riwaya hutoka kwa mwandishi na pia wahusika. Katika riwaya, bombwe hujitokeza katika usimulizi kwa minajili ya kuleta maana ambayo huenda pamoja na dhamira. Katika riwaya kinachorejelewa kama maana ni maudhui (Mohammed, 1995). Riwaya lazima zidhihirishe upatanisho katika nyanja mbalimbali kama vile fani na maudhui, lugha na wahusika na pia lugha na fani. Mohammed anazidi kufafanua kuwa ubunifu huambatana na kigezo cha hisia. Mwandishi huwa na hisia fulani kabla ya kuiandika kazi yake. Hisia zaweza kuwa za huzuni, msiba, furaha, chuki, mapenzi, ari, kukata tamaa, ukweli na unafiki (Mohammed, 1995). Hivyo, hisia humfanya msomaji kuipenda au kuichukia kazi fulani ya sanaa. Kwa kuzingatia mkabala wa kiujumi kazi ya fasihi yafaa kuwa na uzuri wenye mvuto unaowapendeza na kuwagusa wasomaji wake. Kwa jumla kazi za fasihi huwepo na hukubalika kwa sababu ya kunga za uandishi zilizotumika katika ubunifu wake. Maoni haya yalikuwa msingi maalum wa ufafanuzi wa ufaafu wa mbinu za kimajaribio zilizotumika katika riwaya teule katika uwasilishaji wa ujumbe kwa jamii. Kunga zilizoelezwa na Mohammed (1995) yaani nyenzo, ubunaji, umbo na muundo, maana, upatanisho, hisia, uzuri wa kisanaa na mtindo ndizo zinazotumika pia katika riwaya za kimajaribio. Hata hivyo, matumizi yake katika riwaya za kimajaribio hukiuka kaida za utunzi wa kijadi au kihalisia.

## **2.4 Umbo, Maendeleo na Mabadiliko Katika Riwaya ya Kiswahili**

Mlacha na Madumulla (1999) wanaeleza kuwa kati ya mwaka wa 1910 hadi 1920 riwaya ilihusisha hadithi fupifupi zilizoandikwa katika vijigazeti vya zama. Utafiti wa awali kidogo uliofanywa na Mulokozi (1996:164) umedhihirisha kwamba riwaya ilipevuka zaidi katika Karne ya Ishirini ambapo riwaya za kifalsafa zilizojadili maisha, utawala na ujenzi wa jamii mpya ziliibuka. Riwaya hizi ziliifafanua jamii katika mkondo wa ubinadamu, usawa na ustawi. Mulokozi anaongeza kufafanua kwamba katika mwaka 1960 kuliibuka riwaya pendwa na katika miaka ya 1970, riwaya ilipevuka zaidi na kupata uhai mpya. Huu ndio uliokuwa msingi wa riwaya ya kisasa ambayo imekumbwa na mabadiliko mengine chungu nzima ya kiuandishi na kimtindo. Pindi jamii ilivyobadilika na waandishi wengi kuibuka ndivyo mbinu za uandishi zilivyobadilika ili kuafikiana na hali mpya ya kimaisha.

Mlacha na Madumulla (1991) wanaeleza kwamba umbo la riwaya ya Kiswahili ya mwanzo lilishahibiana sana na ngano za kijadi. Ni umbo lililohusu msuko sahili unaowasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa urahisi. Riwaya za mwanzo mwanzo pia zilifanana na ngano za kijadi kifani hasa katika usawiri wa wahusika, msuko wa vitushi, maudhui na dhamira kama vile ilivyo katika riwaya za Shaaban Robert, *Adili na Nduguze* na *Kusadikika* (Njogu & Chimerah, 1999). Riwaya za mwanzo zilichukua umbo la hekaya. Zilijawa na visa vya usisimuzi vyenye masaibu na matukio yasiyokuwa ya kawaida. Hivi ni kusema kuwa riwaya za kijadi zina uhusiano wa karibu na fasihi simulizi. Kuna mfanano wa kifani na kimaudhui baina ya riwaya za kijadi na hekaya (Onyoni, 2012). Uchanganuzi wa riwaya *Ubeberu Utashindwa* ya Kiimbila unaweka wazi hali kwamba riwaya za kijadi zina athari nyingi za hekaya. Ni dhahiri kuwa riwaya za jadi zinafuata mifumo ya hadithi zinazosisimua mithili ya hekaya. Kinyume na haya, riwaya ya kisasa ina mchanganyiko wa hekaya na hadithi nyingi ndogo ndogo zinazorejelea matini nyingine ndani ya hadithi moja. Utafiti huu uliangazia ujumbe muhimu uliojitokeza katika aina mbalimbali za matini-rejelewa katika tungo fupi fupi zinazotumiwa na waandishi wa kisasa kama kunga za ubunifu katika riwaya za kisasa.

Riwaya ya jadi ilijawa na visa vya kuisimua na masaibu ya ajabu ajabu mathalan riwaya ya *Ubeberu Utashindwa* ya Kiimbila (1971). Hivi ni kubaini kwamba riwaya haijasimama mahali pamoja. Inakua kwa mujibu wa mpito wa wakati. Baadhi ya mambo yanayoonyesha ukuaji huu ni ukweli kwamba badala ya kuwepo kwa visa virefu vyenye mwanzo-kati-mwisho, riwaya ya



kisasa imejawa na vipande vingi vidogo vidogo ndani ya hadithi kuu (Mlacha, 1995). Utafiti huu wa awali umekuwa msingi wa kuuelekeza utafiti huu wa sasa katika ubainishaji wa baadhi ya mabadiliko ya uandishi wa riwaya yaliyotokana na mpito wa wakati kwa kuzingatia riwaya teule za Wamitila. Baadhi ya mabadiliko yaliyobainika yalijikita katika fani za maudhui, mtindo, muundo na lugha. Hivyo katika msingi huu mabadiliko wa yaliwasilishwa na sifa bainifu za mbinu za kimajaribio kama vile matumizi ya vipande vidogo vidogo vya hadithi, uradidi uliokithiri, urejeleomatini, mwingilianotanzu, taashira na uhalisiajabu.

Kwa mujibu wa Madumulla (2009) riwaya ya Kiswahili imeathiriwa na mabadiliko ya kihistoria na kiteknolojia. Hali hii imepelekea kuwepo kwa riwaya za kisaikolojia ambazo jukumu lake kuu ni kudodosa nafsi ya mhusika, fikra, hisia, mawazo, imani, hofu, mashaka, matumaini; mambo ambayo humwathiri mwandishi binafsi na labda jamii yake kwa jumla. Kwa mfano riwaya za *Kichwamaji* ya Kezilahabi na *Kiu* ya M.S. Mohammed ambazo zilitungwa katika Karne ya Kumi na Tisa zilifuata mkondo huu. Kwa hivyo, inakisiwa kuwa riwaya za mwanzo mwanzo zilizotungwa kwa njia ya kihalisia ambapo maisha ya kawaida ya jamii yalielezwa kwa kuchunguza matatizo yake (jamii husika), yawe ya kifamilia, kitabaka, kiuchumi, kisiasa au hata kitamaduni. Maoni haya yaliufaa utafiti huu katika kutambulisha na kulinganua utofauti uliopo baina ya utunzi wa kijadi na ule wa kisasa. Mtafiti aliafikia haya kwa kuangazia sifa bainifu mbalimbali za kiuandishi za kimajaribio zilizohusishwa na msanii Wamitila katika riwaya zake za kisasa.

Madumulla (1995) amechunguza mabadiliko ya riwaya kwa kuzingatia kipengele cha uhusika. Anadai kuwa wahusika wakuu katika riwaya za kijadi ni tofauti mno na wale wanaopatikana katika riwaya za kisasa. Hata ingawa mabadiliko yaliyoshuhudiwa yalitokea kwa utaratibu fulani, mtalaamu huyu anafafanua kwamba katika riwaya za kijadi mhusika mkuu alikuwa na nguvu za ajabu, nguvu za kiungu na hamu kuu isiyovia hasa katika juhudi za kutimiza lengo lake. Mfano mzuri ni mhusika Dzombo katika riwaya ya *Walenisi* ya Katama Mkangi. Mhusika huyu amepewa uwezo wa kufahamu kuendesha sayari, jambo ambalo halikuwa limewahi kufanywa na binadamu mwengine yeyote. Madai haya yalikuwa msingi imara wa kazi hii hasa katika uchambuzi wa fani ya uhusika wa kisasa katika riwaya teule za mwandishi Wamitila. Vile vile maoni haya yametumiwa kuuongoza utafiti kufafanua jinsi mwandishi anavyowasawiri wahusika wake na kuwafungamanisha na nyenzo za kimajaribio kwa minajili ya kuinasihi jamii yake.

Sifa bainifu za baadhi ya kazi za fasihi ya Kiswahili za Karne ya Ishirini na Moja ni matumizi makubwa ya mbinu za kiuandishi za kimajaribio (Mwamzandi, 2013). Katika ubunaji wa sifa za kimuundo na kimtindo, mpangilio wa kijadi umekiukwa. Vilevile, mtindo wa kisimulizi katika riwaya za kisasa huonyesha ubunifu mkubwa. Mathalan, katika maingiliano baina ya sauti ya kisimulizi na mhusika, mvunjiko wa mkondo wa usimulizi na uchangamano wa kimuundo kwa jumla (Senkoro, 2011). Wamitila (2010) anadokeza kuwa licha ya kuwa riwaya za kimajaribio zimeainishwa katika misingi ya fani, kuna umuhimu wa kuangaliwa katika misingi ya kidhamira. Hivyo, kinachosababisha utofauti baina ya riwaya za kijadi na riwaya za kisasa ni suala lenye uwezo wa kuibua falsafa mpya za waandishi wa kisasa (Wamitila, 2010). Pendekezo hili la Wamitila liliumotisha utafiti huu hamu kuu ikiwa ni utambuzi na ufafanuzi wa mparaganyiko na uchangamano katika ulimwengu wa sasa ambao pia unajitokeza katika uandishi bunifu. Utafiti huu uliainisha vipengele mbalimbali vya kimajaribio katika uwasilishaji wa dhamira, maudhui na fani nyinginezo za fasihi katika riwaya teule za Wamitila.

## **2.5 Sifa Bainifu za Riwaya ya Kiswahili ya Kimajaribio**

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) riwaya ya kimajaribio hujitokeza katika mikondo miwili. Kwanza ni mkondo wa mjadala-nafsi na pili ni mkondo wa riwaya-kweli. Watunzi wa kimajaribio hudai kwamba umbo la kawaida la riwaya haliwezi kutosheleza mahitaji ya karne hii yenye maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia (Mulokozi, 1996). Hivyo, mbinu za kiuandishi za kimajaribio ambazo ni kunga ya utunzi katika kazi za fasihi zisizofuata kanuni za kijadi huhitajika kufidia upungufu huu. Mbinu za kimajaribio zinapotumika katika uandishi wa kazi yoyote ya fasihi huipa kazi hiyo sura na umbo tofauti na riwaya zinazoegemea mtindo wa uhalisia. Uandishi wa kimajaribio hujitokeza katika fani mbalimbali za fasihi kama vile wahusika, lugha, usimulizi, maudhui na dhamira. Kila msanii wa kazi ya fasihi huwa na sababu zake mahususi za kutumia mbinu anazochagua. Mintarafu ya haya utafiti huu ulichanganua fani za fasihi zilizodhihirisha kuwepo kwa matumizi ya mbinu za kimajaribio katika utimizaji wa malengo ya mwandishi Wamitila kama mmojawapo wa waandishi wa riwaya za kisasa.

Kuwepo kwa mfuatano wa visa au vitushi ndio uti wa mgongo na sifa ya asilia inayotamalaki katika riwaya za kijadi (Madumulla, 2009). Khamis (2005) katika Mwangi (2013) anafafanua kuwa mwandishi wa riwaya ya Kiswahili ameiona jamii ikibadilika katika mila, desturi na mienendo kutokana na nguvu za kiuchumi na kiteknolojia. Mwandishi Wamitila pia amefahamu

kwamba mbinu za kijadi pekee haziwezi kutosheleza mahitaji ya fasihi yenye taswira kamili ya jamii inayowakilishwa. Kwa hivyo, mwandishi wa kisasa ameandika juu ya jamii yake kwa njia ambayo ni tofauti na njia za kijadi.

Sifa hizi zikiwemo katika riwaya ya kisasa zinasababisha uchangamano wa mtiririko wa vitushi na kukatiza usimulizi. Tofauti na utafiti wa Mwangi (2013) ambao ulikuwa msingi bora wa utafiti huu, lengo kuu la utafiti lilikuwa kufafanua sifa mbalimbali za kimajaribio zinazofanikisha ubunifu na uwasilishaji wa maudhui katika riwaya teule za mwandishi Wamitila. Utafiti wa Mwangi ulichunguza na kutambulisha sifa bainifu za riwaya za kimajaribio kwa jumla. Utafiti huo haukuonyesha vipengele vya sifa hizo na jinsi kila kipengele kinavyotumika katika uakisi wa jamii katika kazi husika. Mtafiti alitaja swala la urejeleomatini akijikita katika dhana za uhalisia na uhalisiajabu lakini hakushughulikia aina za matini zilizohusishwa katika utunzi. Kinyume na kazi ya Mwangi, utafiti huu ulibainisha sifa bainifu za vipengele vya kimajaribio kama zinavyotumika katika riwaya teule za Wamitila.

## **2.6 Mitazamo ya Uandishi wa Riwaya Tangu Jadi hadi Sasa**

Mtazamo wa uandishi wa fasihi wa mwanzo kabisa ulikuwa urasimi. Njogu na Wafula (2007) wamebaini kuwa urasimi ulioendelezwa na wanafalsafa wa Kigiriki wakiongozwa na Plato, Aristotle, Horace na Longino ulishikilia kuwa riwaya na fasihi kwa jumla ni sharti itimize dhima yake kwa jamii bila kumkanganya msomaji. Wataalamu hawa wanaendelea kusema kuwa wanafalsafa wa kipindi cha urasimi walikubaliana kwamba fasihi huibua hisia zinazoathiri maadili ya msomaji. Isitoshe, urasimi katika fasihi ya Kiswahili ulianza kudhihirika katika Karne ya Kumi na Nane. Kwa mintarafu ya haya uandishi bunifu ulitarajiwa uwasilishwe katika lugha, mtindo, msuko na muundo unaoeleweka. Aidha, urasimi mkongwe ulizingatia na kusesitiza uhalisia katika utunzi na kusuta mitindo ya kinjozi (Abrams, 1988). Riwaya za urasimi hazichoshi kusoma. Maudhui huwasilishwa kwa kutumia fani chache za lugha teule. Daima kuna ufungamano kamilifu kati ya kinachoelezwa na jinsi kinavyoelezwa (Njogu & Wafula, 2007). Kinyume na haya, mbinu za kimajaribio ambazo ndizo kiini cha utafiti huu, huufanya mtiririko wa riwaya kumkanganya na kumpoteza msomaji. Haya hutokea kwa sababu ujumbe huwasilishwa kwa matumizi ya fani nyingi na njia fiche, yaani uwasilishaji usio wa moja kwa moja.

Baada ya urasimi, riwaya iliingia katika kipindi cha ulimbwende (Mihanjo, 2010). Kwa mujibu wa Wamitila (2003) ulimbwende ulizuka mwishoni mwa Karne ya Kumi na Nane na Mwanzoni mwa Karne ya Kumi na Tisa. Ulimbwende ulisisitiza matumizi ya sifa za kisanaa na muziki (Samson, 2001). Ulimbwende ni mawazo ya kimapinduzi ya kisanaa yaliyolenga kuzikana sheria za urasimi (Ntarangwi, 2004). Mawazo haya yaliwapa watunzi kibali cha kuandika kuhusu jamii zao na kuwasilisha mambo yote ambayo yasingeweza kuwasilishwa katika fasihi ya urasimi. Kwa mujibu wa Kaplan (1986) nadharia hii ilipigwa vita kwa madai kuwa iliendeleza ubinafsi na kutumia udhahania mwingi. Hivi ni kusema kwamba iliikosesha fasihi uhalisia na uyakinifu. Hata hivyo, athari za kilimbwende ziliendelea kubainika katika fasihi. Mifano ya waandishi wa riwaya za Kiafrika waliozingatia mtazamo wa ulimbwende ni pamoja na Shafi Adam Shafi katika riwaya ya *Kuli*, Mbunda Msokile katika *Usiku Utakapokwisha* na Shabaan Robert katika *Kufikirika* miongoni mwa wengine.

Mtazamo wa ulimbwende uliupisha umaumbo ambao ni mojawapo wa nadharia za kisasa. Umaumbo ulikuwa uasi dhidi ya ubepari. Ulivumbuliwa nchini Urusi mnamo 1880 na kuanza utumika katika miaka ya 1920. Mtazamo huu uliibuka nchini Urusi waasisi wake wakiwa Roman Jacobson, Viktor Shklovsky, Boris Eichenbaum na Jurin Tynyanov (Bertens, 2001). Mnamo mwaka 1917 wafanyakazi nchini Urusi walifanya mapinduzi dhidi ya ubepari. Mapinduzi haya yalichochewa na maandishi ya kikereketwa ya Karl Marx na Lenin. Waandishi katika kipindi cha umaumbo walizingatia dhana ya kutoa ukawaida wa kitu na kukipa mtazamo mpya. Wanamaumbo walisisitiza kuwa ukawaida wa kitu katika fasihi utolewe kwa kuzingatia matumizi mbalimbali ya lugha. Mtazamo huu unafanana kwa kiasi kikubwa na mtazamo wa usasaleo hasa pale ambapo lugha inayotumiwa na mwandishi yaweza kuwa na maana tofauti tofauti.

Althuser (1971), akiwarejelea wanaisimu mashuhuri ambao ni Derrida, Foucault, Lacan na Kristeva, anaeleza kwamba mtazamo wa umuundo-mpya ulitumia lugha kama nguzo maalumu ya uainishi wa mpangilio wa jamii, maisha ya jamii, nguvu na urazini wa kibinafsi. Dhima ya lugha katika jamii ni kujenga utambulisho, kutetea maarifa, na kutunza, kukuza na kuendeleza utamaduni wa jamii (Mazrui, 1988). Katika matumizi mbalimbali ya tamathali za lugha, maana za mpangilio wa jamii na matokeo yake ya kisiasa na kijamii hujengwa na pia kupingwa (Waliaula, 2013). Kupitia kwa lugha inayotumiwa katika fasihi, hisia na maana za kibinafsi

hujengwa. Lugha haielezi ubinafsi wa kipekee wa mtu bali hujenga ubinafsi wa mtu kwa njia zilizojengeka katika miundo ya jamii yake. Hivyo, lugha hutumiwa kama kijenzi cha jamii (Bholan & Gomez, 2008). Mintarafu ya maoni ya wataalamu lugha ni fani muhimu katika kazi ya fasihi kwa sababu imetumiwa katika riwaya teule za Wamitila kukuza mitindo mipya ya uandishi bunifu.

Baada ya umuundo-mpya mtazamo wa uumbuaji ulitumiwa kifasihi kuumbua na kuunda upya yaliyokuwepo. Mtazamo wa uumbuaji unashikilia kwamba maana katika kazi yoyote ile hukinzana. Kidhaniwacho ndicho sicho. Hii ni kwa sababu lugha huwa na vibadala. Lolote lisemwalo katika fasihi huwa na maana zaidi ya ile inayodhaniwa na kueleweka katika jamii. Katika fasihi yenye mtazamo wa uumbuaji ishara yaweza kuwa kiashiria au kiashiriwa. Hivyo, kazi za fasihi hutungwa ili zifasiriwe. Msomaji anafaa kujifasiria kwa njia anayoelewa yeye. Hii inapelekea kuzua maana nyingi ambazo huenda zikampelekea msomaji kushindwa kuielewa kazi husika na kwa hivyo kufanya makosa katika uamuzi.

Baada ya kipindi cha umuundo-mpya, riwaya ilianza kuandikwa kwa kuzingatia mtazamo wa utamaushi (Ntarangwi, 2004). Kwa mujibu wa Anderson (2000) mtazamo huu ulianza kama dhehebu lililoanzishwa na mwanafalsafa Kierkgaard wa Uholanzi katika miaka ya 1812-1815. Wafuasi wengine wake walikuwa Macquarrie, Marcel na Nietzsche. Dhehebu hili lilisambaa hadi Ufaransa na kisha likaenezwa ulimwenguni kote na Paul Sartre (Grimsley, 1960). Kwa mujibu wa utamaushi, mtu ni kiumbe cha pekee katika ulimwengu mbaya usiomjali (Manohar, 1984). Manohar anaendelea kufafanua kwamba binadamu ameachwa kujiamulia maisha na mwenendo wake hadi pale atakapokufa. Baada ya imani ya dhehebu la utamaushi kufahamika ulimwenguni, ilianza kutumika kama nadharia ya fasihi (Ntarangwi, 2004). Kwa mujibu wa utamaushi, binadamu ni kiumbe cha kutamausha kwa kuwa huja duniani bila hiari yake (Flynn, 2006). Kwa mujibu wa Macquarrie (1972) binadamu husukumwa duniani na nguvu fulani asizoweza kueleza. Kwa sababu hii binadamu hutamauka kwa kuwa dunia ni kitendawili ambacho hawezi kukitegua. Awapo ulimwenguni binadamu haelewi ni kwa sababu gani wanadamu wengine wana shida nyingi huku wengine wakiwa na raha nyingi (Manohar, 1984). Aidha, haelewi mchango wake duniani una faida gani. Isitoshe, hajui siku yake ya kuondoka duniani, namna alivyokuja bila kujua. Binadamu hubanwa na ulimwengu ambao uwe mbaya au mzuri kwake, ni lazima aendeleo kuishi humo. Inatamausha zaidi kujua kwamba iwapo

binadamu ataepuka dunia ni kupitia kifo tu, jambo ambalo linamtisha pia (Charlesworth, 1976). Katika utamaushi binadamu hufasiri dunia kwa mujibu wa shida zinazomkumba kama inavyoelezwa hapa chini;

“dunia ni ruwaza ya vizingiti vilivyo hai na visivyo hai ambavyo ni sharti mtu akabiliane navyo. Mathalan, mtu huwa kizingiti kwa mwenziwe. Hili hutokea wakati baadhi ya watu wanapojaribu kuwamiliki wenzao na kuwa madikteta” (Sartre, 1956, uk. 20)

Jamii pia yaweza kuwa kizingiti kwa binadamu (Flynn, 2006). Hili hutokea pale ambapo wanajamii huhitajika kufuata na kuzingatia kanuni nyingi. Hatimaye, utamaushi hubainisha kuwa binadamu hukumbana na vizingiti vingi na humbidi autafute uhuru wake (Manohar, 1984). Kwa mujibu wa utamaushi mbinu moja ya kujitafutia uhuru ni mapenzi. Hata hivyo, uhuru unaopatikana kwa mapenzi ni wa muda mfupi, ni mazigazi kabisa (Grimsley, 1960). Hii ni kwa sababu penzi linaweza kugeuka sumu na binadamu akazidi kutamauka. Macquarrie (1972) anasema kwamba mapenzi hutamausha kupitia swala la ngono ambapo mtu hujua asili yake. Uhuru pia hutafutwa kupitia teknolojia mathalan magari ya kupendeza, runinga, video, filamu na sanaa.

Anderson (2000) anaongeza kueleza kuwa binadamu lazima atafute mwenyewe uhuru kwa kujinusuru hata kama inabidi awaumize wengine. Uhuru huhusiana na kufungamana na kuamua, kutenda na kuwajibika. Pia, huhusu kuchagua baina ya wema na ubaya (Ervin, 2011). Hata hivyo, mintarafu ya utamaushi mwishowe binadamu hutamauka kwa sababu uhuru unaopatikana huwa ni wa muda mfupi tu. Hatua ya mwisho ya uhuru wa binadamu ni kifo katika kudura yake asiyoifahamu (Veatch & Ross, 2016). Wake anadai kuwa baada ya binadamu kushindwa kupata uhuru kamili duniani, kifo kinakuwa ni udhuru. Kifo humkumba binadamu yeyote na kumwacha hohe bila uzima. Ukweli ni kwamba kifo ni faradhi inayotamausha zaidi. Kifo humpa binadamu uhuru kutoka katika dunia mbovu yenye dhiki nyingi. Ni kinaya kwamba mtu harudi duniani baada ya kifo kuelezea hali ilivyo baada ya kufa. Kwa mujibu wa mtazamo huu fasihi inafaa kuyazingatia maisha ya mwanadamu anayeishi katika ulimwengu uliojaa dhiki, shida na matatizo mengi yanayosababishwa na binadamu mwenyewe. Matatizo haya yanamfanya binadamu kukata tamaa na kushuku uwepo wa Mungu (Macquarrie, 1972). Maoni haya yamekuwa msingi wa utafiti huu kwa kuuongoza kutambulisha na kufafanua jinsi shinikizo na changamoto tofauti tofauti za maisha zinavyoathiri uandishi wa kisasa. Vilevile, mtafiti ameutumia utafiti huu wa

awali kuonyesha jinsi mwanadamu anavyoishi katika dhiki na matatizo yaliyosababishwa na mwanadamu mwenzake. Vivyo hivyo, mwandishi wa kisasa anakumbana na dhiki na matatizo yanayosababishwa na watendakazi wenzake katika nyanda za utunzi kama vile wahariri na wachapishaji. Kwa waandishi wa kisasa uandishi wa kimajaribio umekuwa kama mbinu ya kujiliwaza.

Mtazamo wa Ufeministi uliufuata Utamaushi. Ufeministi ni dhana inayotokana na neno la kilatini “femina” lenye maana ya mwanamke. Ufeministi katika fasihi unahusu uwakilishaji wa haki za wanawake kufuatana na imani ya usawa wa kijinsia. Mbatiah (2001a) anaongeza kuwa ufeministi hujishughulisha na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ukandamizaji katika jamii yenye mfumo uliodhibitiwa na wanaume. Isitoshe, Ufeministi humwongoza mwanamke katika kupigania ukombozi wake kutokana na pingu za kitamaduni, kiuchumi, kidini, kijamii na kisiasa (Malenya, 2012). Ufeministi ulianza kukita mizizi ulimwenguni katika karne ya 19. Ulienea zaidi katika miaka ya sitini na sabini katika karne ya 20. Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), ufeministi uliibuka katika muungano wa ukombozi wa wanawake uliopamba moto katika miaka ya sitini kule Marekani. Wanawake walizungumzia matatizo yaliyowakumba kwa kuyaandika (Onyoni, 2012). Kwa mujibu wa maoni ya Onyoni inabainika kwamba fasihi inayotungwa itafaa zaidi ikiwa itatimiza malengo manne makuu ya ufeministi. Kwanza, kusawazisha wanadamu kijinsia, pili, kupigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu na wala si kiamumbile na kijadi, tatu, kukuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa na nne kuvumbua na kuziweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake na kupuuzwa kwa sababu ya kuwepo kwa utamaduni unaompendelea mwanamume.

Nadharia ya Usasa iliibuka punde tu baada ya Ufeministi. Usasa ulihusishwa na mabadiliko ya kisanaa yaliyotokea barani Uropa kati ya 1880 na 1930 (Habermas, 2015). Mabadiliko hayo yaitokana na ukweli kwamba hapo awali dini na siasa zilikuwa zimeteka fasihi bakunja hivi kwamba ilipendelea watu fulani huku ikibagua wengine. Kwa mujibu wa Berlin (1992) utanzu wa riwaya uliathirika kimuundo katika mabadiliko hayo ambapo wasanii walianza kuandika riwaya zisizofuata masharti ya utunzi ya kijadi. Mambo yaliyokuwa yakinyima watu maisha bora yalianza kuzingatiwa na kupigwa vita katika fasihi. Maswala ya haki na ukweli yalianza kupewa kipaumbele (Muller, 1979). Baada ya usasa, mtazamo wa usasaleo ulizaliwa. Usasaleo uliendeleza maoni ya usasa. Katika kipindi cha usasaleo mipaka iliyowekwa na utamaduni wa

kisasa ilianza kuvurugwa (Newman, 1984). Wafuasi wa usasaleo hudai kuwa maisha na watu si wataratibu kwa hivyo kazi za fasihi hazipaswi kuwa na utaratibu. Aidha, usasaleo unafungamana sana na utamaduni pendwa ambapo watu hufanya mambo namna wanavyotaka wenyewe bila kufuata kanuni zozote. Ni katika mazingira ya usasaleo ambamo Wamitila amendikia nyingi za kazi zake za kifasihi hususan riwaya.

## **2.7 Riwaya za Wamitila**

Mwandishi Wamitila alizaliwa mnamo 1966 mjini Machakos nchini Kenya. Ameandika tanzu mbalimbali za fasihi zikiwemo ushairi, tamthilia, hadithi fupi, hadithi za watoto na riwaya. Aidha, mwandishi ni mhakiki wa fasihi aliyechapisha makala mbalimbali katika majarida ya kiusomi Afrika, Ulaya na Marekani. Kama mwandishi wa riwaya, kufikia sasa ameandika zaidi ya riwaya kumi. Baadhi ya riwaya zake ni maendelezo ya riwaya nyingine. Kwa mfano, riwaya ya *Musaleo!* ni maendelezo ya riwaya ya *Bina-Adamu!* iliyochukua mwaka mmoja kuandikwa na ambayo hatima yake itakuwa *Pumzi za Kovu*. Katika riwaya yenyewe mwandishi aliendeleza maudhui yake kwa kutumia sitiari nyingi. Sitiari kuu katika riwaya ya *Binadamu!* ni matumizi ya kijiji kuangalia hali ya mataifa ya ulimwengu katika kipindi alichandikia. Katika kipindi husika, hali za kijamii, kisiasa na kiuchumi zimedhibitiwa na ubepari wa mataifa yaliyoendelea. Inaelezea mambo ambayo yanaendelea katika bara la Afrika lakini katika njia fiche iliyofumbwa sana. Kwa kuzingatia fani za lugha zilizotumiwa, riwaya ya *Bina-Adamu!* ni changamano (Njogu & Wafula, 2007). Kwa mujibu huu ni dhahiri kuwa riwaya ya kisasa inahitaji kusomwa kwa makini ili ieleweke. Hii ni kwa sababu imejaa maudhui na wahusika wengi ambao wanatumika kuchangia katika kujenga wazo kuu la riwaya husika. Maoni ya Njogu na Wafula yameufaa utafiti huu kwa kuweka msingi kuhusu uchangamano uliopo katika uandishi bunifu wa Wamitila.

Akimjibu Lutz Diegner katika mahojiano ya moja kwa moja yaliyofanyika mnamo 3/11/2004 kuhusu uandishi wake kwa njia ya baruapepe, Wamitila anasema kwamba alipata msukumo wa kuandika riwaya ya *Bina-Adamu!* baada ya kusoma riwaya ya *Pedro Paramo* ya Juan Rulfo. Diegner aliwahi kuitaja riwaya ya *Bina-Adamu!* kuwa ni riwaya ngumu ingawa mwandishi mwenyewe hakukubaliana naye. Kwa mujibu wa haya ni bayana kwamba uandishi wa Wamitila ni tofauti na uandishi uliozoeleka. Upekee huo ndio uliouchoea utafiti huu. Mintarafu ya haya utafiti huu ulitambulisha sifa bainifu za mbinu za kiuandishi za kimajaribio zinazozua utofauti katika uandishi bunifu wa Wamitila kama mwandishi mmojawapo wa riwaya za kisasa.



Riwaya ya *Musaleo!* ya Wamitila (2004) inajumuisha simulizi inayoenda mbele na nyuma, iliyofichama hadithi mbili tofauti na umazingaombwe usioweza kutabirika (Mwamzandi, 2013:50). Mwamzandi anaendelea kudai kuwa hadithi hii humsukuma msomaji mbele na nyuma na mwingilianomatini uliokithiri na unaohitaji umakinifu ili msomaji apate kuelewa fikra, mbinu, njama, vitimbi na hila wanazotumia wakoloni mamboleo katika kuwazuga wale wanaosimama kidete kuzitetea haki katika jamii. Uhalisia-mazingaombwe na urejeleomatini ni vipengele mojawapo muhimu katika utunzi wa riwaya za kimajaribio. Utafiti wa Mwamzandi haukuleza jinsi uhalisia-mazingaombwe unavyoakisi jamii ya mwandishi wala kufafanua aina mahususi za matini zinazotumiwa katika uandishi Wamitila. Utafiti huu ulijaza pengo hili la kiusomi kwa kutambua na kufafanua matini mbalimbali zilizorejelewa katika riwaya ya *Musaleo!* na riwaya nyingine zilizoteuliwa katika utafiti huu. Vilevile, utafiti huu ulitambulisha vipengele vingine vya kimajaribio kama vilivyojitokeza katika riwaya teule za Wamitila.

Rettova (2016) akirejelea riwaya za *Bina-Adamu!* na *Musaleo!* anamtaja Wamitila kama mwandishi wa “riwaya mpya” au “riwaya ya majaribio” katika lugha ya Kiswahili. Kama watafiti waliotajwa awali, Rettova ameeleza kwamba riwaya hizi mbili za Wamitila zimeandikwa kwa kuuegemea mtindo wa usasaleo au usasa-baadaye. Rettova (2016) anaendelea kueleza kuwa katika riwaya zake mpya, Wamitila anawasilisha maswala ya ndani na ya faragha kupitia kwa matumizi ya hatua nyingi. Hivyo, mtafiti Rettova amezitambulisha riwaya husika kama riwaya-hasi au riwaya zenye mwelekeo wa kupinga. Hata hivyo, Rettova hakutoa maelezo kuhusu vipengele vya kimajaribio vinavyotumika katika uandishi wa riwaya hizi. Utafiti huu uliweka bayana vipengele vya kimajaribio na jinsi vilivyotumika kuendeleza maudhui katika riwaya teule za Wamitila.

## **2.8 Muhtasari wa Riwaya Teule**

Sehemu hii inaeleza kwa ufupi msuko na ploti za riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu. Japo masimulizi katika riwaya zilizoteuliwa ni changamano na yenye uradidi mwingi, mtafiti amerejelea mfuatano wa vitushi vinavyoisukuma hadithi kutoka mwanzo hadi mwisho.

### **2.8.1 Riwaya ya Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji**

Riwaya hii inawazungukia wahusika wakuu watatu yaani Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji. Mwandishi ameikamilisha riwaya yake na yuko tayari kuichapisha. Kabla ya kuchapishwa

kwake, riwaya inahitajika kuhaririwa na kisha idhini ya kuchapishwa kwake itolewe. Tatizo linatokea ambapo baada ya kuisoma msomaji anashindwa kuielewa na hivyo kupendekeza kwa mchapishaji kwamba haingeweza kuchapishika kwani haikuwa ya kawaida. Kauli ya mwisho inapotolewa kwamba riwaya hiyo haingeweza kuchapishika, Mchapishaji pamoja na Msomaji wanamwalika mwandishi katika afisi ya Mchapishaji ili aisome na kuieleza riwaya yake mwenyewe. Mwandishi anaitikia wito huo na kufika afisini mwa Mchapishaji ili kuijadili hadithi yake. Humo ndani Mwandishi anasimulia kuhusu jamii yake inayoshuhudia mabadiliko makubwa. Wakulima hawavuni kama zamani. Baadhi yao wameyapoteza mashamba yao na wanaishi kwenye mahema. Mito imekauka. Misituni miti imekatwa. Anayeikata hajulikani. Watu hawadhibitiki tena. Washirika wa kimaendeleo nao wamechacha. Serikali haijui ifanye nini. Mwandishi anasimulia kwa mapana na marefu kuhusu utofauti wa uandishi wa kijadi na kazi za kisasa. Anabainisaha kuwa kuna tofauti za kisimulizi, uwasilishaji wa maudhui na usawiri wa wahusika miongoni mwa maswala mengine. Isitoshe, ametoa masimulizi yanayohusiana na changamoto wanazokumbana nazo waandishi wa riwaya za kisasa mikononi mwa wahariri na wachapishaji. Kuna mjadala mrefu baina ya Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji usiojulikana mwisho wala athari zake. haijulikani iwapo hadithi ya mwandishi itachapishwa au la.

### **2.8.2 Riwaya ya *Musaleo!***

Riwaya ya *Musaleo!* inahusu hadithi ya mtu mmoja kwa jina Mugogo Wehu ambaye ni mhadumu wa ombaomba anayejaribu kufumbua kitendawili kisichoweza kufumbuliwa. Riwaya hii imebeba masimulizi ya riwaya mbili ambayo yanatolewa kwa wakati mmoja. Moja inasimuliwa na mwandishi na nyingine inasimuliwa na kiongozi wa nchi kwa jina Kingunge au Mzee ambaye anapambana na kipindi asichokifahamu. Riwaya ya *Musaleo!* ni maendeleo ya riwaya ya awali ya Wamitila inayofahamika kama *Bina-Adamu!* Muktdaha wa hadithi hii ni pindi tu baada ya nchi za Kiafrika kujinyakulia uhuru. Mwandishi anazingatia matatizo na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo Waafrika katika ujenzi mpya wa nchi zao changa.

Katika riwaya mwandishi anaangazia maswala ya serikali dhalimu za Kiafrika kwa njia ya kejeli na dhihaka. Mwandishi anabaini jinsi baada ya kuingia Afrika Wazungu wakoloni walivyokuwa mbioni kuwaandalia makazi wenzao ambao baadaye walianza kufurika barani kama nzige. Ili kuwateka wenyeji, wakoloni walitumia mbinu mbalimbali kama elimu yenye uigaji wa kikasuku, dini, na vishawishi vingine kama vile nguo, pipi na ahadi za ulinzi dhidi ya maadui wao.

Baadaye Waafrika walifanikiwa kupata uhuru kutokana na ukoloni. Kinaya ni kwamba viongozi waliokabidhiwa majukumu ya uongozi walianza kuwatesa na kuwadhulumu wenyeji wenzao. Walijilimbikizia mali wakawa makabaila na mabepari.

Katika muktadha huu Kingunge anaamua kuandika hadithi yake ambayo itajisoma yenyewe. Itaitwa *Musaleo!* Maana ya *Musaleo!* ni Musa wa leo. Kama alivyokuwa Musa wa Biblia aliyewakomboa Waisraeli kutoka utumwani Misri, Musaleo atakuwa mkombozi wa leo atakayewakomboa wenyeji (Waafrika) kutokana na dhuluma na mateso ya viongozi. Inaaminika katika riwaya kuwa huyu Musaleo ana sifa nyingi: baadhi ya sifa hizi ni kwamba, yeye ni shujaa, kila kitu, akiondoka utamlilia, mwenye uwezo, mkombozi mwenye uwezo wa kuona kila kitu.

Riwaya inapoanza, upepo mkali unavuma na kuangusha matawi ya mti yaliyokwaruza paa moja na kutoa sauti ya kuchukiza masikio. Chini ya mti wa Mgunga palikuwa na watoto wengi waliokuwa wakijifunza kuvuta bangi huku wakicheza kwa msisimko mkubwa. Huu mchezo ulifuatwa na vicheko vilivyojaa nguvu na matumaini. Mara watoto wanapoendelea na mchezo wao wanashtuliwa na mlipuko wa bunduki. Kingunge hakumbuki sura wala umri wake alipolazimika kuondoka kijijini pao kwa sababu ya tatizo la njaa ila anakumbuka kuwa wanakijiji walimfahamu kama “Kizee.” Pia iliaminika kijijini kuwa alizaliwa na sifa za kishujaa kama vile kuzaliwa mapacha yeye na dada yake na kutoka tumboni huku amekunjia mbegu za kuwangia kiganjani. Siku chache baadaye watu walipoamka walikuta mbegu nyingine nje akapewa kisha akafumbia kiganjani. Akapewa jina jingine, Fumbia Kiganjani. Meno yake yaliotea tumboni, alikuwa mwenye kichwa kinene ajabu, masikio makubwa na uwezo wa kunusa kila kitu. Aliporudi kijijini baadaye alikuwa mganga. Alikaribishwa vyema na wenyeji. Aliporudi, Mzee alikuta idadi ya watu kijijini ilikuwa imeongezeka. Watu walizaana kwa utiifu wa mzazi wao wa kwanza Yunga Mwamba. Kijiji kilishabihiana na nchi au hata bara kama walivyosema wenyeji. Kulikuwa na matatizo mengi kijijini na nchini kwa jumla. Baadhi ya tatizo sugu lililodhihirika lilikuwa ukosefu wa usalama. Wananchi walipolalamikia hali hii viongozi walipuuza kwa kejeli zilizokithiri. Badala ya kuwatumia askari kuimarisha usalama wa wananchi, viongozi waliwatumia kuwatia hofu na kuwanyamazisha wale waliopinga mfumo na sera za serikali. Askari waliua bila kufikiria mradi tu walipokea amri kutoka kwa wakubwa wao.

Kingunge aliendelea kuandika hadithi yake. Katika hadithi yake hiyo anachukua hatua ya kwanza ya kukubali jina lake jipya, yaani Mzee! Tofauti na wengine yeye ametandaridhika na kwa hivyo hana budi kuyakubali mabadiliko yanapofika. Lugha alikuwa nayo, alichohitajika kufanya ni kulainisha msamiati tu. Mzee alitungiwa tenzi za wasifu huku wengine wakimghania sifo, wachache wakicheza ngoma na kumgeuza kuwa kipokeo. Alipata sifa nyingine kwa njia ya jina jipya, *Mzee Mvumbua Usomi*. Wenyeji walianza kuwa waoga wa kusema lolote lile dhahiri. Mzee aliamrisha kuwa hakuna shughuli ambayo ingeweza kufanyika bila idhini yake kwani idhini ya kila kitu ilikuwa yake. Mzee pia alichukua hatua muhimu ya kupenya katika kila upembe na kuhakikisha anatambuliwa na kila mtu. Aliyatembelea maeneo mbalimbali katika nchi nzima. Hii ilikuwa hatua muhimu ya kuuweka msingi wa woga. Popote alipozuru hali ikawa “Mzee, anakuja! Mzee yu njiani, sasa hivi anafika!” Zamda mkewe Mzee, alishangazwa na mabadiliko aliyoyaonyesha mumewe kwa kipindi cha miaka iliyokaribia kumi na mitano. Alimwona kama aliyepagawa. Ili kulinda utawala wake, Mzee alijiundia kikosi cha vijana kilichofahamika kama “vijana wa Mzee.” Licha ya umri wao wa juu waliridhika kuitwa vijana. Walikuwa walinda usalama wa Mzee. Walikuwa tayari hata kumfia.

Mzee alikutana na wazee wakongwe, waliochongwa na ala za maisha ya dhiki baada ya kufaulu kupigania uhuru wa nchi. Walifahamika kama *War veterans*. Waliahidiwa mengi kama mashamba, nishani pamoja na kujengewa minara katika uwanja wa uhuru na majina yao kuigizwa katika orodha ya waandika historia lakini bado walikuwa katika hali ya kusubiri. Mzee anawalaumu waliotangulia kwa kutotambua nafasi ya wazee muhimu kama hawa. Wakati huo huo mkoloni anarejea kwa mara ya pili na kukuta hali mbaya barani Afrika. Barabara ya kuelekea sehemu ya ‘*Government Quarters*’ ilikuwa na mashimo mengi ajabu. Enzi ya wakoloni, barabara hizi zilikuwa za kuvutia sana. Watu wengi wamehamia mijini kutoka mashambani, hali ambayo imeathiri huduma nyingi za miji. Kwa sababu hii, wakazi wa mijini wanahimizwa mara nyingi warudi mashambani kutarazaki.

Mhusika mpya Ngwena anajitokeza kama mwalimu na mtaalamu wa historia mwenye kipawa cha kuchunguza historia. Aidha alikuwa mwenye utaribu katika uandishi wa matokeo ya utafiti. Ngwena alifanya kazi katika chuo kikuu cha pekee nchini kisha akaachishwa kazi kwa madai kuwa alipoteza karatasi za wanafunzi za mitihani. Baada ya kutoka chuoni, aliamua kuanzisha maktaba yake ya kibinalsi na kuendeleza utafiti wake katika Maktaaba Kuu. Ngwena pia alifanya

utafiti kuhusiana na historia ya nchi hii kuanzia ukoloni hadi hivi leo. Utafiti wake wa mwisho ulihusu watoto wa mitaani. Kabla ya ripoti yake kutolewa, alienda uhamishoni katika nchi nyingine.

Mabadiliko mengine yaliyojitokeza ni kwamba watu wengi waliacha kuhudhuria hekalu. Ilikuwa nadra sana kuwaona watu wakiingia makanisani. Wachache walioingia walikuwa wanafiki tu, waliodai sadaka kutoka kwa waumini na kuwahidi miujiza ya urongo. Wakati huo huo wafanyabiashara wa Kiasia walipata umaarufu mkubwa kwa sababu ya kuwa na uhusiano wa karibu na wanasiasa. Ukweli unakosa maana kwani watu wanaotunukiwa majukumu makubwa katika jamii, kama vile viongozi, wanasiasa, watu wa kawaida, wafanyakazi, wote wanageuka kuwa wezi. Jambo hili linawavunja moyo raia na kuathiri hamu ya kufanya kazi. Wote wanatamauka katika kutekeleza wajibu wao. Kiongozi mpya naye aliendeleza bwembwe zake. Alisisitiza kuwa ni sharti watoto waliokuwa wakizaliwa wakati huo wafundishwe nyimbo mpya. Aliziteka nyara hisia zao kupitia ubadilishaji wa maneno ya kimsingi ya lugha. Kwa mfano, maana ya neno ya “uhuru” ikawa “kufuru” nao uzalendo ukawa “uvundo”. Hali hii ikapigiwa chuku kwamba Mzee alipatwa na tatizo la masikio ghafla. Isitoshe, uwezo na nguvu za kikoloni alizopokea zilizidi kumjaa na kumfanya ayaseme maneno ya ajabu, kama: “Sasa kuanzia leo, na wala si kuanzia leo ni tangu zama na azali, kuna MIMI na WENGINE tu. Mimi ndimi msingi wa kila kitu. Mimi sio kama nyie!”

Suala jingine lililokuwa tatizo baya ni lile la ardhi au mashamba. Ardhi ya Waafrika ilitwaliwa na wakoloni kwa manufaa ya kilimo chao pekee. Kwa kutumia ujanja, wakoloni walichukua ardhi yote iliyokuwa na rutuba. Walijichukulia pamaoja na jamaa zao ambao tayari walikuwa wameshafurika barani. Wenyeji walilazimika kuishi pahali pamoja, aghalabu palipokuwa pakavu. Utamadauni wao wa kuhamahama ulifikia kikomo. Aidha, katika mashamba ya wakoloni kazi za sulubu zilifanywa na Waafrika.

### **2.8.3 Riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi***

Katika sehemu hii nitawasiilisha ploti ya riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* kwa ufupi. Mhusika mkuu katika riwaya hii Yosi Kanga amekuwa na kazi nzuri na maisha mazuri. Hata hivyo, siku moja hali ilimbadilikia punde tu aliposherehekea miaka thelathini na mitano tangu azaliwe. Yosi Kanga alitoka ofisini saa saba kwa mapumziko ya mchana. Alijilaza katika bustani

kisha usingizi ukambeba. Aliota ndoto akiwa hatarini kisha msichana wa mbalamwezi akamwoko. Aliekea kujipa chakula cha mchana katika hoteli moja iliyokuwa karibu na makao makuu ya shirika la reli, *Kenya Railways*. Baada ya chamcha anaanguka ghafla na kuugua. Alipelekwa *City Breeze Hospital* na kulazwa mle.

Daktari alisema kwamba Yosi Kanga alikuwa na uvimbe kichwani na kwa sababu hiyo alikuwa na muda mfupi wa kuishi. Huduma mle hospitalini hazikuwa nzuri. Madaktari na baadhi ya wafanyikazi waliwadhulumu wagonjwa. Wengi wa wagonjwa hao walifariki kwa njia ambazo hazikueleweka. Baadaye daktari mwanamke alimtembelea. Mara alipomwona, Yosi alipatwa na hisia fulani. Alijaribu kukumbuka alikokuwa amemwona yule daktari. Daktari alimjulua hali na baada ya mazungumzo mafupi aliamua kumpasulia mbarika. Uchunguzi na “*scan zote za ECG reports*” zilionesha kuwa Yosi alikuwa buheri wa afya. Daktari alimwagiza ajitayarisha kuondoka mle hospitalini. Yosi alifurahi sana kwa kuwa ile “hukumu ya kifo” aliyopewa mle hospitalini ilifutiliwa mbali. Kumbe huyu ndiye aliyekuwa mwokozi wake, Msichana wa Mbalamwezi.

## **2.9 Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya usasaleo. Nadharia hii iliibuka na kuasisiwa katika Karne ya Ishirini ikihusishwa na wanafilosofia Nietzsche, Heidegger, Derrida, Lyotard miongoni mwa wengine. Wataalamu wengine waliotoa michango yao kwa nadharia ya usasaleo ni pamoja na Habermas (1987) ambaye anasisitiza kwamba ulimwengu wa sasa unajiegemeza zaidi kwenye maswala ya usasaleo. Habermas anazidi kufafanua kuwa shughuli zote zinazohusiana na binadamu wa sasa zinamulikwa na fasihi kwa njia ya simulizi nyingi. Mfafanuzi wa hivi majuzi wa nadharia hii ni Jameson (1991). Utafiti huu ulijiegemeza zaidi kwa maoni ya nadharia hii kama yanavyoelezwa na Baudrillard (1988), Habermas (1987), Jameson (1991) na Lyotard (1984).

### **2.9.1 Nadharia ya Usasaleo**

Selden *et al.* (2005) wanaeleza kuwa usasaleo ni dhana pana na tata inayozua mijadala mingi baina ya wahakiki hasa katika kipindi kati ya miaka ya 1980–1990. Wengi wa wahakiki hao wanauona usasaleo kama maendeleo ya usasa ingawa ni dhana pana kuliko usasa. Pia, usasaleo unahusu hali ya kijumla ya binadamu na jamii yake. Isitoshe, usasaleo una mwelekeo wa

kuyahusisha maisha, utamaduni, sanaa na itikadi katika kuiangaza hali ya binadamu. Inabainika kwamba Usasaleo unamulika jinsi jamii ilivyo katika kipindi mahususi cha kihistoria.

Usasaleo ulitumiwa katika utafiti huu kutambua na kufafanua sifa bainifu za uandishi wa kimajaribio katika uwasilishaji wa maudhui na dhamira, tanzu za fasihi, dhana na mitindo ya kifasihi inayohusishwa na miongo ya kwanza ya Karne ya Ishirini yaani baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Ulimwengu (Abrams, 1993). Abrams anaendelea kusisitiza kuwa sifa zinazorejelewa hutofautiana kutegemea wahakiki husika. Katika uhakiki wake, Wamitila (2007) anasema;

“Licha ya tofauti hizo, wahakiki wengi wanakubaliana kuwa msingi wa sifa za Usasaleo ni kujitenga na misingi ya jadi ya sanaa na utamaduni wa Kimagharibi au ule uliokuwako”(uk. 48)

Kwa mujibu wa maoni ya Wana-Usasaleo, ni bayana kwamba nadharia hii ilijitenga kabisa na taratibu za utunzi zilizofuatwa kabla ya Karne ya Ishirini.

### **2.9.2 Mihimili ya Usasaleo**

Nadharia ya usasaleo ni uwanda mpana na wenye vipengele vingi pamoja na waasisi wengi. Utafiti huu ulizingatia matumizi ya nadharia hii kwa kuangazia mitazamo ya wataalamu mahususi walioteuliwa kwa minajili ya kuyatosheleza mahitaji ya utafiti. Mitazamo ya Baudrillard (1988), Habermas (1987), Jameson (1991) na Lyotard (1984) imehusishwa.

Lyotard (1984) anashikilia nadharia tete kwamba ufahamu wa wanajamii umebadilishwa pakubwa na mabadiliko ya kipindi cha maendeleo ya viwanda. Hali hii imepelekea jamii kubadilisha tamaduni zake na kukumbatia tamaduni za kiusasaleo. Kwa kuwa kipindi cha usasaleo kilivuruga mipaka iliowekwa na utamaduni wa jadi, mambo mbalimbali yanayomilikiwa na jamii yalibadilika ikiwemo fasihi. Lyotard anashikilia kuwa maisha na watu si wataratibu na kwa hivyo kazi za fasihi hazifai kuwa na utaratibu wowote. Usasaleo unafungamana sana na utamaduni pendwa ambapo watu hufanya mambo namna wanavyotaka wenyewe bila kufuata kanuni zozote (Jameson, 1991). Kwa mujibu wa Usasaleo, utamaduni pendwa huwa unaigwa kwanza katika mataifa ya magharibi yaliyoendelea hasa Marekani kisha kusambaa katika mataifa mengine. Utamaduni huo unahusisha sana vijana ambao hudai kuwa

wanakerwa na utamaduni wa kale wanaouhusisha na uzee. Mawazo haya yaliweka msingi wa kuchanganua mabadiliko yanayohusiana na utunzi wa kimajaribio katika riwaya teule za Wamitila.

Utamaduni pendwa ambao ni mhimili mkuu wa usasaleo unaambatana na fasihi pendwa. Sifa moja maarufu katika fasihi pendwa ni “mkondo wa ung’amuzi” ambao ni mbinu ya kisimulizi katika uandishi wa kinathari inayotumia maelezo marefu yanayoyamulika mawazo yanayompitikia mhusika akilini (Wamitila, 2006). Kwa mbinu hii mawazo ya ndani aliyonayo mhusika huwasilishwa kwa mapana na marefu. Wamitila anaipa mbinu hii jina la ‘uzungumzinafsi wa ndani’. Lugha ni kifaa muhimu katika uandishi wa kazi za fasihi. Carter (2006) akimnukuu Lyotard anafafanua kwamba usasaleo hukiuka kaida na kanuni zote za utunzi. Kanuni anazorejelea Carter zaweza kuwa za kimuundo na za kilugha. Hivi ni kusema kwamba pamoja na fasihi pendwa, usasaleo huambatana na uigizaji pendwa. Haya ni matumizi ya lugha kwa njia huru sana bila kuzingatia ufasaha na usanifu wake. Pia huhusu kuchanganya lugha mbalimbali kwa mfano Kiingereza na Kiswahili au lugha za kwanza na Kiswahili au hata lugha nyingine ngeni. Uigizaji huu hufanyika popote na haufuati maudhui au utaratibu uliozoeleka. Aghalabu, lengo lake huwa ni kuburudisha jamii na kuielimisha jamii. Uigizaji pendwa hutumia lugha pendwa. Dhana hii ilielekeza utafiti huu katika uchanganuzi wa maswala mahususi ya matumizi ya mbalimbali ya lugha hasa uchanganyaji, uhamishaji ndimi pamoja na matumizi ya tamathali nyingi za semi kwa wakati mmoja katika riwaya teule za Wamitila.

Wamitila (2010b) anadai kuwa usasaleo huchangamkia kukatizwa kwa mkondo wa kisimulizi na upuuzwaji wa kaida na kanuni za kimsingi ambao hujitokeza katika usawiri wa wahusika, muundo wa msuko, matumizi ya mandhari tofauti tofauti na udhihirishaji na uendelezaji wa wahusika. Inawezekana kwamba mbinu na mabadiliko haya ndiyo yaliyompelekea Mwamzandi (2013) kuutaja utunzi wa riwaya mpya kama utunzi uliojawa na mbinu za kimajaribio. Kwa msingi wa maoni haya, utafiti huu ulibainisha kwamba licha ya kuukatiza usimulizi kupitia kwa fani za fasihi zilizotajwa, mwandishi ameafikia malengo yake ya utunzi katika riwaya teule. Ameweza kuwasilisha maswala muhimu yanayoikumba jamii ya leo japo kwa njia changamano.

Kulingana na Lyotard (1997), Usasaleo unaegemea matumizi ya falsafa katika utunzi na matumizi ya simulizi nyingi ndogo ndogo katika hadithi au riwaya kuu. Mtazamo huu



uliuongoza utafiti katika kutambulisha, kufafanua na kuchanganua mbinu hizi mpya kama vifaa vya kuwasilisha dhamira na maudhui. Aidha, mtazamo huu ulitumiwa kuthibitisha kuwa riwaya za kisasa zimetamalaki takriri na mawazo yaliyokiuka mipaka ya uhalisia. Hivyo, maswala mbalimbali ya kifalsafa yaliyorejelewa na mwandishi husika katika ubunifu wake yaliangaziwa na kutathminiwa.

Baudrillard (1988) anashikilia kwamba jinsi maisha ya kisasa yanavyokosa utaratibu ndivyo fasihi ya kisasa ilivyo. Hata ingawa hali ya ukosefu wa utaratibu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali waweza kuonekana kana kwamba haufai, Baudrillard anasema kwamba, unajitosheleza na kutofaa huko ndiko maisha ya kisasa. Isitoshe, Baudrillard anaendelea kudokeza kwamba fasihi inapaswa kumulika jamii jinsi ilivyo, bila kufuata utaratibu maalum kwa kuwa jamii imejaa fantasia za namna mbalimbali. Tanzu za fasihi hasa riwaya zafaa kuwa na simulizi ndogo ndogo ndani yake badala ya hadithi moja ndefu iliyoandikwa kwa njia ya uhalisia kwa sababu hata jamii ya sasa yenyewe ambayo ndiyo inayoangaziwa na riwaya husika haina utaratibu wa kihalisia. Mtazamo huu uliuelekeza utafiti katika uchambuzi na uchanganuzi wa simulizi ndogo ndogo zinazorejelea maswala na matini tofauti tofauti zilizotumika katika riwaya teule za Wamitila na jinsi simulizi hizo zilivyotumika kuwasilisha maudhui na kuimulika jamii ya sasa.

Kwa mujibu wa wataalamu wa nadharia ya usasaleo ni bayana kuwa mtendakazi yeyote yule ana uhuru wa kujaribu mbinu mpya za kutekeleza kazi yake bila kujibana na kujikita katika sheria za jadi. Hivyo basi mtunzi wa kazi za fasihi ana uhuru wa kujaribu mbinu mpya za utunzi bila kubanwa na mbinu za kijadi ambazo zinajiegemeza katika msingi wa uhalisia. Wanausasaleo wana uhuru wa kutumia mbinu za kisasa za utunzi ambazo hazifuati taratibu maalum. Kwa misingi ya maelezo haya ya waasisi wa Usasaleo mihimili ya usasaleo ifuatayo iliungoza utafiti huu katika ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data:

- i. Riwaya ya kimajaribio haiwezi kuwa na mpangilio wa moja kwa moja kuanzia mwanzo hadi mwisho bali inatawaliwa na kuwepo kwa vipande vidogo vidogo vya vihadithi vifupifupi ndani ya usimulizi mkuu (Lyotard, 1984). Mintarafu ya haya, kuna uchanganuzi mpana katika ploti na usimulizi kwa jumla kwa sababu usimulizi wa moja kwa moja haufuatwi. Bunilizi nyingi fupifupi ndani ya bunilizi kuu huudhihirisha ulimwengu kwa njia isiyofuata maagizo ya kijadi, jambo ambalo wasanii wa usasaleo

wanalitaja kama uhalisia wa kweli. Utafiti huu uliongozwa na mhimili huu kuonyesha na kujadili aina mbalimbali za vipande vya hadithi vilivyomo katika riwaya teule na jinsi mwandishi anavyovitumia katika uwasilishaji wa ujumbe na uchoraji wa taswira ya jamii ya leo katika riwaya zake za kisasa;

- ii. Maana, maadili na ukweli hupatikana bila kuegemea mbinu au upande mmoja kwa sababu chanzo chake haswa ni jamii. Mhimili huu ulitoa mwanga kwamba fasihi yoyote iwe ya kijadi au ya kimajaribio ni kioo cha jamii. Huitoa taswira kamili ya jinsi jamii ilivyo. Haya yaliibuka baada ya uchanganuzi wa kina kuhusu mbinu mbalimbali za kiuandishi za kimajaribio zilizotumika kama zilivyotumiwa katika riwaya teule. Maelezo yametolewa kuhusu jinsi mwandishi Wamitila alivyofanikiwa katika kuwasilisha ujumbe wake akijikita katika mbinu za kimajaribio. Aidha, mhimili huu uliongoza shughuli nzima ya utambuzi na ufafanuzi wa maana mbalimbali zilizojificha katika vipande vingi vya hadithi vilivyomo katika riwaya teule za Wamitila; na
- iii. Kitambulisho cha utamaduni wa jamii huundwa kwa nguvu za lugha kwani lugha hiyo hutambulisha jinsi jamii inavyowaza. Riwaya mpya zimetumia tamathali nyingi za lugha katika utunzi wake. Baadhi ya tamathali zilizotumika ni kama vile methali, tashbihi, tashihisi na semi. Ndanimwe mmejificha mambo muhimu ya kijamii. Kwa mujibu wa mhimili huu utafiti huu ulichanganua jinsi tamathali za semi na lugha kwa jumla zilivyotumika kama kitambulisho kamili cha jamii ya sasa.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura hii mtafiti ameangazia na kueleza mbinu zilizotumiwa katika utafiti. Aidha, mtafiti ametambulisha muundo wa utafiti na kufafanua jinsi sampuli ya utafiti ilivyoteuliwa. Maelezo kuhusu mbinu zilizotumiwa katika ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya mbinu za kimajaribio yamefanywa. Sifa bainifu za mbinu za kimajaribio kama zilivyojitokeza katika riwaya teule zimetambulishwa kwa minajili ya kufafanuliwa, kuchanganuliwa na kufasiriwa. Aidha, sehemu hii imetoa muhtasari wa riwaya zilizotafitiwa.

#### **3.2 Muundo wa Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa wa kithamano uliojiegemeza katika mkabala wa kifasili. Matokeo yalitolewa kwa njia ya kimaelezo kwa kuwa data iliyotumika haikuwa ya kitakwimu. Kwa mujibu wa Creswell (2009) katika Maree (2012) data isiyo ya kitakwimu huelezwa kwa maneno. Kwa kuzingatia udurusu wa yaliyomo, mtafiti alitambulisha mbinu mbalimbali za kimajaribio alizotumia mwandishi wa riwaya teule kuwasilishia ujumbe wake kwa jamii. Kwa kuwa utafiti huu ulihusu jinsi mitindo ya kimajaribio katika fasihi ya kisasa inavyowasilisha maudhui yanayoiakisi jamii husika, sifa za mbinu zilizotumika zimejitokeza katika fani za kiutunzi kama vile usimulizi, lugha, wahusika, muundo na hali kadhalika msuko wa kazi husika (Neuendorf, 2002).

#### **3.3 Uteuzi wa Sampuli**

Mwandishi Kyallo Wadi Wamitila ameandika tanzu nyingi za fasihi ila utanzu wake wa riwaya za kimajaribio umeteuliwa kwa lengo la kuwakilisha riwaya za kisasa (Dalen, 1979). Mtafiti ametumia kundi hili dogo ili kupata data ya kumsaidia kufanya hitimisho lake kuhusu uandishi wa kimajaribio kwa jumla (Kothari, 2004). Si kwamba Kyallo Wadi Wamitilla ndiye mwandishi wa kimajaribio peke yake ila ameteuliwa kama kiwakilishi cha idadi kubwa ya waandishi wengine wa kimajaribio. Vile vile, riwaya tatu za mwandishi zilizohusishwa zilichaguliwa kwa njia ya kimakusudi. Sifa zilizoongoza uteuzi wa riwaya ni ujidhihirishaji wa uandishi wa kimajaribio ambao sifa yake kuu ni ukatizwaji wa masimulizi. Kwa mujibu wa Field (2005) sehemu ndogo ya idadi lengwa inapochaguliwa hufanyika kuwa kiwakilishi tosha katika zoezi la ukusanyaji na uchanganuzi wa data kutoka kwa jamii pana. Kama ilivyotajwa awali, si riwaya

hizi pekee zilizo na sifa za kimajaribio bali zimeteuliwa kuwakilisha kundi zima la riwaya za kimajaribio kama wanavyodokeza Mugenda na Mugenda (2003) kwamba;

Hamna sampuli inayoweza kuwa bora zaidi kuliko nyingine (tafsiri yangu).

Uteuzi wa sampuli vilevile uliwiana na hali kwamba ziliandikwa na kuchapishwa katika Karne ya Ishirini na Moja, kipindi muhimu katika uandishi wa kimajaribi. Kwa kuzingatia sifa hizi riwaya za *Musaleo!* (2004), *Msichana wa Mbalamwezi* (2011) na *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* (2014) ziliteuliwa kwa minajili ya kufanyiwa uchanganuzi.

### **3.4 Mbinu za Ukusanyaji wa Data**

Utafiti huu ulifumwa kimaeezo. Kwa minajili ya kutambulisha, kuhoji na kujadili mbinu za kiuandishi za kimajaribio zilizotumika. Mtafiti alisoma riwaya teule kwa umakini. Data ilihusu matini kutoka kwa riwaya teule zenye fani za kisanaa na kunga za kiutunzi kama zilivyodhihirika katika matini teule. Fani za kisanaa kama vile lugha, wahusika, maudhui na usimulizi zilidondolewa na kuchanganuliwa ili kubainisha na kujadili kunga za mbinu za kiuandishi za kimajaribio anazotumia mwandishi Wamitila katika riwaya zake za kisasa. Sifa tofauti tofauti za kimajaribio zilibainika. Hali mbali mbali zilizojitokeza zilifafanuliwa. Aidha, mtafiti alichanganua fani za muundo na msuko katika riwaya husika. Nadharia ya usasaleo ilitumika katika uchanganuzi wa data kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti.

#### **3.4.1 Mpango Maalum wa Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data**


Sehemu hii inatoa maelezo kuhusu jinsi data katika utafiti huu ilivyokusanywa na kuchanganuliwa kwa minajili ya kutolea maelezo. Hatua nne zifuatazo ziliufaa utafiti. Kwanza, mtafiti alisoma riwaya teule na kudurusu yaliyomo kwa lengo la kutambulisha matini mbalimbali za kimajaribio zilizotumiwa na mwandishi katika riwaya teule. Pili, matini zilizotambuliwa zilibainishwa na kuainishwa. Kutokana na uanishaji wa matini zilizohusishwa, mtafiti alidhihirisha kuwa kuwepo kwa matini hizo riwayani kulisababisha hali zifuatazo za kimajaribio:

- i. Mitindo tofauti tofauti ya utunzi;
- ii. Matumizi mapana ya fikra za wanafilosofia, wasomi pamoja na wanasiasa mashuhuri;
- iii. Matumizi mapana ya uhalisia-mazingaombwe au uhalisiajabu;
- iv. Muundo changamano uliovunjikavunjika; na
- v. Ukatazaji wa usimulizi.

Tatu, kutokana na hali zilizobainika, mtafiti alidondoa sifa bainifu mahususi za kimajaribio kama zilizotumika katika riwaya teule. Sifa zilizodondolewa ni pamoja na:

- i. Taashira;
- ii. Urejeleomatini;
- iii. Simulizi fupi fupi;
- iv. Dayolojia;
- v. Mwingilianotanzu;
- vi. Tamathali za semi;
- vii. Umajazi/lakabu;
- viii. Uhalisiajabu; na
- ix. Uzungumzi nafsia.

Sifa hizi zilikuwa data muhimu katika utafiti huu. Kwa sababu hii, katika hatua ya nne mtafiti alichanganua kila sifa zilizotamalaki katika riwaya teule na kuzitolea ufafanuzi kulingana na madhumuni ya utafiti kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti. Data iliyohusisha sifa nyingine chache ilihifadhiwa kwa minajili ya utafiti wa baadaye. Kwa muhtasari hatua za utafiti zimeangazwa katika kielelezo kifuatacho.



**Kielelezo 3.1: Muundo wa Mpango Maalum wa Ukusanyaji na Uchanganuzi wa Data**

### 3.5 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Uchanganuzi wa data ya utafiti huu ulifanywa katika hatua tatu. Katika hatua ya kwanza ya udurusu wa yaliyomo, mtafiti alitambulisha na kuchanganua fani za kifasihi zinazohodhi mbinu za kimajaribio. Kwa mujibu wa uelekezi wa Neuendorf (2002) udurusu na ufafanuzi wa yaliyomo ni njia mwafaka ya uchanganuzi wa data inayowasilishwa kwa maneno. Katika hatua ya pili mtafiti alichambua sifa zote zilizojitokeza katika kila fani na kuzigawa katika makundi ya (A), (B) na (C). Kundi A lilisimamia sifa jumuishi ambazo zimeibuka katika takriban riwaya zote. Kundi B linarejelea mada za kipekee ilhali kundi C limewasilisha mada nyinginezo. Mifano ni kama katika Jedwali 3.1 lifuatalo.

**Jedwali 3.1: Sifa Bainifu za Kunga za Kimajaribio katika Riwaya Teule za Kisasa za K. W. Wamitila**

	<b>A</b>	<b>B</b>	<b>C</b>
	<b>Mada Jumuishi Zilizoibuka</b>	<b>Mada za Kipekee</b>	<b>Mada Nyinginezo</b>
i.	Taashira	Uhalisiajabu	Mwingiliano-tanzu
ii.	Urejeleomatini		Uchanganyaji wa lugha
iii.	Dayolojia		
iv.	Muundo changamano		

Katika hatua ya tatu mtafiti alifasili maswala muhimu ya kunga za kiuandishi za kimajaribio yanayosababisha ukatizwaji wa usimulizi katika riwaya za kisasa zilizotafitiwa. Hatua ya ufasili ilijikita katika mihimili teule ya nadharia ya usasaleo. Uamilifu wa sifa bainifu za mbinu za kimajaribio zilizopatikana katika kazi teule ulifafanuliwa. Sifa iliyotamalaki ilielezwa. Mbinu ya kithamano ilitumika kueleza na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Mifano ya maswala muhimu yaliyorekodiwa yamebainisha katika Jedwali 3.2.

**Jedwali 3.2: Maswala Muhimu Yanayohodhi Kunga za Kiuandishi za Kimajaribio katika Riwaya za Kisasa za K.W. Wamitila**

	<b>Sifa Bainifu za Mbinu za Kiuandishi za Kimajaribio</b>	<b>Aina/zinapopatikana/ zinavyojidhihirisha</b>	<b>Riwaya</b>
i.	Taashira	Taashira ya aina ya sinekidoki Lakabu	MMM, ML, MWM
ii.	Urejeleomatini	Kitaaluma Dini Falsafa Siasa	MMM, ML, MWM
iii.	Dayolojia	Simulizi fupi Taashira	MMM, ML, MWM
iv.	Muundo changamano	Muundo Mtindo Msuko Usimulizi	MMM, ML, MWM
v.	Uhalisiajabu	Uhusika Usimulizi Mandhari	ML, MWM
vi.	Mwingiliano-tanzu	Hekaya Hurafa Methali	MMM, ML, MWM
vii.	Uchanganyaji lugha	Kiingereza Kifaransa	MMM, ML, MWM


MMM; *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji.*

ML; *Musaleo!*

MWM; *Msichana wa Mbalamwezi.*



Kwa muhtasari uchanganuzi wa data ulifuata mpangilio katika Kielelezo 3.2.



**Kielelezo 3.2: Muundo wa Uchanganuzi wa Data**

**Chanzo: Creswell (2009)**

## **SURA YA NNE**

### **KUNGA ZA KIUANDISHI ZA KIMAJARIBIO KATIKA RIWAYA ZA KISASA ZA KYALLO WADI WAMITILA**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika sura hii mtafiti ameshughulikia uchanganuzi wa data ambayo ilihusu kunga za kiuandishi za kimajaribio zilizodhihirika katika vipengele tofauti tofauti vya fasihi kama vile maudhui, lugha na kunga nyinginezo za uandishi katika riwaya teule. Sifa kuu ya kimajaribio iliyotamalaki ni ukatizwaji wa usimulizi. Kunga zilizobainika ni pamoja na matumzi ya majina ya watu, vitu na mahali, matumizi ya matukio yasiyo ya kawaida (uhalisiajabu) urejeleo wa maswala ya dini, mitholojia, simulizi za Kiafrika na matumizi ya matini za historia na sanaa. Data ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo. Madhumuni ya jumla yalikuwa ni kuweka bayana kunga za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya teule za Wamitila kama mmojawapo wa waandishi wa kimajaribio. Utafiti ulibainisha kuwa kuna ulazima wa msomaji wa kazi za kimajaribio kujihami na ufahamu wa maswala mengi yanayohusu historia, fasihi, sanaa, filamu na maswala mengine ya kijamii ili kuelewa ujumbe wa mwandishi wa riwaya za kisasa. Hata hivyo, mwandishi wa kisasa amefanikiwa katika matumizi ya mbinu za kimajaribio kama kunga ya utunzi kwenye juhudi za kuwasilisha maudhui yanayoifichua taswira kamili ya jamii ya kisasa katika uandishi bunifu wa riwaya.

#### **4.2 Ukatizwaji wa Usimulizi**

Katika riwaya zote tatu, ukatizwaji wa usimulizi umedhihirika katika fani tofauti tofauti za kifasihi. Ukatizwaji wa usimulizi ni hali ambapo mwandishi anazungumzia jambo fulani kisha kabla ya kulikamilisha akaliacha na ghafla akaanza kuzungumzia jingine. Aidha, ni aina ya usimulizi ambao umeathiri riwaya za kimajaribio kwa kuzifanya kukosa mtagusano wa kifasihi uliozoeleka.

Ukatizwaji wa usimulizi katika riwaya teule umesababisha kuwepo kwa muundo wa riwaya ulio changamano. Ukatizwaji wa usimulizi umejidhihirisha katika mitindo na miundo mbalimbali ya sifa za kimajaribio zilizotumiwa katika riwaya teule. Ujenzi wake umejitokeza katika vipengele mbalimbali vilivyodhihirika katika utunzi wa kimajaribio. Vipengele vilivyobainishwa vimejitokeza katika simulizi fupi fupi zilizotapakaa katika usimulizi mkuu wa riwaya

zilizoteuliwa. Vipengele hivi ni pamoja na; simulizi fupi, urejeleomatini, na mwingilianotanzu. Uandishi wa kimajaribio unawiana na maoni ya Lyotard (1984) kwamba riwaya haiwezi kuwa na mpangilio wa moja kwa moja kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa sababu hii ukosefu wa mpangilio wa moja kwa moja umesababisha uchangamano mpana katika ploti na usimulizi kwa jumla katika riwaya teule (Rettova, 2016). Hata hivyo, mwandishi amefanikiwa katika kuwasilisha ujumbe muhimu kuhusu maswala yanayoikabili jamii. Vile vile amefanikiwa kuichora taswira kamili ya jamii ya leo kwa kutumia riwaya za kimajaribio. Kunga za kiuandishi zilizochanganuliwa katika sehemu hii ni pamoja na uhalisiajabu, matumizi ya majina (halisi na bunifu), matumizi ya simulizi za Kiafrika, historia na sanaa. Taswira kamili ya jamii ya kisasa inayojidhihirisha kutokana na aina hii ya uandishi ni kwamba jamii ya sasa haipendelei kufuata utaratibu. Ni jamii inayofahamu mengi ambayo inayawasilisha kwa pamoja pasi na kufuata mpangilio wowote.

#### **4.2.1 Uhalisiajabu**

Katika riwaya zilizoshughulikiwa katika utafiti huu, hili ni swala linalojitokeza mno na kwa njia tofauti tofauti. Ni kunga ambayo mwandishi ameitumia kimatilaba ili kuakisi zama za leo ambazo zinafafanuliwa na matukio yasiyoweza kueleweka barabara. Uhalisiajabu pia hufahamika kama uhalisimazingaombwe. Asili ya dhana ya uhalisiajabu katika sanaa ni mnamo mwaka 1920 katika kazi za bunilizi za Jorge Luis Borges wa nchi ya Argentina (Zamora & Faris, 1995). Waandishi wengine wa kimajaribio walioboea katika matumizi ya uhalisiajabu katika bunilizi zao za kinathari walikuwa Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, Isabel Alende wa Chile, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia na John Fowles wa Uingereza (Abrams, 1999). Waandishi wanaotumia uhalisiajabu katika kazi ya fasihi husuka uhalisia pamoja na uhalisiajabu kwa njia maalumu inayobadilika badilika kwa lengo la kuwasilisha matukio ya kihalisia na maelezo ya kina kwa njia ya kifantasia au kindoto. Aidha, waandishi husika hutumia visasili na hekaya kutimiza malengo yao (Wardhaugh, 1986).

Katika utafiti huu, sifa zilizoangaziwa katika utambulishaji wa kuwepo kwa uhalisiajabu ukiwa kitengo kimoja cha usasaleo na kama zilivyobainika katika utafiti wa Walibora (2010) ni pamoja na:

- i. Matumizi ya wahusika wasio wa kawaida;
- ii. Kuwepo kwa matukio ya kiajabu;

- iii. Kukiukwa kwa mipaka ya kimandhari;
- iv. Kuwepo kwa hali za kushangaza na kuogofya;
- v. Kuwepo kwa matukio ya kindoto na kifantasia;
- vi. Katika kazi za uhalisiajabu wakati hausongi; na
- vii. Hakuna mpaka wowote kati ya yanayowezekana na yasiyowezekana.

Baadhi ya aina za uhalisiajabu zilionukuliwa ni matumizi ya wahusika wasiokuwa wa kawaida, matukio ya ajabu, ukiukaji wa mipaka ya kimandhari na kuwepo kwa hali za kuogofya kama katika nukuu hili;

“Lazima zilikuwa *slides* hizi! Mara hii niliviona visichana vilivyomzonga mwanamume aliyekuwa hana kichwa. Alitishia kuingiza mkono wake kotini kisha wale wasichana wakafyatuka ghafla. Alicheka kwa sauti kubwa ajabu. Kimya. Giza” (Wamitila, 2004, uk. 130)

Wahusika wanaorejelewa hapa katika riwaya ya *Musaleo* wanatembea katika sehemu inayoogofya. Kwa sababu ya giza totoro iliyopo wahusika hawawezi kuona mbele. Walitembea kwa matumaini makubwa kwamba mbele wangepata mwangaza. Walielezwa kwamba wayafungue masikio yao ili wasikie sauti muhimu, bila shaka kutoka kwa Mamanchi. Hivyo, waliongozwa na wosia wa Anima Mamanchi ambaye hawakuwa na uwezo wa kumwona ila waliisikia sauti yake. Mwandishi anasema kwamba sauti yenyewe ilifanana na ya watoto. Maneno yaliyotokana na sauti yaliwahamasisha kuhusu chanzo cha giza iliyowasumbua. Baada ya kupata uhuru kutoka kwa wakoloni, Waafrika walijikuta katika giza ya kudhulumiwa na viongozi ambao walikuwa Waafrika wenzao. Haya yaliibua enzi mpya ya kujitafutia ukombozi kwa kutumia mbinu ya uhamasishaji na mapinduzi. Uhalisiajabu umetumika kuwakilisha funzo jingine kwamba safari ya wanajamii ya kujikomboa kutokana na maovu ya dhuluma itokanayo na uongozi mbaya hupangwa na kutekelezwa na wanajamii wenyewe;

“Nilisema! Nilisema! Nilisema! Ung’amuzi haufi! Giza halitandi milele.” Nilimsogea Mamanchi kumuuliza, Je, alikufa lini huyu?” nilisema kwa sauti ya chini lakini aliyasikia. “Minong’ono hainiwezi. Mimi sijafa, bado ninaishi milele! Mimi Veritas sio mtu wa kufa. Nifeje? Uliyekufa ni wewe!” (Wamitila, 2004, uk. 69)

Uhalisiajabu katika dayolojia hii unarejelea dhana mbili muhimu, kifo na giza. Kifo ni tukio la kuondokewa na uzima au uhai. Kifo huleta athari hasi katika jamii inayohusika. Ni njia moja ya

kusababisha giza lisilokuwa na mwisho kwa mhusika. Katika upande mwingine hali ya kutokufa ambayo imefananishwa na *Veritas* imetajwa katika kipande kifupi cha urejeleomatini wenye uhalisiajabu. Katika dayolojia hii msimulizi anasisitiza kwamba ufahamu anaourejelea kama ung'amuzi hauwezi kufa, unadumu milele. Mtu anaweza kufa lakini ukweli utabakia milele. Ukweli ndiyo silaha ya kuwakomboa waja na kuwaweka huru. Ufahamu kuhusu ukweli unadumu milele. Ukweli ndiyo njia ya pekee ya kuwarudishia waja tumaini lililodidimizwa na dhuluma za viongozi pamoja na hali ngumu za maisha. Jamii ya sasa inahimizwa kuusaka ukweli iwapo inatamani maisha mazuri kwani ukweli huo ni kifaa cha kuiweka jamii huru.

“Je, unaamini kuzaliwa mara ya pili? Kuzaliwa kisha kufa na kuzaliwa tena” (Wamitila, 2004, uk. 79)

Katika riwaya ya *Musaleo!* kuzaliwa, kufa kisha kuzaliwa tena ni tendo la uhalisiajabu. Ni jambo lisilowezezana katika ulimwengu wa uhalisia. Kwa kawaida, binadamu akifa huenda kabisa na kusahaulika na hawezi kurudi tena ulimwenguni kama mwanadamu aliyezoeleka. Kunga hii ya utunzi imeambatanishwa na taashira ili kuwasilisha maudhui ya ukoloni, ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Mwandishi amebainisha kuwa ukoloni ni jambo linalodumu milele, halifi. Hii ni kwa sababu hata baada ya Waafrika kujipatia uhuru, bado wanatamani kutawaliwa na kuongozwa na mkoloni waliyemfukuza. Mwafrika daima ameweka tumaini la maendeleo yake katika matendo na mipango ya wageni, aghalabu Wazungu. Badala ya kukuza uchumi wake daima anategemea misaada kutoka “nje”. Kwa mfano, badala ya kuwaamini madaktari wake waliofunzwa na kuhitimu katika nchi zao, kila Mwafrika anapokuwa mgonjwa matibabu yafaayo ni yale ya Ughaibuni. Isitoshe, Mwafrika anayaenzi masomo katika nchi nyingine nje ya Afrika badala ya kuimarisha elimu katika taifa lake. Mambo haya yote yanazidi kumzamisha katika lindi la madeni, jambo linalochangia pakubwa katika kifo cha taifa lake. Mwandishi amefanikiwa kutumia kunga ya uhalisiajabu kuionya jamii dhidi ya utegemezi kwa wageni uliokithiri kwa minajili ya ufanisi. Anayaona matendo haya kama mbinu ya mkoloni ya kuendeleza dhuluma yake dhidi ya Mwafrika, hivyo kuufufua ukoloni. Jamii ya sasa inaonyesha taswira ya ukosefu wa uwezo wa kujiamulia maswala yake. Katika taifa lolote linaloendelea ni sharti kuwe na mipango mizuri ya kuimarisha elimu, kuwalipa wafanyakazi mishahara mizuri, kuwepo kwa barabara nzuri, kuimarisha hali ya mawasiliano na kuwa na chakula cha kuwatosha raia wote. Kinyume na haya Waafrika wanaamini kuwa fanaka yao itapatikana tu kwa

kuwategemea Wazungu. Kwa sababu hii wanawekewa vikwazo ambavyo vinawadidimiza zaidi (Nanjira, 2010). Ndio maana riwaya teule zinazimulika hali hizo na kukiri kwamba ukoloni hauwezi kuisha Afrika. Unazaliwa, unakufa na kuzaliwa tena, yaani unabadilisha majina tu. Ukoloni wa kwanza ulikuja na dhuluma ilhali ukoloni mamboleo unakuja na mambo mawili: dhuluma na vikwazo. Nyabunga (2005) anataja baadhi ya vikwazo vinavyowekewa nchi zinazotawaliwa na kasumba za ukoloni kama: kupunguza idadi ya wafanyakazi, kuanzisha viwanda vinavyofaidi nchi za kigeni pekee ili bidhaa ziuzwe kama rasilimali viwandani kisha Waafrika wanunue vitu vilivyotengenezewa ugenini. Maswala mbali mbali ya siasa pia yanawekewa masharti kama vile kuwa na vyama vingi vya kisiasa na kubinafsisha mashirika ya kiserikali ili kuleta uhuru na demokrasia miongoni mwa raia. Uhalisiajabu unaohusu bundi unapambanua zaidi kama ilivyo katika nukuu hili:

Zamani nilipokuwa kijana bundi walipolia sana nje ya banda letu, nilivuta blanketi na kujifunika gubigubi. Nikayaziba masikio yangu kwa vidole na kuamini kuwa nimefungia kila kitu nje nilipofunua baadaye na kuisikia ile sauti ya kukirihi tena na kujifunika mara nyingine kwa kasi ya ajabu (Wamitila, 2014, uk. 32)

Bundi ni ndege mwenye sifa za ajabu ajabu. Kuhusu umbo lake James (2003) anaeleza kuwa ni ndege mwenye kichwa cha mviringo chenye uwezo wa kugeuka pande zote na mwenye macho makubwa yanayofumbwa na kufumbuliwa kama ya binadamu. Aidha, bundi ana mdomo na kucha zilizochongoka zinazomwezesha kukamata na kurarua mawindo yake kwa urahisi. Mbawa na manyoya yake humwezesha kupaa kimya kimya pasi na kusikika. Yeye hulala mchana na kuwinda usiku wanyama wengine wanapopumzika. Bundi hujikinga dhidi ya maadui wake kwa kukaa kwenye matawi ya miti au sehemu nyingine bila kutingishika hivyo kuonekana kama kiumbe kisicho na uhai kama jani au kisiki (Hosking & Flegg, 1982). Mitazamo mbalimbali humwona bundi kama ndege asiyekuwa wa kawaida. Wamarekani wanaamini kuwa bundi ni ndege hatari na mwenye nguvu za ajabu (James, 2013). Harvey na Pagel (1991) wanafafanua kuwa bundi ni ishara ya furaha na bahati. Barani Afrika ambamo mwandishi anaandikia bundi ni ndege anayeashiria mikosi, shida, magonjwa na kifo (Konig *et al.*, 1999). Ni dhahiri kwamba matumizi ya bundi yanaibua hamu ya kutambulisha umbo na tabia zake ambazo zinabainisha kuwepo kwa uhalisiajabu katika utungo unaorejelewa. Kunga hii imetumika kukizindua kizazi cha leo kwamba kinaishi katika enzi hatari ambapo kisipozinduka kitaangamizwa. Msimulizi

anasema kwamba kila aliposikia mlio wa bundi aliyafunga macho yake na kujifunika gubigubi. Kila alipojifunua aliusikia ule mlio wa bundi tena. Ukweli ni kuwa hali ya hatari imo ndani ya jamii. Njia ya pekee ya kuondoa hatari ni kusimama tisti na kuikabili bila woga. Baadhi ya hatari zinazorejelewa ni pamoja na uongozi dhalimu, ukosefu wa matibabu bora hospitalini, umaskini na ukosefu wa elimu bora.

#### 4.2.2 Matumizi ya Majina ya Watu, Mahali au Vitu

Katika riwaya teule mwandishi ametumia majina aina aina yakiwemo ya watu, vitu na mahali Aidha, mna majina ya vitu halisi kama kifo na giza miongoni mwa mengine. Msomaji wa kazi za kimajaribio ni sharti afahamikiwe na watu au vitu vilivyotajwa ili aupate ujumbe wa mwandishi. Jedwali 4.1 linabainisha muhtasari wa baadhi ya majina yaliyochanganuliwa.

**Jedwali 4.1: Matumizi ya Majina**

<b>Jina</b>	<b>Aina</b>	<b>Maelezo</b>
Yesu	Halisi	Mkombozi wa Wakristo
Nicollo Machiavelli	Halisi	Mwanasiasa, mwandishi na mwanafalsafa wa Italia.
Veritas	Halisi	Mungu wa kike wa Kirumi
Euripides	Halisi	Mtunzi mashuhuri wa mitholojia za trajedia
<i>La Amistad</i>	Halisi	Meli ya Kihispania
Diana	Halisi	Aliyekuwa Malkia Mtarajiwa wa Uingereza
Sigmund Freud	Halisi	Tabibu na Mwanasaikolojia wa nchi ya Austria
Pablo Neruda	Halisi	
Joseph Guillotin	Halisi	Mwanzilishi wa mbinu ya “ <i>guillotine</i> ” ya kuwaangamiza wahalifu
Sphinx	Halisi	Jitu lenye kichwa cha mwanamke na mwili wa simba
King Oedipus	Halisi	Mfalme wa Thebe aliyewaua wazazi wake
Hammurabi	Halisi	Mfalme wa sita wa mji wa Babeli
Kifo	Halisi	Mwisho wa uhai
Mbegu	Halisi	Sehemu yam mea inayopandwa na kumea

Giza	Halisi	Ukosefu wa mwangaza
Jehanamu	Halisi	Mahali panapoaminika katika Ukristo kuwa mahali ambapo waovu wataishi wakiteseka milele
djambok	Jina la kubuni	Viboko au mijeledi
Mamanchi	Jina la kubuni	Mwanzilishi na mlezi wa taifa
Kingunge	Halisi	Aliyekuwa kiongozi wa chama cha kisiasa cha TANU kule Tanzania
Masogi	Jina la kubuni	Ishara ya utumwa
Profesa	Jina la kubuni	Msomi stadi
Musaleo	Jina la kubuni	Mkombozi wa leo; kiongozi wa leo mwenye kuleta mafanikio katika kizazi kipya.
Mashamba ya Mawe	Jina la kubuni	Mahali pasipo uzalishaji
Ukolongwe	Jina la kubuni	Ukoloni mkongwe
Kimbunga	Halisi	Upepo mkali
Baa-lini	Jina la kubuni	Utohozi wa jina linalorejelea mji wa Berlin wa Ujerumani
Alinacha	Jina la kubuni	Mhusika katika mitholojia ya kale
Vita vya Fyuraa	Jina la kubuni	Vita Vikuu vya Dunia
Jangwani	Jina la kubuni	Ukavu; shida, magumu, matatizo
Mkombozi Mzee	Jina la kubuni	Kiongozi mwenye fanaka, uhuru na furaha



Matenzawa	Jina la kubuni	Shujaa anayefahamika kwa kutonyolewa
Mwana-Mpotevu	Jina la kubuni	Ishara ya urejesho

---

Jina la Yesu limetumiwa katika utunzi na ubunifu wa riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi*. Katika dini ya Kikristo inaaminika kwamba Yesu ndiye mkombozi wa waja wote kutokana na dhambi. Inaaminika kwamba Yesu ana uwezo wa kuwapa uzima wa milele wote wamwanio. Hili laweza tu kuafikiwa iwapo wahusika watatubu dhambi zao yaani kutambua kwamba ni sharti waifishe jana yao ili wafanikiwe.

“Jana yao ifariki – kabisaaa! Lazima unafsi wao ufe; ili umoja wao uzaliwe. Mbegu lazima ife ndipo mche uweze kuota” (Wamitila, 2011, uk. 132)

Masimulizi yamekatizwa na kipengele cha ngano kuhusu Yesu kinachopachikwa katika simulizi kuu kuendeleza hoja kwamba “kifo” kilichokithiri katika jamii ya sasa kinaweza tu kuangamizwa na jamii yenyewe. Suluhu la jamii ni jamii. Ili kubainisha taswira ya jamii ya sasa hadithi (ngano) iliyosikika kanisani wakati wa sherehe ya arusi ilirejelewa. Hadithi husika ni kifaa muhimu cha kuijua jamii kwamba ili kupiga hatua kimaendeleo na kuimarisha huduma kwa wanajamii wote ni sharti kila mmoja afishe makosa ya kihistoria na kuyazika katika kaburi la sahai. Maneno katika usimulizi huo yalisemwa na mhubiri kwa bwana na bibi arusi. Alikuwa akiwapa wosia kwamba iwapo watapenda kuishi vizuri katika maisha ya ndoa itawabidi wafishe “jana yao”. Jana inaashiria wakati uliopita. Mhubiri alisistiza kuwa ni lazima ya kale miongoni mwao kama ubinafsi yafe ili umoja wao uzaliwe. “Ni lazima mbegu ife ili mche uote”.

Aidha, jina la Yesu limetumika katika kipengele cha kimajaribio cha mwingilianotanzu kuwasilishia ujumbe kuhusu kifo kama njia ya ukombozi.

“Kifo lazima kitangulie mapenzi au hata mapenzi yawe chanzo cha kifo kama ilivyotokea zamani. Yesu alikufa kwa kuwapenda wenye dhambi; kifo chake kikawa mwanzo wa mapenzi – bila kifo hakuna mapenzi. Hakunaaa!” (Wamitila, 2011, uk. 132)

Isitoshe, kifo hutangulia mapenzi kama ilivyokuwa katika kisa cha Yesu Masihi. Ilibidi afe msalabani ili wenye dhambi wapokee msamaha kwa mujibu wa dini ya Kikristo. Kwa hivyo, kifo chake kilikuwa chanzo cha mapenzi kwa wenye dhambi. Kwa mujibu wa haya jamii ya kisasa inawajibika katika kufisha historia yake hasi ili maendeleo yapate kuota. Ukosefu wa huduma bora ni mambo yanayozalishwa na ukoloni mamboleo ambao ni zao la historia. Kitendo cha “*kufisha historia*” ndiko kuzaliwa kwa mara ya pili. Hivyo, taswira ya jamii ya sasa ni kwamba kutakuwa na kizazi kipya au tumaini jipya la jamii. Jamii mpya hiyo itakuwa ile iliyosahau jana yake kwa kufisha hali hasi zilizoikumba na kuzingatia mienendo mipya kwa lengo la kuinufaisha kama wasemavyo wahenga “yaliyopita si ndwele tugange yajayo”.

Katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* mna matumizi ya jina Diana. Japo kwa mtajo tu, mwandishi anamzungumzia Diana Frances Spencer, Binti wa Mfalme wa Uingereza, Malkia mtarajiwa na ambaye alifanyika kuwa mpenzi wake Dodi Al Fayed wa Misri. Mwandishi anafananisha mapenzi ya Msichana wa Mbalamwezi na yale ya Diana. Katika riwaya mwandishi anataja kuwa mapenzi ya Msichana wa Mbalamwezi yalipotea kama yale ya Diana. Msomaji asiyemfahamu Diana anamlazimika kutafiti kumhusu ili afahamikiwe jinsi mapenzi yake yalivyopotea, yaani ayatafute yale ambayo hayakusemwa katika riwaya.

Hivyo basi ili kumwelewa mwandishi na kupata taswira kamili ya jamii ni sharti hadhira ifahamu muktadha wa jina Diana lililorejelewa kwamba: baada ya Binti-mfalme Diana kutamaushwa na mapenzi baina yake na mumewe ambaye alikuwa Mwanamfalme Charles Philip Arthur George Mountbatten kutumbukia nyongo na kupewa talaka, Diana alijipatia mpenzi mwingine, Dodi Al Fayed kutoka Misri (Bradford, 2007). Hata hivyo, tumaini lake jipya la mapenzi lilikatizwa na kifo cha ajali barabarani kilichotokea katika hali tatanishi. Wakati mmoja wapenzi hawa wawili walialikwa na babake Dodi kujivinjari katika ziara ya majini kule Corsica na Sardinia ndani ya meli ya kibinafsi na kifahari maarufu kama *Jonikal* (Bradford, 2007). Baada ya kufahamu kuhusu uhusiano wa Diana na Dodi wanahabari waliwafuata kila uchao (Junor, 2012). Mnamo tarehe mbili Agosti 1997, mpigapicha tajika Mario Brenna aliwasili Sardinia kwa mwaliko wa Diana (Smith, 2007). Baada ya siku mbili alipiga picha za Dodi na Diana zilizopachikwa jina, “picha za busu” na kuzichapisha (Snell, 2013). Agosti tarehe ishirini na moja Malkia Diana alijiunga na mpenzi wake tena kwa ziara ya pili iliyofanyika Paris, Ufaransa (Bradford, 2007). Habari kuhusu uhusiano wao zilikuwa zimeenea kote ulimwenguni kwa kasi kiasi cha

kuwafanya mapaparazi kuwafuata kila mahali. Wanahabari pia walichapisha habari kuwahusu Diana na Dodi kila uchao. Mnamo saa sita tarehe thelathini mwezi Agosti mwaka 1997 wapenzi hawa waliondoka kuelekea Paris (Smith, 2007). Walipotua katika uwanja wa ndege katika mji wa Le Bourget, Paris wanahabari na mapaparazi walikuwa tayari wakiwasubiri ili kuutangaza uhusiano huo kwa dunia nzima. Kwa mujibu wa Brown (2008) Dodi alimwelekeza dereva mjini Bois de Boulogne kinyume na mpango wa awali wa kuelekea Ritz kwa lengo la kuwaepuka wanahabari na mapaparazi. Baadaye walienda hadi kwenye makazi ya kifahari ya Fayed kule Rue Arsne-Houssaye. Kinyume na matarajio yao, mapaparazi walizidi kuwafuata. Katika hali hii gari la Diana na mpenzi wake aina ya *Mercedes Benz* lilianguka na kubingirika kutokana na kuendeshwa kwa mwendo wa kasi (Brown, 2007). Diana na Dodi walipelekwa hospitalini ambamo kifo chao kilithibitishwa (Bradford, 2007).

Kisa cha Diana na Dodi kimetumiwa katika riwaya teule kubaini kuwa kifo cha aina yoyote kina uzito wa kuleta huzuni isiyo kifani katika jamii. Ni onyo kwa jamii ya sasa kwamba ikiazimia kuishi ni sharti ijiepushe na hali zinazoweza kusababisha mauko miongoni mwa wanajamii wake. Jamii inahimizwa kuendeleza maadili yanayokubalika. Kwa mara nyingine, riwaya zimesisitiza kwamba jamii ndiyo yenye suluhu la matatizo yanayoikabili. Kauli hii imetiliwa mkazo kwa matumizi ya swali la balagha kwamba; “...uhai na kifo. Riale kwa ya pili?” Kwa maneno mengine kile kinachopitishwa riwayani ni kwamba jamii itakuwa jinsi itakavyojichagulia kuwa. Uhai na kifo ni matukio mawili yanayoshabihiana kama shilingi kwa ya pili ambayo yako mikononi mwa jamii yenyewe.

Kando na kuwa simulizi fupi yenye taashira, matini imehodhi vipengele vingine vya kunga za kimajaribio kama urejeleomatini, falsafa ya utamaushi na hali kadhalika mwingilianotanzu. Hadithi yenyewe inaonyesha ukweli kwamba mapenzi yanapokatizwa hamu na tamaa ya kuishi hukatizwa pia. Hii ndiyo sababu mapenzi yanafananishwa na kifo. Mapenzi hukatizwa na mambo aina aina ila adui mkuu wa mapenzi ni kifo. Baada ya kupatana na kuchumbiana, Diana na Dodi pamoja na wazazi wao walikuwa na matumaini ya maisha mazuri ya baadaye lakini hayo yote yalikatizwa na kifo. Mintarafu ya mfano wa kisa cha Diana, riwaya imewasilisha taswira kwamba kifo kinachotokana na mapenzi hutamausha zaidi. Japo vyao vilikuwa vifo kwa sababu ya tukio la kimapenzi ni dhahiri kwamba kifo ni kifo na athari zake zina machungu kwa jamaa licha ya kile kilichokisababisha. Kwa mujibu wa riwaya teule, kwa vyovyote vile kifo

husababisha kupotea kwa matumaini na raha maishani. Kama mbinu ya kiuandishi mwandishi ameitaja hadithi ya Diana katika usimulizi mkuu pasi na kuisimulia chochote kwa matumaini kwamba hadhira itajaliza mapengo aliyoyaacha na kupata ung'amuzi wa funzo analowasilisha.

Jina jingine halisi lililotumiwa ni Sigmund Freud. Huyu alikuwa mwanasaikolojia tajika kutoka aliyezaliwa nchini Austria (Clark, 1980). Alifanya utafiti kuhusu ndoto za binadamu (David, 2009). Amenukuliwa katika riwaya ya *Musaleo* kuhusu maelezo yake ya tabia aliyoitia *Phallus Envy*.

“Walifuata maneno ya Sigmund Freud aliposema shida yake ni *Phallus Envy*” (Wamitila, 2004, uk. 82)

Muktadha wa nukuu hili unamrejelea mhusika mwanamke aliyepewa jina la kimajazi la Mamanchi ambaye alikuwa akitafutwa baada ya kutelekezwa na jamii. Maneno haya ni malalamishi ya wenyeji dhidi ya waliomtelekeza mwanamke huyu. Mwandishi anarejelea usemi wa Sigmund Freud ili kutoa picha ya jinsi mwanamke anavyosawiriwa na jamii za Kiafrika. ‘*Phallus Envy*’ inarejelea elimu kuhusu maendeleo na ukuaji wa nafsi na mahusiano ya wanawake. Freud (1975) anaeleza kuwa wasichana wanapokua hupatwa na dukuduku wanapotambua kuwa wako tofauti na wanaume kimaumbile. Wanakosa utambulisho wa kijinsia. Wakati huu wasichana huacha kuwategemea mama zao na badala yake kujiegemeza zaidi kwa baba zao. Kwa sababu hii, wanawake wanaonekana na jamii kama viumbe dhaifu wasioweza kujitegemea. Hapa maudhui yanayoangaziwa ni kuhusu taswira ya mwanamke katika jamii. Hakuna usawa baina ya mwanamume na mwanamke katika jamii ya sasa. Kinachoendelea ni kwamba mwanamke daima yu vitani vya kutaka kujikomboa na kujipatia jina katika jamii yake. Jamii ya sasa inayowatelekeza wanawake husahau kuwa mti uliokatwa unaweza kuchipuka tena. Kuna umuhimu wa kuwa na usawa wa kijinsia katika jamii. Aidha, ni vyema jamii ifahamu kwamba kile kilichokataliwa huenda kikanawiri baada ya mpito wa wakati. Hivi ndivyo mama aliyetelekezwa alivyofanyika kuwa Mamanchi. Jamii itatahadharishwa dhidi ya kumwona mwanamke kama kiumbe kilicho mbioni kwa lengo la kujikomboa tu.

“Tulimfuata Niccolo Machiavelli. Je, umesoma *The Prince*? Niliitikia kwa kichwa tu. Aliniangalia kabla ya kuendelea” (Wamitila, 2004, uk. 116)

Hapa pana majina mawili; Nicollo Machiavelli na *The Prince*. Machiavelli ni mwanafalsafa na mwandishi wa kitabu mashuhuri kiitwacho *The Prince*. Yeye ni mwenyeji wa Italia. Majina haya mawili yametajwa na kutumiwa kama kunga ya kuwasili ujumbe katika riwaya ya *Musaleo!* Mambo anayotakiwa kufahamu msomaji wa riwaya husika ya Wamitila ni imani ya Machiavelli kwamba: binadamu anapingwa, kuchukiwa na kulaaniwa na wengi. Aidha, falsafa ya Nicollo Machiavelli zimejaa ubabe, utapeli na ulaghai mwingi ambao haufai kufuatwa na viongozi katika nchi za kidemokrasia (Tinkler, 1988). Katika falsafa yake Machiavelli anawapa wosia wana wa wafalme katika enzi zake. Machiavelli anawaelekeza wana hao kwamba kushika falsafa hizo za ubabe, utapeli na ulaghai ili waweze kushika madaraka, kujenga himaya yenye nguvu na kuogofya, kuongoza katika vipindi vya msukosuko, kudumu katika madaraka na kujilinda dhidi ya maadui (Machiavelli, 1981). Falsafa yake haikupendwa na wengi hivyo alipokuwa akiandika alipingwa sana na marafiki wake wa karibu na pia watu wengine wa mbali. Alichekwa na kukejeliwa kwa kile kilichoonekana kama kupoteza wakati kwa kuandika kitabu ambacho hakingepata wa kukisoma. Hata hivyo, Machiavelli hakukata tamaa, aliendelea kujipa moyo ili atimize shauku ya moyo wake. Aliwaaminisha wasomaji wake kwamba ili jamii za kifalme ziishi maisha tukufu ya kifahari wana uhuru wa kuwakandamiza wananchi wao. Kwake, ni sawa iwapo kiongozi atawadhulumu watu kwa lengo la kujipatia raha na utukufu (Tinkler, 1988). Funzo linalopitishwa katika urejeleo wa simulizi hii ni kwamba wanajamii wanafaa kutambua kwamba uongozi si wa watu wa kawaida. Isitoshe, hapa mwandishi anachora picha ya ubinafsi wa viongozi wa kisasa ambao watafanya lolote lile bila kuwajali wanaowaongoza bora tu wajipatie enzi na umaarufu. Simulizi zenye majina ya Machiavelli na Prince zimetajwa tu katikati ya simulizi kuu. Ukatizwaji wa usimulizi unaibuka kwani asiyewafahamu hawa humlazimu kusita kwanza huku akitafuta kuwajua ndipo ang'amue malengo ya mwandishi katika riwaya husika.

Katika hadithi fiche ni kwamba baada ya bidii nyingi, kitabu cha Nicollo Machiavelli kilichapishwa. Yeye mwenyewe alichukua nakala moja akampelekea mtawala wa Florence kama zawadi. Mfalme huyo alivutiwa nacho sana kiasi cha kuamua kumpa Machiavelli cheo kikubwa katika serikali yake, jambo ambalo Machiavelli alikataa. Badala yake aliamua kuwa mshauri mkuu wa mtawala huyo. Kuanzia wakati huo uandishi wake ulipata mashaka, ukubalifu na umaarufu. Mintarafu ya haya; kila mwanajamii anafaa kujiwekea malengo yake na kuhakikisha kwamba ni malengo ya uhakika. Kwa kufanya hivi atakuwa akitambua uwezo wake na kupanga

mambo yake kulingana na uwezo huo. Licha ya hayo, binadamu asikubali ushauri ambao unakusudia umrudisha nyuma. Badala yake afanye uamuzi wa kuachana na marafiki wabaya wenye nia za kitamaushi na amtangulize Mungu katika kila jambo analolifanya. Aidha, jina Veritas limetumika katika usimulizi. Tazama;

“Minong’ono hainiwezi. Mimi sijafa, bado ninaishi milele! Mimi Veritas sio mtu wa kufa. Nifeje? Uliyekufa ni wewe!” (Wamitila, 2004, uk. 69).

Katika mitholojia ya Kirumi, *Veritas* ni jina la mungu wa kike anayewakilisha ukweli. Mungu wa kweli kwa hakika hawezi kufa. Katika muktadha wa nukuu, ukoloni unalinganishwa na huyu mungu wa ukweli asiyefariki. Hivyo inabainisha jinsi ilivyo vigumu kumaliza athari za ukoloni barani Afrika. Afrika ndiyo itakayokufa wala si mkoloni. Kwa mujibu wa riwaya, mkoloni hawezi kufa yaani uwepo wake utaendelea kuhisiwa kwa sababu anatawala kila sekta ya maisha ya Mwafrika. Baadhi ya sekta zinazotawaliwa ni uchumi, elimu na siasa.

Katika riwaya ya *Musaleo!* kwa mbinu ya simulizi fupi mwandishi Wamitila ametumia jina *La Amistad* kurejelea meli ya Kihispania iliyotumika wakati wa enzi za biashara za watumwa. Hadithi ambayo msomaji anafaa kuwa nayo ni kuhusu dhiki ya Waafrika walipokuwa wakisafirishwa Ughaibuni walipotumika kama watumwa:

Wakati huu giza lilienea kila mahali na sikuweza kujua kama lilikuwa giza la jana au la leo. Nilisimama na kujaribu kuyakodoa macho yangu ambayo sasa hivi yalikuwa yamelizoea giza hilo. Baada ya muda niliisikia ile sauti tena. Mara hii niliweza kuyanasa maneno yake yote. “Alikuwa ni mtu wa matumaini alipokuwa kijana. Kila mtu alimwamini; sote ..e.e.e tulimwamini! Unasikia bwana, soo-ote kila mahali. Kijijini, mijini, nchi nzima, bara zima. Unasikia tena, bara zima! ... “Kila mtu aliikumbuka dhiki ya jana. Visa vya kufungwa kwa wenyeji kwenye kongwa na kusafirishwa kwenye meli kama AMISTAD vilikumbukwa na kila mmoja. Dhiki ya kuwa manamba kwenye mashamba ya mikonge ya Wazungu, kufia migondini kurithisha Wareno, watu kuliwa na simba wakijenga reli na umma kucharazwa *djambok*. Vyote vilikumbukwa na kila mmoja. Nakumbuka jinsi kila mmoja alivyotokwa na machozi kisa cha Mamanchi kiliposimuliwa... kule kuna... ashakum: hayasemekiki mengine yahe! (Wamitila, 2004, k. 91-92)

Kwa mujibu wa Osagie (2000), mnamo mwezi Agosti mwaka 1839 meli ya Kihispania kwa jina *La Amistad* ilitua katika ufuo wa bahari wa kisiwa cha Long jijini New York, Marekani. Shehena yake ilikuwa watumwa, Waafrika hamsini na wanne kutoka katika jamii ya Mende ya Sierra Leone ya sasa. Walikuwa wanaume arobaini na tisa na watoto wanne wasichana wakiwa

watatu na msichana mmoja. Walikuwa wamenuliwa na Pedro Montes na mwenzake Jose Ruiz ili wakatimike katika mashamba yao ya mikonge kule Cuba (Jones, 1987). Wakati huo Cuba ilikuwa chini ya ukoloni wa Uhispania. Safari ilipokuwa ikiendelea baharini, wale watumwa waliasi, wakawanasa na kuwaua wafanyikazi melini akiwemo mpishi na nahodha kisha wakafanikiwa kuchukua usukani wa meli hiyo. Waliwaamrisha Montes na Ruiz kuirudisha meli Afrika. Hata hivyo, walihadaiwa na meli ikapelekwa hadi Montauk Point, Kisiwa cha Long, Marekani katika safari iliyochukua siku sitini na tatu. Wakati huo biashara ya watumwa ilikuwa imeharamishwa na kupigwa marufuku na mataifa ya Marekani na Uingereza (Jones, 1987). Kwa sababu hii, ingawa wale Waafrika walishikwa na kufungiwa korokoroni, kesi iliyohusiana na uvunjaji wa sharia za kiutumwa ilianzishwa. Waafrika walipata watetezi mahakamani na wakashinda kesi hiyo. Waliruhusiwa kurudi kwao Sierra Leone.

Katika simulizi fupi iliyoboreshwa na matini ya kihistoria, macho ya mhusika Musaleo yanasemwa kuwa yalikuwa yameizoea giza. Hakuwa na uwezo wa kuona mbele katika safari yake. Safari hii inalinganishwa na ile ya watumwa waliokuwa katika meli ya *La Amistad*. Hawakuwa na matumaini yoyote ya kupata uhuru wao. Hawakuwa na uwezo wa kubashiri jinsi maisha yao ya baadaye yangukuwa. Katikati yao pakaibuka kiongozi ambaye alikuwa chemichemi ya tumaini kwa watumwa wengine. Kiongozi huyu analinganishwa na Musaleo ambaye aligeuka kuwa kipenzi cha wengi. Mwandishi anasema kuwa watu wote mahali popote pawe kijijini au mjini walimfahamu kama mtu mwenye matumaini. Mwandishi anazidi kusema kwamba wote waliomfahamu walimwamini. Historia ya maisha ya hapo awali ya utumwa ambayo yalikuwa machungu yaliyojaa dhiki yanatolewa katika simulizi hii kama kumbukumbu. Hadhira inakumbushwa jinsi Waafrika walivyosafirishwa katika meli huku wakiwa wamefungwa kwenye kongwa ili wasitoroke.

Kutokana na simulizi hii mwandishi wa riwaya mpya amebainisha kuwa jina mkombozi wa Mwafrika ni Mwafrika mwenyewe. Mwafrika aliyeikata minyororo ya utumwa katika *La Amistad* alithibitisha kuwa hakuwa binafsi kwa kuwasaidia wenzake kujifungua. Baada ya kuwaweka wenzake huru, kwa pamoja waliungana kuutafuta uhuru kikamilifu. Taashira zilizotumika katika simulizi hii zinaitahadharisha jamii dhidi ya ubinafsi. Zinabaini kwamba ubinafsi ni ugonjwa wenye uwezo wa kuliangamiza taifa. Kwa upande mwingine, umoja ndio silaha ya ufanisi wa taifa. Kinaya ni kwamba jamii ya sasa ina mbinu zote zinazohitajika katika

kujitwalia ukombozi lakini haizitumii.

Simulizi fupi ambayo inahusisha jina la meli ya *La Amistad* inayofaa kufahamika na msomaji wa riwaya husika inahitimishwa kwa maelezo kwamba; waliobahatika kufika katika nchi walikouzwa kama watumwa, walipata dhiki ya kutumikishwa katika mashamba makubwa ya mikonge. Wengine walifia migodini mikononi mwa mabwana zao, Wareno. Hapa Kenya, wenyeji walipata dhiki ya kuliwa na simba wakijenga reli huku wananchi wengine wa kawaida wakiumizwa kwa kucharazwa mijeledi. Simulizi zilizorejelewa zimefumwa kwa taashira mbali mbali za majina. Kulingana na miktadha ambamo simulizi hizi zimetumiwa riwayani, mwandishi amezitumia kuwasililishia maudhui ya ukoloni na hali kadhalika ukoloni mkongwe ambao bado unadhihirika katika jamii ya sasa. La muhimu zaidi ni ufahamu kwamba binadamu wa sasa ndiye aliye na uwezo wa kujikomboa kutokana na dhiki inayompata. Hata hivyo, inahuzunisha kwamba wanajamii husahau historia yao, hali inayomfanya mwandishi wa riwaya mpya kuiwasilisha historia hiyo katika riwaya. Aidha, mna matumizi ya jina halisi la Hammurabi. Urejeleo wa kisa cha Hammurabi ni mfano wa madhila wafanyiwayo wanajamii wanaougua hospitalini kama ilivyorekodiwa katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* kwamba;

“Si anakumbuka ni mara ngapi hata wenyewe walikivunja kile kiapo cha Hammurabi?”  
(Wamitila, 2014, uk. 132)

Msimulizi ametumia dayolojia kubainisha jinsi madaktari wanavyowadhulumu wagonjwa katika hospitali za jamii za kisasa. Madaktari hawa wawili wanakumbushana hadithi ya mfalme Hammurabi, mfalme wa sita wa Babiloni iliyokuwepo Mesopotamia kati ya miaka 1894 – 1595 kabla ya Yesu Masihi. Hammurabi alifahamika kwa kubuni na kurekodi jumla ya sheria mia mbili themanini na mbili zilizofahamika kama “Kiapo cha Hammurabi.” Sheria hizo ziliandikwa katika jiwe na kuwekwa mahali ambapo kila mtu aliziona. Kiapo hicho kilinua kuleta maadili, ushirikiano na uwiano katika jamii. Iwapo binadamu yeyote angevunja sheria yoyote angepewa adhabu kali. Kwa mujibu wa Hammurabi, kipimo ambacho mtu angetumia kwa mwenzake kicho hicho kingetumika kwake. Sheria za Hammurabi kwa jumla ziliruhusu ulipishaji wa kisasi. Watu wa Babiloni waliogopa sana kuzivunja. Mtu akimwua mwenzake kwa upanga, angekufa kwa upanga huo huo. Kupitia kwa mazungumzo yao, maadili ya madaktari wa kisasa na utendakazi wao yanatiliwa shaka. Mwandishi anaonyesha kuwa baadhi ya madaktari wako mbioni



kujinufaisha huku wagonjwa wakiumia na kuteseka kwa kisingizio kuwa, “kiapo cha Hammurabi kilivunjwa, sembuse cha madaktari”. Taswira inayobainika ni kwamba mnyonge hana haki yoyote kwani daktari anapokosa kuwajibika kazini kisha mgonjwa afariki dunia katika mikono yake, haki ya mfu itasalia kuwa maziko pekee.

Katika riwaya, daktari mmoja anamkumbusha mwenzake jinsi walivyovunja kiapo cha udaktari walipokuwa wakifanya kazi hospitalini huku wakijilinganisha na Wababiloni waliovunja kiapo cha Hammurabi. Ikumbukwe kwamba katika hali halisi hakuna mtu yeyote kule Babiloni angethubutu kufanyia mzaha kiapo hicho cha Hammurabi. Hapa riwaya zinaonyesha taswira ya kutojali miongoni mwa madaktari wa kisasa. Mwandishi anadai kwamba utendakazi wa madaktari umekosa maadili na hisia za imani kwa wanaohitaji huduma zao. Falsafa ya utamaushi inabainishwa na kinaya hiki cha maisha kwamba daktari anaamua kumdhuru mgonjwa wake kwa kumfanyia upasuaji usiohitajika kwa lengo la kupata pesa. Vile vile, ni kinyume cha matarajio kuwaona madaktari hao hao wakishirikiana kuwafanyia wanawake upasuaji usio wa lazima ili wapate pesa za kulipia malimbikizo ya karo za wanao waliosomea katika shule za Wazungu. Isitoshe, kisa kinachotamausha zaidi ni kile cha mzee aliyefanyiwa upasuaji huku madaktari wakifahamu fika kuwa angefariki wakiwa na lengo la ‘kuukamua utomvu wa mwisho kwenye muwa uliokauka wa jamaa yake.”

Madaktari wahusika walifahamu fika kuhusu gharama iliyopatikana na mgonjwa anayerejelewa. Hata hivyo, walikata kauli ya kumfanyia upasuaji ili wachukue kile kilichosazwa katika jamii husika. Labda walikisia kuwa baada ya upasuaji huo jamaa ingekongamana kisha ichangishe fedha za kulipia bili hiyo. Kitendo hiki kibainisha kuwepo kwa jamii ya kisasa isiyo na utu. Aidha, madaktari wengine waliwafanyia wanawake upasuaji kisha wakaondoka kwenda ulevini kabla ya kuukamilisha upasuaji wenyewe. Waliofanyiwa upasuaji walibaki wakigaagaa vitandani wakiwa katika hali mahututi. Kwa mujibu wa simulizi fupi hivi kwenye riwaya teule ni dhahiri kwamba wanyonge wanazidi kuumizwa na wenye nguvu, wenye ujuzi na wenye maarifa licha ya kuwa wamepewa majukumu hayo na serikali. Inasikitisha kwamba wafanyakazi wanaotegemewa zaidi na wanajamii kama madaktari hawana hisia zozote za kiutu katika kizazi cha leo. Haijalishi kwamba wao hula kiapo cha kufanya kazi kwa uaminifu na ukamilifu. Kinaya ni kwamba kiapo chao kimegeuka tamaa ya mali iliyokithiri.

Majina mengine yaliyotumika ni **barafu ya kumbukumbu, kunyamazisha sauti, utumbo wa ardhi na kufungua njia**. Majina haya yote yamejumuishwa katika baadhi ya kunga za utunzi za mwandishi. Riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* inasema kwamba;

“Ili kuukatiza mkondo huo wa mawazo, niliamua kulizima joto la hali iliyonizunguka kwa barafu ya kumbukumbu zangu. Kumbukumbu ni ganzi nzuri ya kupoza maumivu ya sasa” (Wamitila, 2014, uk. 38)

Mhusika Yosi Kanga katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* alikuwa katika lindi la mawazo alipokuwa hospitalini kwa sababu ya afya yake iliyokuwa ikididimia. Ijapokuwa wakati huu alikuwa taabani, aliyakumbuka mambo mazuri ya zamani kwa minajili ya kujisahaulisha kuhusu yaliyokuwa yakitendeka wakati huo. Mwandishi anasema kwamba kumbukumbu ni ganzi nzuri ya kupoza maumivu. Kufisha ganzi ni kitendo cha huduma ya kwanza ya kupunguza makali ya uchungu baada ya kupata maumivu au kujeruhiwa. Yosi Kanga alijawa na kumbukumbu za kupendeza kuhusu maisha yake akiwa shuleni. Alikumbuka ujanja alioufanya yeye na wenzake katika bwawa la shule ambapo walitupa madini ya *potassium* ili kuwatisha wenzao. Madini hayo yalipotumbukia majini kuliibuka mlipuko mkubwa. Wote waliosikia mlipuko ule waliamini kwamba kulikuwa na pepo wabaya bwawani. Hii ndiyo iliyokuwa furaha ya Yosi na wajanja wenzake. Kumbukumbu hizi zilimpa Yosi faraja alipokuwa akisubiri kifo kwa mujibu wa daktari wake. Ingawa binadamu anapitikiwa na mambo mengi yanayomsumbua anaweza kuyasuluhisha kwa kupunguza makali yake kwa kumbukumbu za mazuri yaliyompitikia wakati mmoja katika maisha yake. Hivyo, kumbukumbu ni mbinu moja ya kusuluhisha matatizo. Hali kadhalika katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* kumbukumbu imeangaziwa kama suluhu katika nukuu hili:

*Akanyamazisha sauti za akina Marugurugu na wenzake. Mwenzake naye akamtumia ujumbe wa kuja kuangalia jinsi alivyokuwa amepiga hatua. Ujumbe wa kufuatilia kujua kama msaada wao ulikuwa wa kufaa au la. Ujumbe huu ndio uliomfikishia barua iliyotokea kwao. Akakumbukushwa jambo ambalo alielekea kulisahau. Ilikuwa Barua ya Kumbukumbu. Ahadi ni deni* (Wamitila, 2014, uk. 75)

Ukosefu wa uhuru wa usemi ni njia moja ya kuwadhulumu raia. Istilahi “*kunyamazisha*” imetumiwa kuashiria kuhitimisha uhuru na kumaliza nguvu za wanajamii wazalendo. Taswira inayoibuka ni kwamba viongozi wa mataifa ya Kiafrika yanayoendelea hawana nafasi ya

kukosolewa, yaani hawakosolei. Yeyote anayethubutu kukosoa uongozi wao hunyamazishwa kwa njia tofauti tofauti. Wako wale wanaokamatwa na kuteswa ilhali wengine hufa kwa njia zisizoelezeka. Kwa mfano, barani Afrika katika nchi ya Uganda Robert Kyagulanyi Ssentamu maarufu kama Bobi Wine na Kizza Bessigye wameumizwa na utawala wa nchi kwa sababu ya kumpinga kiongozi wao kama ilivyorekodiwa katika gazeti la *East African* (tarehe 18.10.2019). Isitoshe, nchini Kenya Raila Odinga, Marehemu Charles Rubia na Marehemu Kenneth Matiba wameripotiwa kuteswa sana wakati wa utawala wa aliyekuwa rais wakati huo kama ilivyoripotiwa katika gazeti la *Daily Nation* (4.10.2013). Mambo kama haya yanapotokea katika jamii ni ishara tosha ya ukoloni mamboleo. Muktaba wa riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* unabaini kwamba lengo kuu la mkoloni la kumnyamazisha Marugurugu na wazalendo wenzake lilikuwa kujipatia nafasi ya kujipenyeza zaidi nchini na kuendelea kupora rasilimali zake. Vivyo hivyo, imebainika kuwa viongozi walafi hawawezi kuwapa nafasi wazalendo kwa hofu kuwa wataufichua ulafi na uovu wao na kuutangaza hadharani.

Mkoloni pia ana kumbukizi zinazouliwaza moyo wake. Baada ya kuondoka kwake, waliobaki kuendeleza ukoloni mkongwe walipiga hatua kubwa kuuendeleza. Walihakikisha kwamba wamefisha nguvu za uwezekano wa mapinduzi ya aina yoyote kwa kudidimiza usemi wa viongozi kama vile Marugurugu. Majina “kunyamazisha sauti” yametumika kueleza vilio vya wanyonge vinavyokosa kusikizwa na “wenye nguvu” yaani viongozi wa enzi hizo za ukoloni. Msimulizi anaendelea kusema kwamba vitendo vyote vya wakoloni vilihifadhiwa katika “Barua ya Kumbukumbu.” Kama vile inavyowasilishwa riwayani, kumbukumbu ni njia moja ya kuliwaza akili baada ya kipindi kirefu cha kumkosesha mwanadamu amani. Mwanadamu anapotazama nyuma na kuona yote yaliyompitikia analiwazika. Hata ingawa mkoloni alikuwa ameshaondoka kutoka nchi ambayo kwa wakati mmoja aliitawala, alijiliwaza kwa kumbukizi za awali. Alikumbuka jinsi alivyokuwa na mamlaka juu ya kila hali hata nafsi za wenyeji. Alikumbuka jinsi alivyotawala sekta zote kama vile uchumi, siasa, elimu na maisha ya jamii kwa jumla. Haya yote yalipojumuika akilini pake kama kumbukumbu alifarijika. Baada ya kumbukumbu hizi mkoloni alimotishwa kurudi kwa mara ya pili barani Afrika, wakati huu kwa kutumia ujanja kama inavyoelezwa hapa:

...Sasa yeye anachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kuwa amefungua njia. Atafute ujanja wowote ule lakini sharti, vyovyote atakavyofanya, afanikishe kupasuliwa kwa huo

utumbo wa ardhi na kukakatuliwa kwa majabali hayo ili kufichua yaliyokuwa ndani. ...Watu husema unaweza kutoka walipo ndovu ukashusha pumzi kumbe unaelekea waliko mbogo (Wamitila, 2014, k. 75-76)

Mapito ya wakoloni wa jadi yaliandaliwa na wamisheni. Nia ya wamisheni hao ilikuwa kueneza dini ya Kikristo. Vivyo hivyo, wakoloni wachache waliobaki barani Afrika wengi wao wakiwa wafanya biashara, walimu na wanasiasa walikuwa na jukumu moja muhimu la kuandaa mapito ya wakoloni wakongwe. Haya ndiyo yanayorejelewa katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* kama “*kufungua njia.*” Msimulizi anazidi kufafanua kuwa Wazungu wakoloni walitumia ujanja ili wapate rasilimali zilizohifadhiwa Afrika kwa ajili ya viwanda vyao kule nyumbani. Katika riwaya msimulizi anasema, “*afanikishe kupasuliwa kwa huo utumbo wa ardhi na kukakatuliwa kwa majabali hayo ili kufichua yaliyokuwa ndani.*” Hii ni taashira inayoendeleza maudhui ya ukoloni. Nia kuu ya wakoloni ilikuwa kutambua utajiri wa madini yaliyofichika ardhini, kuyachimba na kuyasafirisha Ughaibuni ili yatumike katika viwanda vyao. Kwa kutwaa rasilimali za Afrika, wakoloni walichangia katika kufifiza uchumi na maendeleo ya Afrika kama anavyosema Rodney (1981), hali ambayo inashuhudiwa hadi sasa. Katika muktadha huu, riwaya imebainisha historia ya udororaji wa uchumi wa nchi kadha za Afrika. Jina la Pablo Neruda pia linajitokeza katika utunzi wa Wamitila. Mwandishi anatumia sifa ya kimajaribio ya ushairi ambao unaletwa ndani ya simulizi kuu:

Samahani...nilichelewa kujibu. Nilitaka kuopoa kitabu cha ushairi wa Pablo Neruda nilichokiweka mahali fulani. Kwa bahati nimekipata sasa (ni saa sita usiku) baada ya kukisaka siku nzima...kuna maneno aliyoyaandika ambayo japo ni ya kusikitisha, ni mazuri; siku moja utajua uzuri wake. Anasema: Usiku huu natongoa mistari yenye uchungu mno. Kwa kufikiri kuwa sinaye tena, kuhisi kuwa nimempoteza Kuusikia usiku mzito na mnene, mzito na mnene zaidi kwa kuwa sinaye. Yamkini palikuwako na telepathia fulani baina ya sisi wawili (Wamitila, 2011, k. 181-182)

Tanzu za fasihi zimechanganywa ili kubaini kuwa katikati ya machungu tumaini na raha huchipuka. Mhusika Yosi Kanga katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* anaamua kujiliwaza licha ya maumivu anayopitia kwa kusoma mashairi yaliyotungwa na mwandishi mashuhuri wa Chile, Pablo Neruda. Ndani ya fasihi mna ushairi unaoliwaza waja wanapojipata katika hali ngumu. Uandishi wa Pablo Neruda ni wa pekee kama asemavyo mwandishi. Hadhira ya matini za kifasihi inahimizwa kwamba ndani ya fasihi kuna matumaini. Japo hali wanazopitia wanadamu ni chungu na za kukatisha tamaa, mwishoni kuna matumaini ya kuishi tena. Ni

dhahiri kuwa taabu na raha zote hupatikana duniani na humkumba binadamu. Kupitia kwa neno "telepathia" mhusika anaeleza jinsi anavyojinasibisha na Pablo Neruda. Katika mazungumzo haya, inadhihirika kuwa fasihi ina uwezo wa kubaini mawazo, nia na fikra za wengine. Baada ya kuyasoma mawazo ya wanajamii, inapendekeza mbinu za kuwakomboa kutokana na hali zinazowakosesha amani na raha.

Wamitila ametumia jina giza kwa wingi katika riwaya zake. Giza ni hali ya ukosefu wa mwangaza au nuru. Palipo na giza binadamu hawezi kuona mbele. Katika Karne ya Kumi na Tisa nchi za Afrika zilivamiwa na kutawaliwa wa Wazungu waliotoka katika nchi mbalimbali za Ulaya (Pakenham, 1992). Wazungu hao waliazimia "kuwastaarabisha" Waafrika kwa madai kwamba Waafrika waliishi gizani. Madai haya yanaafikiana na kile mwandishi anachotaja katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* kwamba;

“Akakumbuka hata visa alivyofundisha mwenyewe alipokuwa shuleni: kule “giza” linatamalaki; wenyeji na wala watu” (Wamitila, 2014, uk. 49)

Katika nukuu hili bara la Afrika linapewa jina giza. Linaitwa bara lenye “wenyeji wala watu”. Katika enzi za ukoloni nchi za Afrika hazikuwa na maendeleo kama walivyodai wakoloni (Pakenham, 1992). Dhana *giza* imetumika kama taashira kuikumbusha hadhira sura ya Afrika kabla ya majilio ya Wazungu. Wazungu wakoloni walidai kuwa walikuja Afrika ili kuwaondoa wenyeji katika hiyo giza. Mwandishi kwa kutumia mbinu za kimajaribio anaichorea hadhira yake taswira ya Afrika kabla ya utawala wa kikoloni. Hata hivyo, Waafrika wenyewe waliridhika na kufurahia jinsi walivyoishi hata ingawa Wazungu waliwaona wakiwa gizani. Hali hii inawiana na hali ya mhusika Yosi Kanga wa riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* alipokuwa hospitalini akiganga ugonjwa ambao haukuelewika machoni na akilini pake. Ni dhahiri kwamba kuwa giza ni hali inayotetemeshwa na kutamausha kama katika nukuu hili:

Nilihisi kitetemeshi fulani mwilini kisha vimulimuli vya machoni vilivyonifanya nione taswira za vipopeo katika giza la macho yangu yaliyofungwa. Kwenye giza la macho yangu, nilijaribu kutafuta kama ningeweza kupekuapekua na *kupekenyua* hapa na pale na kufichua yaliyojificha hayo maisha yaliyocheza mwajificho nami na labda niyacheke kama tulivyofanya zamani nilipocheza mwajificho na vijana wenzangu. Nilitamani kuyaona kwenye giza hilio, labda kwa kuona macho yake yanayoangaza gizani kama macho ya paka yaliyopigwa na mwanga wa kurunzi, na kuyauliza msururu wa maswali niliyokuwa nayo (Wamitila, 2011, k. 32-33)

Wafrika walipigana na wakapata uhuru kutokana na minyororo ya ukoloni. Hata hivyo, inabainika kuwa bado wanaishi gizani. Baadhi ya mambo yanayoonyesha kuwepo kwa giza katika mataifa ya Afrika ni ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana, ufisadi, magonjwa yasiyo tiba, matumizi ya mihadarati na ukosefu wa usalama. Taswira ya jamii ya leo ambayo mwandishi anaangazia ni kuwa, “*wenyeji ni wala watu*”. Hii ni kwa sababu maovu yanayoirudisha Afrika nyuma yanaendelezwa na wenyeji wenyewe. Ufisadi unaoendelezwa na viongozi ni mfano mzuri wa ulaji. Neno “*ulaji*” laweza kurejelea vitendo vinavyosababisha dhuluma, maumivu na machungu kwa raia. Kwa sababu hii, wananchi hawawezi kuona mbele wala kuubashiri mustakabali wao wala wa nchi zao. Matatizo anayoyapitia Yosi Kanga mikononi mwa daktari aliyejigamba kuwa alisoma sana tena katika shule tajika ni aina ya giza. Ni hali inayomtamausha kabisa. Baada ya kulazwa hospitalini akiwa katika hali mahututi, Yosi Kanga hapati huduma zozote za kimatibabu. Anapewa habari baadaye na daktari kuwa alikuwa na siku chache za kuishi licha ya kitofanyiwa uchunguzi wote katika maabara. Giza linazidishwa na kuwepo kwa madaktari ghushi katika mataifa yanayoendelea.

Nchi ya Kenya ambamo mwandishi wa kisasa anaandikia ilinyakua uhuru mnamo mwaka wa 1963 (Waller, 2014). Baada ya kuanza kujitawala ilikuwa ni jukumu la Wakenya wenyewe kupitia kwa viongozi wao wapya kuboresha hali zao za maisha. Baadhi ya matatizo waliyokabiliana nayo ni magojwa, umasikini na ukosefu wa kusoma na kuandika. Hata hivyo, chini ya uongozi mpya ulioshika hatamu wakati huo, viongozi waliweka ahadi ya kuboresha hali ya maisha ya Wakenya. Dayolojia ifuatayo inarejelea majukumu ya kiongozi huyo mpya ambayo yakizingatiwa yataitoa taifa kwenye giza.

Awaongoze kuhakikisha kuwa *kimbunga cha ufukara* kinachopiga *hakiupukuti majani mti wa ustawi wa jamii yao*. Awaongoze kuhakikisha kuwa hayo maarifa mapya aliyoyapata yamesambazwa kijijini. La nchi nzima. La Bara zima. Si ana ujuzi wa kutosha? Si anazijua siri na jadi yao? Si anaujua ujanja wa rafiki yake aliyeondoka? (Wamitila, 2014, uk. 51)

Jina “*kimbunga cha ufukara*” limetumika tena pamoja na neno giza katika simulizi hii kwa lengo la kurejelea umasikini uliokithiri. Kimbunga ni upepo mkali unaovuma kwa nguvu na kusambaa haraka. Wakati mwingine nguvu zake huharibu mali na kuhatarisha maisha ya binadamu. Mwandishi anaendelea kusema katika sentensi hiyo hiyo, “*hakiupukuti majani mti wa ustawi wa jamii yao*”. Giza linapoendelea kutamalaki katika nchi, kuna hatari ya kuwepo kwa

umasikini mkubwa ambao huwakumba wengi. Hali hii huwakosesha wenyeji matumaini ya kuendelea kuishi. Kwa jumla kupitia kwa taashira hii ya giza riwaya zinaitaka hadhira lengwa ifahamu kuwa umasikini ni kikwazo kikubwa cha ustawi wa jamii. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa suluhu la kuondoa giza hupatikana miongoni mwa wananchi au wanajamii wenyewe. Wanahitaji kufahamu kwamba giza lina mwisho wala haliwezi kudumu milele. Aidha, wenye ujasiri wanaweza kukabiliana na giza lolote lile. Isitoshe, utafiti umeibua hoja muhimu kwamba tumaini la jamii litapatikana katika kizazi kipya. Kizazi chenyewe kinahimizwa kuchukua nafasi yake katika kulisafisha taifa. Inabainika katika riwaya teule ya *Musaleo!* kwamba;

“Sasa vuka mto huu wewe na kijana. Mimi sasa siwezi, anayeweza ni Mamanchi na Kijana. Ng’ambo ya pili kuna njia inayopita karibu na mapango. Sehemu yenyewe in giza lakini usiogope. Hakuna giza lisilochewa” (Wamitila, 2004, uk. 128)

Atakayeliyondoa taifa na jamii ya sasa kutoka kwenye kilindi cha usumbufu ni mwanajamii mwenyewe. Japo kutakuwa na vikwazo vingi, bidii na ujasiri vitamwezesha kuleta tumaini jipya na tabasamu. Kwa kusema, “*hakuna giza lisilochewa*”, mwandishi anadhihirisha kwamba hakuna tatizo lisilokuwa na mwisho. Dhuluma, madhila na shida zote katika jamii ya sasa ni nyingi na zinaumiza hisia, nafsi na mioyo lakini zina mwisho. Kwa maneno haya mwandishi anaipa jamii ya sasa tumaini la kupata maisha mazri mradi iwe na ujasiri wa kukabiliana na hali zinazoidhulumu kwa lengo la kupata suluhu la kudumu. Zaidi ya haya, ni dhahiri kwamba kuna ng’ambo ya pili iliyojawa na furaha ambayo kila mwanajamii anafaa kuitazamia kama inavyodhihirishwa na maandishi haya:

Iliendelea kuwaka bila ya kuzimwa na kunikumbusha mwanamume mmoja wa kijijini ambaye alipokuwa akitoka kwenye soko la karibu, alikotoka takriban saa nne au tano za usiku kila siku, alikuwa na mazoea ya kuiwasha kurunzi yake njia nzima kwa sababu ya kuliogopa giza – walivyosema watu (Wamitila, 2011, uk. 74)

Muktadha wa usemi ulionukuliwa ni wakati fulani baada ya kifo cha mhusika Mukangu katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* aliyekuwa amelazwa katika hospitali ya *City Breeze* pamoja na Yosi Kanga. Msimulizi anaeleza kuwa hata baada ya kifo chake, taa iliyokuwa katika kitanda chake iliachwa ikiwaka. Licha ya ukweli kuwa giza lilitanda katika ulimwengu wake na wa jamii yake, mwangaza wa kurunzi unaotajwa ni ishara ya matumaini ya baadaye. Mwandishi anaeleza kuwa taa iliyowaka bila kuzimwa ilimkumbusha Yosi Kanga kuhusu mwanamume mmoja huko kijijini kwao ambaye daima kila alipotembea usiku aliwasha kurunzi kwa sababu ya

kuliogopa giza. Ni dhahiri kwamba giza huogofya. Penye giza watu hawawezi kutembea wakiwa huru. Suluhu ya giza yake ni kurunzi iliyokuwa daima mkononi mwake. Vivyo hivyo, suluhu la matatizo yaliyo katika jamii ya sasa li mikononi mwa wanajamii wenyewe. Ni juhudi watakozifanya wenyewe zitakazowaondoa katika majanga yanayowakumba. Wanajamii wanatahadharishwa dhidi ya kuyategemea mataifa mengine kwa minajili ya kuondoa giza katika maisha yao. Mwanamume anayerejelewa katika simulizi hii alihakikisha kuwa kamwe kurunzi yake haikutoka mkononi ili kuliondoa giza lililotanda katika njia aliyopita. Mwangaza ni taashira ya tumaini. Japo mwanajamii wa sasa anapitia katika hali ngumu inayomzuia kubashiri mustakabali wake, anahimizwa kukazana kushikilia ukweli anaoujua ili kufaulu maishani. Mwangaza ni ishara kwamba japo mambo yamekuwa mabaya sana (kama giza) kwa muda mrefu, kuna matumaini ya msaada, fanaka na furaha baada ya kipindi hicho kirefu cha mateso. Haya yanabainika kama inavyodokezwa katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* kwamba;

“Kwanza sikuweza kukiona chochote akilini isipokuwa giza jeusi tititi lililokuwa na taswira zilizochezacheza tamthili ya kivuli wakati wa mbalamwezi” (Wamitila, 2011, uk. 185)

Ni kweli kuwa mwanzoni giza linapotanda maishani hapaonekani tumaini lolote lakini katikati ya giza hilo, mna suluhu. Hata hivyo, ifahamike kwamba zoezi la kutafuta tumaini maishani ni jambo linalohitaji juhudi kubwa kutoka kwa wahusika yaani wanajamii wenyewe. Wakati mwingine, kadri binadamu anavyojikaza kukabiliana na giza, hali inaweza kudhoofika na kuwa mbaya zaidi. La muhimu ni uvumilivu na kusonga mbele. Istilahi ya giza imetumika katika katika riwaya ya *Musaleo!* kubaini zaidi umuhimu wa kila mwanajamii kutafuta suluhu ya matatizo yanayompata. Msimulizi wa *Musaleo!* anasema;

“Ilivyoelekea kadiri nilivyojikaza ndivyo nilivyozama katika kiini cha lile giza. ...lile giza lilipunguapungua ikawa naweza kuona japo kwa shida” (Wamitila, 2004, uk. 52)

Giza la matatizo linapozama zaidi, waja wanashauriwa kutokata tamaa. Imebainika kuwa kunazo hatua mbalimbali za kujiondoa gizani. Hatua ya kwanza ni kutambua tatizo aina ya giza inayomkumba mtu kisha kufahamu kwamba suluhu yake i mikononi mwake. Hatua ya mwisho ni kusonga mbele na kutokata tamaa hata wakati ambapo mwanga hujaangaza vizuri. Mwandishi anasema, ....*giza lilipunguapungua ikawa naweza kuona japo kwa shida* kumaanisha kuwa hali ya kutoona alipokuwa akielekea ilikuwapo lakini alichagua kuvumilia na hatimaye kufaulu



kuitimiza ndoto yake hadi aitimize. Hivyo, kizazi cha leo kinahimizwa kuwa penye nia pana njia. Licha ya ugumu unaoweza kupatikana, siri ya kufaulu ni kutokata tamaa na bidii kama inavyobainika katika maneno ya mhusika Musaleo katika *Musaleo!*;

“Nilishindwa kuyafungua lakini sikutaka kuishi katika giza. Nilijitahidi kuyafungua”  
(Wamitila, 2004, uk. 130)

Ni dhahiri kwamba juhudi za mwanadamu zina uwezo wa kumtoa katika giza lolote linalomkabili. Riwaya za kisasa zinatoa himizo kwa hadhira au msikilizaji wake kwamba anapotembea katika ulimwengu wenye dhiki nyingi ahakikishe kuwa ameyafungua masikio yake ili asikie mambo muhimu yatakayomfaa katika safari yake ya kutafuta ukombozi. Mahali ambapo anatembelea pamepewa jina la “*ng’ambo ya pili*”. Mwandishi anasema kuwa ni karibu na mapango na sehemu yenyewe ina giza ila asiwe na hofu. Alipokuwa akiendelea na safari, jua la tumaini liliwaka na kumfanya ajihisi kuwa mwenye nguvu mpya. Alikusanya nguvu zake zote na kuanza kukimbia. Mara kwa mara alianguka kwa kishindo akajaribu kuinuka akashindwa. Macho yalifungika akashindwa kuyafungua. Kwa sababu hakutaka kuishi katika matatizo haya milele alijitahidi kuyafungua macho yake na kuendelea na safari. Jamii ya sasa inabainishiwa kuwa hakuna shida ambayo inadumu milele. Mwangaza wa furaha na tumaini hupatikana panapo bidii zisizotamauka. Hata hivyo, ni wakati ule ambapo punda anapoamua kuyatua masogi yake ya giza. Kwa mujibu wa riwaya teule juhudi za kujitoa kwenye giza zinazidi kubainika zaidi kama ifuatavyo:

Akaufungua na kuangalia nyuma kisha, kama mwigizaji wa filamu, filamu inapokaribia mwisho, akaanza kutembea na kumwonyesha Rama Payo mgongo wake. Akajihisi kama hadhira iliyokuwa ikimwangalia mwigizaji wake akipotelea upande wa pili. Payo akakumbuka wimbi kubwa lililokuwa linaanza kuumuka nchini. Hatimaye punda naye ameelekea kuchoshwa na masogi ya miaka. Aliangalia mbele huko na kuona giza totoro. Akajiwa na taswira ya mti mkubwa uliokatwa na kuanguka chini kwa kishindo. Ile methali ya Kiswahili ya mti mkuu ukigwa, ndege wa mashakani ikamjia. Kisha akasikia sauti za watu wengi waliokuwa wanalia. Wengine wanacheka. Akashangaa hicho kilio cha kicheko kilikuwa na maana gani?” (Wamitila, 2004, uk. 148)

Giza linalorejelewa linaendelezwa na viongozi dhidi ya wananchi. Riwaya inawachorea wasomaji taswira ya wanajamii ambao wamechoshwa na masogi ya usumbufu waliyoyabeba miaka na mikaka. Istilahi “masogi” ni taashira ambayo imetumiwa kuashiria mateso na madhila wanayoyapata wanajamii kutoka kwa wenye mamlaka ambao wanaongozwa na tamaa. Kwa

kuwa ni wanadamu pekee walio na suluhu ya matatizo yanayozikumba jamii zao imebainika kwamba panahitajika kufanywa uamuzi wa kuandaa mageuzi yenye lengo la ukombozi. Mageuzi yanaamuliwa lakini unapofika wakati wenyewe wanajamii wanakosa motisha ya kuendelea kwa sababu ya kukosa kiongozi mwafaka. Wanajamii wakitazama mustakabali wao wanaona giza totoro, yaani hamna tumaini lolote la kufanikiwa. Methali, “**mti mkuu ukigwa, ndege wa mashakani**” kuashiria kwamba ukosefu wa viongozi wanaowajibika umeifanya jamii kukumbwa na shida kubwa ya. Tegemeo la jamii ni kuelekezwa vizuri. Haya yanapokoseka katika jamii yoyote mlango wa mahangaiko hufunguliwa na kuathiri jamii vibaya. Kwa sababu hii wanajamii hawana uhakika kwamba wakianza watafaulu kwani giza la jana bado linazidi kuenea.

Jina lililojitokeza kwa mapana na marefu katika ubunifu wa mwandishi Wamitila ni kifo. Kifo ni mwisho wa uhai (Blum, 2004). Kifo hutokana na sababu aina aina kama vile, umri mkubwa unaosababisha michakato ya kimsingi mwilini kusimama polepole na ajali zinazoharibu viungo muhimu mwilini. Mambo mengine yanayosababisha kifo ni pamoja na ukosefu wa chakula, maji, hewa au kinga dhidi ya mazingira magumu, athari haribifu kutoka kwa viumbe wengine au mazingira (Mullin, 2008). Vilevile, kifo hutokea ikiwa binadamu amekuwa na muda mrefu wa maisha unaoruhusu makosa na kasoro kujumuika na kusababisha madhara kama saratani na magonjwa mbalimbali yanayovuruga michakato ya uhai hadi kuyasimamisha maisha (Gilbert, 2003). Kifo hutamausha zaidi kwa sababu hakuna kinachobaki baada ya mauti (Yuswanto, 2015). Ni mwisho wa binadamu kimwili na kiroho. Kifo kimefananishwa na mgeni mwenye wivu mwingi anayetembea katika nchi ng’eni. Ni mgeni mwenye wivu kwa sababu huchukua kile kilichonawiri na kinachotegemewa na jamii pamoja na taifa.

Katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi*, kifo kilikuwa kikimkodolea macho mhusika Yosi ambaye kwa wakati huo alikuwa katika umri wa makamo. Alikuwa kijana barubaru aliyetegemewa sana kazini mwake na katika taifa lake kwa jumla. Yosi alipata ugonjwa uliodaiwa kutokuwa na tiba mara tu baada ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwake ya kutimu umri wa miaka thelathini na minne. Imedhihirika kuwa kifo humchukua mtu wakati anapohitajika zaidi na familia pamoja na taifa. Kwa mujibu wa riwaya, jamii ya sasa imeathiriwa na vifo vya aina aina vinavyoletwa na mambo mbali mbali. Mambo hayo ni pamoja na dhuluma, ubinafsi, uzorotaji wa uchumi na uhasama wa kikabila. Maafa haya yote yamesababishwa na

uongozi mbaya. Yanatishia kuziangamiza jamii za Kiafrika za kisasa wakati zinapohitajika zaidi. Mwandishi anafananisha vifo hivi na mtu anayejizungukia huku na kule. Anapoonna mlango wowote ulio wazi anajitoma ndani ghafla na kuwanyakua waliomo. Kulingana na riwaya, jamii ya sasa ndiyo inayochangia katika maangamizi yake kwa kufungua milango yake kwa yeyote anayetaka kuingia. Kando na haya mwandishi anaitaka jamii iweke mikakati kabambe kuhusu uwekezaji katika mataifa husika bila kuwategemea wageni wasioaminika. Haya yanabainishwa na usemi kwamba:

Mizizi ya mti wa uwezo wangu alikuwa anaanza kuitafuna chini kwa chini kama fuko. Ilibidi niwahi tumba la uovu kabla halijachanua na kutapakaza harufu ya uhasama nchi nzima. Wiki tatu baadaye profesa alikufa katika ajali ya barabarani. Niliongoza nchi nzima katika maombolezi ya kifo hicho. Jamaa zake niliwaahidi kuwasaidia. “Ikiwapata shida yoyote, nipigieni simu tu!” niliwakumbusha (Wamitila, 2004, uk. 69)

Katika ulimwengu wa usomi Profesa ni binadamu aliyesoma kwa mapana na marefu. Ana ufahamu wa mambo anuwai tena kwa undani. Kwa mujibu wa Nyabunga (2005), Profesa anaona yale wengine wasiyoyaona. Profesa anayerejelewa katika nukuu hii alifanya utafiti kuhusu kisa cha Mamanchi; mama mmoja aliyedaiwa kuwa dadake kiongozi wa taifa wakati huo aliyefahamika kwa jina la Mzee. Matokeo ya utafiti huo hayakuufurahisha uongozi wakati huo. Baada ya wiki tatu Profesa alifariki katika ajali ya barabarani iliyokuwa tatanishi. Mzee aliliongoza taifa katika maombolezi na mazishi ya Profesa. Katika hotuba yake wakati wa mazishi, Mzee alieleza jinsi kifo cha Profesa kilivyoacha pengo kubwa ambalo halingezibika. Kama ilivyo kawaida ya viongozi wa kisasa, Mzee aliongeza kuahidi kuisaidia jamaa ya Profesa kwa vyovyote vile.

Imebainika kuwa watu werevu ambao wanaona yasiyoonekana na wengine hawatakikani katika jamii. Labda ung’amuzi huu unaeleza jinsi wasomi kama Profesa hutoweka katika hali zisizoelezeka kila wanapoonyesha uzoefu wao wa ujuzi. Katika simulizi fupi iliyotumiwa na mwandishi wa riwaya ya *Musaleo!*, taswira tofauti tofauti za jamii ya kisasa zimebainika katika matumizi ya taashira *kuitafuna nchi kama fuko*” na *“tumba la uovu”*. Kwanza, katika jamii ya kisasa viongozi huwahofia watu wenye akili nyingi yaani wasomi kwa sababu wana uwezo wa kuweka hadharani mambo yafanywayo sirini hasa katika ngazi za uongozi. Pili, watu hao wenye ujuzi na wanaotegemewa katika jamii wanapofariki, daima viongozi hao hao huonyesha unafiki

wao hadharani kwa kutoa ahadi ambazo hatimaye hutokea kuwa za uongo. Tatu, binadamu mwenye ujuzi katika mataifa yanayoendelea hana haki ya kuishi; uhai wake humtoka kwa njia tatanishi. Kwa hivyo, inabainika kuwa Profesa hangeishi kwa sababu ya ufahamu wake kuhusu mambo mbalimbali yaliyoikumba jamii yake; kwake kuyasema hadharani kulikuwa kama kujitia kitanzi. Baada ya mazishi ya mhusika ahadi za viongozi hubakia kuwa ahadi tu. Nne, hakuna kiongozi yeyote anayetaka kuambiwa ukweli kuhusu jinsi anavyotekeleza kazi yake hasa pale anapofanya makosa. Matukio yaliyotajwa yanaashiria ukosefu wa uhai katika usomi na maendeleo katika jamii.

Vilevile, athari za utandaridhi zinatishia kusababisha kifo na kuiangamiza Afrika kila uchao (Nyabunga, 2005). Hii ni kwa sababu ya kuwepo kwa ukoloni mkongwe unaowakilishwa na jina “Ukolongwe” Ukweli huu unabainishwa na usemi ufuatayo unaopatikana katika riwaya ya *Musaleo!* Kwamba;

“Nilisema kuwa Ukolongwe hakuzikwa: tazama kaburi lake bado li wazi. Niliwaambia wasiojifunza kutokana na historia wamelaaniwa kuyarudia makosa ya jana: makosa ya historia yenyewe!” (Wamitila, 2004, uk. 70)

Mtu anapokufa na kuzikwa huanza kusahaulika pole pole. Mazishi huashiria mwisho wake, uwepo wake, kazi zake, na athari zake. Ukolongwe ni lakabu iliyotumiwa kuashiria ukoloni-mkongwe. Kwa mujibu wa riwaya teule jina jingine la ukoloni-mkongwe ni ukoloni mamboleo. Jina hili limetumika kurejelea tabia ya nchi tajiri zilizoendelea kuingilia maswala ya nchi zinazoendelea hata baada ya nchi hizo kupigana na kujipatia uhuru (Barongo, 1980). Hata hivyo, tabia hii ni kinyume cha azimio la Umoja wa Mataifa (Birmingham, 1995). Kwa mujibu wa riwaya ya *Musaleo!* ukoloni wa aina hii unawakilishwa na athari hasi kama inavyobainishwa na Suret-Canale (1988) kwamba wafanya biashara binafsi na makampuni ya biashara za kigeni huendelea kunyonya rasilimali za mataifa yanayoendelea muda mrefu baada ya enzi za ukoloni. Ndio maana mwandishi anasema kwamba mhusika Ukolongwe hakuzikwa na hata kama alizikwa kaburi lake li wazi. Katika riwaya hii mwandishi ameitumia lakabu hii kumaanisha kuwa athari za ukoloni zingali hai katika mataifa ya Afrika yanayoendelea hata baada ya kujipatia uhuru. Hata hivyo, Afrika inajuzwa kwamba iwapo inaazimia kupiga hatua mbele kimaendeleo ni lazima isahau “jana” yake. Ni sharti itupitilie mbali historia dhalimu na kukumbatia nguvu na uwezo wake kama mataifa huru. Haya yatawezekana ikiwa Waafrika

watatambua kuwa wako usingizini na sharti wafahamu kwamba wao wenyewe ndio wenye uwezo wa kujitoa katika usingizi huo.

“...Nilimwonya akakataa. Ilikuwa lazima siku moja atafanya jambo la kumuudhi Mzee!” alitulia kisha akaendelea kama mtu anayejisemea, “Nilisema yule ni kizalia cha Ukolongwe wakakataa! Sasa wanayaona haya! Watu wanalala kwa miaka na miaka, usingizi wa aina gani huu?” (Wamitila, 2004, uk. 71)

Simulizi fupi iliyotumika imefanikishwa na uzungumzi nafsia unaoambatanishwa na maswali ya balagha. Jina Mzee limetumiwa kuashiria kiongozi. Riwaya zimebaini kwamba kiongozi yeyote anayeendeleza dhuluma ni kizalia cha Ukolongwe. Athari za ukoloni mkongwe ndizo zinazomfanya mkoloni kuendeleza ukoloni baada ya uhuru hali maarufu kama ukoloni-mamboleo. Kwa mujibu wa riwaya za kisasa athari hizi zinajitokeza katika tabia kama ubinafsi, wizi wa mali ya umma, uchafuzi wa mazingira na unyanyasaji. Wanaoiba mali ya umma wanafanya hivyo kwa kisingizio kwamba kila mtu nchini ni mwizi. Ujumbe kwamba adui ya Mwafrika ni Mwafrika mwenyewe unarejelewa tena. Jamii ya sasa imejawa na unafiki na uongo. Wanaosema uongo wanajionyesha kama wakweli. Kwa sababu hii, jamii ya leo imekumbwa na mateso mikononi mwa viongozi wake. Aidha, mwandishi anabainisha mtazamo wa kiuhalisia hakiki wa kimaksi ambapo tatizo hubainishwa na kuachwa bila kupendekezewa hatua za kulitafutia suluhisho. Kutokana na riwaya ya *Musaleo!* inabainika kupitia kwa majina **mashamba ya mawe** na *guillotine* kuwa:

Unajua siri ya Mashamba ya Mawe?” Nikoseje? Utahusika katika kukiandaa kitu kisha usikikumbuke? Sikuhitaji maelezo zaidi. Profesa: Ikawa kama kisa Joseph Guillotin aliyevumbua *guillotine* na kuishia kuuliwa nayo! Ngwena: Hasa! Ndiyo siri ya msumeno kukata huku na huku! Profesa: Ndiyo siri ya neno pia! Ngwena: Ni kweli (Wamitila, 2004, uk. 102)

Majina ya “Mashamba ya Mawe” na “Joseph Guillotin” ambayo ni majina ya mahali na mtu mtawalia yametumiwa katika riwaya ya *Musaleo!* kama kunga ya kuwasilishia ujumbe. Usimulizi huu umechukua mkondo wa dayolojia. Mazungumzo baina ya wahusika Ngwena na Profesa yanarejelea mambo mengi kwa pamoja. Kwanza, yanahusu kile mwandishi anachokifahamu kama *Mashamba ya Mawe*. Kwa mujibu wa riwaya hakuna kitu kinachomea na kunawiri katika mashamba ya mawe, hivyo hamna uzalishaji. Hali ya ugumu wa maisha katika mataifa ya Afrika yanayoendelea hutokana na ukosefu wa uzalishaji, jambo linaloanzishwa na

viongozi dhalimu wasiojali. Pili, Joseph Guillotin alikuwa mwanzilishi wa njia rahisi ya kuwaua wahalifu waliopewa hukumu ya kifo. Mbinu aliyopendekeza ilipewa jina lake, yaani *guillotine*. Baadaye, Joseph mwenyewe aliuliwa kwa njia aliyoibuni mwenyewe. Mazungumzo haya yanaashiria ukweli fulani kuhusu maisha. Kuna ukweli kuwa mchimba kisima huingia mwenyewe. Mtu akiwapangia wengine mabaya huenda mabaya hayo yakampata yeye mwenyewe. Papo hapo, mwandishi amefananisha ukweli wa maisha na msumeno unaokata mbele na nyuma. Hali kwamba yale yanayopatikana katika jamii yawe mabaya au mazuri yameletwa na wanajamii wenyewe na athari zake ni kwa wanajamii hao hao inazidi kubainika. Huu ukoloni mkongwe ulianza vipi? Swali hili linajibiwa na simulizi fupi kadhaa zinazotumia jina “Ukolongwe” ambalo ni jina lililobuniwa na mwandishi kuwakilisha uongozi wa Kimagharibi. Aidha, simulizi fupi hii inayoendelezwa na dayolojia inaongeza kwamba:

Hiyo ni kauli ya ukweli, walisema wengine walimsamehe, “Ni mtoto huyu, hajui alisemalo, mwacheni tu!”...Miaka michache baadaye jamaa za Ukolongwe walifuatia. Ukolongwe alitumia nafasi yake kuwatafutia ardhi ya kulima. Alishatambua wapi palikuwa na ardhi nzuri na wapi mbaya. ...Ukolongwe alitumia ujanja wake. Ardhi yote iliyokuwa na rutuba aliichukua na kuwakabidhi jamaa zake hao. ...Ardhi ambayo wenyeji hawakuwa wameitumia kutokana na mfumo wao ilichukuliwa na Ukolongwe na jamaa zake na kubatizwa ‘Ardhi haribifu’. Ndugu zake nao lazima walikuwa wazembe: walishindwa kuyalima mashamba makubwa waliyoibiwa na mwenzao. Walihitaji vibarua. Walimwendea Ukolongwe. “Mzee hatuna njia ya kuilima migunda hii;tunahitaji wasaidizi. Wajua tena mikono yetu laini, imezoea kalamu bwana, sio kupambana na magugu ya huku magumu kama natives wenyewe!” walisema.” (Wamitila, 2004, uk. 36)

Hii ni aina ya simulizi fupi yenye dayolojia kati ya mhusika Mzee na raia katika riwaya ya *Musaleo!* ambapo msimulizi anaangazia msururu wa vitushi vilivyowapelekea Waafrika kunyang'anywa mashamba yao na Wazungu katika kipindi cha kihistoria cha ukoloni. Usimulizi unaendelea kwamba baada ya Wazungu kufika Afrika walijinasibisha na sehemu za ardhi zilizokuwa na rutuba kwa haraka. Kilichofuatia ni kwamba wakoloni hao waliwaalika wenzao waliokuja kwa wingi. Kwa kuwa hawakuzoea kufanya kazi ngumu za shambani, walihitaji wafanyakazi kutoka kwa wenyeji. Hivyo ndivyo walivyowageuza wenyeji kuwa watumwa, yaani wafanyakazi katika mashamba yao. Mintarafu ya simulizi hii, ni bayana kwamba jamii ya kisasa ina udhaifu wa kuwakaribisha kila aina ya wageni katika nchi zao. Wageni hao wanakuja “kwa majina” ya kustaarabisha, kuelimisha na kuendeleza.” Tahadhari inatolewa kwa njia ya

kimajaribio kuwa jamii inafaa kuwa angalifu isije ikajipata katika hali tatanishi. Ufafanuzi zaidi umetolewa kwa maneno haya:

Alipokuja huku aliwapendekezea wenyeji njia mpya za kutafutia maarifa na kujifundisha mageni. Watu walisusia kwa kusema kuwa walikuwa na njia zao za jadi zilizowafaa kwa miaka na dahari. Walimtajia baadhi kama jando, unyago, miviga na ngomezi. Ilibidi atafute njia nyingine ya kuwavuta. Kuna kisa kinachosemwa na watu wengi kuwa hata alijaribu kuwavuta kwa kuwaonjesha sukari. Wazee hawakuwa na hamu ya mambo mageni tena. umri wao ulikuwa unaelekea machweo lakini waliamua kuwatuma watoto wao kwenye vituo vya jamaa za Ukolongwe (Wamitila, 2004, uk. 41)

Jamii ya leo inashawishiwa kwamba japo si tamaduni na desturi zote za Kiafrika zinazokubalika, ni muhimu kukumbatia desturi zinazokubalika ili kukuza utangamano badala ya kuiga ya wageni. Elimu ya kizungu (Ukolongwe) iliwasaidia Waafrika kustaarabika. Hata hivyo, ni bayana kwamba ustaarabu huo ndio uliokuwa chanzo cha mafarakano na utabaka unaoshuhudiwa katika mataifa ya Afrika yanayoendelea hivi leo. Kwa jumla, ukweli ni kwamba kizazi cha leo kinapenda kuiga na kupokea ya wageni hata kabla ya kupima athari zake. Ni dhahiri shahiri kuwa ukoloni uliingia Afrika kwa ujanja mwingi. Wazungu wakoloni walitumia mbinu mbalimbali za kuzipenyeza tamaduni zao kwa wenyeji wa Afrika. Waafrika walikataa tamaduni hizo mpya wakidai kwamba walikuwa na tamaduni zao binafsi walizoenzi kama jando, unyago, miviga na ngomezi (Nanjira, 2010). Haya ndiyo mambo yaliyowaleta pamoja. Kwa Wazungu hizi ni tamaduni zilizopitwa na wakati. Hata hivyo, Waafrika walikataa kushawishika kuacha mila, desturi na tamaduni zao. Kwa kuwa anayetaka hachoki na akichoka keshapata, wakoloni walizua mbinu nyingine za kuendeleza ujanja wao. Walizindua masomo rasmi ili kuwazindua Waafrika (Smith, 1995).

Wakoloni walijaribu kutumia hila ya kuwaonjesha Waafrika sukari kupitia kwa zile pipi walizokuwa wakiwapa watoto shuleni. Baada ya kuwepo kwa pingamizi nyingi mwishowe Wazungu walifaulu. Yote waliyokusudia kuwaletea wenyeji Waafrika yalikubalika kwa wanajamii wote. Masomo shuleni yalianza kwa kasi. Kwa kuwa wazee walikuwa wameshapitisha umri wa kwenda shuleni, waliwatuma wanao. Vituo vya masomo ya kizungu hali maarufu shule vilijengwa na kufurika wana wa Kiafrika. Kupitia shule hizi, elimu ya kizungu ilienezwa na ikawapa wakoloni fursa ya kuathiri hisia za Waafrika. Ukoloni ulipoumiza sana Waafrika walipigania uhuru wao lakini ukweli ni kwamba bado upo. Wakoloni wenyewe

wanaweza kukosa kuonekana lakini athari za ukoloni zinadhihirika katika maswala mbalimbali kama uongozi, elimu na uchumi. Riwaya za kimajaribio zilizochanganuliwa katika utafiti huu zimebainisha kuwa ni muhimu kuiga yanayoendeleza taifa na kwa upande mwingine kusuta yale yasiyofaa. Maswali yanayojitokeza ni; wageni wataendelea kuyatembelea mataifa ya Afrika? Je, Waafrika wataiga kila mmoja wao? Msimulizi katika hadithi ya *Musaleo!* anabaini kuwa baada ya Ukolongwe kuondoka na uhuru ukapatikana Afrika iliendelea kupata wageni wengine ambao hawakuwa tofauti. Shauku yao kubwa kama ilivyokuwa ya Wazungu ilikuwa ni kujitajirisha kwa kutumia rasilimali za Afrika. Jina Ukolongwe aidha lilirejelea wageni wote walioingia Afrika kwa lengo la kujijenga na kujitajirisha kama katika usemi huu;

“Miaka yoyote kulikuwa na jamii nyingine ya Wahindi iliyokuwa inanza kukua. Jinsi walivyokuja ni mchezo kama ule wa Ukolongwe tu!” (Wamitila, 2004, uk. 48)

Hivi ni kumaanisha kwamba hakuna wakati watu wataishi katika mabara yao bila kutembea katika mabara mengine. La muhimu ni wenyeji kujifahamisha kuhusu mipaka yao kielimu, kisayansi, kiteknolojia, kijamii, kiuchumi na nyanja zote zinazohusika katika ujenzi wa taifa lenye nguvu. Hii ndiyo njia ya pekee ya kujiepusha na kifo. Aidha, kuna matumizi ya jina “kimbunga” katika riwaya teule. Hali mpya inayotarajiwa katika jamii inafananishwa na upepo mkali (kimbunga) uvumao kwa nguvu nyingi kama inavyosemwa katika riwaya teule ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* kwamba;

“Kimbunga cha hali mpya kilimzoa kila mtu kama ubua na kumpeperusha pepetu kwenye anga za ndoto; anga za Alinacha” (Wamitila, 2014, uk. 73)

Jina upepo mkali, ni taashira inayobainisha jinsi mabadiliko yanayotarajiwa na jamii yatakuja kwa kasi na nguvu nyingi. Hata hivyo, iwapo mabadiliko hayo yatakuwa ya kudumu ni sharti jamii ifahamau kwamba hayatajileta yenyewe. Itawabidi wanajamii wahusike katika kuwachagua na kuwaweka mamlakani viongozi wafaa. Taswira iliyopo ni kuwa viongozi wa jamii ya sasa wanafahamika zaidi kwa kutoa ahadi nyingi wakati wa kampeni ambazo huishia kutotitimizwa. Hivyo, mwamko mpya na mabadiliko yanayotarajiwa na jamii husika yanabakia kuwa ahadi tu. Jamii inatarajia mwamko mpya wenye mabadiliko yatakayoleta ubora wa maisha kwa wenyeji yaani wanajamii wote ila inakuwa ndoto tu kama zile za Alinacha. Ahadi za viongozi kwa wanajamii zinasalia kuwa mawazo na maneno matupu kama vile zilivyokuwa ndoto za Alinacha. Kando na kuyafahamu mafunzo yanayotolewa na mwandishi, msomaji hana budi kujua kuwa



katika ndoto zake, Alinacha alitamani kuuza vyombo vya gilasi ili ajipatie utajiri mkubwa, maisha ya anasa pamoja na kumwoa binti wa Waziri Mkuu. Haya yote hayakutimia kwa sababu yalikuwa ni mawazo tu bila matendo. Alinacha hakufanya lolote la kujiendeleza na kuboresha maisha yake jinsi alivyotamani; aliota tu! Jamii ya Afrika inafahamishwa kwamba iwapo inataka kuona mabadiliko ya kweli katika uongozi na maendeleo katika mataifa yao ni lazima ihusike katika kuyaleta mabadiliko hayo kwa udi na uvumba. Kuwaza na kutamani pekee bila kutenda hakutaleta mabadiliko yoyote. Hivyo basi jamii inahimizwa kuambatanisha hamu na ndoto zake na matendo ili fanaka ipatikane. Kimbunga cha kusaka na kutafuta maisha bora kimeendelezwa na ujasiri uliotoka kwenye Vita vya Fyuraa kama inavyorejelewa na simulizi fupi kwamba:

Inasimuliwa kuwa watu walipata nguvu mpya baada ya kutoka kwenye Vita vya Fyuraa. Vyenyeve vilipangwa huko mbali na wenyeji wengi walishawishiwa kujiunga na jeshi kwenda kupigana upande wa jamaa za Ukolongwe. Huko ndiko walikotambua kuwa nyuma ya figu la ujasiri alilovaa Ukolongwe kulikuwa na woga wa kujinyia nguoni. Sasa walichachawa na hata kuanza nyimbo za kuhimizana (Wamitila, 2004, uk. 66)

Usimulizi huu unahusu jinsi Waafrika walivyohusika katika Vita Vikuu vya Dunia huko Burma na kwingineko duniani walipopata fursa ya kutambua kuwa hata Wazungu waliowatawala ni waoga (Banks, 2001; Beckett, 2007; Collins, 2007). Kuhusika kwao vitani kuliwapa athari chanya ya ujasiri. Waliporejea katika nchi zao wakiwa na ujasiri huo mpya waliamua kuungana na kupigania uhuru wa mataifa yao. Wenyeji walitunga nyimbo za ukombozi zilizowahimiza wote kuungana kuusaka ukombozi wao. Haya yameandikwa kimajaribio ili kufunza jamii ya sasa kuwa umoja wake ndio nguvu zake. Vilevile, funzo jingine kwa jamii ni kwamba inafaa itumie ujuzi na uzoefu wake kwa manufaa ya taifa lote kwa jumla. Njia bora ya kuleta maendeleo na uwiano ni kushirikiana. Kila mara adui anapoinuka ni vyema kuungana na kupigana ili kujikomboa badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi yaani Ughaibuni. Ukweli kuwa jamii ndiyo suluhu ya matatizo yanayoikumba umerudiwa. Wageni hawawezi kuleta suluhu lolote la kudumu. Nyimbo na maneno yanayoamsha ari za wanajamii ni mbinu nzuri ya kuwaunganisha watu wenye lengo moja. Mbinu ya pekee ya kujipatia uhuru kutokana na uongozi dhalimu ni umoja uletwao kuhamasisha jamii, kuungana na kuamua kukataa unyanyasaji kwa vyovyote vile.

Kukosa maisha bora katika jamii aidha kumepewa jina la “jehanamu”. Imebainika kwamba binadamu wa jamii ya leo anaishi katika hali inayomtesa na kumwumiza kiasi cha kufananishwa

na mtu aishiye Jehanamu. Katika dini mbali mbali inaaminika kuwa Jehanamu ni mahali ambapo binadamu hapendi kuhusishwa napo. Mwandishi anasema;

“Nilimfuata bila swali wala kudadisi kama muumini aliyesimuliwa madhara ya jehanamu. Yaelekea hata hii ilikuwa jehanamu ya aina fulani” (Wamitila, 2004, uk. 48)

Vilevile, inaaminika kuwa Jehanamu ni mahali pa uharibifu na mateso ya milele. Anayetamalaki kule ni shetani. Jehanamu ni kifo cha pili kitakachowakumba wanadamu waliokataa kumtii Mungu Muumba wakiwa ulimwenguni. Ni kifo ambacho hakiwezi kubadilika. Kifo cha kwanza kilisababishwa na kosa la binadamu wa kwanza, Adamu. Kifo hicho kilikombolewa na kifo cha Yesu Masihi kwa njia ya msalaba kama ilivyorekodiwa katika Biblia Takatifu (Ufunuo wa Yohana 20:14). Ifikapo siku ya kiama, watakaotupwa Jehanamu watateswa mchana na usiku milele na milele. Kuna sehemu kadha duniani ambazo zimewahi kupewa jina “Jehanamu”. Hili ni jina linalowakilisha sehemu au maeneo yasiyokalika kwa kuwa ni hatari na hayana afya inayowastahiki wanadamu. Mifano ya sehemu kama hizi ni Blood Falls (Antarktika), Danakil Depression (Ethiopia), Door to Hell (Turkmenistan), Kamchakta Peninsula (Russia) na Jela la Gitarama (Kigali) miongoni mwa nyingine (Braitseva, 1995; Jill *et al.*, 2004; Katarzyna *et al.*, 2014; Williams *et al.*, 2010). Taswira iliyomo katika sehemu hizi ni shida na mateso pekee. Kwa sababu hii ni lazima jamii ijitafutie “Musa” au “Mzee” wake yaani mkombozi. Majina “Musa” na “Mzee” yanaashiria ukombozi kama isemwavyo katika nukuu hili;

“Mimi Ngwena, ni Musa. Nina jukumu la kuikomboa jamii: kuwaondoa Misri ya historia na uchumi. Lakini Musa pia alikumbana na shida. Jamaa walipokuwa jangwani walikumbuka samaki, matikiti na vitunguu saumu” (Wamitila, 2004, uk. 100)

Kwa mujibu wa dini ya Kikristo, Musa alitumwa na Mungu kuwakomboa wana wa Israeli kutoka utumwani Misri. Mhusika Ngwena ndiye mkombozi wa leo au Musa wa leo anayerejelewa katika riwaya ya *Musaleo!* Anachukua wadhifa kama wa Musa wa dini ya Kikristo aliyetumwa na Mungu kuwakomboa wana wa Israeli kutoka utumwani Misri. Safari hiyo ya ukombozi haikuwa rahisi. Njiani kulikuwa na matatizo na pingamizi chungu nzima hata kutoka kwa wale waliokuwa wakisaidiwa. Waisraeli walipokosa maji na chakula jangwani walimzomea Musa na kumkumbusha kuhusu samaki, matunda na viungo vizuri vya mapishi walivyoviacha Misri. Jina jangwa linaleta taswira ya mahali pakavu ambapo hapana uwezo wa kuzalisha chochote. Viongozi wowote wa mataifa ya Afrika yanayoendelea wanafahamishwa

kwamba uongozi si rahisi. Kwanza, viongozi wafaa kuelewa mahali jamii wanayoongoza imetoka na magumu iliyopitia ili wapange mikakati ya kuipa uongozi bora. Pili, mara kwa mara jamii inayoongozwa hutamani kuyarejelea magumu waliyoyapitia kwani huyaona yakiwa bora kuliko uongozi mpya ambao ni zao la uhuru. Jamii ya sasa ina wepesi wa kusahau. Ni dhahiri kuwa taswira inayojitokeza inapelekea kudai kuwa nchi za Kiafrika zilizo huru bado zinatamani misaada kutoka mataifa yaliyozitawala hata baada ya kujikomboa kutoka kwenye minyororo ya ukoloni. Kwa ufupi, Waafrika ametoka utumwani ila wamekataa katu kuusahau.

Riwaya zinaendelea kusesitiza kuhusu umoja na utangamano wa kijamii na wa kitaifa kwa jumla. Inabainika kwamba ili jamii na taifa ziendeleo ni sharti binadamu aangamize ubinafsi wake na kuzalisha umoja. Jamii ya sasa inafundishwa jinsi ya kuchagua viongozi wazuri. Sura ya jamii ya kisasa inadhibitika kwamba ni jamii inayowachagua viongozi kwa kutegemea historia za familia zao. Hivi ni kusema kuwa watu waliozaliwa uongozini wanapendelewa na kupendekezwa zaidi kuongoza kuliko wengine ambao hawana historia ya uongozi katika familia na ukoo wao kwa jumla. Maendeleo hayawezi kupatikana nchini pasipo na utangamano katika jamii. Katika kusistiza ukweli huu mfano wa Yesu Masihi wa Biblia anayeaminika kwamba alivua ubinafsi na kuupeana mwili na uhai wake kama dhabihu kwa minajili ya kuwakomboa wenye dhambi umetolewa. Kitendo hiki kinabainisha kwamba ukombozi wa mtu au nchi una gharama kubwa.

Aidha, ni dhahiri kwamba gharama ya umoja ni ghali na yenye machungu. Ni sharti kila mmoja katika jamii ajitolee kulipa gharama hiyo ili kuafikia umoja na utangamano katika jamii yake. Ubinafsi katika mataifa ya Afrika yanayoendelea unadhihirika katika vitendo vya ufasidi, ukabila, ukabaila, ubepari na ubwanyenye (Poncian & Mgaya, 2015). Ili kujitoka katika athari hasi ambazo Afrika ilirithi kutoka kwa wageni wakoloni na kuhakikisha kwamba zimeangamizwa, riwaya mpya zimetumia simulizi hii yenye urejeleomatini kuimbusha jamii kusahau yaliyopita na kuganga yajayo. Usemi kwamba , *“mbegu lazima ife ndipo mche uweze kuota”* unaweka wazi kuwa kizazi kipya kinatarajiwa kuwa tofauti na kizazi cha kijadi. Inatazamiwa kuwa kizazi kipya kitachipuka bila mbegu ya ubinafsi uliokithiri. Kizazi hicho kitakumbatia wema na umoja kwa lengo la ujenzi wa jamii mpya. Jina mbegu limetumika kuhamasisha jamii kwamba kuna matumaini ya kuendelea. Japo hali zinazidi kuonekana zikiwa si hali tena, kuna matumaini ya kuwa na kizazi kipya kilichozinduka. Mwandishi anasema katika usimulizi kwamba mche huota baada ya kifo cha mbegu. Hivyo, kizazi kipya kitatokana na jamii iliyopo lakini kitakuwa bora.

Mche utakuwa bora kuliko mbegu kwa sababu ya kuwepo kwa uongozi bora. Kiongozi atakayekuja atakuwa na sifa sufufu.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa kulingana na riwaya teule nchi za Kiafrika zinazoendelea zinakumbwa na uhaba wa viongozi bora. Kuna jangwa la viongozi. Ili kukimu na kumudu uchumi wake kisha kupata uwezo wa kujitegemea ni lazima jamii za Kiafrika ziwe na kiongozi anayejinasibisha na mazingira ya Kiafrika. Kiongozi huyo atakapopatikana atakuwa mkombozi kwa kuwa atatarajiwa kukomboa kila hali iliyodhoofika katika taifa lake. Iwapo hivyo, wenyeji watamuenzi na kumwabudu. Sifa mahususi za kiongozi mpya atakayekubalika katika jamii zinaendelezwa na matumizi ya majina “Mkombozi Mzee” kama katika:

Mkombozi Mzee! Mkombozi Mzee! Mkombozi Mzee! Mara tatu! Katika utabiri (ambao nasikia upo) mkombozi huyo wa jamii alipaswa kuzaliwa katika mazingira ya ajabu. Hilo nishafuzu. Alitakiwa kuwa na uwezo mkubwa wa lugha. Mlumbi mkubwa nilikuwa! Tatu mwenendo wake haukuwa wa kawaida (Wamitila, 2004, uk. 13)

Tatizo lililopo ni kuwa wenyeji wanapochagua viongozi wanazingatia sifa ambazo hazilengi ukombozi unaotarajiwa. Kwao kiongozi ni wa kusifiwa na kuabudiwa hata anapofanya makosa. Kiongozi anayerejelewa katika riwaya amejichagua mwenyewe kwa sababu ya sifa za nguvu alizozaliwa nazo. Hana sifa za uongozi ambazo zinahitajika katika kuiendeleza jamii yake. Inaaminika kuwa kiongozi ni mtu yeyote ambaye alizaliwa katika hali isiyokuwa ya kawaida, mwenye weledi wa usemi na mwenendo usiokuwa wa kawaida. Matini iliyorejelewa inalinganisha uongozi wa "Mkombozi" na viongozi wa dini mbalimbali ambao inaaminika kuwa kuwepo kwao duniani hakukuwa kwa kawaida.

Vile vile matamshi haya yanarejelewa ili kuwafafanua viongozi-tajika ambao walichukuliwa kama wakombozi wa jamii. Kwa mfano, Mtume Mohamed ambaye ndiye mwanzilishi wa dini ya Kiislamu alifiwa na wazazi wake akiwa na umri wa miaka sita. Alilelewa na babu yake ambaye aliaga dunia baada ya miaka michache kisha mtume akachukuliwa na mjomba wake. Baadaye aliamua kujitenga na kwenda kuishi katika upweke mlimani katika pango. Akiwa na umri wa miaka arubaini, inaaminika kuwa Gabrieli alimtokea na kumpa ufunuo mpya kutoka kwa Mungu Muumba. Baada ya miaka mitatu alianza kuhubiri yale aliyofunuliwa na Gabrieli. Hivyo ndivyo alivyoanzisha dini ya Kiislamu ambayo kwa sasa imetamba ulimwenguni kote (Conrad, 1987). Kwa upande wa Ukristo, Mkombozi Yesu kama inavyorekodiwa katika Biblia

katika Injili za Mathayo, Marko, Luka na Yohana, anaaminika kuzaliwa na Bikira Mariamu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Hivyo, ni dhahiri kuwa anayedhaniwa kuwa ataiongoza nchi vizuri anafaa kuwa na ujasiri unaotokana na mwanzo usiokuwa wa kawaida. Mwandishi katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* anatumia jina la Samsoni kufafanua zaidi;

“Hajainyoya kwa miaka mingi...Ni kama ya Shujaa Samsoni katika Biblia. Matenzawa, asiyenyolewa! Kisa cha Matenzawa wanakifahamu sana. Hakunyolewa. Naye Matenzawa hatanyolewa. Hakuna atakayemnyoa” (Wamitila, 2014, k. 56-57)

Jina la Shujaa Samsoni aliyerekodiwa katika Biblia takatifu katika kitabu cha Waamuzi limetajwa katika simulizi fupi ya riwaya rejelewa. Samsoni alikuwa mnaziri wa Mungu aliyemiliki nguvu zilizokithiri. Kwa mujibu wa Biblia tangu kuzaliwa kwake Samsoni, wembe haukuwahi kupita kichwani pake. Iliaminika kuwa nguvu zake zilikuwa katika nywele zake. Daima aliwashinda maadui wake wote ila tu wakati aliponyolewa kupitia kwa ujanja wa mke wake Delila. Baada ya kushikwa na Wafilisti alitobolewa macho na kutiwa kizuizini. Baada ya kipindi kirefu chenye mateso mengi, alifanikiwa kujikomboa tena. Wafilisti walisahau kuwa wakati huu, nywele za Samsoni zilikuwa zikiota upya pole pole. Zilipopata urefu fulani nguvu zilimrudia na akawaua Wafilisti wengi wakati wa kifo chake kuliko hata wakati mwingine wowote katika maisha yake ya uongozi katika uongozi wa jamii yake. Kwa mujibu wa usimulizi, kiongozi mpya amelilinganishwa na Shujaa Samsoni kwa kupewa jina linalorejelea sifa ya kufuga nywele. Awali alipewa jina la Maburende. Anajidai kuwa yeye alibadilika na wala si yule waliyemfahamu kijijini hapo awali. Hii ni kwa sababu aliamua kufuga nywele zake bila kuzikata.

Mwandishi anasema kuwa mhusika hakuzikata nywele zake kwa miaka mingi. Kwa sababu hiyo, jina lake likabadilishwa na akaitwa “Matenzawa” yaani mtu asiyenyolewa. Kitendo cha kutonyolewa kinaashiria kuwepo kwa umbile lisilo la kawaida. Nywele zinatumiwa kuashiria nguvu au uwezo. Ni kana kwamba kitendo cha kumyoa binadamu humdunisha na kumfanya dhaifu. Kwa mujibu wa mwandishi kupatikana kwa kiongozi mpya wa jamii kunaamuru kuwepo kwa sherehe. Ili kuukamilisha ujumbe, jina Mwana-Mpotevu limeongezwa. Jina hili ni urejeleomatini ya hadithi ya dini ya Kikristo inayopatikana katika Biblia Takatifu. Ili kumwelewa mwandishi lazima msomaji wa riwaya husika aufahamu muktadha wa hadithi ya mwana mpotevu pamoja na masihara aliyofanya nyumbani kwao. Inaelezwa kwamba huyu mwana aliomba kurithishwa mali yake yote na babake mzazi. Alipopewa mali aliyodai, mwana

mpotevu alienda katika nchi ya mbali alipozitumia fedha zake zote katika miasha ya anasa. Alipomaliza pesa zake zote aliamua kutafuta kazi. Mwana-Mpotevu aliajiriwa kazi ya kuwalisha nguruwe. Kazi hii ilikuwa ngumu na yenye madhila mengi. Ilipomshinda aliamua kurudi nyumbani na kumwomba babake msamaha. Baba alipomwona mwanawe aliamuru kuandaliwe karamu kubwa ya kumkaribisha tena myumbani. Kulichinjwa fahali mzuri na ikaamrisha kwamba watu waalikwe ili pamoja na jamii washerehekee kurudi kwa mwana ambaye iliaminika kuwa alikuwa mautini ila yu hai sasa. Wakubwa wake walilalamika kuwa baada ya kupotea katika anasa kwa miaka mingi hakufaa kuandaliwa karamu kama ile. Baba yake alishikilia kuwa mwanawe alikuwa amekufa na kwa hivyo kurudi kwake nyumbani kulikuwa sawa na kufufuka.

“Maburende, Mwana-Mpotevu...Atafutwe fahali mzuri achinjwe. Wakubwa zake wakasema haistahili. Miaka yote hii alikuwa amewaacha na kuyoyomea wapi Mungu. Sijui. Harakati za kupambana na mjanja alizikosa. Iweje sasa amefika na kuandaliwa karamu?” (Wamitila, 2014, uk. 50)

Mwana akipotea kwa muda mrefu kisha ajitokeze ghafla katika boma husika huandaliwa sherehe kubwa ya kumkaribisha. Kila mwanajamii anahimizwa kukumbuka alipopotezea mwelekeo na kurudi pale pale na kulainisha mapito yake upya. Si kila mmoja atafurahi kwamba binadamu amelakiwa vizuri hasa baada ya kufanya makosa. Hata hivyo mwandishi anahimiza watu wakumbatie wema na msamaha katika hali zote. Kusiwe na hali ya kuzozana kwa sababu mmoja aliyepotoka amesamehewa na kuruhusiwa kutangamana na jamii yake tena. Majina ya kubuni “Baa-Lini” na Njaamani yametumika kufafanua zaidi kuhusu historia ya maovu yaliyotekelezwa na Wazungu wakoloni na athari zake kama ilivyoashiriwa katika ulumbi katika *Musaleo!* kuwa;

“Sasa twende kwenye utafiti uliofanywa. Kisa cha Ukolongwe kinavutia. Alizaliwa mwaka wa 1884 katika mji wa Baa-Lini katika nchi ya Njaamani” (Wamitila, 2004, uk. 27)

Hapa simulizi fupi imejikita katika mbinu ya kimajaribio ya urejeleomatini kwa minajili ya kukuza kunga ya matumizi ya majina aina aina. “Baa-Lini” na “Njaamani” na majina yanayobainisha historia kamili ya chanzo cha ukoloni barani Afrika. Mintarafu ya riwaya, Ukolongwe alizaliwa mnamo mwaka 1884 katika mji wa Baa-Lini katika nchi ya Njaamani. Jina “Ukolongwe” linalotajwa linamwashiria mkoloni. Kwa mujibu wa historia chanzo cha ugavi wa nchi za Kiafrika miongoni mwa mataifa ya Ulaya kilikuwa mkutano mkuu uliofanyika mjini Berlin (Baa-Lini), Ujerumani (Njaamani). Peacock (1982) anaeleza kuwa mnamo Novemba 26

1884 hadi Februari 26 1885 kongamano liliandaliwa kule Berlin, Ujerumani na kuhudhuriwa na mataifa mengine ya Ulaya. "Azimio la Berlin" lilipitishwa ambapo mataifa washiriki yalikubaliana kuigawa Afrika kati ya madola ya Ulaya. Lengo kuu lilikuwa kuiendeleza na kuistaarabisha Afrika ili kutoa gizani kama wenyewe walivyodai. Baadaye, Afrika ilifanyika kuwa eneo lindwa la mataifa ya Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Italia. Simulizi hii inaifahamisha jamii kuhusu chanzo cha ukoloni barani Afrika. Kwa mujibu wa riwaya teule, Afrika ingali bado chini ya nguvu na uwezo wa wakoloni. Baada ya kujipatia uhuru, viongozi wapya wa Kiafrika wamo mbioni kujitajirisha huku wakiwatelekeza wanyonge. Taswira inayowasilishwa na riwaya teule ni kuwa uhuru wa Waafrika ulikuwa mwanzo wa "Ukolongwe" yaani ukoloni mkongwe. Kwa mintarafu hii inabainika kuwa sifa kuu ya uandishi wa kimajaribio inayojitokeza ni kwamba kazi husika zina uwezo wa kutumia fasihi yenye falsafa ya Usasaleo katika kuifundisha jamii historia yake japo kwa njia changamano.

"Inasemwa ilijengwa na Mayahudi waliokimbia huku kuepuka mauaji ya Hitler huko Ujerumani na Ulaya muda mfupi kabla ya Vita Vikuu vya Pili vya Ulimwengu" (Wamitila, 2004, uk. 30)

Jina Ukolongwe limetamalaki sana katika riwaya teule. Kulihusu msimulizi anasema haya:

Aliamua kuwafanya watu kadha aliowajua kwanza alipofika wakuu akawaita *Paramount Chiefs*. Huo ukawa mwanzo wa uchifu na uchafu na udufu wake! ..."Kwa njia hii tutaupunguza uzembe na uovu wa jamaa wa huku kwa sababu watakuwa na kazi ya kufanya badala ya kujizungukia majiani tu!" Wafanyikazi hao waliruhusiwa kukaa kwenye mashamba ya jamaa za Ukolongwe (ambayo kusema kweli yalikuwa yao wenyewe!) ili kuweza kufanya kazi vizuri. Kauli iliyotamkwa na mmoja wa jamaa hao walioishia kuitwa Waselelezi inakumbukwa mpaka leo. Alisema "Sasa tumeshaiba ardhi yao, kilichobakia ni kuviiba na kuvimiliki viungo vyao. Hii ni hatua ya pili!" Ukolongwe na jamaa zake walitaka kuwadhhibiti wafanyakazi hao. Ili kulifanya hili walishurutika kuzuka na mbinu nyingine (Wamitila, 2004, uk. 37)

Dondoo hili limetumia majina ya Ukolongwe na *Paramount Chiefs*. Katika muktadha huu mwandishi anaichorea jamii taswira ya jinsi historia ya Afrika ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Matatizo ya utabaka na ufisadi yalianzishwa na wakoloni. "*Paramount Chiefs* walipewa nguvu na uwezo mkubwa dhidi ya wanajamii wenzao. Aidha, machifu hao hao walipewa uhuru wa kumiliki mashamba makubwa makubwa (Pakenham, 1992). Jambo hili lilipelekea kuwepo kwa ukosefu wa ardhi na mashamba kwa wanajamii. Hili ni tatizo sugu hivi leo. Matatizo yaliyopo Afrika hivi leo yamesababishwa na kuwepo kwa ukoloni mkongwe ambao ndio uliokuwa chanzo

cha *Paramount Chiefs* yaani Machifu wakuu. Uongozi wao ulitumia ujanja kama asemavyo msimulizi katika simulizi fupi ifuatayo ambayo bado inarejelea jina la Ukolongwe:

Hiyo ni kauli ya ukweli, walisema wengine walimsamehe, “Ni mtoto huyu, hajui alisemalo, mwacheni tu!”...Miaka michache baadaye jamaa za Ukolongwe walifuatia. Ukolongwe alitumia nafasi yake kuwatafutia ardhi ya kulima. Alishatambua wapi palikuwa na ardhi nzuri na wapi mbaya. ...Ukolongwe alitumia ujanja wake. Ardhi yote iliyokuwa na rutuba aliichukua na kuwakabidhi jamaa zake hao. ...Ardhi ambayo wenyeji hawakuwa wameitumia kutokana na mfumo wao ilichukuliwa na Ukolongwe na jamaa zake na kubatizwa ‘Ardhi haribifu’. Ndugu zake nao lazima walikuwa wazembe: walishindwa kuyalima mashamba makubwa waliyoibiwa na mwenzao. Walihitaji vibarua.walimwendea Ukolongwe. “Mzee hatuna njia ya kuilima migunda hii; tunahitaji wasaidizi. Wajua tena mikono yetu laini, imezoea kalamu bwana, sio kupambana na magugu ya huku magumu kama *natives* wenyewe!” walisema (Wamitila, 2004, uk. 36)

Jamaa za Ukolongwe walipata nafasi ya kuingia Afrika na kuvuruga maisha ya Waafrika ya kila kwa kuchukua ardhi yao huku wakisingizia kwamba wao ni watoto wasiojua walilolisema. Kisingizo kingine kilichotumika ni kwamba wenyeji walikuwa na mashamba makubwa ila hawakujua kuitumia. Mkoloni alitumia ujanja kuwaondoa wenyeji kutoka kwenye umiliki wa ardhi yao (Rodney, 1981). Tatizo kubwa lilikuwa pia kwamba baada ya kuyatwaa mashamba hayo waliendelea kutumia ujanja ili wawaweke wenyeji mtegoni na kuwafanya kuwa wafanyakazi katika mashamba ya wakoloni. Hivi ndivyo Waafrika walivyoishia kuwa watumwa katika nchi zao. Iwapo jamii ya sasa ilijikomboa sasa ni jukumu lake kushikilia kwa nguvu uhuru walionyakua.

Jina “Hitler” linapotajwa hisia za ukosefu wa ubinadamu huibuliwa. Majina mengine yaliyotajwa katika nukuu hili ni Mayahudi na Vita Vikuu vya Pili vya Ulimwengu. Hapa kunga hii ya kimajaribio imetumiwa kueleza historia ya mateso waliyopata wayahudi kutoka kwa wajerumani. Kwa kurejelea historia hii kongwe, msimulizi anatoa mwanga kuhusu umuhimu wa amani na usalama katika mataifa yanayoendelea. Anawatahadharisha Waafrika dhidi ya machafuko ya kisiasa na chuki za kikabila. Mukadha wa usimulizi huu unaelezea kuhusu jinsi Wayahudi walioroka nchi yao kwa sababu ya vita. Walijipata wakiendelea utamaduni wao katika nchi ngeni. Kwa mfano, katika riwaya mwandishi anaeleza kwamba Wayahudi walijenga hekalu mahali ambapo ilikuwa nadra sana kuwaona watu wengine wakiingia. Wakati huo huo Hitler alikuwa akiitawala Ujerumani baina mwaka 1933 na 1945 (Alan, 1999). Hitler aliendelea



uongozi wake kwa njia ya udikteta chini ya chama cha NAZI. Alianzisha Vita Vikuu vya Pili vya Dunia mnamo mwaka wa 1939 vilivyoendelea hadi mwaka 1945 (Adamthwaite, 2011). Lengo kuu la Hitler la kuanzisha vita hivyo lilikuwa ni kuwaangamiza Wayahudi katika maafa yaliyofahamika ulimwenguni kama "*Holocaust*." Wayahudi takriban milioni sita waliuawa huku mamilioni ya wengine wakiathirika vibaya (Yehuda, 2000). Kwa kurejelea hadithi fupi hii, mwandishi anafafanua funzo la muhimu kwa kizazi cha kisasa kuwa tatizo la kuwepo kwa wakimbizi litaondolewa kabisa iwapo Waafrika watakumbatia amani na utangamano. Kwa mujibu wa haya tukio la kihistoria limetajwa ili kujenga riwaya ya kisasa.

Hali ya siasa aghalabu huwadhulumu wanajamii katika nchi za Kiafrika zinazoendelea. Wanasiasa na viongozi hutumia vijana kutekeleza matakwa yao. Katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* kisa kinasimuliwa kinawataja wanajeshi fulani. Msimulizi anaeleza kuwa sura za wanajeshi hao zilimkumbusha "*mapando ya wanaume*" waliotumiwa na matajiri kuwatishia wadeni wao. Katika kisa hicho kulikuwa na mhusika Moylee Gaga aliyenunua nyumba katika mtaa wa Golden Gate mnadani wakati mwenye nyumba aliposhindwa kulipa rehani yake akiwa bado anaishi ndani. Mwenyeji alihitaji kuhama kutoka kwenye nyumba hiyo ambayo sasa ilipata bwana mwingine. Moylee Gaga, mnunuzi wa nyumba hiyo alishauriwa atafute genge la vijana kama wafanyavyo wanasiasa. Zaidi ya hayo, Gaga alishuritishwa apeane fedha za kuwanunulia vijana pombe kwenye mtaa wa "Madongokuinama". Baadaye, waende pale usiku na kuivurumisha nje mizigo ya mwenye nyumba bighairi ya vilio na kelele za jamaa yake. Madongokuinama ni jina la kubuni linaloashiria makazi ya mabanda ambamo watu wa mapato ya chini huishi tena kwa njia ya uchochole. Matumizi ya jina hili yanatambulisha maskini wanavyotumiwa na wanasiasa kuzua vurugu katika jamii zao. Zaidi ya haya, istilahi au jina "operesheni" limetumika kuonyesha jinsi wenye nguvu wanavyoendeleza dhuluma kwa wanyonge. Istilahi hii inadhihirisha jinsi jamii ya kawaida inavyoumia mikononi mwa wale wanaotarajiwa kuilinda. Kwa mfano Moylee Gaga anazidi kushauriwa kuhusu jinsi ya kufaulu katika ulimwengu uliojawa na ufasadi na ukosefu wa haki. Mnyonge daima anadhulumiwa na kukoseshwa haki. Umoja wa viongozi walio mamlakani ni kwa lengo la kujinufaisha wao pekee kama inavyodaiwa katika nukuu lifuatalo;

“hakikisha tu kuwa mkuu wa polisi wa eneo hilo anajua tu-nadhani unanielewa – kuwa una “operesheni” fulani tu; akijua tu basi huna la kuogopa kabisa. Kila jambo litakwenda sawasawa (Wamitila, 2011, uk. 85)

Njogu (1987) amebaini kwamba watu wa tabaka la chini (wanaoishi Madongokuinama) daima hupigana na ubwanyenye. Hata hivyo, mintarafu ya utafiti huu wanyonge wanaonekana kukubali hali yao. Isitoshe, wanakubali kutumiwa “vibaya” na mabwanyenye kwa kuhongwa kwa vitu vidogo vidogo kama pombe ili kutekeleza maovu dhidi ya wenzao. Wenye nguvu wanatumia mamlaka yao vibaya kuwaumiza wale walio katika tabaka la chini. Dhuluma iliyokithiri inabainika katika usemi kwamba, “bora tu mkuu wa polisi ajue kuhusu *operesheni* fulani.” Hiki ni kinyume cha matarajio ya jamii kwani vikosi vya usalama vimewekwa katika taifa ili kuwalinda wananchi wote. Kwa mujibu wa mbinu hii taswira iliyopo katika jamii ni kwamba vikosi vya usalama katiaka jamii ya kisasa hutumika kuwadhulumu na kuwanyanyasa wananchi wa kawaida. Maoni haya yanawiana na usemi wa Kamunde (1983) kwamba wanajamii wa tabaka la chini hudhulumiwa na wale wa tabaka la juu hata ingawa baadaye wao huzinduka na kuipigania haki yao. Riwaya ya kimajaribio imerejelea jina la makala ya *The Wild Man's Pedigree* kuzua sababu za kuwepo kwa taswira kwamba haki ya mnyonge ni dhuluma. Simulizi husika imewasilishwa kama ifuatavyo:

Alisema mengi lakini kufupisha habari kadai rangi yake ilikuwa bora na iliashiria ubora wa akili. Inasemekana siku moja alitokeza hadharani, huku amekishika kitabu kimoja kitiwacho *The Wild Man's Pedigree*. Humo aliwasomea watu sehemu fulani aliyodai kuwa ilieleza sifa zao. “Weusi: wasiochangamka, watulivu, wenye pua pana, wajanja, wazembe na wanaotawaliwa na ugeugeu!” (Wamitila, 2004, uk. 35)

Katika usimulizi mwandishi wa riwaya ya kimaribio ya *Musaleo!* anaeleza kwamba mkoloni alitumia maarifa yaliyorekodiwa katika “*The Wild Man's Pedigree*” kuwakandamiza Waafrika (watu weusi). Mkoloni aliwaona Waafrika kama viumbe weusi wasio wachangamfu, hivyo akasingizia kutumia mbinu ya utawala ili kuwachangamsha (Larson, 2004). Katika makala yake, Ritland (2000) anatoa ufafanuzi kuhusu asili ya vizazi vyote na kuratibisha tabia nafsi za wanadamu mbalimbali kwa mujibu wa asili zao. Kulingana na makala, mateso anayopitia Mwafrika ni kudura inayotokana na rangi ya umbo lake. Riwaya ya kimajaribio ya *Musaleo!* imetumia *The Wild Man's Pedigree* kubainisha jinsi wakoloni walivyowahadaa Waafrika kwa kusingizia kwamba hatima ya binadamu yeyote mweusi ni taabu na dhiki. *The Wild Man's*

*Pedigree* imejengwa katika misingi na imani ya nadharia ya Asili ya Spishi iliyoasisiwa na Charles Darwin.

Mwanasayansi Darwin alikuwa mtaalamu wa bayolojia na jiolojia ( Bowler, 1996). Nadharia yake ya maendeleo ya uhai hali maarufu kama mageuko ya spishi inashikilia kuwa spishi zote za viumbe-hai zinatoka kwa babu mmoja (Browne, 2002). Viumbe-hai vimetokana na spishi asilia zilizogeuka baada ya mpito wa wakati (Mbao, 2005). Mageuko asilia yalifuata uteuzi asilia ambapo viumbe-hai wanaoishi vizuri katika mazingira mazuri huzaana kwa wingi kuliko wale wanaoishi katika mazingira duni (Mbao, 2005). Nadharia ya Darwin ilipendekezwa katika makala ya *Asili ya Spishi* iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1859 (Freeman, 1977).

Larson (2004) anafafanua kuwa mhimili mkuu wa nadharia ya Darwin ni kwamba tabia za viumbe-hai wasiofaa sana zinaweza kutoweka kwa sababu wanakufa mapema na huwa hawana watoto wengi wa kuwarithi na kuendeleza tabia zao. Mawazo ya Darwin yalitumiwa na mzungu mkoloni kwa lengo la kuendeleza unyanyasaji wao dhidi ya Waafrika. Tatizo kubwa ni kwamba hata baada ya ukoloni kung'atuliwa dhiki za Waafrika hazikufika mwisho. Riwaya za kisasa zimebainisha kwamba uhuru umepatikana katika mataifa ya Afrika yanayoendelea ila sifa za ukoloni zingali zinatamalaki. Hali hiyo imefafanuliwa kama ukoloni mamboleo ambapo mzungu anajiona akiwa bora kuliko Mwafrika. Ukoloni mamboleo unazidi kuthibitika katika jamii ya sasa pale ambapo walio uongozini wameendelea kuwanyanyasa na kuwakandamiza raia wanaowaongoza. Madai yanayotumiwa na viongozi yana misingi katika madai ya Burke (1997) anayesema kwamba binadamu wote hawawezi kuwa sawa kwani wamepangwa katika makundi kulingana na uwezo na utendakazi wao.

Burke (1997) anadavua kuwa makundi matano ya kimaumbile yana sifa zifuatazo; Kundi la kwanza ni la viumbe wenye miguu minne, wenye nywele katika miili yao na wasiozungumza. Wanyama wote hupatikana katika kundi hili. Kundi la pili linajumuisha Wamarekani. Hao wana pua pana, nywele nyeusi laini na wanaongozwa na desturi maalumu. Kundi la tatu linawakilishwa na Wazungu ambao wana umbo lenye rangi ya kahawia, macho ya samawati na wenye kupenda kufuata na kutii sheria. Kundi la nne linahusu Waasia. Wameelezwa kama viumbe wenye misimamo thabiti, macho meusi, wenye wivu, wanaovalia mavazi yasiyobana na

kuongozwa na maoni. Waafrika na watu weusi wameorodheshwa katika kundi la tano. Wamepewa sifa kwamba ni watu wasiochangamka, watulivu, wenye pua pana, wajanja, wazembe wanaotawaliwa na binadamu waliojawa na ugeugeu. Kwa kutumia matini yenye jina, *The Wild Man's Pedigree*, riwaya teule za kimajaribio zimebainisha picha ya jamii ya Kiafrika isiyo na ujasiri wa kujiamini. Mbinu za kimajaribio za simulizi fupi, urejeleomatini na uchanganyaji wa lugha zimetumiwa kuizindua Afrika kwamba haifai kuchukulia sifa kuhusu maumbile yake kama udhaifu. Badala ya kujidunisha, Afrika inafundishwa kwamba ina uwezo wa kujiinua kutoka kwenye mavumbi yake hasa iwapo itajifunza kutokana na uzoefu iliyo nao kama inavyodhihirika katika usimulizi ufuatao kutoka katika riwaya teule ya *Musaleo!*:

Sasa nasikia kuna tatizo hapa. Maabara ya hospitali haina vifaa vinavyopasa kufanyia uchunguzi wa aina hii. Vingine vimo katika chumba cha daktari mkuu na amekwenda likizo!” Anima: Amekwenda likizo na funguo? Daktari: Ndio, ehh! Kingunge: Sasa tufanye nini? Daktari: Njia tuliyo nayo ni Wazito Nursing Home lakini ni ya kibinafsi, wanataka pesa kabla ya kufanya lolote! Kitungule: Mpelekeni huko tatalipa! Kutokana na mipango ya Kitungule na msaada mkubwa wa Kingunge waliishia kumpata daktari mmoja mzuri wa kibinafsi aliyejitolea kuifuatilia hali yake. “Nchi hii, kama mtu huna akili utakufa tu! Alisema Kitungule (Wamitila, 2004, k. 95-96)

Katika dayolojia hii mwandishi anamrejelea mwanasiasa mashuhuri wa Tanzania aliyefahamika kama Mzee Kingunge Ngombale Mwiru (Khamis & Omar, 1994). Kwa mujibu wa Maliyamkono (2000) Kingunge alikuwa mbunge shupavu nchini Tanzania aliyesimamia na kuwakilisha ukweli na haki katika yote aliyoyatenda. Aliutekeleza uongozi wake katika kile kipindi ambacho jamii za Afrika zilikuwa zikiupigania uhuru wa mataifa yao ambayo yalikuwa katika utumwa wa Wazungu wakoloni. Katika enzi zake aliupigania umoja wa Watanzania wote, jambo aliloanza akiwa katika ujana wake (Nyerere, 1995). Wakati huu alikuwa mwanachama wa chama cha kisiasa cha TANU (Tanzania African National Union). Hatimaye alijiunga na Chama cha kisiasa cha CCM (Lofchie, 1963). Kama yalivyokuwa majukumu yake ya hali halisi nchini Tanzania, jina Kingunge limetumiwa katika riwaya ya *Musaleo!* kuleta hisia za mtu mwenye huruma na mwenye kujali masilahi ya wengine. Daima yu mbioni kuwasaidia wanajamii wenzake. Katika muktadha wa dondoo lililorejelewa, Kingunge anaonekana akimsaidia mwanajamii kupata matibabu katika hospitali ya kitaifa (Lofchie, 1965). Kwa mujibu wa mwandishi wa riwaya husika za kisasa hii mienendo na tabia za Kingunge ndiyo taswira kamili ya kiongozi ambaye atakuwa wa msaada katika jamii.

#### 4.2.3 Matumizi ya Dini, Mitholojia na Simulizi za Kiafrika

Kila mwanajamii anafaa kujitambulisha na uwepo wa Mwenyezi Mungu Muumba (Heyd, 1992). Riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* inabaini kuwa ni sharti kila binadamu atambue kwamba “hataishi kwa mkate pekee.” Hapa, Wamitila anarejelea dini ya Kikristo. Katika dini ya Kikristo, neno linaloaminika kuwa limetoka kwa Mungu na kurekodiwa katika vitabu vitakatifu hufahamika kama “mkate wa uzima.” Hiki ndicho chakula cha kiroho kwa Wakristo. Matini iliyorejelewa inashikilia kwamba mwanadamu hawezi kukua na kukomaa kiroho pasi na kusoma na kulielewa neno la Mungu kama lilivyorekodiwa katika vitabu vya dini. Matumizi ya maneno “chakula cha kiroho” yanadhihirisha kuwepo kwa Mungu na uungu. Kuna nguvu na uwezo ambao umepiku uwezo wa binadamu. Jamii inahimizwa kuwa kuna umuhimu wa kuukumbatia kama katika maneno haya;

“Wakati huu waumini walikuwa wakipaza sauti wakijiandaa, tofauti na wanaopanda kwenye Ghala la Mlo, kwa ajili ya ‘mlo wa kiroho’. Labda kwa kutambua kuwa binadamu **hataishi kwa mkate peke yake**” (Wamitila, 2011, uk. 5)

Katika muktadha huu, msimulizi yuko hotelini ambapo anasubiri kuandaliwa chamcha. Akiwa pale anatambua kwamba waumini nao walikuwa wakijiandaa kuanza ibada katika kanisa lililokuwa mkabala na "Ghala la Mlo". Mwandishi anaeleza kuwa walihitaji "mlo wa kiroho". Inabainika kwamba japo binadamu anahitaji chakula cha kimwili ili apate nguvu za kuitumikia nchi yake, zaidi anahitaji kulishwa kiroho. Mwandishi anapendekeza umuhimu wa dini kwa kila mja. Ni muhimu kwa waja kutambua kuwa hawawezi kukitegemea chakula cha kujenga mwili pekee bali pia kile cha kujenga roho na nafsi. Kwa kutumia matini hii ya kidini, jamii inafahamishwa kuhusu uwepo wa Muumba mwenye uwezo kuliko wote na vyote. Mwandishi anapendekeza kwamba kila mtu ajitafutie nafasi ya kusikia kutoka kwa Mungu wake. Chakula cha kiroho hupatikana katika kusikia na kutii maagizo ya Muumba na pia kutangamana na wengine wenye nia hiyo (tafsiri yangu). Chakula cha kiroho huleta uzima. Hushibisha nafsi na kufidia mahali ambapo chakula cha kimwili hakiwezi kufikia. Humpa mlaji amani na zaidi humkomaza ili akabiliane na changamoto anazokumbana nazo maishani.

Katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* mwandishi amemchora mhusika Yosi Kanga akiwa katika lindi la matatizo mengi ya kiafya yaliyosababishwa na ajali za utotoni. Kila alipokuwa na

tatizo akiwa mdogo Yosi alipelekwa hospitalini kwa toroli lenye gurudumu lililopiga kelele nyingi. Watoto wa jirani waliposikia kelele ya gurudumu la toroli hiyo walijua Yosi anapelekwa hospitalini hivyo walisimama karibu na ua wa seng'enge wa shamba lao la matunda na kumfanyia ishara za vicheko vilivyoambatana na dharau. Unyonge aliokuwa nao ulimwacha akijizungumzia. Katika mazungumzo yake, Yosi alitamani kuwa na nguvu kama za Daudi aliyemwua Goliati kwa jiwe. Kuhusu haya msimulizi anasema;

“Nilitamani ningelikuwa na uwezo wa **Daudi wa Biblia**. Niinuke kwenye ile toroli, nitafute tunguja mwitu au hata labda jiwe la tumbawe na kuwagotoa kwenye tosi za vichwa vyao na kuunyamazisha **ugoliati** wao” (Wamitila, 2011, uk. 21)

Matini iliyorejelewa ni ya dini ya Kikristo. Goliati amefahamika kama jitu lililowadhulumu na kuwakejeli wana wa Israeli baada ya kutoka utumwani Misri na kuingia katika nchi ya ahadi, Kanaani. Yosi anasema kuwa watoto walipomkejeli alitamani angekuwa na uwezo kama wa Daudi wa Biblia aliyemnyamazisha Goliati kwa jiwe moja tu. Yosi anarejelea vicheko na dharau ya watoto hao kama *ugoliati* kwani vivyo hivyo Goliati alimkejeli. Kutokana na kisa cha Goliati na Daudi hadhira inafahamishwa kwamba dhuluma na dhiki zitakuwepo duniani japo kwa muda. La muhimu kutambua ni kwamba matatizo hayo hayatadumu milele hasa iwapo kila mja atajenga imani yake kwa Mungu anayemjua. Kuondolewa kwa dhuluma kunahitaji kuwepo kwa nguvu za kiungu, imani na bidii isiyo ya kawaida. Ijapokuwa Daudi alikuwa kijana mdogo kimwili na mwenye silaha duni ikilinganishwa na Goliati, imani yake kwa Mungu ilimwoko kutokana na ghadhabu na kejeli za Goliati. Juhudi na imani ya Daudi iliokoa kizazi kizima cha Israeli. Jamii ya sasa ya Kikristo inapokea tumaini jipya kwamba japo inapitia mambo magumu, mwisho wake utakuwa mzuri kuliko mwanzo. Watakaosababisha mageuzi na mabadiliko miongoni mwa jamii husika si watu wa kawaida ila watu wenye imani kuwa kusudi la mabadiliko linaweza kutimizwa. Zaidi ya hayo, himizo limetolewa kwamba ufanisi wa jamii uko mikononi mwa wanajamii wenyewe. Ili kuafikia azma hii, wanajamii wanahimizwa kuwa na lengo moja na kuvuta pamoja kwani umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Mhusika Konzi katika riwaya teule ya *Msichana wa Mbalamwezi* alikuwa na hoteli ambapo alifanya kazi pamoja na mkewe. Mwandishi anaeleza kuwa Konzi alikuwa na mazoea ya kuwadhulumu wanawake; jambo lililomwia kama ugonjwa. Iitarajiwa kuwa ugonjwa huo ungepona alipooa. Kinyume na matarajio, Bwana Konzi aliendelea kumdhulumu mkewe kwa

kuwatamani wanawake wengine waliokuja hotelini, machoni pake. Tabitha mkewe Konzi anaiona tabia hii kama kutomtii Muumba. Anayerejelewa kama Muumba ni Mwenyezi Mungu. Katika hali halisi, uumbaji huhusishwa na dini. Kwa Tabitha dhuluma kama hii ni tendo la kutotii mojawapo wa amri kumi za Mungu inayoonya dhidi ya uzinzi. Vitendo vya Bwana Konzi na Tabitha vimetumiwa kuendeleza maudhui ya ulipizaji kisasi. Tabitha analipiza dhuluma kwa dhuluma. Mwandishi anasema kwamba kila wakati Tabitha alipomwona mumewe alipasua kicheko kikubwa akigeuka huku na kule kama mtu aliyetaka kuuomba ushirika wa wenzake. Mwishowe alimwuliza mumewe iwapo alimjua vizuri. Maneno yake, “Ikiwa wewe ni bafe, basi mimi ni bingwa wa kuitopoa sumu yake!” yanadhihirisha uhasama uliokuwepo baina ya wanandoa hawa wawili.

Bafe ni aina ya nyoka mwenye sumu kali kwenye mate yake. Tabitha anaamini kuwa ulimi wa mumewe ni kama ule wa bafe. Hivi ni kusema kwamba Bwana Konzi hutoa maneno makali kwa mkewe. Tabitha mkewe anapolipiza kisasi anatoa maneno makali zaidi kuliko ya mumewe na kujidai kwamba ana uwezo wa kuitopoa sumu atoayo mumewe. Matini inayorejelewa katika simulizi hii ni ya imani za kiasili au kishirikina. Katika jamii za kale mja yeyote mwenye uwezo wa kuizima sumu ya nyoka anaaminika kuwa na nguvu za kishirikina zisizo za kawaida. Nguvu za kishirikina zinadhihirika pale ambapo inasemekana kwamba baada ya vitisho vya Tabitha Bwana Konzi hakuweza kwenda haja kubwa wala kufanya haja ndogo. Haikuwezekana tena kwa Bwana Konzi kufika hotelini tena kutangamana na wanawake jinsi alivyozoea. Kama jina lake linavyoashiria, alitiwa “konzi” (komeo) yaani alifungwa.

Ni dhahiri kuwa mkewe Konzi alitumia nguvu za ushirikina kumroga mumewe ili kumdhibiti kutokana na “jicho la nje”. Konzi alipopelekwa katika hospitali kuu ya Machakos madaktari walishindwa kumsaidia. Mwandishi anasema hata picha za uyoka hazikuonyesha tatizo lolote. Tumbo lake liliposikizwa kwa stetoskopu kilichosikika ni sauti iliyofanana na kuwika kwa jogoo. Alishauriwa na daktari kurudi nyumbani ambapo mkewe alicheka na kumzomea. Baadaye alimpiga kofi dogo shavuni na tatizo lake likaisha. Imebainika kuwa Tabitha alitumia uchawi kumwadhibu mume wake kwa kumvunjia heshima. Jamii ikikosa mbinu mwafaka za kuipa haki inajitafutia mbinu zake mbadala. Katika muktadha huu, mbinu aliyotumia Tabitha inavunja utaratibu na maadili katika jamii. Inaharibu mahusiano katika ndoa kwa kiwango kikubwa. Kwa kawaida mke humtunza na kumheshimu mumewe kwa vyovyote vile. Vilevile, ni bora kutambua

kwamba mizozo ya kijamii huleta madhara makuu. Mambo ya ushirikina yanachukuliwa kama tabia zilizopitwa na wakati lakini kwa mujibu wa matini hii ni dhahiri kwamba bado zinategemewa kama mbinu ya utafutaji suluhu ya matatizo ya jamii ya kisasa. Funzo linalopitishwa ni kuhusu umuhimu wa uaminifu katika maisha ya ndoa. Uaminifu huu ukikosekana jamii nzima huathirika kwa njia hasi. Inambidi kila mwanajamii aanze kutafuta utambulisho wake. Simulizi ya imani ya kijadi zinazohusu matumizi ya kondo kama kitambulisho imetumika kuelezea;

“Nitarudi **kondo yangu** ya nyuma imezikwa huku!” (Wamitila, 2004, uk. 4)  
Msimulizi wa riwaya ya *Musaleo!* ametumia taashira, “kondo” kurejelea imani za kijadi. Imani zinazohusishwa na kondo zaweza kuonyesha jinsi jamii inavyoathamini kitu chochote ambacho inamiliki. Katika muktadha wa nukuu hili, umilisi unaorejelewa ni wa ardhi (tafsiri yangu). Riwaya inaeleza kwamba mahali binadamu alipozaliwa pana historia muhimu kuhusu asili na jadi yake. Hivyo, kila mwanajamii ana haki ya kumiliki ardhi ambamo alizaliwa, yaani pale kondo yake ilipozikwa. Kondo ni mfuko anaokalia mtoto ndani ya tumbo na ambao hutoka baada ya mtoto kuzaliwa. Ni kiungo muhimu katika ukuaji wa mtoto. Uunganishaji wake na mtoto huonyesha uhusiano usiotenganishika baina ya mtoto na mama ila tu baada ya kuzaliwa kwa mtoto. Hata hivyo, baada ya mtoto kuzaliwa, uhusiano huo huendelezwa na nguvu za damu na mapenzi. Umiliki unaolinganishwa na kondo unatiliwa maanani kiasi kwamba hata binadamu husika akiondoka au akiondolewa anaweza kurudi na kudai ardhi yake kwa ushahidi kwamba kondo yake imezikwa mle. Riwaya Mpya teule zimepanua wazo hili kuhusu matatizo ya umiliki wa ardhi katika mataifa yanayoendelea na kuonyesha kuwa iwapo wanajamii wangeheshimu asili zao za kijadi hakungekuwa na matatizo ya umiliki wa ardhi. Vivyo hivyo, jamii inakumbushwa tena kwamba suluhu ya matatizo ya ardhi imo mikononi mwao. Kinachohitajika ni kufanya uamuzi wa busara kisha kutenda haki kwa mujibu wa sheria zilizowekwa kwani zinatambulika vizuri na wanajamii. Kumbukumbu za yaliyopita ni njia nzuri ya kuwasaidia wanajamii kutafuta suluhu kwa matatizo yao. Vile vile, riwaya zimetoa wosia kwa wanajamii kuwa wazalendo wa nchi zao na kuzitetea kwa vyovyote vile badala ya kuhalalisha maovu. Riwaya ya *Musaleo!* Inadokeza;

“...nani asiyeiba nchi hii? Alijiuliza. Nani ambaye anaweza kuaminiwa kwa kusema ukweli? Alishangaa. ...anayesema ukweli ni mimi tu, mimi Mzee!” (Wamitila, 2004, uk. 33)



Wanaoendeleza wizi ni viongozi ambao mara nyingi wanajitokeza kama waja wasioridhika. Kila wanapoiba mali ya umma wanajiliwaza kwa maneno, “*nani asiyeiba nchi hii?*” kumaanisha kuwa kila mtu ni mwizi nchini kwa hivyo wizi si kitendo kibaya. Viongozi huwadhulumu raia kwa kupora rasilimali zake na kusingizia kuwa ni sawa kwa sababu kila mtu anaiba. Uporaji wa rasilimali za umma ndio unaosababisha umaskini uliokithiri, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana na ukosefu wa huduma bora. Hali ya dhuluma inasababisha uasi dhidi ya serikali. Raia wanajiunga pamoja katika makundi ya ukombozi ili kutafuta suluhu ya matatizo yanayoikumba jamii yao. Serikali nayo hupinga mapinduzi kwa nguvu nyingi. Wakati mwingine vijana hutumiwa na walio mamlakani kupinga mapinduzi labda kwa sababu hawana kazi nyingine. Ujumbe unaowasilishwa hapa ni kuwa vijana katika mataifa yanayoendelea wanatumiwa vibaya na viongozi.

Ujumbe huo pia umewasilishwa kwa kunga ya simulizi fupi ambayo imeendelezwa kwa kuzingatia kipengele cha mwingilianotanzu ambapo mitholojia ya kisanduku cha Pandora. Hadithi ya kisanduku cha Pandora ambayo imefichika katika masimulizi ya riwaya teule inapatikana katika mitholojia moja ya jadi ya Kiyunani. Katika mitholojia hii maarufu inaaminika kuwa baada ya miungu kumwumba mwanamke ilimpa jina, Pandora. Miungu hiyo ilimtunukia sifa kem kem kama urembo, ucheshi, haiba, lugha shawishi, udadisi na pia udanganyifu. Kisha mungu Zeus alimpa Pandora kisanduku kwa maagizo kwamba asikifungue. Pandora alikishikilia kwa muda mfupi lakini roho ya kudadisi ikampa hamu ya kutaka kujua kilichokuwa ndani na ikamsukuma kukifungua. Ndani ya kisanduku hicho mlitoka kila aina ya uchafu. Simulizi inaendelea kueleza kuwa wakati maovu yalipokuwa yakitoka, Pandora alishtuka sana na kukifunga kisanduku ghafla, kumbe alifungia tumaini ndani! Angesubiri kidogo badala ya kufunga. Uchafu huo ni ishara katika riwaya husika inayowakilisha mateso na maovu kama vile hila, udanganyifu, vurumai, chuki na njaa. Kwa mujibu wa mitholojia hii, vijana wanapewa vifedha vidogo vidogo ili kupinga mapinduzi.

Maafa mbali mbali yanayofanana na yale yaliyotoka kwenye kisanduku cha Pandora huikumba taifa, mambo huharibika na kukawa na vita nchini. Kisanduku cha Pandora pia kimetumiwa katika riwaya kama ishara ya kuwapa wanajamii hasa wanaume (kwa mujibu wa muktadha wa simulizi fupi) matumaini katika ulimwengu wa sasa wenye mateso mengi. Vilevile, hadithi hii inabainisha kuwa mwanamume anahitaji kujihami na mbinu za kukabiliana na ila zinazodumu

katika bongo za wanawake. Ili kuwaelewa wanawake vizuri, ni sharti kila mwanamume aelewe vidumuvyo katika akili zao. Mintarafu ya maelezo haya taswira ya jamii ya sasa inashabihiana na kisanduku cha Pandora. Imejaa maovu ya kila aina. Baadhi ya maovu yanayofananishwa na kisanduku cha Pandora, yanayorejelewa na kutajwa katika riwaya teule ni kama inavyodhihirika katika nukuu lifuatalo;

“*Coup d’etat*. Ukabila. *Ethnic Cleansing*. Wazazi wakafa, wakabakia watoto waliolazimishwa kushika bunduki. Shule wakasusia. Kwa kifupi, sanduku la Pandora lilifunguliwa upya. Lilibakia wazi maskini!” (Wamitila, 2004, uk. 101)

Mwandishi Wamitila ametumia mitholojia nyingine za kale kuzungumza na jamii yake. Hivi ni visa vya Mashimo ya Mfalme Suleiman na Robinson Kruso. Mfano huu umebeba ujumbe kuhusu chanzo cha wizi kwa hadhira. Simulizi hii imempa mwizi jina mwinyi:

Mikono yake ilizoea kushikashika na kupakatapakata vitu vya wengine; huku kwetu tunasema ukimwona mtoto anafanya hivyo jua umezaa mwizi. Wazee wanaosimulia kisa cha jitu hili wanasema kuanzia siku hiyo lilijulikana kama Jivi. Lilijaa kiburi na kujiona bora kuliko wengine. Basi Jivi lilianza kujiendea huku na huku; likavuka kwake na kuhamia kwa jirani. Kila lilichopata lilitwaa na kubugia kinywani. Lilipokatazwa lilitumia ile mikono mingi likabinya, likasongoa na likaua. Haukupita muda mrefu likawa limesababisha maafa, watu wakatoroka makwao. Mwili wake ulikuwa mkubwa sasa. Likashindwa na kutembea na kuishia kuagiza lifanyiwe kila kitu. Kazi yake ikawa kukaa tu kusimulia visa vya Mashimo ya Mfalme Suleimani, Robinson Kruso na kuimba wimbo wa Arya na mwingine wa Bora-mimi-Kitovu. Watu walipoliangalia wakasema hili limezidi sasa. Likapewa jina jingine: Mwinyi (Wamitila, 2004, k. 89-90)

Hii ni hadithi iliyo ndani ya hadithi kuu. Msimulizi anaeleza kuhusu tabia za wezi. Wizi huanza kwa kitendo cha kuviziavizia. Jivi huanza kuiba kwa jirani kisha kusambaza vitendo hivyo katika kijiji kizima. Hadithi hii imetumika kuashiria chanzo cha ubepari na umwinyi kwamba wahusika walianza na kuchovyachovya kidogo kidogo, kisha wakaanza kutwaa bila hofu huku wakitawaliwa na kiburi. Kwa mujibu wa riwaya, baada ya kutwaa vya kutosha wakoloni walishindwa kurudi makwao kisha wakaanza kuzitawala hisia za watawaliwa kwa kuwapumbaza kwa kasumba za kikoloni walizowasomesha kwenye vitabu vya kigeni kama *Mashimo ya Mfalme Suleiman* na *Robinson Kruso*.

Maovu mengi yametapakaa katika jamii na taifa kwa jumla ila yapo matumaini. Ingawa mambo yameharibika nchi inaweza kuchipuka tena na kupaa kimaendeleo iwapo wenyeji watachukua

majukumu yao kikamilifu. Kuna uwezekano wa kupata uhuru kutokana na madhila yaliyopo. Iwapo jamii itatia bidii kujikomboa kuna uwezekano wa kupata tumaini jipya lenye mustakabali mzuri kwa sababu ya “kuzaliwa upya” na kuwepo kwa “mwanzo mpya” kama katika wazo hili:

Baadaye ilitangazwa hata kwenye redio ya taifa. Hiki ni kipindi cha mwanzo mpya. Hiki ni kipindi cha kuzaliwa upya. Ya kale hayapo tena. Mtu hawezi kuzaliwa upya asipokuwa na jina jipya na kwamba hicho kinachozaliwa upya kina uwezo mkubwa kuliko kilichokizaa (Wamitila, 2014, uk. 2)

“Kuzaliwa upya” ni ishara ya nchi au taifa lenye mwamko mpya. Baada ya uzinduzi kutoka gizani kutakuwa na jamii mpya ambayo itapendeza zaidi kuliko jamii ya jadi. Ujenzi wa jamii mpya utazaa kizazi kinachowajibika. Maovu ya awali kama ubadhirifu wa mali ya umma, dhuluma, vita vya kikabila, mapinduzi ya serikali, ukosefu wa ajira hasa miongoni mwa vijana, hali ya uchumi kudorora, madeni miongoni mwa mengine yatazikwa katika historia. Kizazi kipya kitang’aa gizani. Kitakuwa bora kuliko kizazi cha jadi.

#### **4.2.4 Matumizi ya Matini za Kitaaluma**

Kwa lengo la kukamilisha ujumbe katika riwaya zake za kisasa mwandishi Wamitila ametumia kunga ya urejeleomatini. Istilahi urejeleomatini ni tafsiri ya neno la Kiingereza “*intertextuality*” lililotumika kwa mara ya kwanza na mwanafalsafa mfaransa, Julia Kristeva katika kitabu chake cha ‘*Dialogue and Novel*’. Kwa mujibu wa Kristeva (1980), kila neno ni urejeleo wa maneno mengine. Hivyo, kuna msisitizo kwamba matini huhusiana na kutegemeana ili kuleta maana. Stam (2000) katika Anderson (2004) ananukuliwa;

“Matini yoyote ile iibukayo lazima iwe imelala pamoja na nyingine au na matini nyingine ambayo ile ya awali imelala nayo” (uk.1)

Usemi huu unadhihirisha kuwa kazi ya fasihi iliyotafitiwa haikutoka kwenye akili ya mtunzi pekee au katika ombwe tupu bali ni mkusanyiko wa matini nyingine tofauti tofauti. Anderson (2004) anadai kuwa urejeleomatini huhusisha “yale yaliyosemwa tayari”. Urejeleomatini ni kipengele muhimu cha usasaleo ambamo mwandishi wa kisasa anatumia kuandikia kazi yake. Hivyo, urejeleomatini ni mojawapo wa kunga kuu ya uandishi wa kimajaribio ambayo imetumika katika riwaya zilizotafitiwa.

Enani (2005) anadai kwamba urejeleomatini huathiri namna ya usomaji wa matini mpya hasa unapokuwa mwingi na wenye mitindo tofauti tofauti. Riwaya teule zimethibitisha kuwepo kwa urejeleomatini wa kimtindo. Vipande vingi vilivyorejelewa katika riwaya teule vimeathiri msuko na ploti katika riwaya za kisasa. Hadhira (msomaji) inatiliwa huko na kutolewa kule. Msomaji anasoma kipande cha hadithi kilicho na matini rejelewa na kabla ya kukikamilisha kingine kinaanzishwa. Mbinu hii ya uandishi inachangia pakubwa katika kuleta uchangamano katika riwaya husika hivyo kuukatiza usimulizi. Wamitila (2010) anadai kuwa urejeleo wa aina hii waweza kuzua kuwepo kwa kazi hasi au chanya. Utafiti huu umebaini kuwa urejeleomatini ni kisababishi cha uchangamano katika riwaya za kimajaribio na kupendekeza mbinu za kuukabili.

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981:271) yale ambayo mwandishi wa kisasa anayasema ni zaidi ya matamko yenyewe. Hii ni kwa sababu miktadha mbalimbali huathiri kazi ya fasihi kwa njia tofauti. Miktadha kama ya kiuchumi, kijamii au kisiasa huathiri mahusiano fulani katika kazi za fasihi (Wamitila, 2010). Kwa mujibu wa haya, uchanganuzi huu umetambulisha aina za miktadha tofauti tofauti iliyorejelewa katika riwaya teule, mahusiano yake na jinsi inavyochangia katika uwasilishaji wa maudhui. Kupitia kwa mbinu ya kimajaribio ya urejeleomatini, mwandishi amefanikiwa kubainisha shughuli, imani na tabia za jamii anamoandikia. Hivyo, taswira kamili ya jamii imebainishwa kwa kuangazia mambo ya aina aina yanayojidhihirisha katika jamii husika kupitia kwa matini zilizorejelewa na mtunzi.

Mintarafu ya haya matini zinazorejelea falsafa mbalimbali za fasihi kama utamaushi zimetumika. Vile vile, sanaa ya utendaji na filamu imebainika riwayani. Taaluma nyingine iliyorejelewa ni matibabu na saikolojia; zote hizi kwa minajili ya kuihamasisha jamii. Kwa kutumia matini rejelewa za kitaaluma, riwaya zimewasilisha maudhui ya dhuluma, ukoloni-mamboleo na ukoloni-mkongwe, ubepari na matumizi mabaya ya mamlaka na ufisadi. Isitoshe, kunga ya urejeleomatini imetumika kubaini chanzo cha uozo uliomo katika jamii ya sasa kwa jumla. Matini zilizorejelewa zimewasilishwa katika simulizi fupi fupi, dayolojia na matumizi mbalimbali ya lugha.

Kwa uwiano na Nanjira (2010) inabainika kutoka kwa riwaya mpya kwamba nchi zinazoendelea huwadhulumu wananchi wake kwa njia tofauti tofauti. Njia hizo hujitokeza zaidi katika jinsi huduma zinavyotolewa. Kwa sababu mbalimbali ambazo msanii huenda akawa nazo, dhuluma

kwa raia huwasilishwa kwa njia ya uandishi wa fasihi. Kazi za fasihi zilizoangaziwa katika utafiti huu zimeweka bayana mateso na dhuluma za raia mikononi mwa walio mamlakani. Baadhi ya mateso yaliyoangaziwa ni pamoja na ukosefu wa huduma muhimu kama matibabu, makazi safi, ukosefu wa mashamba na ajira kwa vijana. Athari kuu ni kuitamausha jamii.

Falsafa ya utamaushi inathibitika pale daktari anapomwambia mhusika Yosi Kanga kuwa alikuwa na uvimbe kichwani. Kwa mujibu wa Diegner (2005) falsafa hii inashikilia kuwa hatima ya binadamu ni kifo. Aidha, mwandishi amebainisha falsafa ya kitaaluma kwa kutumia uzoefu wake kama daktari. Japo ni kinaya kuwa hakuna uchunguzi wowote aliofanyiwa mgonjwa, daktari alizidi kumtaja kwamba hakuwa na siku nyingi za kuishi kama inavyodhihirika katika uchanganyaji wa lugha katika uzungumzi nafsiya wa daktari anapozungumza na kumshauri mgonjwa wake hospitalini:

Inavyoelekea ...mmm...ana tatizo la *brain tumour*...au hata *intracranial hypertension*...! Ikiwa *diagnosis* yangu ni sawa kwa sababu sijawahi kukosea katika miaka yote hii niliyofanya kazi ya udaktari, ana siku kama ishirini na nane za kuishi...*in fact it might even be less!* (Wamitila, 2011, uk. 31)

Falsafa ya utamaushi pamoja na ujuzi wa kitaaluma umetumiwa kumdhulumu Yosi kimawazo na kihisia badala ya kutumika kumpa matibabu yafaayo. Ni dhuluma kwa sababu daktari anatoa uamuzi wa kutamausha kabla ya uchunguzi wa kimatibabu kufanywa. Baadaye kabisa, picha za uyoka zilipopigwa ilibainika kuwa Yosi alikuwa buheri wa afya. Daktari husika alikuwa amejigamba jinsi alivyokuwa mtaalamu aliyesomea udaktari katika vyuo-tajika, “*alumnus wa prestigious universities*”, Hivyo, alipozungumza kuhusu hali ya mgonjwa wake, Yosi alijua na kuamini ukweli kwamba siku zake duniani zilikuwa zimefikia ukingoni. Kuna umuhimu wa kuchunguza jinsi masomo yanavyoendeshwa katika vyuo vikuu. Visibakie kuwa vyuo tajika tu na “*alumnus*” wake hawawezi kuifaa jamii katika mambo yawategemeayo zaidi kama afya. Ni hali ya kusikitisha kuona kwamba katika mataifa yanayoendelea hali ya afya inazidi kudorora licha ya kuwa na madaktari wengi waliohitimu katika vyuo tajika. Sababu zinazoyafanya mataifa yanayoendelea kuamini na kutafuta matibabu ya magonjwa sugu kama saratani Ughaibuni zimefafanuliwa. Kuna uwezekano kwamba ni kwa sababu ya ukosefu wa maarifa miongoni mwa madaktari wa nchi husika. Suluhu ni kuwa iwapo mitalaa ya masomo vyuoni itafumwa vizuri na sera ziangaziwe ifaavyo, mataifa ya Afrika yataweza kujitibu na kujiinua kiafya na pia kiuchumi.

Hata hivyo, hali ya maisha inapombadilikia binadamu, binadamu huyo huyo anakubali hali yake na kutafuta mbinu nyingine za kujiliwaza.

Kwa kujikita katika maoni ya Lyotard (1997), usimulizi umeendelezwa katika riwaya mpya kwa kuzingatia matumizi ya maoni ya kifalsafa au kitaaluma. Lyotard amefafanua kwamba shinikizo na changamoto za ndani hueleweka vyema zikihusishwa na falsafa au usomi fulani, jambo analozingatia mwandishi wa kisasa kwa dhati. Pia katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* maudhui ya dhuluma yamewasilishwa katika simulizi fupi inayorejelea maoni ya falsafa ya kitamaushi;

“...vyuma vilivyolika na kuanza kuonyesha shumizi ya kutu hapa na pale, godoro dogo la usumba na kufunikwa shuka iliyochujuka rangi na kufanana na nguo iliyomwagiwa maji na kutoa mabakabaka” (Wamitila, 2011, uk. 25)

Ujumbe uliowalishwa kwa kutumia falsafa ya utamaushi ambayo imeipelekea hadhira kukubali kuwa dhuluma anayopitia mhusika Yosi Kanga akiwa hospitalini ni hatua moja katika safari ya hatima yake ambayo ni kifo. Mazingira ya hospitalini alipolazwa Yosi ambaye ndiye mhusika mkuu katika riwaya hii yalikuwa mabaya. Mwandishi anasema kwamba vitanda vilikuwa vya zamani. Jamii ya leo inafahamishwa kwamba yenyewe imekubali kunyanyaswa na kudhulumiwa hasa kupitia kwa uongozi mbaya usiojali mahitaji ya kimsingi ya jamii. Mwandishi anasimulia kuwa mazingira ya hospitalini alimolazwa Yosi yalikuwa mabaya. Magodoro yalikuwa ya usumba yaliyofunikwa shuka zilizochujuka rangi. Hali hii ya dhiki ilikuwepo kwa muda mrefu pale hospitalini wala hakuna yeyote aliyedhubutu kutoa malalamishi yoyote. Kupitia kwa dayolojia hii riwaya imefanikiwa katika kuufichua uozo uliopo serikalini kwa kuonyesha huduma duni wanazopokea wagonjwa katika hospitali za umma.

Isitoshe, hali ya ukosefu wa huduma bora hospitalini inamdhulumu mhusika Yosi Kanga aliyekuwa tayari ameambiwa na daktari kwamba alikuwa akingojea kifo kwa sababu ya uvimbe uliosemekana kuwepo katika ubongo wake. Zaidi ya hayo, Yosi anadhulumiwa katika hisia zake. Ifikiapo mwisho wake wa mawazo, Yosi anajiliwaza kwa mawazo ya kitamaushi kwamba:

...nitapumzika nitakapokuwa mfu baada ya siku chache na kama watu wetu wasemavyo siku zilizohesabiwa ni chache – huisha kwa kufumba na kufumbua”. Inasemwa kuwa alipowasiliana na jamaa zake huko kwao alikotoka walimshauri aondoke. “Hakuna haja ya kuendelea kukaa huko, utakuja kufa bure!” lakini walimshauri ahahakikishe

amejipenyeza katika bongo za wenyeji wa sehemu hiyo. Hakikisha unajipenya ndani kwenye kiini cha bongo zao. Hakikisha kuwa unapenyeza kabisa katika uboho wa mifupa yao. Hakikisha kuwa umezama katika kiini cha seli zao! Lazima uwe halisi na ndoto wakati huo huo (Wamitila, 2004, uk. 67)

Matini iliyorejelewa inahusu taaluma ya falsafa elimu nafsia inarejelewa. Mukstadha matini husika ni wakati ambapo mzungu mkoloni alikuwa akiondoka katika mataifa ya Kiafrika baada ya mataifa hayo kujipatia uhuru ambapo Wazungu walishauriwa na wenzao wayaokoe maisha yao kwa kuondoka na kurudi kwao. Walizidi kushauriwa kwamba hata ingawa ni sharti waondoke wahakikishe kwamba wameziteka hisia za waafrika kwa kujipenyeza kwenye bongo zao na kuingia katika uboho wa mifupa yao. Huu ndio uliokuwa mwanzo wa ukoloni-mamboleo na ukoloni-mkongwe. Japo mzungu mkoloni aliondoka Afrika, Waafrika bado wanamtegemea katika maswala mbalimbali kama siasa, afya, uchumi miongoni mwa mengine. Jambo jingine linalobainika ni jinsi jamii ya sasa ilivyokosa matumaini ya kujitegemea yenyewe. Daima mataifa ya Kiafrika yamezama katika vilindi vya madeni kutoka kwa “mefu” (IMF) na mashirika mengine ya ughaibuni kwa sababu ya kukosa kujiamini (Nyabunga, 2005). Mzungu mkoloni aliondoka Afrika lakini bado anatawala. Waafrika wanajidai kuwa na uhuru lakini bado wako katika jela la utumwa kama vile matini hii inavyobaini;

“Kilio cha haki hakifi! Wafao ni watu wenyewe. Sauti inabaki hai kama yalivyo maneno yenyewe!” (Wamitila, 2004, uk. 77)

Japo binadamu anaweza kuondolewa duniani pamoja na athari zake, hali zilizomkumba, maoni yake na imani yake kuhusu yaliyompitikia hubaki. Usemi “kilio cha haki hakifi” unawatia waja ari ya kuzidi kupigania na kutafuta haki hadi ipatikane. Kizazi cha leo kinafahamishwa kuwa haki inapotafutwa, kuna hatari ya kuupoteza uhai. Hata hivyo kizazi hicho kinafaa kujua kwamba hata ingawa kuna uwezekano wa kuyapoteza maisha yake, ni muhimu iwapo kila neno kilichotamka kuinusuru jamii likisalia na kukumbukwa na wanajamii watakaobaki. Vitendo na wosia wake wa sasa utavifaa vizazi vingine vya baadaye. Himizo ni kwamba kila mmoja atie bidii ya kuacha hiba itakayokumbukwa baada ya kuondoka kwake.

Taaluma ya utafiti pia imetumika. Msimulizi katika riwaya teule za kisasa ametumia sanaa ya uandishi bunifu kuongeza maarifa kwa jamii kupitia katika uwanda wa taaluma ya utafiti. Utafiti ni kitendo kinachofuata hatua mbali mbali, moja baada ya nyingine. Jambo la kwanza analofanya mtafiti ni kukusanya data inayohusiana na mada ya utafiti. Baadaye anaipanga data kabla ya

kuichanganua. Hatimaye mtafiti huandika ripoti kuhusu matokeo ya utafiti wake ambayo huelekeza binadamu katika uboreshaji wa hali na maisha yake kwa jumla. Kwa mfano, iwapo utafiti umefanywa katika shirika fulani matokeo hutumiwa kurekebisha makosa yaliyobainika na kubadilisha jinsi ya kuendesha shughuli mbalimbali katika shirika husika ili kuafikia mafanikio zaidi. Jamii inahimizwa kujitolea kufanya utafiti kuhusu matatizo yake ili ipendekeze njia bora za kuleta suluhu kama inavyoelezwa katika dayolojia ifuatayo:

Ikiwa unataka kufanya utafiti fulani, lazima uende ilipo data-chasili yako. Ardhi tunayotaka kuchunguza iko msituni; katika msingi huu basi hatuwezi kuuchukua penginepo. Udongo wa baharini hauwezi kutufaa. Au sijui mwenetu una pendekezo la kisasa zaidi? Unaweza kuwa unajua jambo tusilolijua sisi! (Wamitila, 2014, uk. 85)

Kwa mujibu wa riwaya teule imeendelea kubainika kwamba data inayochunguzwa lazima itoke katika eneo linalotafitiwa ili iwe kiwakilishi cha jamii nzima. Hiyo ndiyo itakayokuwa sampuli ya utafiti. Vivyo hivyo, shida nyingi zinazopatikana katika mataifa yanayoendelea hutokana na wanajamii wenyewe. Wanajamii wanawakilishwa na “data-chasili” iliyorejelewa na mwandishi. Mojawapo wa njia za kupata suluhu ni kuelewa chanzo cha shida zenyewe. Hivyo, utafiti mwafaka unaofuata hatua zinazohitajika hutoa matokeo bora. Utafiti usipofanywa huenda jamii ikakosa kupata ufahamu kisha ikajipata katika hali ya maangamizi. Hata hivyo, riwaya zinadokeza kuwa wakati mwingine utafiti unaweza kufanywa lakini ukawa ghushi. Aghalabu, ili kupata suluhu la kudumu kwa matatizo yanayoikumba jamii ya sasa, inapendekezwa katika riwaya mpya kuwa ni lazima utafiti ufanywe mahali panapofaa na kwa njia inayofaa. Hii ndiyo njia ya kuangamiza dhuluma inayoendelezwa na viongozi kwa wanajamii.

Taaluma ya historia aidha haikuachwa chuma. Mambo ya kale yamewekwa katika riwaya ili kumpa msomaji nafasi ya kuyatafiti na kuyaelewa zaidi. Aghalabu historia huambatana na siasa. Matini zilizorejelewa katika riwaya teule ambazo zinahusu taarifa za matokeo ya zama zilizopita zimechanganuliwa. Taarifa hizo zinawahusu watu mahususi wakiwa katika shughuli zao katika wakati fulani uliopita. Matini husika zimetumiwa na mwandishi wa riwaya teule kuwasilisha hali mbali mbali katika jamii yake kama itakavyodhihirika katika uchanganuzi wa simulizi ifuatayo:

Katika ziara hii nilikutana kibahati na wazee kadha waliokuwa wakiishi katika vibanda dhafu na waliochongwa na ala za maisha ya dhiki. “Mzee hawa ni wakongwe



walioifanyia nchi hii kazi kubwa! Ni wapiganaji wa uhuru; unaweza kuwaita War Veterans. Waliahidiwa mengi kama mashamba, nishani pamoja na kujengewa minara katika Uwanja wa Uhuru na majina yao kuingizwa katika orodha ya waandika historia lakini bado wanasubiri (Wamitila, 2004, uk. 19)

Matini iliyorejelewa inawakumbuka mashujaa walioupigania uhuru wa nchi za Kiafrika. Walifanya kazi nzuri lakini waliishia kusahaulika. Msimulizi anaangazia jinsi viongozi wa kisasa wanavyowaahidi wananchi mambo mazuri wasiyoyatimiza hata baada ya kuwa uongozini kwa muda mrefu. Wananchi wanaishia kuhadaiwa tu. Hivi sasa katika jamii mbalimbali za Afrika mashujaa hao wameshasahaulika na uongozi wa nchi zao. Wengi wao wanaishi katika hali zinazokatisha tamaa. Mashujaa husika walipokuwa wakipigana waliahidiwa mengi mazuri lakini baada ya kupatikana kwa uhuru walishasahaulika kabisa. Riwaya za kisasa zimehimiza kuhusu umuhimu wa wanajamii kuhifadhi na kuheshimu kumbukumbu za historia ya jamii yao. Aidha, riwaya zinazidi kutoa wito kwamba jamii za sasa zinapaswa kuwafidia watu maalumu waliopigania uhuru wa mataifa yao badala ya kuwatelekeza. Hali ya kutelekeza makundi fulani ya watu katika jamii imezalisha utabaka katika jamii ya kisasa ambapo tabaka la chini hukandamizwa na tabaka la juu.

Nilishika njia kutoka tulipokuwa na kuufuata ujia ulioelekea sehemu iliyokuwa zamani ikiitwa *Government Quarters*. Huko kuliishi watu waliokuwa wakifanya kazi serikalini wakiwepo wakurugenzi wa mashirika ya umma, mawaziri na makatibu wakuu kadha. Miaka mingi imepita tangu nilipokuwa sehemu hii mara ya mwisho, sikuwa na dhamira maalum katika matembezi yangu isipokuwa kupoteza muda tu (Wamitila, 2004, uk. 23)

Urejeleomatini katika simulizi fupi hii unabaini kwamba hali ya utabaka inakithiri katika jamii ya kisasa. Mwandishi anasimulia kuwa watu waliokuwa na vyeo vikubwa serikalini wakati wa ukoloni walitengewa sehemu za kuishi mbali na akina yakhe wanaofahamika kama walala-hoi yaani mbali na kelele na vumbi. Mwandishi anasema kuwa sehemu walizoishi wenye vyeo serikalini zilifahamika kama *Government Quarters*. Kwa mujibu wa riwaya inayorejelewa nyumba zilizokuwa zimetengwa zilijengwa kwa kutumia rasilimali za taifa. Katika misingi hii mwandishi ametumia simulizi hii fupi kuonyesha taswira ya jamii ya kisasa ambapo viongozi wakuu serikalini wameendelea kutumia rasilimali za umma kujinufaisha na kuboresha maisha yao pekee. Inasikitisha zaidi kuona kwamba baada ya wakoloni kuondoka, mandhari ya *Government Quarters* yalianza kuharibika. Kwa mujibu wa simulizi hii, msimulizi anaonyesha taswira kwamba Waafrika hawawezi kuaminiwa na utawala wala uwajibikaji katika nchi zao.

Inabainika katika riwaya kwamba mara tu mkoloni alipoondoka sura ya nchi ilibadilika. Viongozi Waafrika waliojawa na tamaa na ubinafsi walichukua usukani. Badala ya kutumika kuboresha maisha ya wanajamii, walijinufaisha wenyewe. Ajabu ni kuwa viongozi wanafurahia na kuishi maisha ya raha mustarehe huku wananchi wanaolipa ushuru wakiangamizwa na matatizo mengi ya kijamii. Baadhi ya matatizo hayo ni kama njaa, barabara mbaya, ukosefu wa elimu bora, ukosefu wa ajira kwa vijana na uchafuzi wa mazingira. Hata hivyo, riwaya zinashikilia kuwa njia ya pekee ya kuisaidia jamii ni kufanya utafiti.

Kwa kusema “kikulacho ki nguoni mwako” mwandishi ametumia kunga ya mwingilianotanzu ambayo ni ufundi katika taaluma ya fasihi. Utanzu wa fasihi simulizi kipera cha methali umewekwa katika utanzu wa riwaya. Usemi huu unaipa wosia jamii ya sasa na kuitaka kutojiingiza katika matatizo yaletwayo na ukoloni mamboleo kwa kuwaaminia wageni rasilimali zake. Mwandishi anawakumbusha wasomaji wake ambao ndio wanajamii kuwa, ni muhimu kwa Waafrika kutambua kwamba wanafaa kuwa waangalifu kuhusu viongozi wa mataifa yao baada ya kupatikana kwa uhuru. Japo mkoloni alikuwa dhalimu, riwaya zimeonya kuwa viongozi Waafrika wamekuwa dhalimu zaidi. Kuhusu viongozi hawa, riwaya zimebaini kwamba kuwa na kiongozi Mwafrika ni kama, *“kutoka walipo ndovu ukashusha pumzi kumbe unaelekea waliko mbogo”*. Usemi huu unamwashiria ndovu kama mnyama mkubwa, mwenye nguvu nyingi na ambaye wakati mwingine huwa mharibifu sana. Kwa upande wake mbogo ni mnyama mkali na mharibifu. Akilinganishwa na mbogo, ndovu ni mtulivu. Kwa hivyo, ni hatari zaidi kusazwa na ndovu kisha kutupwa au kuelekezwa kwa mbogo.

### **4.3 Hitimisho**

Sura ya nne imebaini kuwa uandishi wa Wamitila wa kimjaribio umejikita katika matumizi ya kunga tofauti tofauti za uandishi. Kunga zilizobainika katika utafiti huu ni matumizi ya majina ya watu, vitu na mahali, matumizi ya matukio yasiyo ya kawaida (uhalisiajabu), matumizi ya dini, mitholojia na simulizi za Kiafrika na matumizi ya matini za kitaaluma. Simulizi fupi fupi zenye matini mahususi rejelewa zimetumiwa ili kuonyesha taswira kamili ya jamii ya sasa. Imebainika kwamba mtendakazi yeyote yule ana uhuru wa kujaribu mbinu mpya za kutekelezea kazi yake bila kujibana na kujikita katika sheria za jadi. Vivyo hivyo, imeibuka kuwa mtunzi wa riwaya ana uhuru wa kujaribu mbinu mpya za utunzi bila kubanwa na mbinu za kijadi ambazo zinajiegemeza katika msingi wa uhalisia. Hata hivyo, kuna hatari kwamba usomaji na uelewa wa

riwaya zilizotumia mitindo mingi kwa pamoja unahitaji ufahamu wa kiada wa maswala mengi yanayohusiana na majina ya watu, mahali na vitu, falsafa mbalimbali, taaluma mbalimbali, dini, simulizi za Kiafrika, siasa, lugha pendwa na mengine.

## SURA YA TANO

### MCHANGO WA MBINU ZA KIMAJARIBIO KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI KATIKA RIWAYA ZA KISASA ZA KYALLO WADI WAMITILA

#### 5.1 Utangulizi

Sura hii imeonyesha mchango wa mbinu za kimajaribio katika riwaya teule kwamba yamewasilishwa kwa njia fiche. Maudhui yaliyowasilishwa yanaonyesha taswira kamili ya jamii ya kisasa. Madhumuni ya pili na ya tatu yamefafanuliwa katika sura hii. Matokeo yamefafanua madhumuni ya pili na ya tatu. Katika kuafikia hayo, mtafiti amebainisha jinsi uandishi bunifu wa kisasa ulivyo kama ilivyobainika kutokana na uchanganuzi wa riwaya zilizoteuliwa. Riwaya zinatoa mwito wa kipekee kuhusu mchakato mzima wa uandishi bunifu yaani utunzi, uhariri na uchapishaji. Vile vile changamoto wanazokumbana nazo waandishi wa kisasa hasa pale kazi zao zinapopitia mikononi mwa wahariri na wachapishaji zimebainishwa. Aidha, baadhi ya mapendekezo yatakayoboresha na kukuza riwaya za kisasa kama yanavyojitokeza katika riwaya teule yamefafanuliwa.

#### 5.2 Uwasilishaji wa Maudhui kwa Njia Fiche

Mbinu za kimajaribio zimechangia katika uwasilishaji wa maudhui ya aina aina japo kwa njia fiche. Mwandishi ameyaficha maudhui yake katika mbinu za kimajaribio alizotumia. Kila palipohusishwa kipengele chochote cha kimajaribio kama vile, simulizi fupi, taashira, dayolojia, urejeleomatini, miongoni mwa vingine, ujumbe kwa hadhira ulipitishwa. Katika sehemu hii, maudhui yaliyowasilishwa yamemwangazia mtunzi kama mshikadau mkuu katika swala zima la uandishi bunifu. Aidha, matatizo ambayo yameukumba uandishi bunifu wa kisasa kama mwito wa kipekee wenye hisia kali yamefafanuliwa. Hususan, sehemu hii imeangazia ule mwito wa kipekee ambao humsibu mtunzi wa kisasa pindi anapojipata katika changamoto zinazomkosesha amani na matumaini ya kuendelea. Changamoto hizo huwa njia ya pekee ya kubainisha ukweli kuhusu jamii kama inavyoakisiwa na msimulizi wa riwaya ya *Musaleo!* pale anaposema;

“Kariha yake ya kuandika humjia nyakati kama hizi anapokuwa amezongwa na hali kama hizi” (Wamitila, 2004, uk. 34)

Hali zinazorejelewa ni kwamba zoezi zima la utunzi, uhariri na uchapishaji wa kazi za fasihi ni gumu. Taswira inayoibuka ni kwamba mwandishi wa kazi yenyewe hufaulu zaidi nyakati zile

anapozongwa na hali ngumu. Katika muktadha wa mwandishi hapo juu hali zinazotajwa ni kukataliwa kwa mswada wa mwandishi aliouwasilisha kwa minajili ya kuchapishwa. Ni hali ambazo zinaonekana kumtia kiwewe. Kwa kuwa kila mwandishi bunifu wa fasihi ana uwezo wa kujiangamiza au kujijenga (Gallop, 2011), yeye mwenyewe anaamua kuwa japo kuna viunzi vinavyozuia ukamilifu wa kazi yake, kamwe hatanaswa na viunzi hivyo. Uamuzi anaoufanya ni kwamba, kadri viunzi na vizingiti vinavyokuwa vikali hamu yake ya kuandika humjaa pomoni. Uandishi kama mwito wa kipekee huimarika zaidi wakati mambo yanapokuwa magumu. Mwandishi hupata msukumo na nguvu zaidi za kuandika hali zinapomwia ngumu. Kama ilivyo kwamba kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa mapishi riwaya zinazidi kuhimiza kuwa kukataliwa kwa mswada si mwisho wa uandishi. Ari na motisha ya uandishi haiwezi kuzimwa na changamoto za aina yoyote ile. Mwenye uwezo wa kuuzima mwito wa uandishi bunifu ni mwandishi mwenyewe pekee. Aidha, katika upekee wa uandishi, maswala ya kindani yanayoibua hisia kali kuhusu uandishi na uchapishaji wa riwaya za kisasa yanaibuliwa. Huku wahariri na wachapishaji wakiuchukulia uandishi bunifu kama kitega uchumi, mwandishi anauenzi kama jambo linalofikiriwa kwa umakini na kuwasilishwa kwa ustadi. Mintarafu ya haya, kuzidi kuandika katikati ya magumu ni mbinu moja ya kuwahimiza waandishi chipukizi kuwa wasikate tamaa.

Burke (1992) anadai kuwa mtunzi ni binadamu wa kisasa aliyejengwa na jamii. Mtunzi anaweza kutenganishwa na nafsi yake lakini kamwe hawezi kutenganishwa na jamii. Kwa mujibu wa haya riwaya za kisasa zimebaini kuwa kama mwanajamii na binadamu mwenye wito wa kipekee, mtunzi ana uwezo wa kuchora taswira kamili ya jamii anamoishi kupitia uandishi wake. Hivyo, mwandishi anafanyika kuwa mwenye kumiliki kariha, yaani binadamu mwenye ile ari na kani inayomshika hadi akawa na dukuduku la kutaka kueleza jamii yake katika tajriba yake ya kiutunzi (TUKI, 2015). Uandishi ni mfano wa donge linalomkaa rohoni na ambalo ghafla hupata njia aula ya kueleza kupitia kazi ya kifasihi atakayoitunga. Donge hili linalomsakama mtunzi kooni, lazima litoke ili mtu apumue! Katika utaratibu huo, kariha ni nguvu zinazomsukuma mwandishi katika mustakabali wake wa uandishi. Hata hivyo, si kila binadamu humiliki zihii. Katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji!* riwaya inasema;

“...kila mwandishi huwa na kariha ya utunzi...kitu fulani ambacho huwa ni kama utambi unaowasha mshumaa wake wa utunzi. Nadhani Aristotle alikiita *divine afflatus*...

Alisema bila hicho mtunzi hawezi kutunga. Ukijaribu utababaisha tu!” (Wamitila, 2004, uk. 17)

Mwandishi kama mshikadau muhimu katika taaluma ya uandishi anaelewa fika kile kilichomchochea kuandika hadithi yake jinsi alivyoandika. Kutokana na usimulizi huu mwandishi anatumia uandishi kuitetea ari yake kuwa uandishi si jambo la kawaida bali ni mwito ambao hata pengine yeye binafsi hawezi kuukadiriwa wala kuelewa. Uandishi unaotokana na msukumo uliojawa na sauti nyingi zisizomaizika ndio unaodumu; uandishi mwingine utababaisha tu. Kwa hivyo, ni pendekezo la riwaya mpya kwamba kazi ya mtunzi ichukuliwe kama matokeo ya uvumbuzi wa sauti ambazo haziwezi kuhusishwa na uvumbuzi wowote mahususi, ila ubunifu wa mwandishi wa kipekee wenye nguvu za kiungu. Wazo hili linatiliwa mkazo na Burke (1995) anaposema; hisia za kuandika zinapompata mwandishi huwa hawezi kuzizuia wala kuzipuuza. Inambidi ayaandike yaliyo akilini mwake katika muundo na mtindo wowote anaouona sawa kwa kuwasilishia ujumbe wake. Uwezo wa kutunga unajitokeza pale mwandishi anapowaumba wahusika na kuwaweka katika hali zinazosadikisha kile anachosimulia.

Akimrejelea Aristotle, msimulizi wa *Mwandishi Msomaji na Mchaphishaji* anafafanua wazo la uandishi kama msukumo wa ndani unaoitwa “*divine afflatus*.” Neno hili la Kilatini linamaanisha nguvu zilizomo ndani ya mwanadamu zinazomsukuma katika kutekeleza jambo fulani. Kulingana na riwaya, ni dhahiri kuwa ndani ya mtunzi mna nguvu zinazompa msukumo usioweza kusitishwa kwa lolote lile. Japo wahariri na wachapishaji huwa na tabia ya kumtamausha mwandishi kwa kuipuuza na kuitupilia mbali miswada yake, hatima ya uandishi bado huwa ni ufanisi. Hii ni kwa sababu msukumo na upekee wa mwandishi bunifu husababisha kazi za fasihi zenye mantiki (Wilson, 2004). Ndio maana katika riwaya ya *Musaleo!* msimulizi anadai kwamba ari ya mwandishi haiwezi kusimamishwa na lolote lile. Ni wazimu; unapokuja haupingiki wala kuzuiliwa. Maudhui haya yameibuliwa na nukuu kwamba;

“Ninachojua tu ni kwamba hamna mwandishi mwenye akili timamu. Zamani nilifundishwa kuwa wanapoandika wanajiwa na kitu kilichoitwa *Divine Afflatus*, kitu kama wazimu hivi tuseme!” (Wamitila, 2004, uk. 133)

Nadharia ya kiutunzi ya Aristotle inasisitiza kuwa mtunzi hupatwa na hali ya uendawazimu inayomfanya abuni kazi ambayo hata yeye mwenyewe hawezi kubaini namna alivyoibuni. Huwa amepagawa na hali hiyo inapomkumba, uwezo fulani wa kiungu humjia na kumfanya kutunga

kazi yake. Swala la kariha linapounganishwa moja kwa moja na dhana ya Aristotle kuhusu ubunifu huufanya uandishi bunifu kuwa tukio moja kuu la mwandishi.

Riwaya teule zimefafanua kuwa, ili uandishi wa kisasa upate ubora utakaoleta fanaka katika zoezi zima la uandishi na uzalishaji wa kazi za fasihi ni sharti kila mtunzi awe na sifa ya msukumo usiozuilika. Iwapo mwandishi yeyote anaazimia kufaulu katika utunzi anafaa kufahamu kwamba kufaulu kwake ku mikononi mwake pekee. Ni yeye pekee aliye na uwezo wa kuifaulisha kazi yake. Hivyo iwapo uandishi bunifu utakosa kufaulu lawama zote zi kwa mwandishi atakayeshindwa kuutoa msukumo uliomo ndani yake katika maandishi. Huu ni wito kwa waandishi bunifu kwamba wasiwalaumu wahariri na wachapishaji tena ila wajitwike mzigo wa kuhakikisha kuwa kazi zao zimefikia hadhira lengwa kwa vyovyote vile. Kwa mujibu wa wataalamu wa fasihi mwandishi bunifu hawezi kufaulu bila kuutendesha kazi msukumo ulio ndani yake. Ndio ujumbe unaowasilishwa katika usemi kuwa;

“Wataalamu wa fasihi wanasema kuwa huwezi kuandika wala hakuna mwandishi aliyewahi kufanya hivyo pasi na kuupata msukumo huo. Kitu fulani kinachowasha!” (Wamitila, 2014, uk. 17)

Kwa mujibu wa Freud na Strachey (2010) hisia za kiroho na kiakili zina misingi katika mivurugo ya kumbukumbu kwenye sehemu za nafsi zisizoeleweka vizuri na mtu mwenyewe. Mivurugo hiyo hujidhihirisha katika ndoto za binadamu. Ule “wazimu” wa mtunzi humpelekea kutimiza ndoto ya uandishi na uzalishaji wa kazi ya fasihi. Tendo hili linabainishwa katika maneno ya riwaya teule ya *Musaleo!* kuwa;

“Ninaota siku moja kuiandika riwaya. Na sio riwaya tu lakini riwaya mahususi ambayo haitakaa tu isomwe bali itasaidia usomaji wake” (Wamitila, 2004, uk. 2)

Kwa kutumia simulizi fupi mwandishi anadai kuwa angependa kuiandika riwaya mpya ambayo ingejisoma yenyewe. Katika simulizi hii, taashira "*kujisoma yenyewe*" imetumiwa kudhihirisha kwamba hadithi husika itakuwa kioo halisi cha jamii inayorejelewa. Ili jamii ifahamike, mwandishi bunifu atahitajika kukubali msukumo usiozuilika wa uandishi ili ndoto yake ya kuionyesha jamii yake kwa nyingine itimizwe. Katika simulizi fupi hii, iliyorejelewa kutokana na dini ya Kikristo, mwandishi anaendelea kusema kuwa hadithi atakayoitunga itaitwa *Musaleo*. Katika muktadha unaorejelewa, "*Musaleo*" ni ufupisho wa "*Musa wa leo*" yaani mkombozi wa leo. Matini hii ya kidini imetumiwa kuleta kumbukumbu ya kiongozi wa kabila la Israeli

aliyefahamika kama Musa. Katika dini ya Kikristo, imerekodiwa katika Biblia kitabu cha *Kutoka* kuwa Musa alikuwa mkombozi wa wana wa Israeli. Inaaminika katika dini hiyo kwamba Musa alitumwa na Mungu kuwakomboa Waisraelei kutoka utumwani Misri walikotumikishwa na Firauni. Hivyo ndivyo alivyofanyika kuwa mkombozi. Vivyo hivyo, inabainika kuwa baadhi ya mataifa ya Kiafrika yanayoendelea yanahitaji mkombozi wa kuyatoa katika utumwa wa maovu yanayoyakumba. Baadhi ya maovu husika ni kama vile njaa, mauaji na ufisadi unaosababishwa na matumizi mabaya ya mamlaka. Mintarafu ya haya, riwaya mpya itajisoma yenyewe kwa kuibaini taswira hii ya jamii ya kisasa, matatizo yake na mapendekezo kuhusu ukombozi wake. Aidha, inatarajiwa kuwa “Musa wa leo” ataikomboa jamii kutokana na uongozi dhalimu miongoni mwa matatizo mengine. Kwa kutenda haya, nguvu za kipekee zilizomo katika uandishi zinampa mwandishi uwezo wa kuisawiri jamii jinsi ilivyo, kuonyesha matatizo yake na kupendekeza mbinu za kupata suluhu. Hivyo mtunzi amechorwa kama chombo cha mawasiliano yanayoleta suluhu la matatizo ya kijamii. Kupitia kwa uandishi wake, utendakazi wa kawaida unaendelezwa pale ambapo uwezo mkubwa wa uandishi unapitishwa. Maelezo haya yanawiana na maoni ya Halliwell (1992) anaposema kwamba uwezo wa kuwa na mhemuko wa ubunifu wenye nguvu hutokana na mwongozo wa kiungu. Mintarafu ya haya, kazi ya mtunzi utambuzi na zoezi la kiakili linaloonyesha uwezo na urazini wala si silika; ni jambo lililofikiriwa kwa umakini mkubwa.

Riwaya za kisasa zimeifaninisha kazi ya mtunzi na msukumo uliosanwa kwa njia ya kipekee. Aidha, zoezi la uandishi ni sanaa ambayo hufanywa kwa uangalifu (Malenya, 2012). Riwaya za kisasa husika zinapendekeza kwamba riwaya zenyewe zisipuuziliwe mbali kwa madai kwamba muundo wake umekiuka ukawaida. Hii ni kwa sababu ni riwaya zilizosanwa na kufumwa kwa njia ya kipekee. Kwa mujibu wa msimulizi katika riwaya teule, ukamilifu wa riwaya hutokea baada ya muda mrefu sawa tu na jinsi msanii anavyochukua muda wake kutengeneza vifaa kwa umakini huku daima matumaini yake yakiwa ni kuwavutia wapokeaji wake.

Mtunzi anapopata msukumo na wazo la kuandika lazima ajiandae vilivyo katika mazoezi ya kupanga hoja, mbinu za lugha na nadharia za utunzi ili ziambatane na wazo lake kwani ni zoezi linalochukua muda mrefu. Mtunzi huandika kutokana na msururu mrefu wa vidondoa vingi vyenye misingi ya kitamaduni isiyohesabika. Barry (2009) akimnukuu Barthes amedadavua kuwa matini bunifu si sentensi moja ya maneno yanayowasilisha maana moja inayofahamika na



kila msomaji bali ni uwasilishaji wa mawazo mengi yasiyo asilia mengine yakipatana huku mengine yakikinzana. Katika misingi hii riwaya zimebaini kuwa mtunzi “*husana*” kazi yake kwa ubunifu mkubwa. Usanii humfanya mtunzi kubuni kazi yake kwa umakini huku akilenga kuiweka katika kiwango kinachozidi ukawaida mithili ya mbegu ya haradali. Hata ingawa kwa wahariri na wachapishaji mwanzo wa uandishi huonekana kama uvumi, mwisho wake huwa fanaka kwa sababu ya subira ya mtunzi. Simulizi fupi yenye urejeleomatini wa hadithi ya Shakespeare inayohusu haradali imetumika katika riwaya ili kuelezea ukweli huu. Haradali ni mbegu ndogo sana ambayo inapopandwa na kuota huchukua muda mrefu kukua lakini baadaye huwa mti mkubwa. Mti huo unapozaa, mbegu zake hutumika kukipa chakula ladha nzuri. Aidha, mti huo huwa makao ya ndege wengi. Haradali ya ubunifu imetumika kuashiria subira katika utunzi bunifu ambao matokeo yake huwafaidi wote, msomaji na mchapishaji wakiwemo. Kwa mujibu wa riwaya teule, mtunzi hutumia mambo madogomadogo katika jamii ambayo mara nyingi huanza kama uvumi ili kujenga ubunifu wake. Hatimaye subira na ukomavu huzaliwa kama inavyopendekezwa katika;

“Kwamba katika kiini cha kimbunga cha uvumi kuna haradali ya ubunifu. Ni kama kilele cha wimbi ambacho alisema Shakespeare kuwa kuna ufanisi” (Wamitila, 2014, uk. 19)

Hata hivyo, riwaya zimekiri ukweli kwamba ubunifu wa kisasa umekiuka ukawaida. Ingawa ubunifu hutokana na msukumo wa ndani wa hisia za mtunzi, kwa msomaji kufahamu yatokanayo na msukumo wenyewe, ni sharti atambue kwamba uandishi wa kisasa umesanwa kwa njia changamano. Uandishi changamano unahitaji ufahamu wa mambo mengi kiada ili ufasirike. Hii ni kwa sababu ujumbe ukusudiwao haujitokezi waziwazi. Utafiti huu umebaini kwamba licha ya ukweli kuwa riwaya za kimajaribio zimetokana na msukumo mzito wa hisia za mtunzi, utunzi wenyewe umewasilishwa kwa njia zisizoeleweka. Hivyo, mtunzi wa kisasa anafaa kuchunguza uwezo na kiwango chake cha ubunifu ili ajiepushe na fedheha ya uandishi wa kubabaisha. Kazi ambayo haikufanyiwa uchunguzi wa kiada inalinganishwa na mganga anayerogonya tu. Riwaya ya *Mwandishi Msomaji na Mchapishaji* inasema:

...waandishi wengi hawana uelewa wa kina wa masuala na nadharia ya fasihi. Wanachokuwa nacho ni huo mdadi unaowajia na kuwapa raghba na kuwafanya waandike kazi huku wametwaliwa na nguvu za ajabu, tena wengi wanasombwa tu na kimbunga cha mdadi kama mganga anayepandwa na mdadi na kuanza kurogonya na kuandika tu mambo wasiyoyajua vizuri (Wamitila, 2014, uk. 18)

Riwaya inapendekeza kuwa kila mtunzi anafaa kuandika kuhusu yale anayoyafahamu vizuri na iwapo sivyo, atafute uongozi wa nadharia katika utekelezaji wa wajibu wake. Msimulizi anajaribu kueleza kuwa uandishi wa kijazba usioegemezwa kwenye nadharia hautakuwa na muwala. Uandishi wa kijazba, kama anavyosema msimulizi huwa bora zaidi unapoegemezwa katika nadharia maalum ya fasihi. Hivi ni kusema kwamba mtunzi anapoongozwa na nadharia ya utunzi hujibana katika kutunga kazi yenye wigo bunifu ikizingatia maisha ya binadamu. Badala ya kurogonya nadharia itamwongoza msanii kubuni kazi yenye ujumbe mzito itakayowasilishwa katika lugha inayosadikika. Kwa mujibu wa riwaya, nadharia ni kifaa bora cha kumwongoza mtunzi katika kugusa hisia za ndani ya nafsi za hadhira lengwa.

Isitoshe, riwaya zimebaini kwamba uandishi bunifu hutokana na umaizi, ufunuo, mvuto na uwezo wa kuathiri. Maoni haya yanawiana na yale ya Roland Barthes katika Mike na Gane (2004) wanapodai kuwa uandishi wowote hutarajiwa kuathiri hadhira na kutoa taswira kamili ya jamii yake. Katika riwaya teule msimulizi anatoa ufunuo kuhusu uandishi wa kisasa kwamba si swala la kujipatia pato pekee bali ni jambo lililofikiriwa na kupangwa kwa umakini mwingi. Isitoshe, si kila uandishi uliopo ama utakao kuwa una uwezo wa kuiathiri jamii. Kwa minajili ya haya kuna umuhimu wa kuchunguza kile kinachopelekea kuwepo kwa aina za uandishi usio na mvuto wa kuiathiri jamii kama inavyokusudiwa katika fasihi. Katika riwaya teule, msimulizi anaonyesha kuwa uandishi usiotokana na ujuzi, umahiri na msukumo wa ndani humotishwa na swala la kiuchumi hasa katika kizazi hiki cha Karne ya Ishirini na Moja ambapo kila mja huwa mbioni kutafuta pesa. Ajabu ni kuwa huu ndio uandishi unaokubalika machoni pa wasomaji, wahakiki, wahariri na wachapishaji. Kinyume na matakwa ya mchapishaji, riwaya zimesema kuwa mtunzi hupata msukumo wa kuandika kutokanana na watu anaolingiliana nao. Kwa hivyo, kama mwanajamii, mtunzi husoma kwa mapana na marefu na kufanya utafiti wa kina kuhusu yale anayokusudia kuandika kuhusu jamii yake. Mintarafu ya riwaya za kisasa, ufahamu wa kina wa jamii, matumizi ya nadharia na utafiti hukamilisha tajriba ya uandishi bunifu.

Riwaya zimeongeza kuwa utafiti ni nguzo kuu ya uandishi bunifu. Mtunzi bunifu anafaa kusoma ili kufanya utafiti kuhusu maswala mbalimbali kama vile dini, uongozi na historia kabla ya kuanza zoezi la uandishi bunifu. Hivyo, mtunzi stadi hawezi kutunga riwaya kabla ya kufanya utafiti wa kina kuhusu jamii anamoandikia. Usomaji wa mapana na marefu ukiambatana na utafiti utamwelekeza mtunzi kwenye uteuzi wa mbinu za lugha na sanaa ili kuwasilisha taswira

kamili ya jamii jinsi aionavyo. Nadharia pamoja na utafiti ni mambo mawili ambayo hayawezi kutenganishwa katika ulimwengu wa uandishi bunifu. Matokeo ya matendo haya mawili ni uandishi uliopangwa kwa utaratibu na ustadi wenye mantiki. Utafiti huu umeafikia kuwa kila mtunzi mwenye shauku ya kuathiri jamii kupitia kwa ubunifu wake ana shuruti ya kubukua vitabu vingi. Kwa kutumia riwaya, msimulizi anapendekeza kuwe na matumizi bora ya maktaba zilizomo kufanyia utafiti kwa minajili ya kupata ufahamu na kunufaisha akili.

### **5.3 Taswira ya Jamii ya Kisasa**

Mabadiliko ya kiubunifu yaliyoshuhudiwa yanawiana na taswira kamili ya jamii ya kisasa inayopendelea kufanya mambo pasi na kufuata utaratibu maalum kwa mfano, miundo na mitindo tofauti ya utunzi iliyotumika na kutapakazwa kote katika riwaya. Japo mwandishi anatekeleza jukumu lake la kuiwasilisha taswira kamili ya jamii katika uandishi, mtafaruku baina yake kwa upande mmoja na msomaji na mchapishaji kwa upande mwingine unatishia kuiangamiza tajriba yake. Riwaya zilizochunguzwa zilithibitisha kuwa mtunzi wa riwaya za kisasa si mtunzi tu bali ni binadamu mwenye uwezo na mwito wa kipekee. Zinaulinganisha utunzi wake na jambo linaloibua hisia kali ndani ya nafsi yake.

Kwa mujibu wa Lyotard (1984) uandishi wa kisasa unafungamana sana na utamaduni pendwa ambapo watu hufanya mambo namna wanavyotaka wenyewe bila kufuata kanuni zozote . Mawazo haya pia yameangaziwa na Jameson (1991) anayesema kwamba jamii ya kisasa haina uzoefu wa kufuata taratibu zozote katika shughuli zake. Katika misingi ya maoni haya, utamaduni pendwa ambao ni mhimili mkuu wa usasaleo unaambatana na fasihi pendwa. Sifa moja maarufu katika fasihi pendwa ni “mkondo wa ung’amuzi” ambao ni mbinu ya kisimulizi katika uandishi wa kinathari inayotumia maelezo marefu yanayoyamulika mawazo yanayompitikia mhusika akilini (Wamitila, 2010). Kwa mbinu hii mawazo ya ndani aliyonayo mhusika huwasilishwa kwa mapana na marefu. Carter (2006) akimnukuu Lyotard anafafanua kwamba uandishi wa aina hii hukiuka kaida na kanuni zote za utunzi. Kanuni anazorejelea Carter zaweza kuwa za kimuundo au/na za kilugha. Katika uandishi wa kimajaribio, lugha hutumiwa kwa njia huru sana bila kuzingatia ufasaha na usanifu wake. Pia, mwandishi huwa na uhuru wa kuchanganya lugha mbalimbali kwa mfano Kiingereza na Kiswahili au lugha za kwanza na

Kiswahili au hata lugha nyingine ngeni. Aghalabu, lengo lake huwa ni kuiburudisha na kuielimisha jamii.

Jinsi maisha ya kisasa yanavyokosa utaratibu ndivyo fasihi ya kisasa ilivyo (Baudrillard, 1988). Hata ingawa hali ya ukosefu wa utaratibu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali waweza kuonekana kana kwamba haufai, Baudrillard anasema kwamba, unajitosheleza kwani kutofaa huko ndiko maisha ya kisasa. Isitoshe, Baudrillard anaendelea kudokeza kwamba fasihi inapaswa kumulika jamii jinsi ilivyo, bila kufuata utaratibu maalum kwa kuwa jamii imejawa na fantasia za namna mbalimbali. Tanzu za fasihi hasa riwaya zafaa kuwa na simulizi fupi fupi ndani yake badala ya hadithi moja ndefu iliyoandikwa kwa njia ya uhalisia kwa sababu hata jamii ya sasa yenyewe ambayo ndiyo inayoangaziwa na riwaya husika haina utaratibu wa kihalisia. Mtazamo huu uliuelekeza utafiti katika uchambuzi na uchanganuzi wa simulizi ndogo ndogo zinazorejelea maswala na matini tofauti tofauti. Matini husika ni zile zilizotumika katika riwaya teule katika uwasilishaji wa maudhui. Aidha, zilitumika kuangaza maswala mbalimbali ya kijamii ya sasa hasa katika uwanda wa uandishi bunifu zikiwemo nyanda nyingine. Mawazo haya ndiyo yaliyoweka msingi wa kuchanganua mabadiliko yanayohusiana na utunzi wa kimajaribio, changamoto zake na umbo la mwandishi wa kisasa kama mwanajamii na kazi yake kama alivyoubika katika riwaya teule za Wamitila.

### **5.3.1 Changamoto za Uandishi Bunifu wa Kisasa**

Sehemu hii imeshughulikia baadhi ya changamoto anazokumbana nazo mtunzi wa riwaya mpya kama ilivyoelezwa katika riwaya zenyewe kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za kimajaribio. Utafiti umebaini jinsi kando na uandishi kuwa mwito wa kipekee wenye kuibua hisia kali, ukamilishaji wake u mikononi mwa wahariri na wachapishaji. Mwandishi anaweza kujiandaa vilivyo kwa kufanya utafiti na kuchagua nadharia ifaayo kuiongoza kazi yake ila jitihada zake zikakwamizwa na mhariri na mchapishaji. Mintarafu ya haya, sehemu hii imefafanua jinsi juhudi za mtunzi zinavyolemazwa na shauku yake kukatizwa na washikadau wenzake, yaani mhariri na mchapishaji. Hapa utafiti umetambulisha na kunakili chanzo cha changamoto anazopata mtunzi baada ya kuwasilisha mswada wake, visababishi vya changamoto hizo na jinsi anavyokabiliana nazo. Aidha, mapendekezo kwa mtunzi ili kujinasua kutokana na ukandamizaji wa wahariri na wachapishaji, uandishi bunifu kwa jumla, usomaji na uchapishaji bora kama yalivyowasilishwa katika riwaya teule mefafanuliwa. Riwaya zimeziwasilisha changamoto hizo kwa kutumia mbinu

tofauti tofauti za kimajaribio kama vile simulizi fupi zilizohodhi dayolojia nyingi na taashira, urejeleomatini, na uhalisiajabu.

Kama ilivyotajwa awali katika utafiti, uandishi unaoathiri ubunifu kisawasawa unahitaji kufanyiwa utafiti kiada tena kwa kina. Kwa hivyo, mtunzi husika hana budi kubukua vitabu vingi. Katika usomaji wake, simulizi fupi ifuatayo imebaini kwamba mwandishi bunifu hukumbwa na tatizo la ugumu wa kufanya utafiti wa kiada kutoka maktabani kwa sababu ya ukosefu wa vitabu vinavyofaa. Riwaya zimesema kuwa vitabu vilivyomo maktabani na makavazini havitoshelezi shauku hii. Aidha, idhini ya kuvipata haipo ila kwa “kujuana” kama inavyodaiwa katika simulizi fupi ifuatayo:

Tangu siku nyingi akitamani kujuana na mfanyikazi wa pale kwa ajili ya utafiti wake kuhusiana na uandishi wake. Alijua fika kuwa vitabu na maandiko yote yaliyopigwa marufuku yalipatikana katika jumba hili. Palikuwa na maktaba ndogo kwenye jengo hilo iliyojaa tungo za wasifu wa kiongozi wa nchi na tafsiri za hadithi nyingi za kizamani kutoka Ulaya, visasili vya Uyunani na mashairi ya Ki-Urdu. Palikuwa pia na matokeo mbalimbali na ya zamani ya tafsiri za Biblia. Lakini ajabu ya ajabu: hapakuwa na kitabu hata kimoja cha Historia! (Wamitila, 2004, uk. 65)

Kwa mujibu wa msimulizi wa *Musaleo!* makavazi na maktaba yaliyopo yamejaa maandishi kutoka Ughaibuni. Inatarajiwa kwamba katika maktaba na makavazi ya nchi kuwe na vitabu vinavyohusu historia za nchi husika. Kinyume na haya maktabani hakukuwa na kitabu hata kimoja cha historia ya taifa. Mtu yeyote angevihitaji vitabu vilivyokuwepo ingawa havikumfaa hakuwa na budi “kujuana” na mfanyikazi mmoja maktabani. Ni kinaya kuwa lazima kuwe na “hali ya kujuana” ili kuvifikia vitabu vilivyo maktabani. Maktaba inafaa kuwa wazi kwa kila atakaye kuitumia. Swali analojiuliza mwandishi ni, “mbona iwe rahisi kupata maandishi kuhusu historia ya nchi nyingine ilhali isiwezekane kupata ya historia ya mwenyeji?” (ufasiri wangu). Imebainika dhahiri kuwa mtunzi anapoitunga kazi yake anahitajika kuwa na ufahamu wa mazingira anamoandikia, jambo ambalo maktaba zilizomo hazina uwezo wa kulifanikisha.

Baada ya mtunzi kuukamilisha uandishi wake, anauwasilisha mswada kwa mhariri kwa minajili ya kukaguliwa na kutolewa idhini ya kuchapishwa. Mhariri na mchapishaji kwa pamoja wanaandaa kikao cha kujadili mustakabali wa mswada ambapo mwandishi pia anaalikwa ili autetee. Changamoto iliyopo ni kwamba msomaji ambaye ndiye mhariri ameshasoma mswada wenyewe na akashindwa kuuelewa. Kwa sababu hiyo kauli yake kwa mchapishaji inakuwa

kwamba riwaya haingeweza kuchapishwa kwa madai kuwa haikuwa ya kawaida kwani mtindo na muundo wake ulikiuka uhalisia. Maneno ya mwisho ya mhariri yalimtamausha mwandishi kwani yalikuwa;

“Kauli ya mwisho: haichapishiki!” (Wamitila, 2014, uk. 3)

Hali ya kukataliwa kwa mwandishi inadhihirika zaidi katika dayolojia iliyomo ndani ya simulizi fupi ambapo wahusika wanazumgumza kuhusu ripoti aliyoiandika mhariri na kuiwasilisha kwa mchapishaji. Kupitia dayolojia hii riwaya zimebaini kwamba mwandishi wa kisasa hudhulumiwa na mhariri na mchapishaji. Ni kinaya kuona kwamba juhudi zote za mwandishi zinaelekea kukomeshwa na mhariri mmoja tu! Mchapishaji anayategemea maoni ya mhariri ambaye tayari ameshaiambatanisha kazi ya fasihi na mwandishi. Uambatanishaji wa fasihi na mwandishi wake ni jambo analopinga Barthes (1968) kwa kusema; kuimbatanisha kazi ya fasihi na mwandishi ni kupunguza makali yake. Kwa upande mwingine madai ya mhariri ya kuutupilia mbali mswada wa mwandishi ni tetezi kuwa mtindo na muundo wake haukuwa wa kawaida hivyo riwaya ingekuwa tata na changamano kwa wasomaji. Sababu hizi zinatofautiana na maoni ya Fish (1972) anayedai kwamba uchunguzi na ukubalifu kamili wa kazi ya fasihi hauwi mikononi mwa mwandishi, mhariri wala mchapishaji bali u mikononi mwa hadhira. Hivi ni kusema kwamba zao la uandishi bunifu ni mali ya hadhira na jamii kwa jumla. Barthes (1968) anaendeleza mjadala huu kwa kupendekeza kwamba ili kuipa uhuru kazi ya fasihi ni sharti msomaji aitenganishe kazi husika na mwandishi na aitazame kama kazi mahususi ya fasihi. Ili kuepuka ufasiri uliojawa na utawala wa mtu mmoja mhariri na mchapishaji wantendee haki mwandishi kwa kuichapisha kazi yake ili kuiruhusu hadhira ipate nafasi yake ya kufanya uamuzi kuhusu yaliyomo pamoja na ubora wake (Graham, 2003). Fish (1972) anaongeza kuwa hadhira ndiyo mstahiki dhanifu katika uchunguzi wa kifasihi. Katika misingi hii, mwandishi anatoa taswira kwamba hadhira kama watumiaji wa fasihi haina budi kuchukua nafasi yake ya kuifanyia riwaya uchunguzi na uhakiki na kisha kutoa kauli ya mwisho kuhusu kazi husika. Kwa hivyo, thamani ya riwaya inapatikana kwa hadhira. Hapa riwaya zinaonyesha kuwa uzembe wa mhariri ndicho kikwazo kikuu cha uandishi bunifu. Hivyo basi haifai na wala haitoshi kusema kuwa riwaya ina mtindo usio wa kawaida kwani huku ni kuikosesha thamani kazi ya mwandishi kama inavyohibitishwa katika dayolojia hii;

“...jinsi wasomaji na wachapishaji wanavyokosa kuithamini riwaya ya mwandishi kwa kuwa wao wenyewe hawaielewi...” (Wamitila, 2014, uk. 18)

Ingawa matumizi ya miundo na mitindo isiyo zoeleka huwafanya wachapishaji kupuuza riwaya za kisasa na hatimaye kuiangamiza ari ya mwandishi, kwa upande mwingine mwandishi mwenyewe hujiangamiza (Gallop, 2011). Aidha, dhana ya “kifo cha mwandishi” inayochangiwa na Barthes (1968) inashikilia kuwa panapotokea mwachano baina ya mwandishi na hadhira yake kwa sababu ya ukosefu wa uhalisia katika uandishi, mwandishi husika huu taaluma yake. Mintarafu ya haya mwandishi yafaa ajitwike mzigo wa kukataliwa kwa kazi yake wala si kwa sababu ya mhariri. Kwa mfano katika riwaya teule, mwandishi anafahamu fika kuwa riwaya yake haikuwa imeandikwa katika mtindo uliozoeleka na ingekuwa vigumu mswada wake kuchapishwa haraka. Kwa haya, mwandishi anajiangamiza mwenyewe. Riwayani mwandishi anasema kuwa alitamani sana kuyasikia maoni ya mhariri kama vile mama mjamzito atamanivyo kuona mwisho wa mimba yenye usumbufu mkubwa. Tunaelezwa kupitia kwa matumizi ya taashira ndani ya simulizi fupi kwamba;

“Ikiwa kuna muswada wa riwaya ambao alitaka kuyasikia maoni ya msomaji ni huu. Mimba ya kuzaliwa kwake ilikuwa na usumbufu mkubwa na kama mjamzito mwenye himila ya aina hiyo anayetaka kuona mwisho wake, alitamani kuona mwisho wake ni nini” (Wamitila, 2014, uk. 3)

Taashira hii inabaini changamoto ya jinsi mwandishi anavyobaki katika safari ndefu ya kusubiri uchapishaji wa kazi yake. Tumaini lake likiwa ufahamu kwamba hata ingawa ‘mimba’ yaweza kuwa ya usumbufu, mwisho wake huwa bora kuliko mwanzo. Mtoto anapopakakwa furaha inayohanikiza huwasahaulisha mama na wahusika wengine taabu na matatizo waliyoyapitia wakati wa ujauzito. Vivyo hivyo, ingawa uandishi na uchapishaji wa riwaya unachukua muda mrefu na kukumbwa na changamoto tele, mwisho wake ambao ni chapa ya riwaya yenyewe ndiyo furaha ya mtunzi. Mwandishi huhisi vyema baada ya kuishika riwaya yake mkononi inapochapishwa. Akiirejelea kauli ya mwanafalsafa Barthes, Jonathan (2002) anasema kwamba ni wakati kama huo ambapo mtunzi pamoja na kazi yake huzaliwa kwa wakati mmoja. Riwaya zinatoa suluhu la tatizo hili kuwa mwandishi akuze kipawa chake cha uvumilivu na subira ambayo hatima yake ni heri. Mintarafu ya haya ni dhahiri kuwa ufanisi wa uandishi bunifu unapatikana palipo na uvumilivu, bidii na subira. Mwandishi anawasilisha fanaka yake kwa kutumia simulizi fupi ifuatayo;

“Jitayarishe naja mimi hadithi uliyenitafuta, labda utajua mwishowe au nitakueleza baada ya safari ndefu kwenye makaratasi haya. Haya jiandae” (Wamitila, 2004, uk. 2)

Dhuluma kwa mwandishi inazidi kuenezwa na ubinafsi wa wahariri na wachapishaji. Riwaya zimebaini hali hii kwa kufafanua kwamba wachapishaji wanajali maslahi yao ya jinsi watakavyopokea mifedha mingi wakiuza machapisho ya kazi za fasihi kwa wingi. Dhima yao kuu ni mauzo wala si kumkuza mwandishi. Ubinafsi, ubahili na udanganyifu katika sekta ya uchapishaji ni vitendo ambavyo vimeendeleza pakubwa kifo cha mwandishi wa kisasa. Wachapishaji wanaupa kipaumbele ubunifu unaowapa faida kubwa tena kwa haraka. Hatimaye, maslahi ya waandishi wanaotoa jasho jingi katika mradi mzima wa uandishi na uchapishaji yanapuuziliwa mbali. Hali hii ya ubinafsi inadhihirika katika dayolojia hii;

“Upitie haraka haraka...unaweza hata kufanya *skip reading* hapa na pale lakini hakikisha udhaifu wake unatawala. Amekuwa king’ang’anizi mno” (Wamitila, 2014, uk. 103).

Dhana ya “kuwa king’ang’anizi” ni taashira inayotoa taswira kwamba wachapishaji wanawaona waandishi wa riwaya za kisasa wakiwa wasumbufu badala ya kuwaona kama watu wenye hima na bidii ya kutimiza ndoto zao za ubunifu. Ili kuuzima usumbufu huo, wachapishaji wanawatumia wahariri kwa kuwaelekeza kwamba wakishasoma miswada kauli iwe moja, “haichapishiki”. Kwa kutumia mbinu ya kimajaribio ya simulizi fupi yenye dayolojia, ubinafsi wa wachapishaji unadhihirika pindi tu msomaji anapopendekeza kwamba, “ni hadithi isiyo ya kawaida hasa kwa wasomaji wetu, ifanyiwe *skip reading*” yaani isomwe haraka haraka na ripoti ikitolewa ionyeshe kazi yenye dosari nyingi. Dayolojia hii kati ya mwandishi na mchapishaji katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji* inabaini tamaa na ubinafsi katika vitengo vya uhariri na uchapishaji kama inavyodhibitishwa na maneno haya:

“Ni hadithi isiyokuwa ya kawaida...” hasa kwa wasomaji wetu eh...ehh. ehhh!” akachekacheka kabla ya kuendelea, “wajua soko letu kubwa ni shuleni bwana, huko nje hakuna atakaye kusoma, ni wasomaji wetu wachache tulio nao bwana, wanapenda njia walizozizoea. “Eh wasomaji wanaweza kushtuliwa na wasichokizoea” (Wamitila, 2014, uk. 16).

Taaluma ya uandishi inafikwa na msiba mwingine pale msimulizi anapoonyesha waziwazi namna wachapishaji wanavyothamini mauzo ya vitabu vya fasihi na faida watakayopata kutokana na mauzo hayo bila kuzingatia utendakazi wa vitabu hivyo kwa hadhira. Eagleton (2008) anaonyesha dhima moja ya fasihi kwamba ni kuwafanya wapokeaji wake kuzifikia hisia



zilizovilindini mwa miyo kuhusu tabia za watu ambazo hazingesemwa kadamnasi. Vilevile, fasihi hutumika kufunzia lugha kwa sababu ya kuwepo kwa tamaduni mbalimbali ndani yake (Damon *et al.*, 2006). Waandishi hawa wanaendelea kufafanua kuwa kuwepo kwa maswala ya kitamaduni katika fasihi hukuza mbinu za ujifunzaji lugha kwani lugha yenyewe ni sehemu ya utamaduni. Kando na haya, fasihi humkuza msomaji kisaikolojia na kumpa uelewa wa hisia zinazompa hofu (Hogan, 2011). Zaidi ya yote dhima ya fasihi ni burudani na kuwafaidi wajumi kwa kuwapa umaizi wa maoni ya mwandishi kuhusu hali mbalimbali za kibinadamu (Lombardi, 2020). Maoni haya kuhusu majukumu na dhima ya fasihi yanatofautiana na ya mchapishaji anayemchukulia mwandishi kama mzizi wake wa utajiri. Kwake fasihi ni kitega uchumi, jambo linalomwangamiza mwandishi bunifu.

Hali kwamba wachapishaji wa riwaya hawana haja ya kuchapisha kazi zinazouzika shuleni pekee ni kinyume na dhima ya fasihi. Hili ni pigo kubwa kwa uandishi wa riwaya mpya na ukuzaji wa kazi za fasihi kwa jumla. Hali hii inazidi kufunua ubinafsi wa wahariri na wachapishaji waziwazi kwamba hamu yao kubwa ni kuzalisha faida na si kueneza ufahamu wala kumkuza mwandishi. Kando na haya, riwaya zinabaini kwamba wasomaji waliopo hawako tayari kupokea kazi tofauti kifani huku wachapishaji wakitegemea shule kama soko kuu. Haya yanaibua taswira mpya miongoni mwa jamii kwamba wapokeaji wa fasihi ni wanafunzi labda kwa minajili ya kufaulu katika mitihani. Katika kutatua tatizo hili mwandishi kama mwanajamii anamtaka kila mmoja katika jamii awe msomaji na mpokeaji wa kazi za fasihi. Hata ingawa wanajamii hawapendi kuondoka kwenye mitindo waliyoizoea riwaya zimependekeza kuwa kukumbatia na kusoma riwaya za kisasa zenye fani zisizozoeleweka ni mbinu moja ya kupanua mawazo.

Hakuna riwaya yoyote iliyo kamilifu, riwaya zote hukamilishwa na wasomaji. Ni jukumu la kila msomaji kuikamilisha riwaya kwa kujaliza mapengo yalioachwa na mwandishi. Hivyo, lalama kwamba hadithi kamilifu pekee ndizo zinazofaa kuchapishwa hazina mashiko. Ni wajibu wa wahariri na wachapishaji kusoma na kuchapisha riwaya kutoka kwa waandishi ili kuipa hadhira nafasi ya kupanua ufahamu na ujuzi wao wanapojaza mapengo yalioachwa na mtunzi. Mintarafu ya haya wasomaji wote wanafaa kujilia na kujitafunia chakula walichoandaliwa na mwandishi kama inavyodhihirika katika dayolojia hii;

“Kwa kifupi tuseme hivi...hakuna hadithi yoyote inayosimuliwa katika ukamilifu wake...kila hadithi huwa na mapengo fulani? Hata hii ina mapengo? Akauliza Mchapishaji. Hii ni hadithi pia! Sasa hayo basi ndiyo tunapaswa kuyazungumzia” (Wamitila, 2014, uk. 19).

Hapa mwandishi na mchapishaji wanatambulisha kwamba hadithi ni matokeo ya kazi ya mwandishi yenye haki ya kupewa nafasi ya kuifikia hadhira. Dhana hii inatetewa na William Shakespeare katika mojawapo ya semi zake kama ilivyorekodiwa katika tamthilia yake ya *Henry VI* anapodokeza kuwa kazi ya mwandishi ni kuchukua kalamu na wino na kuandika yaliyo akilini mwake (Dobson, 1995). Isitoshe, mwandishi hubuni kazi mahiri ambamo hueleza mambo jinsi ayaonavyo japo kwa kutumia uchangamano wa hali ya juu.

### **5.3.2 Mapendekezo Kuhusu Uandishi na Uchapishaji wa Riwaya Mpya**

Sehemu hii inatoa mapendekezo ya kukuza uandishi bunifu wa riwaya za kisasa kama yanavyoakisiwa katika riwaya teule. Licha ya changamoto anazopitia mwandishi wa riwaya mpya, kuna matumaini kwamba uandishi bunifu wa riwaya mpya unaweza kufaulu, kukua na kuendelea mbele. Inakisiwa kuwa iwapo washikadau wote watayakumbatia mapendekezo yaliyodokezwa na riwaya huenda kwa kiasi fulani uandishi bunifu na uchapishaji hasa wa riwaya za kisasa ukapata nguvu na sura mpya. Mapendekezo hayo yanaelekezwa kwa mwandishi, msomaji na mchapishaji. Japo riwaya zimefafanua changamoto si haba katika uandishi, uhariri na uchapishaji wa riwaya mpya, riwaya zizo hizo zenyewe zimependekeza mbinu mbalimbali kwa mwandishi, msomaji na mchapishaji za kuyasuluhisha matatizo hayo.

Kuhusu mwandishi, riwaya zimempendekeza kuwa japo uandishi ni kariha yenye mwito wa kipekee huchukua muda mrefu kwani ni sharti kazi ipangwe hatua kwa hatua. Kwa mujibu wa riwaya, utaratibu ufuatao unakisiwa kumwelekeza mwandishi ifaavyo. Jambo la kwanza, kama mwanajamii, mwandishi atahitaji kufanya utafiti ili kujaliza kikamilifu mapengo ya kiusomi yaliyomo katika jamii anamoandikia. Pia, mwandishi auone utafiti kama mbinu au njia bora ya kutatua matatizo yanayoikabili jamii. Uandishi unaofaulu na wenye mnato hujiri baada ya kusoma kwa mapana na marefu kama asemavyo mtunzi katika simulizi fupi ifuatayo,

“Alivipitia vitabu alivyovipata na kuandikaandika madondoo fulani kwenye kidaftari chake cha kukusanyia mawazo anayoyatumia aandikapo. Kingunge alikuwa amebukua vya kutosha na kupata mawazo mengi aliyoyataka” (Wamitila, 2004, uk. 65)

Aidha, riwaya zimentaka mwandishi yeyote wa kazi za fasihi ajiepushe na mwenendo wa kijadi wa kuchapisha kazi ambazo hazijatafitiwa kwa kina. Ili kutimiza haya waandishi watarajiwa wazitumie maktaba zilizomo kwa manufaa ya kazi zao. Habari zote ziwe za siasa, dini, uchumi, mahusiano, lugha na nadharia hupatikana maktabani na huwa vijenzi muhimu vya uandishi bunifu. Zaidi ya hayo, utaratibu wa utafiti pia ni hatua ya kimsingi ambayo ni muhimu katika uandishi bunifu. Hatua hii imezungumziwa kwa kirefu katika riwaya zilizotumika katika makala hii. Mintarafu ya haya, uandishi utakaofaulu na wenye mnato huafikiwa baada ya kusoma.

Msimulizi katika *Musaleo!* anazidi kumdokezea mwandishi namna ya kuandika fasihi bora iliyokomaa baada ya kufanyiwa utafiti. Kwa kutumia simulizi fupi, riwaya zimeonya dhidi ya tabia za waandishi wengine ambao wanahusudu matumizi ya njia za mkato katika shughuli zao za uandishi. Ili jambo lolote lifaulu lazima mikakati na utaratibu uliowekwa ufuatwe kikamilifu tena kwa ustadi. Kwa mujibu wa haya ni sharti kila mwandishi aliye na shauku ya kuiathiri jamii kupitia kwa uandishi atimize masharti yote yaliyopendekezwa katika riwaya kuhusu utunzi bora; kusoma na kufanya utafiti. Katika kitengo cha kusoma, imependekezwa kwamba msomaji anukuu na kuhifadhi aliyoyasoma katika vijidaftari ili yasisahaulike. Aidha, katika kuhakikisha kuwa mpango na ratiba bora imefuatwa kikamilifu, kila mtunzi ajiwekee makataa ya kazi yake na kufuata bila kusita. Katika safari ya utunzi kutakuwa na panda-shuka mbalimbali lakini waandishi wanahimizwa kuwa la muhimu ni uamuzi watakaoufanya wenyewe. Ifuatayo ni simulizi fupi ambayo inaweka wazi ukweli huu;

“Alipofika nyumbani aliamua kuiendeleza hadithi yake ambayo sasa kapania kuimaliza baada ya kushindwa kuimaliza wakati aliotarajia” (Wamitila, 2004, uk. 66)

Vilevile, riwaya zimebaini kwamba kila mtunzi ni sharti awe na nidhamu na msukumo wa kipekee ili aikamilishe kazi yake kwa wakati ufaao. Msimulizi ametumia mfano wake mwenyewe kuonyesha jinsi alivyofaulu katika mradi wake wa uandishi wa riwaya mpya ya *Musaleo!* katika simulizi fupi hii:

Hadithi yangu nimekuwa nikiisimulia kwa miaka mingi. Utangulizi wake ulichukua miaka kama kumi kumaliza. Mwanzo hadhira yangu ilikuwa ndogo. Niliposema “paukwa” tu wengine waliondoka kwenda kujiandalia sherehe za kusherehekea matamu ya ukombozi. Waliobakia walikuwa wachache wengi wao wakulima, wanafunzi waliokuwa wakifanya utafiti pamoja na mwalimu wao (huyu Profesa), watoto

wanaopenda hadithi. Watu walianza kurudi mmoja mmoja baadaye nilipokuwa nimejibiwa “pakawa” na wachache waliokuwako (Wamitila, 2004, uk. 72)

Muda mrefu katika zoezi la utunzi husababisha kazi bora iliyofumwa kwa ustadi. Ubora wa kazi hii hujidhihirisha kwa hadhira mahususi ya wasomaji walioongoka na ambao pia ni watafiti. Aidha, kazi husika hukumbatiwa na wasomaji chipukizi wanaopenda kuisoma kwa minajili ya kujifurahisha. Polepole, idadi ndogo ya wasomaji hujengwa na kwa mujibu wa mpito wa wakati kazi hiyo hupata wasomaji zaidi. Riwaya zinamkemea mhariri dhidi ya uzembe katika zoezi la usomaji kama inavyobainika katika nukuu hili;

“usikiapo lolote lipindue uangalie kama kinyume chake kinaweza kuwa na maana mbaya” (Wamitila, 2004, uk. 10)

‘Kulipindua na kuliangalia jambo’ ni taashira inayoashiria tendo la kulichunguza jambo kwa makini. Uchunguzi wa kindani unapofanywa majawabu hupatikana. Kwa mujibu wa haya, usomaji wa riwaya usiwe wa juujuu bali uwe na nia ya kuchunguza kile mwandishi anachotaka kuifahamaisha jamii. Kuchunguza kwa undani ni njia moja ya kujaliza mapengo yaliyoachwa na mwandishi kama ilivyoelezwa awali. Aidha, ni mbinu ya kufanya utafiti ambao mwishowe huleta majibu yanayoifaa jamii. Utafiti kama njia bora ya kutatua matatizo yanayoikabili jamii utapunguza hali ya uzembe wa kusoma iliyokithiri katika jamii ya kisasa. Kwa mujibu wa riwaya, mbinu mojawapo ya kukabiliana na uzembe wa usomaji ni kuwasilisha hadithi isiyo ya kawaida. Usomaji wa kazi za uhalisia zilizozoeleka na zinazowasilishwa kwa njia ya moja kwa moja husababisha uzembe kwa sababu mapengo yote yamezibwa. Hamu kubwa ya mwandishi ni kuikuza hadhira. Kwa sababu hii riwaya zinahimiza hadhira kuacha kuwategemea wahakiki kila uchao kwa minajili ya kuifafanulia hadithi. Japo kazi za kisasa zinawakanganya na kuwazungusha wasomaji, uhalisia pekee si suluhu. Mambo yaliyozoeleka hayaongezi maarifa kwani;

“Hii sio dunia ya kuridhika na tulichozoea” (Wamitila, 2004, uk. 55)

#### **5.4 Hitimisho**

Sehemu hii imezingatia mchango wa mbinu za kimajaribio katika mchakato mzima wa uandishi na uchapishaji wa riwaya mpya ya Kiswahili. Mchakato umeangazia pambetatu ya uandishi bunifu iliyofumwa na mwandishi, msomaji na mchapishaji. Kwa mujibu wa riwaya, uandishi ni mwito wa kipekee wenye hisia na msukumo usiozulika. Mwito huu umetimiza hatua mbalimbali

kama vile uteuzi wa lugha faafu, uchaguzi mwafaka wa nadharia na utafiti wa kina. Hata hivyo, imedhihirika kuwa kimuundo na kintindo uandishi wa riwaya ya kisasa umekiuka ujadi uliozoeleka. Kwa sababu hii mwandishi wa kisasa amezua vita kati yake na wahariri na wachapishaji. Vita hivi vinatishia kuiangamiza tajriba ya waandishi bunifu. Vilevile, riwaya zimeangazia uhusiano uliopo baina ya washikadau katika sekta ya uzalishaji wa kazi bunifu za riwaya hususan namna jitihada za kibunifu za mwandishi zinavyokwamizwa na mhariri na mchapishaji. Hata hivyo, pamoja na changamoto zilizoangaziwa, riwaya zimethibitisha kuwa uandishi bunifu ni zoezi la wateule; si la kila mja. Utafiti umeng'amua kwamba ili kazi bunifu ya kisasa ikue ni sharti wahariri na wachapishaji wabadilishe mielekeo yao kuhusu waandishi wa kisasa. Vilevile, ni sharti uzembe uliopo miongoni mwa wahariri uondoke na wakubali kuzifanyia riwaya mpya uchunguzi wa ndani ili kuuelewa usanii wake baada ya kubaini yaliyomo. Kuhusu uchapishaji, japo ni kweli kwamba riwaya za kisasa ni changamano na huenda zikakosa kuwapendeza wengi kama asemavyo Rettova (2016), kauli mbiu ni kuwa kazi zote zina haki ya kuchapishwa ili hadhira ipate nafasi ya kutoa uamuzi wake. Hatimaye, utafiti huu unahimiza kuwa ufanisi wa riwaya mpya ya Kiswahili utaimarishwa na ushirikiano baina ya washikadau wote watatu yaani; mwandishi, msomaji na mchapishaji. Utafiti huu ni sehemu moja tu katika ufahamu wa utunzi wa kisasa kwa kuangazia matumizi ya mbinu za kimajaribio kama kunga za ubunifu katika riwaya mpya.

## SURA YA SITA

### MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 6.1 Utangulizi

Sura hii ya mwisho ya utafiti huu imetoa muhtasari wa matokeo ya utafiti kwa kugemea madhumuni matatu ya utafiti. Riwaya zilizotafitiwa ni pamoja na *Musaleo* (2004), *Msichana wa Mbalamwezi* (2011) na *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* (2014). Aidha, hitimisho kuhusu jinsi uandishi wa Wamitila ulivyo limetolewa. Mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusu mbinu za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya za kisasa kwa kuangazia riwaya teule za Wamitila yameangaziwa. Dhana tafitiwa jinsi zilivyotambulishwa katika sura ya kwanza zimeangaziwa.

#### 6.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu umebaini na kutambulisha kunga mbali mbali na tofauti tofauti za kiuandishi za kimajaribio kama zilivyotumiwa na kubainika katika riwaya teule za kimajaribio zilizotungwa na Wamitila. Kwa kuzingatia sifa bainifu na vipengele tofauti tofauti za kunga za kiuandishi za kimajaribio, imedhihirika kwamba riwaya za kimajaribio zimefanikiwa katika ufumaji wa sifa bainifu za kimajaribio kwa minajili ya kuonyesha taswira kamili ya jamii ya leo. Taswira ya jamii imepitishwa katika maudhui. Sifa kuu ya uandishi wa kimajaribio iliyotumika kwa wingi katika riwaya teule ni ukatizwaji wa usimulizi. Ukatizwaji huu umejengwa kwa fani za fasihi na sanaa kama vile urejeleomatini, taashira za aina aina, dayolojia, uhalisiajabu, mwingiliano-tanzu, tamathali za lugha/sanaa na matumizi ya simulizi fupi fupi zilizotapakazwa kote katika riwaya husika. Uandishi wa kimajaribio umeibuka kama njia mojawapo ya kutambulisha mambo hasa maovu na mafunzo yanayoikumba jamii ya sasa japo kwa njia fiche (Rettova, 2016).

Sura ya Kwanza imebaini jinsi uandishi wa riwaya za kisasa ulivyo tata na changamano. Uandishi wa kisasa unaegemea mtindo wa uhalisia mpya uliojawa na uchangamano ilhali ule wa kijadi uliegemea mfumo wa kihalisia wenye sifa ya usahili. Kazi za kijadi ziliandikwa kwa kuzingatia mtindo wa moja kwa moja. Kwa sababu hii zilieleweka kwa njia ya urahisi. Riwaya za kisasa zimejawa na matumizi ya kunga za kiuandishi za kimajaribio ambazo husababisha ukatizwaji wa usimulizi na hatimaye kuzua uchangamano hasa katika mfuatano wa vitushi. Hata hivyo, ilikisiwa kuwa sifa bainifu za mbinu mahususi za kimajaribio zinazotumiwa na waandishi wa kisasa kukamilishia maazimio na dhima yao ya ubunifu hazibainiki kikamilifu. Vilevile, mtafiti alibainisha kuwa haikujulikani jinsi waandishi wanavyozitumia mbinu husika katika

uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira kwa minajili ya kutoa taswira kamili ya jamii wanamoandikia. Kwa kuzingatia hitaji hili la kiusomi, imemshurutisha mtafiti kutambulisha, kubainisha na kutathmini vipengele tofauti tofauti vya kimajaribio katika riwaya teule na kuchambua jinsi vilivyotumiwa na mtunzi kujenga kunga zake za kiuandishi kwa njia ya kipekee ili kuwasilisha taswira kamili ya jamii yake.

Madhumuni mahususi ya utafiti huu yalikuwa: Kubainisha kunga za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya za kisasa za Wamitila; Kujadili mchango wa kunga za kiuandishi za kimajaribio katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya za kisasa za Wamitila; na Kufafanua jinsi kunga za kiuandishi za kimajaribio anazoitumia Wamitila zinavyoiakisi jamii ya leo. Aidha, utafiti uliazimia kujibu maswali matatu ya utafiti ambayo yalikuwa; Mwandishi Wamitila anatumia kunga zipi za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya zake za kisasa?; Kunga za kiuandishi za kimajaribio anazotumia Wamitila zina mchango gani katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya zake za kisasa? na Kunga za kiuandishi za kimajaribio anazotumia mwandishi Wamitila zinaiakisi vipi jamii ya leo? Data iliyotumiwa katika kuafikia malengo haya na kujibu maswali ya utafiti ilikuwa maudhui, mitindo mbali mbali ya utunzi, fani mbalimbali za sanaa na mbinu za lugha na tamathali za lugha.

Sura ya Pili imeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Maoni ya wasomi kuhusu chanzo, historia na ukuaji wa riwaya za kimajaribio yamezingatiwa. Aidha, mtafiti ameonyesha maoni ya wasomi kuhusu uandishi wa Wamitila. Baadhi ya wasomi kama Rettova (2016) wamemtaja kama mwandishi mwenye uchangamano mwingi katika ubunifu wake. Kile kinachosababisha uchangamano huo ndilo pengo kuu la usomi lililozibwa na utafiti huu. Nadharia ya Usasaleo ambayo iliongoza shughuli za ukusanyaji na uchanganuzi wa data imefafanuliwa. Kwa mujibu wa nadharia husika, mwandishi bunifu ana uhuru wa kuwasilisha ujumbe wao kwa hadhira jinsi wpendavyo. Ni jukumu la wasomaji kujibidiisha kung'amua yale wayakusudiayo waandishi wa kisasa kwa kufanya utafiti zaidi. Sura ya Tatu imejikusisha na mfumo wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

Katika Sura ya Nne, utafiti umewasilisha matokeo yanayohusiana na madhumuni ya kwanza ya utafiti. Riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji* (2014) imeangaziwa. Mwandishi Wamitila ametumia taashira; kunga mojawapo ya kimajaribio kufafanua changamoto

wanazopata waandishi wa kisasa mikononi mwa wahariri na wachapishaji. Vile vile, kwa kutumia kunga zizo hizo, utafiti umebainisha mapendekezo ya kuboresha uandishi wa kisasa licha ya kuwepo kwa magumu yanayowakabili watunzi. Sura ya Tano imewasilisha matokeo ya utafiti yanayohusiana na madhumuni ya pili na ya tatu. Kwa mujibu wa utafiti, riwaya za kimajaribio zimefafanua maswala yanayoibaini taswira kamili ya jamii ya kisasa. Kwa jumla, fasihi ya kisasa inafanana na jamii ya mtunzi kama ilivyo shilingi kwa ya pili.

### **6.3 Hitimisho**

Kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza ya utafiti, imebainika kwamba sifa kuu ya utunzi wa kimajaribio inayotumika katika riwaya za kisasa za Wamitila ni ukatizwaji wa usimulizi. Kunga za kimajaribio zinazojenga na kupambanua ukatizwaji wa usimulizi ni uhalisiajabu, ujinaishaji na matumizi ya simulizi fupi fupi. Baadhi ya simulizi fupi fupi zilizotumika zinarejelea matini za taaluma za fasihi, falsafa tofauti tofauti, isimu na matibabu. Aidha, matinirejelewa nyingine ni dini. Katika ubunifu wake, Wamitila amejumuisha matini ya dini ya Kikristo ya hadithi ya Daudi na Goliati. Katika dini ya Kiislamu, hadithi ya Mtume Mohammed imetumika japo kwa mpito tu miongoni mwa matini nyingine mseto. Hali kadhalika, simulizi nyingine zimejumuisha majina ya watu mashuhuri, majina ya mahali na majina ya vitu. Kwa mfano, kisa cha meli ya *La Amistad* katika riwaya ya *Musaleo* kimetumika kuonyesha kuwa suluhu la Mwafrika ni Mwafrika mwenyewe.

Mintarafu ya madhumuni ya pili, mbinu za kimajaribio zimechangia katika uwasilishaji wa maudhui kwa njia fiche. Maudhui yaliyowasilishwa yanafichika katika mbinu za kimajaribio zilizotumika katika riwaya. Imebainika kwamba kuna uchangamano katika usimulizi ambao hukatizwakatizwa hivyo kuwafanya wasomaji kuwa na wakati mgumu wa kuelewa. Hata hivyo, maudhui yanapatikana katika uchangamano huo. Mwandishi anaanza jambo fulani na kabla ya kulikamilisha anaanza jingine.

Kwa mujibu wa madhumuni ya tatu, utafiti umebainisha kwamba maisha katika jamii ya kisasa hayana utaratibu. Jinsi riwaya zilivyo bila utaratibu wa mpangilio wa vitushi ndivyo taswira kamili ya jamii ya kisasa ilivyo. Kwa sababu riwaya za kimajaribio hazina usimulizi wa moja kwa moja, ni lazima kila msomaji wa kazi hizi awe na ufahamu wa kiada wa mambo anuwai ili apate kuzielewa. Kwanza, ni sharti awe na uelewa wa uandishi wa mitindo mipya ya utunzi wa



Karne ya Ishirini na Moja. Pili, ni muhimu zaidi awe na uzoefu na umilisi wa kunga za kimajaribio ili kumudu taswira ya jamii ya kisasa.

#### **6.4 Mapendekezo**

Mapendekezo ya utafiti huu yametolewa kwa makundi mawili ya washikadau wa taaluma ya fasihi. Kwanza ni kwa wasomaji (yaani wapokeaji wote wa kazi za fasihi ya Kiswahili wakiwemo wanafunzi) na waandishi chipukizi wa riwaya za kisasa. Pili, kwa wasomi na watafiti wa baadaye wa riwaya za kimajaribio. Kwa wanaobuni sera za elimu na hasa katika uwanda wa elimu ya fasihi inapendekezwa kuwa hawana budi kutoa mwanga zaidi kuhusu utunzi wa kimajaribio. Aidha, wale wanaoamua vitabu vya fasihi vinavyotahiniwa katika shule za upili hawana budi kushirikisha swala la uchanganuzi wa kunga za kimajaribio katika mtalaa wa fasihi. Ni vyema kutambua kwamba kuna uandishi mpya wa riwaya ya Kiswahili ambao unahitaji mbinu mpya za usomaji. Hii ni kwa sababu kutungwa kwa riwaya hizi kunaashiria kuzuka kwa mikakati ya kipekee ya kuzishughulikia.

Hali kadhalika, inapendekezwa kwa wasomaji wa kazi za kisasa za fasihi wawe na uzoefu wa kusoma kwa mapana. Iwapo hivyo, watapata ufahamu tosha kuhusu majina mbali mbali ya watu, vitu na mahali. Kwa kuwa uandishi wa kimajaribio ni uasi dhidi ya jinsi ambavyo waandishi wengi wamekuwa wakiandika, wasomaji wa fasihi ya kisasa wanahimizwa kujihami na ufahamu wa kiada wa maswala mengi ya kihistoria, kidini, kijamii na kitaaluma ili waelewe au wafahamikiwe na yaliyomo katika riwaya za kimajaribio. Pasipo kufanya hivi wasomaji hawatakuwa na uwezo wa kufahamu yale yanayowasilishwa na mwandishi wa kisasa wa kimajaribio.

Isitoshe, kwa waandishi chipukizi inapendekezwa kwamba kuna umuhimu wa kufanya utafiti kuhusu utunzi wa kimajaribio. Waandishi wanahitaji kujifahamisha njia mwafaka zaidi ya kutumia kunga za kimajaribio katika uandishi bunifu bila kuikanganya hadhira. Hii ni kwa sababu uandishi bunifu ni mpango kamilifu wa kiusomi unaohusisha taratibu zote za kitaaluma. Yeyote anayepania kujitosa katika uwanda wa uandishi hivyo basi ni sharti aanze kwa kufanya utafiti mwafaka huku akifahamu pia kwamba uandishi ni zoezi lenye changamoto tele na linalochukua muda mrefu.

#### **6.4.1 Tafiti za Baadaye**

Utafiti huu unapendekeza kwamba kuwe na utafiti wa kilinganishi unaolenga kubainisha ufaafu wa kunga za kiuandishi za kimajaribio dhidi ya uandishi unaozingatia matumizi ya mbinu za kijadi (zinazozingatia uhalisia). Aidha, watafiti wa baadaye wafanye utafiti wa kina unaolenga kuchanganua matumizi ya kunga za kiuandishi za kimajaribio katika riwaya za waandishi wa tanzu nyingine za fasihi kama tamthilia, ushairi, fasihi simulizi na pia fasihi ya watoto. Isitoshe kuwe na utafiti wa muundo na mtindo wa simulizi fupi fupi zinazotumika na kuchupwa popote riwayani katika riwaya za kimajaribio. Uchunguzi wa riwaya nyingine za mwandishi ufanywe ili kutambulisha na kubainisha ruwaza tofauti tofauti zinazojitokeza katika ulimwengu wa ubunifu wa mwandishi. Ni muhimu pia kuchanganua sababu zinazowapelekea waandishi wa kisasa wa kimajaribio kuandika riwaya jinsi wanavyoandika. Hivyo, ni muhimu kufanya uchunguzi kuhusu waandishi wengine wa riwaya za kimajaribio.

## MAREJELEO

- Abrams, M.H. (1993). *The Norton Anthology to English Literature II*. New York na London: W.W. Norton.
- Abrams, M.H. (1999). *A Glossary of Literary Terms*. Ithaca: Cornell University Press.
- Achebe, C. (2009). *Things fall Apart*. Toronto: Anchor Canada.
- Adamthwaite, A.P. (2011). *The Making of the Second World War 2<sup>nd</sup> ed*. New York: Routledge.
- Alan, B. (1999). *Hitler: A Study in Tyranny*. New York: Konecky & Konecky.
- Alomo, S.O. (2016). *Uwasilishaji wa Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili iliyoandikwa na Said A. Mohamed na K.W. Wamitila*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Egerton.
- Anderson, S.L. (2000). *On Kierkegaard*. Belmont: Wadsworth/Thompson Learning Inc.
- Armah, A.K. (1973). *Two Thousand Seasons*. Popenguine: Per Ankh.
- Banks, A. (2001). *A Military Atlas of the First World War*. Barnsley: Pen & Sword.
- Barongo, Y.R. (1980). *Neocolonialism & African Politics: A Survey of the Impact of Neocolonialism on African Political Behaviour*. New York: Vantage Press.
- Barth, J. (1984). "The Literature of Exhaustion" in *The Friday Book: Essays and Other Non-Fiction*. London: The John Hopkins University.
- Barthes, R. (1968). *The Death of the Author*. New York Blackwell Publishers.
- Blum, L. (2004). Stereotypes and Stereotyping: A Moral Analysis. *Philosophical Papers*, 33 (3) 251-289. Tarehe ya kuingia 20<sup>th</sup> June, 2021.
- Baudrillard, J. (1988). *Selected Writings*. Stanford: Stanford University Press.
- Baudrillard, J. (1994). *Simulacra and Simulation*. Ann Arbor: University of Michigan Press.
- Beckett, S. (1988). *Stirrings Still*. New York: Bluemoon Books, London: John Calder.
- Beckett, I.F.W. (2007). *The Great War: 1914-1918*. New York: Routledge.
- Bertens, H. (2001). *Literary Theory*. England: Routledge.
- Bertoncini, E. (2006). Globalization Unmasked in Two Kiswahili Novels. *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI-2005*, ed. By Seleman S. Sewangi na Joshua S. Madumulla. Dar es Salaam: TUKI, pp. 84-94.
- Besha, R. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Best, S., & Kellner, D. (2001). *The Postmodern Adventure*. London, England, na New York: Routledge and Guilford Press.

- Birmingham, D. (1995). *The Decolonization of Africa*. Ohio: Ohio University Press.
- Boothe, B. (2017). Freudian Dream Interpretation. 10.1007/978-3-319-28099-8\_13.79-1; University of Zurich. (Tarehe ya kuingia, 22.8.2019).
- Bowler, P.J. (1996). *Charles Darwin; The Man and his Influence*. London: Cambridge University Press.
- Bowler, P.J. (2013). *Darwin Deleted. Imagining a World Without Darwin*. Chicago: University of Chicago Press.
- Bradford, S. (2007). *Diana*. London: Penguin Books.
- Braschi, G. (1998). *Yo-yo Boing*. University of Michigan: Latin American Literary Review Press.
- Breton, A., & Soupalt, P. (1920). *LesChamps Magnetiques*. France: Gallimard.
- Brown, E.J. (2002). *Charles Darwin Vol 2: The Power of Place*. London: Jonathan Cape.
- Brown, T. (2008). *The Diana Chronicles*. New York: Anchor Books.
- Buchi, E. (1977). *Slave Girl*. United Kingdom: Allison and Busby.
- Burke, J. (1997). "The Wild Man's Pedigree", In *The Wild Man Within*. USA: University of Pittsburgh Press.
- Burrough, W.S. (1959) *Naked Lunch*. New York: Grove Press.
- Calvino, I. (1981). *If on a Winter's Night a Traveller*. New York: Harcourt Brace Jovanovich.
- Carter, D. (2006). *Literary Theory*. Harpenden, Herts, AL5 IX: Pocket Essentials.
- Charlesworth, M.J. (1976). *The Existentialists and Jea-Paul Sarte*. London: Geroge Prior.
- Chiraghdin, S., & Mnayampala, M. (1977). *Histori ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Chrisman, L., & Parry, B. (2000). *Postcolonial Theory and Criticism (ed)*. Cambridge: English Association.
- Collins, R.F. (2007). *World War I: Primary Documents on Events from 1914-1919*. Westput: Greenwood Press.
- Conrad, L. (1987). "Abraham and Muhammad: Some Observations Apropos of Chronology and Literary topoi in the Early Arabic Historical Tradition." *Bulletin of the School of Oriental and African Studies*, 50 (2), 225-240. doi:10.1017/S0041977X00049016.
- Creswell, J. W. (2009). *Research design: Qualitative, quantitative, and Mixed methods Approaches*. Los Angeles: Sage.
- Danielewski, M.Z. (2000). *House of Leaves* (2<sup>nd</sup>.Ed.). New York: Pantheon Books.

- Dehejia, R. (2005). Insuring Consumption and Happiness Through Religious Organizations. *National Bureau of Economic Research Working Paper*. Vol 11576.
- Deleuze, G., & Guattari, F. (1986). *Kafka: Towards a Minor Literature*. Minneapolis: University of Minnesota Press.
- Enani, M. M. (2005). *Theories of Comparative Literature*. Cairo: Cairo University.
- Elliot, P. (2017). A Review of *Z213:Exit* by Dimitris Lyacos. *Compulsive Reader*.  
<http://www.compulsivereader.com/2017/08/16/a-review-of-z213-exit-poena-damni-dimitris-lyacos>. Tarehe ya kuingia: 25.03.2017
- Farlex Dictionary of Idioms*. (2015).  
<https://idioms.thefreedictionary.com/light+at+the+end+of+the+tunnel>. Tarehe ya kuingia: 16.12.2019
- Falconer, D.S., & Mackay, T.F.C. (1996). *Introduction to Quantitative Genetics*. Harlow: Longman Group.
- Feluga, D. (2013). *General Introduction to Postmodernism*. College of Liberal Arts: Retrieved August 16<sup>th</sup>, 2013.
- Flynn, T.R. (2006). *Existentialism: A Very Short Introduction*. Oxford: Oxford University Press.
- Freeman, R.B. (1977). "On the Origin of Species" *The Works of Charles Darwin: An Annotated Bibliographical Handlist (2<sup>nd</sup> Ed)*. England: Dawson.
- Freud, S., & Strachey, J. (2010). *Civilizations and its Discontents*. New York: W. W. Norton.
- Frey, B.S., & Stutzer, A. (2002). *Happiness and Economics*. Princeton: Princeton University Press.
- Gaylard, G. (2005). *After Colonialism. African Postmodernism and Magical Realism*. Johannesburg: Wits University Press.
- Grimsley, R. (1960). *Existentialism Thought*. Cardiff, Wales: University of Wales Press.
- Gromov, M.D. (1998). "Nagona and Mzingile- Novel, Tale or Parable?" *Afrikanistische Arbeitspapiere. Swahili Forum: (55) 73–78*.
- Gromov, M.D. (2004). "Postmodernistic Elements in Recent Swahili Novels." *The Nairobi Journal of Literature, (2) 28-36*.
- Habermas, J. (1987). *The Philosophical Discourse of Modernity*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Halliwell, S. (1992). *Teaching English in the Primary Classroom*. New York: Longman.

- Harmon, W., Holman, C.H., & Thrall, W.F. (2006). *A Handbook to Literature*. New Jersey: Pearson/Prentice Hall.
- Harvey, P.H., & Pagel, M.D. (1991). *The Comparative Method in Evolutionary Biology*. New York: Oxford University Press.
- Heyd, D. (1992). *Genethics: Moral Issues in the Creation of People*. Berkeley CA: University of California Press.
- Hosking, E., & Flegg, J. (1982). *Eric Hoskings Owls*. United Kingdom: Mermaid Books.
- Irele, F., & Gikandi, S. (Eds). (2000). *The Cambridge History of African and Caribbean Literature*. Cambridge: Cambridge University Press.
- James, D. (2003). *Owls of the World*. Toronto: Key Porter Books.
- James, D. (2013). *The Complete Book of North American Owls*. San Diego: Thunder Bay Press.
- Jameson, F. (1991). *Postmodernism, or the Cultural Logic of Late Capitalism*. London: Verso.
- Jazdzewska, K. (2015). "From Dialogos to Dialogue: The Use of the Term from Plato to the Second Century CE". *Greek, Roman and Byzantine Studies* 54.1 pp. 17-36.
- Johansen, J.D. (2007). A Semiotic Definition of Literary Discourse. *Semiotica*, 165 (1/4), 107-132.
- Jonathan, C. (2002). *Bathes: A Very Short Introduction*. Oxford: Oxford University Press.
- Joyce, J. (1969). *Ulysses*. London: Bodley Head.
- Junor, P. (2005). *The Firm: The Troubled Life of the House of Windsor*. London: Harper Collins Publishers.
- Kaplan, C. (1986). *Criticism: The Major Statements*. New York: St. Martin Press.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji*. Nairobi: East African Publishing House.
- Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Khamis, K.S., & Omar, H.H. (1994). *Historia Fupi ya Zanzibar*. Zanzibar: Al-Khayria Press.
- Khamis, S.A.M. (1998). "Implication as a Literary Technique in Mohamed S. Mohamed's Novels: *Kiu* and *Nyota ya Rehema*". [www.qucosa.de/qucosa/5\\_08khamis](http://www.qucosa.de/qucosa/5_08khamis). Tarehe ya kuingia; 28.04.2017.
- Khamis, S.A.M. (2003). "Fragmentation, Orality and Magic Realism in Kezilahabi's *Nagona*" katika *Nordic Journal of African Studies*.
- Khamis, S.A.M. (2005). *Signs of New Features in Swahili Novel: Research in African Literature*

36 (1), 92-108.

- Khamis, S.A.M. (2007). "The Swahili Novelist at the Crossroads: The Dilemma of Identity and Fecundity". *Swahili Forum*, (14) 165 – 180.
- Khamis, S.A.M. (2008). "Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili." *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*, ed. by Nathan O. Ogechi, Naomi L. Shitemi na Inyani Simala. Eldoret: Moi University Press, pp.3-23.
- Khamis, S.A. M. (2012) "*Riwaya Mpya ya Kiswahili. Utandawazi au Utandawizi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya Ya Kiswahili Inavyodai*". Bayreuth: Bayreuth University Press.
- Khamis, S.A.M. Bertoncini, E., Gromov, M., & Wamitila, K.W. (2009). *Outline of Swahili Literature: Prose, Fiction and Drama*. 2<sup>nd</sup> Edition. Leiden: E.J. Brill.
- Kiimbila, J.K. (1971). *Ubeberu Utashindwa*. Dar es Salaam: Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili.
- Konig, C., Weick, F., & Becking, J. (1999). *Owls: A Guide to the Owls of the World*. London: Yale University Press.
- Knepper, W., & Deckard, S. (2016). "Towards a Radical World Literature: Experimental Writing in a Globalizing World in *A Review of International English Literature*, 47 (1-2), 1-25.
- Kristeva, J. (1980). Word, Dialogue and Novel. In L. S. Roudiez (Ed.), *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art* pp. 64-91. New York: Columbia University Press.
- Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Semi*. Dar es Salaam: E.A L.B.
- Lima, J.L. (1988). *Paradise*. University of Texas: University of Texas Press.
- Lofchie, M.F. (1963). "Party Conflict in Zanzibar", *Journal of Modern African Studies*. (2) 128 – 142.
- Lofchie, M.F. (1965). *Zanzibar: Background to the Revolution*. Princeton: Princeton University Press.
- Lyacos, D. (2010). *Z213:Exit*. Brooklyn, New York: Shoestring Press.
- Lyotard, J.F. (1984). *The Postmodern Condition: A Report on Knowledge*. Translated by Bennington, G na Massumi, B. Minneapolis: University of Minnesota Press.
- Lyotard, J.F. (1997). *Postmodern Fables*. Minneapolis: University of Minnesota Press.
- Machiavelli, N. (1981). *The Prince*. New York: Panguin Books.
- Macquarrie, J. (1976). *Existentialism*. London: The Chaucer Press Ltd.
- Madumulla, J.S. (1995). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

- Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Historia, Nadharia na Misingi ya Uchambuzi. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers.*
- Malenya, M.M. (2012). *Matumizi ya Lugha katika Fasihi Simulizi.* Mwanza: Mwanza Inland Press.
- Maliyamkono, T.I. (2000). *The Political Plight of Zanzibar.* Dar es Salaam: Tema Publishing Company Ltd.
- Manohar, R.M. (1984). “*Existentialists Conception of Man. A Critical Study in the Light of Psychoanalytic and Marxist Persepctives*” PhD Thesis, University of Poona.
- Maree, J. G. (Ed.), (2012). *Complete your Thesis or Dissertation Successfully: Practical Guidelines.* Cape Town: Juta.
- Maree, K., & Pietersen, J. (2012). *First Steps in Research.* Pretoria: Van Schaik.
- Martha, C. (2008). “On the Work of Italo Calvino”, *The Writers Chronicle* 24-32.
- Maxwell, J. (2005). *Qualitative Research Design, In Applied Social Research Methods Series.* Vol. 41.
- Mbao, B. (2005). *Mageuzi ya Binadamu; Utangulizi Mfupi Sana.* New York: Oxford University Press.
- Mbatiah. (2001a). *Maana na Matumizi ya Upambanyaji: Tahakiki ya Rosa Mistika. Katika Kioo cha Lugha.* University of Dar es Salaam: Journal of the Kiswahili Department.
- Mbatiah. (2001b). *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks and Graphics Publishers.
- Mhando, P., & Balisidya. (1996). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho.* Dar es Salaam: TUKI.
- Mihanjo A. (2010) *Falsafa na Ufunuo wa Maarifa.* Toriam: Morogoro.
- Mlacha, S.A.K., & Madumulla, J.S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mohammed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohammed, S.A. (1985). *Kiu.* Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mulokozi, M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.
- Musokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mwamzandi, I.Y. (2000). “Nadharia na Usomi: Vizingiti na Mikabala katika Fasihi ya Kiswahili” katika Njogu, K., King’ei, K., Momanyi, C. na Musau, P. (Eds.) *Kiswahili*



- katika Karne ya Ishirini ya Moja*. (Series 17., pp. 97-106). CASAS, Cape Town, South Africa: CHAKITA.
- Mwamzandi, I.Y. (2013). "Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia ya Fasihi". *Swahili Forum*, (20), 48-66.
- Mwangi, J.W. (2013). *Uhalisia na Uhalisiajabu katika Riwaya Mpya*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nanjira, D.D. (1995). *Crop Production: Evolution, History and Technology*. New Jersey: John Wiley & Sons. Nanjira, D.D. (2010). *African Foreign Policy and Diplomacy from Antiquity to the @1<sup>st</sup> Century*. Santa Barbara, CA: Praeger.
- Neuendorf, K.A. (2002). *The Content Analysis Handbook*. Thousand Oaks: Sage.
- Northrop, F. (1985). *The Harpes Handbook of Literature*. New York. Harpes and Row.
- Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustina College.
- Nyabunga, V.A. (2005). Uhakiki wa Binadamu na Musaleo! na K.W. Wamitila: *Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nyerere, J.K. (1995). *Our Leadership and te Destiny of Tanzania*. Harare: Jongwe Printing and Publishing and African Group.
- Onyoni, J.K. (2012). "Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Natala na Mama Ee. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Osagie, L.F. (2000). *The Amistad Revolt*. Athens & London: University of Georgia Press.
- Poncian, J., & Mgaya, E.S. (2015). "Africa's Leadership Challenges in the 21st Century: What can Leaders Learn from Africa's Pre-Colonial Leadership and Governance?" *International Journal of Social Science Studies*, (3) 3106-115.
- Pynchon, T. (1973). *Gravity's Rainbow*. New York: Viking Press.
- Quayson. (2000). *Modernism and Postmodernism in African Literature*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Ramen, & Chaudbarry. (2011). Common Themes and Techniques of Postmodern Literature of Shakespeare in *International Journal of Educational Planning and Administration*, ( 2) 1, 189-198.

- Rao, S. (2016). *Indian Dukawallas: Their Contribution to Political and Economic Development of Kenya*. New York: Free Press Publishers.
- Rettova, A. (2016). "Writing in the Swing? Neo-realism in Post- Experimental Swahili Fiction". *Research in African Literatures*, (47) 2 15-31.
- Richards, J.C. (1984). *Error Analysis Persepectives on Second Language*. London: Longman Group Ltd.
- Ritland, K. (1996). "Marker-based Method for Inferences about Quantitative Inheritance in Natural Populations. In *Evolution*, 50, 1062-1073.
- Ritland, K. (2000). Detecting Inheritance with Inferred Relatedness in Nature. In *Adaptive Genetic Variation in the Wild*, (10), 187-199.
- Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Nairobi: Nelson.
- Robert, S. (1977). *Adili na Nduguze*. Nairobi: Macmillan.
- Roliins, J.D. (1983). *A History of Prose*. Leiden.
- Rulfo, J. (2002). *Pedro Paramo*. Austin: University of Texas Press.
- Saro-Wiwa, K. (1994). *Sozaboy*. London: Longman.
- Sartre, J.P. (1956). *Existentialism is a Humanism*. Cleveland: Kaufmann and Walter.
- Selden R., Woddowson, P., & Brooker, P. (2005). *A Readers Guide to Contemporary Literary Theory (Fifth Edition)*. United Kingdom: Pearson Longman.
- Senkoro, F.E.M.K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi Andishi*. Dar es Salaam: Kauttu Ltd.
- Smith, C.W. (2010). *African Foreign Policy and Diplomacy from Antiquity to the 21<sup>st</sup> Century*. Oxford: Greenwood Publishing Group.
- Smith, S. B. (2007). *Diana: The Life of a Troubled Princess*. London: Aurum Press Ltd.
- Snell, K. (2013). *Diana: Her Last Love*. London: Andre Deutsch Ltd.
- Strauss, A., & Corbin, J. (1998). *Basics of Qualitative Research: Techniques and Procedures for developing Grounded Theory*. New York: SAGE Publications.
- Suret-Canale, J. (1988). *Essays on African History: From The Slave Trade To Neo-Colonialism*. London: Hurst.
- Tinkler, J. F. (1988). Praise and Advice: Rhetorical Approaches in More's Utopia and Machiavelli's the Prince. *The Sixteenth Century Journal*, 19(2), 187–207. <https://doi.org/10.2307/2540406>.

- Todoror, T. (1984). *Mikhail Bakhtin. The Dialogical Principle*. Trans. Wlad Godzi. Manchester: Manchester University Press. 17 (2010), 143-157.
- Vargas, L.M. (1984). *The War of the End of the World*. New York: Farrar, Straus na Giroux.
- Veatch, R.M. & Ross, L.M. (2016). *Defining Death: The Case for Choice*. Washington D.C: Georgetown University Press.
- Waliaula, K.W. (2013). The State of Swahili Studies: Remembering the Past, Present and Future. *Katika Studies in Literature nad Language*. Juz. 6. (8-17).
- Walibora, K. (2010). *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum*. Swahili Forum.
- Walibora, K. (2013). Ujasiri wa Kujumulika katika Uandishi wa Kiswahili. Imepakwa Jumanne, 22, 2013 17:31 EAT.  
<http://www.swahilihub.com/habari/MAKALA/-/1310220/1672466/-/ouhmen/-/index.html>. Tarehe ya kuingia; 12.04.2017.
- Waller, R. (2014). *Kenya: A History Since Independence*. London: I.B. Tauris.
- Walter, R. (1981). *How Europe underdeveloped Africa*. Washington, D.C. : Howard University Press.
- Wamitila, K.W. (1991). “Nagona na Mzingile: Kezilahabi’s Metaphysics.” *Katika Kiswahili*: (60), 62- 67.
- Wamitila, K.W. (2002a). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K.W. (2002b). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix: Mombasa.
- Wamitila, K.W. (2003a). “Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi’s *Nagona and Mzingile* and Juan Rulfo’s *Pedro Paramo*.” *Katika Kiswahili*, (66), 49-58.
- Wamitila, K.W. (2003b). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Wamitila, K.W. (2004). *Musaleo!* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Wamitila, K.W. (2007). “Narrative Structure and Metaphor: Towards a New Aesthetics of the Kiswahili Novel.” *Katika Kiswahili*, (70), 67-72.
- Wamitila, K.W. (2008). “*Point of View in Kiswahili Narrative Fiction. Reading Shafi A. Shafi’s Vuta N’kuvute*.” *Katika Kiswahili*, (71), 84- 97.
- Wamitila, K.W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.
- Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

- Wamitila, K.W. (2011). *Msichana wa Mbalamwezi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Wamitila, K.W. (2013). *Tikitimaji*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Wamitila, K.W. (2014). *Mwandishi, Msomaji na Mchaphishaji*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Wardhaugh, R. (1986). *An Introduction to Socio-Linguistics*. New York: Blackwell Publishers.
- William, H. (2003). *A Hand Book to Literature. 9th Edition*. Upper Saddle River, New Jersey: Prentice Hall.
- Worton, M., & Judith, S. eds. (1990). *Intertextuality Theories na Practices*. Manchester: Manchester University Press.
- Yehuda, B. (2001). *Rethinking the Holocaust*. New Haven: Yale University Press.
- Yuswanto, F.A. (2015). "Diversity of Existentialism Theory, Patterns and its Reflection in Jurispudence. *South East Asia Journal Contemporary Business. Economics and Law*.
- Zabus, C. (1997). *Postmodernism in African Literature in English*.  
<https://www.researchgate.net/publication/300837404> doi:10.1075/chlel.xi.59zab  
 Tarehe ya kuingia; 01.05.2017.  
<https://www.nation.co.ke/news/politics/-I-was-kicked-in-the-seat-of-my-pants-/1064-2018326-s52oisz/index.html> Tarehe ya kuingia; 27.01.2020.  
<https://www.theestafrican.co.ke/news/ea/Bobi-wine-an-enemy-of-Uganda-says-yoweri-museveni/4552908-5315786-ad306sz/index.html> Tarehe ya kuingia; 27.01.2020
- Zamora, P.L., & Faris W.B. (1995). *Magical Realism: Theory, History and Community*. Durham: Duke University Press.



 *Journal Homepage: -www.journalijar.com*  
**INTERNATIONAL JOURNAL OF  
ADVANCED RESEARCH (IJAR)**  
Article DOI: 10.21474/IJAR01/9038  
DOI URL: <http://dx.doi.org/10.21474/IJAR01/9038>  
ISSN NO. 2320-5407 

**RESEARCH ARTICLE**

**UREJELEOMATINI KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI YA DHULUMA KATIKA RIWAYA YA MSICHANA WA MBALAMWEZI (K.W.WAMITILA).**

Janice M. Mutua<sup>1</sup>, Abdul Rahim Taib<sup>1</sup> and Issa Mwamzandi<sup>2</sup>.

1. Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
2. Chuo Kikuu cha Kabianga, Kenya.

**Manuscript Info**

**Manuscript History**  
Received: 10 March 2019  
Final Accepted: 12 April 2019  
Published: May 2019

**Key words:-**  
Urejeleomatini, riwaya za kimajaribio,  
mbinu za kimajaribio.

**Abstract**

Waandishi wa riwaya ya Kiswahili ya kisasa wanawasilisha ujumbe kwa hadhira kwa kujikita katika mbinu za kiuandishi za kimajaribio. Urejeleomatini ni mojawapo wa vipengele muhimu vya mbinu hizo za kimajaribio. Riwaya zenyewe zimeitwa "riwaya za kimajaribio" au "riwaya za kisasa". Watalaamu wengine wamezibaini kama "riwaya za Karne ya Ishirini na Moja. Mwandishi Kyallo Wadi Wamitila ni mmojawapo wa waandishi wa kisasa anayetumia mtindo huu mpya wa kiuandishi katika kuzungumzia maswala mbalimbali yanayoikumba jamii. Nadharia ya usasaleo imeongoza utafiti huu katika uchanganuzi wa kipengele cha urejeleomatini. Aina mbali mbali za matini zilizorejelewa katika uwasilishaji wa maudhui ya dhuluma zilitambulishwa na kufanuliwa. Riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* ilichaguliwa kimaksudi kwa kuwa inawasilishwa kwa simulizi nyingi fupi fupi zinazorejelea matini tofauti tofauti. Mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo mkabala wa kimaolezo ilitumika kuchanganua deta iliyohusiana na swala zima la urejeleomatini. Deta ilichanganuliwa kwa kuangazia maudhui, mandhari na mbinu za kiuandishi za kimajaribio. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya kimaolezo. Ilibainika kuwa ukosefu wa utaratibu katika uendeshaji wa mambo ndiyo taswira kamili ya jamii ya sasa. Matini zilizorejelewa zimeonyesha kuwa mwananchi amedhulumiwa na kupewa huduma duni na viongozi. Makala hii imehakiki na kutathmini jinsi mwandishi anavyotumia mbinu ya urejeleomatini kama kunga ya uwasilishaji wa maudhui ya dhuluma katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi*.

Copy Right, IJAR, 2019. All rights reserved.

**Introduction:-**

**1.1 Utangulizi**

Makala hii imeshughulikia swala la urejeleomatini kama nyenzo ya kuwasilisha maudhui ya dhuluma katika riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi* (2011) ya Kyallo Wadi Wamitila. Lengo kuu ni kutambulisha aina mbalimbali za matini zilizorejelewa katika juhudi za kuwasilisha maudhui ya dhuluma. Mintarafu ya haya, makala imeonyesha jinsi riwaya ya kisasa ya Kiswahili inavyoisawiri taswira kamili ya jamii ya kisasa. Hali hii imejadiliwa katika misingi ya nadharia ya usasaleo.

**Corresponding Author:-Janice M. Mutua.**  
Address:-Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

# MWANGA WA LUGHA

The cover of the journal 'Mwanga wa Lugha' features a central blue globe showing the continents of Africa, Europe, and Asia. The globe is set against a background of blue and white rays emanating from the top left, suggesting sunlight. The sky is a deep blue with several white, stylized clouds scattered across it. At the top of the cover, there is a green and blue gradient banner.

**Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika  
Chuo Kikuu cha Moi**

**Juzuu 6 Na.2**

**Septemba 2021**

---

## Yaliyomo

Dhima za Vibainishi Vioneshi katika Kiswahili Sanifu <i>Adventina Y. Buberwa</i> na <i>Shaibu I. Champunga</i> .....	1
Mchakato wa Uandishi Bunifu kama Unavyoakisiwa katika Riwaya za Kisasa za K.W. Wamitila <i>Janice M. Mutua</i> , <i>Issa Mwamzandi</i> na <i>AbdulRabim Taib</i> .....	15
Nihilism and Postproverbials in Euphrase Kezilahabi's Poetry Anthology <i>Dhifa (Feast)</i> <i>Tom Olali</i> and <i>Ahmad Kipacha</i> .....	27
Mwingiliano wa Kanuni za Kimofosintaksia wa Ngeli Nomino za Luganda katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu <i>Martin Mulei</i> , <i>Beverlyne Asiko Ambuyo</i> na <i>Deborah Nanyama Amukowa</i> .....	39
The Depiction of Women in Bongowood and Ghallywood Video Films <i>Josephine Dzabene-Quarshie</i> and <i>Augustina E. Dzregah</i> .....	51
Sheng kama Lugha ya Biashara jijini Nairobi: Masiala ya Kijamii Yanayoathiri Nafasi yake katika Utangazaji wa Biashara <i>Oyinda Patrick</i> , <i>Ayub Mukhwana</i> na <i>Lisanza Muaka</i> .....	65
Mchango wa Tangu za Kimaigizo za Fasihi Simulizi katika Umahuluti wa Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi wa Riwaya ya <i>Mafuta</i> <i>Simiyu Benson Sululu</i> , <i>Richard Makhanu Wafula</i> na <i>Joseph Nyehita Maitaria</i> .....	77
Juhudi za Fasihi katika Kukabiliana na Janga la UKIMWI: Kifani cha Riwaya ya <i>Ua la Faraja</i> <i>Arinaitwe Annensia</i> na <i>Mosol Kandagor</i> .....	85
Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za <i>Sudana</i> na <i>Dunia Hadaa</i> <i>John Mutua</i> , <i>Rocha Chimerah</i> na <i>Nancy Ngowa</i> .....	93
A Contextual Meaning Mislaid in Translation: A Case of Hedges in Presidential Political Speeches in Kenya <i>Gitonga Josephat John</i> , <i>Zaja Omboga</i> and <i>Jayne Mutiga</i> .....	103
Ukubalifu wa Silabi Funge katika Fonolojia ya Kiswahili <i>David Majariva</i> .....	113

---



## Mchakato wa Uandishi Bunifu kama Unavyoakisiwa katika Riwaya za Kisasa za K.W. Wamitila

Janice M. Mutua<sup>1</sup>, Issa Mwamzandi<sup>2</sup> na AbdulRahim Taib<sup>1</sup>

<sup>1</sup>Chuo Kikuu cha Egerton

<sup>2</sup>Chuo Kikuu cha Kabianga

### Ikisiri

Makala hayaimejibana katika ufafanuzi wa upekee wa mtunzi wa riwaya za Kiswahili za kisasa pamoja na changamoto anazopitia mikononi mwa wahariri na wachapishaji kama inavyopendekezwa katika riwaya zenyewe. Aidha, makala imependekeza njia za kuboresha na kukuza riwaya mpya za Kiswahili. Madhumuni yake ni kufafanua mchakato mzima wa uandishi wa riwaya mpya kwa kuwaangazia wahusika watatu muhimu yaani mwandishi, msomaji na mchapishaji. Nadharia ya usasaleo imeuongoza mjadala huu katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Mintarafu ya nadharia, mtunzi wa kazi bunifu ana uhuru wa kuandika jinsi apendavyo, hailazimu kwamba riwaya zifuata utaratibu mahususi. Mkabala wa uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kuchanganua data iliyohusiana na swala zima la ubunifu na uchapishaji wa riwaya mpya ya Kiswahili. Data ilichanganuliwa kwa kuangazia maudhui na vipengele vya mbinu za kimajaribio kama vile dayolojia, urejeleomatini, simulizi fupi na taashira. Riwaya za *Mwandishi*, *Msomaji na Mchapishaji* na *Musaleo!* zimetumika kuangazia mchakato huu. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Imebainika kuwa sura na ubunifu wa riwaya mpya ni zao la usomi. Ili kuelewa ujumbe katika riwaya za kisasa ni muhimu kwa 'mhariri' kufanya utafiti wa kina kabla ya kutoa mapendekezo yake kwa mchapishaji. Aidha, inailazimu hadhira kuwa na ufahamu wa mambo mengi kiada ili kung'amua yanayowasilishwa katika riwaya za kisasa.

**Maneno Muhimu:** *Kariba, Riwaya za Kisasa, Mwandishi, Uandishi bunifu, Mhariri, Mchapishaji.*

### Utangulizi

Makala hayaimezingatia shughuli zote za mtunzi wa riwaya za kisasa za Kiswahili na uandishi wake kama ilivyokodiwa katika riwaya zilizoteuliwa. Riwaya zinatoa mwito wa kipekee kuhusu uandishi wa riwaya pamoja na kubainisha changamoto wanazokumbana nazo waandishi wa kisasa hasa pale kazi zao zinapopitia mikononi mwa wahariri na wachapishaji. Aidha, zimeonyesha baadhi ya mapendekezo yatakayoboresha na kukuza riwaya za kisasa. Lengo kuu la kufanya hivyo lilikuwa ni kupambanua nafasi za mwandishi, mhariri na mchapishaji katika mchakato mzima wa uandishi na uchapishaji wa riwaya mpya kama unavyoakisiwa katika riwaya teule za K.W. Wamitila.

Mabadiliko ya kiutunzi yaliyoshuhudiwa yamemchora mtunzi wa riwaya mpya kama mwanajamii anayetumia mbinu zisizozoeleka katika kuwasilisha ujumbe mwafaka kwa hadhira. Mabadiliko ya kiubunifu yaliyoshuhudiwa yanawiana na taswira kamili ya jamii ya kisasa inayopendelea kufanya mambo pasi na kufuata utaratibu maalum kwa mfano, miundo na mitindo tofauti ya utunzi iliyotumika na kutapakazwa kote katika riwaya. Japo mwandishi anatekeleza jukumu lake la kuiwasilisha taswira kamili ya jamii katika uandishi, mtafaruku baina yake kwa upande mmoja na msomaji na mchapishaji kwa upande mwingine unatishia kuiangamiza tajriba yake. Riwaya zilizochunguzwa zinathibitisha kuwa mtunzi wa riwaya za kisasa si mtunzi tu bali ni binadamu mwenye uwezo na mwito wa kipekee. Zinaulinganisha utunzi wake na jambo linaloibua hisia kali ndani ya nafsi yake; kariha ya utunzi. Katika makala hayaistilahi riwaya za kisasa, riwaya za kimajaribio na riwaya mpya ya Kiswahili zina maana sawa. Aidha, istilahi uandishi imerejelewa pia kama utunzi huku msomaji akirejelewa kama mhariri.

**C: Mbinu za Kimajaribio katika Riwaya ya *Musaleo!***

<b>Riwaya</b>	<b>Simulizi Fupi</b>	<b>Mbinu Za Kimajaribio</b>	<b>Marejeleo (Ukurasa)</b>
<i>Musaleo!</i>	Wengine wanasema kifo chake kilitokana na juhudi za kuuchukua ubavu aliowanyang'anya wanaume. Sijui labda baba, babu, ukoo na jamii nzima ya wanaume vilihusika.	simulizi fupi	<b>UK. 3</b>
	Nitarudi kondo yangu ya nyuma imezikwa huku!	uzungumzi nafsia	<b>UK. 4</b>
	Sasa miongoni mwa wengi nilikuwa kiongozi anayetokana na kizazi cha Yunga Mwamba mwenye uwezo hata wa kuathiri majira ya ukame na mvua. Sasa nikawa Mzee Mleta Mvua.	simulizi fupi	<b>UK. 9</b>
	Kila hatua ina sifa zake. Sasa ilibidi nijengewe nyumba nzuri kwenye kiini cha nchi.	simulizi fupi	<b>UK. 9</b>
	Mjanja alikuwa huyu, nasi tukamwita Kitungule ingawa jina lake asili lilikuwa Mngumi.	simulizi fupi, lakabu	<b>UK.11</b>
	Kuna ithibati ipi nyingine kuliko kule kuja na uganga wa kugeuza chembe chembe?	simulizi fupi	<b>UK.12</b>
	Niliwaita “Vijana wa Mzee”	dayolojia	<b>UK.17</b>
	Siku zote babu akiniita Ukolongwe.	lakabu	<b>UK.19</b>
	Mashamba ya Mawe!”	lakabu	<b>UK.29</b>
	“Huyu inavyoelekea alizaliwa kabla ya wakati wake; hajaiva sawasawa; na watoto wote wanaozaliwa wakati huo wana sifa moja: vichwa vikubwa ambavyo havina chochote, unaweza kuwaita vichwamaji!”	simulizi fupi	<b>UK.35</b>
	Niliamua kufuata ushauri wake. Huko mbele nilimwona bundi aliyetua juu ya kitu kilichofanana na meli au jahazi. Meli ilikuwa ishara kuu nchini. ...Hii ilikuwa njia nzuri ya	simulizi fupi	<b>UK.58</b>

kumtambulisha Mzee kama nahodha wa nli ya taifa.

“Je, unamjua Mzee?” Aliniangalia kisha akaangua kicheko.	dayolojia	<b>UK. 62-63</b>
Daraja huvukwa baada ya kufikiwa!”	semi	<b>UK.68</b>
Mizizi ya mti wa uwezo wangu alikuwa anaanza kuitafuna chini kwa chini kama fuko. Ilibidi niwahi tumba la uovu kabla halijachanua na kutapakaza harufu ya uhasama nchi nzima. Wiki tatu baadaye profesa alikufa katika ajali ya barabarani. Niliongoza nchi nzima katika maombolezi ya kifo hicho. Jamaa zake niliwaahidi kuwasaidia. “Ikiwapata shida yoyote, nipigieni simu tu!” niliwakumbusha.	simulizi fupi, semi, dayolojia	<b>UK. 69</b>
Nilimsogea Mamanchi kumuuliza, Je, alikufa lini huyu?” nilisema kwa sauti ya chini lakini aliyasikia. “Minong’ono hainiwezi. Mimi sijafa, bado ninaishi milele! Mimi Veritas sio mtu wa kufa. Nifeje? Uliyekufa ni wewe!”	simulizi, dayolojia	<b>UK. 69</b>
“Nilisema kuwa Ukolongwe hakuzikwa: tazama kaburi lake bado li wazi. Niliwaambia wasiojifunza kutokana na historia wamelaaniwa kuyarudia makosa ya jana: makosa ya historia yenyewe!”	dayolojia	<b>UK.70</b>
“Nilimwonya akakataa. Ilikuwa lazima siku moja atafanya jambo la kumuudhi Mzee!” alitulia kisha akaenelea kama mtu anayejisemea, “Nilisema yule ni kizalia cha Ukolongwe wakakataa! Sasa wanayaona haya! Watu wanalala kwa miaka na miaka, usingizi wa aina gani huu?”	uzungumzi nafsia, semi	<b>UK.71</b>
Karibuni. Mama ni Mungu wa pili, niliwaambia na kuwakaribisha. Mtoto akinyea kiweo hakikatwi kabisa!”	simulizi fupi, semi	<b>UK.72</b>
“Hii ni nchi ya vinyume: mchana huweza kuwa usiku na usiku mchana.”	dayolojia	<b>UK.74</b>

<p>“Ile ni sanaa ya dhahania. Ehhh... Unaona mikono ya binadamu inajitokeza karibu na makalio. Juu huko kuna jichwa la kiumbe nimwitaye Jivi ambaye ana macho kadha kipajini ingawa sidhani kama yanaona chchote: Hayo matone ni machozi ingawa anayelia haonekani. Mara nyingine huhisi kama tunapapasapapasa uhalisi bila kuuona: kitu kama kile kisa cha wale vipofu na tembo!”</p>	<p>dayolojia, simulizi fupi, urejeleomatini, mwingilianotanzu</p>	<p><b>UK.75</b></p>
<p>Waliteswa na Ukolongwe na Kinyonga!”</p>	<p>lakabu</p>	<p><b>UK.77</b></p>
<p>“Je, unaamini kuzaliwa mara ya pili?”</p>	<p>semi</p>	<p><b>UK.78</b></p>
<p>“Kuzaliwa kisha kufa na kuzaliwa tena.”</p>	<p>dayolojia</p>	<p><b>UK.79</b></p>
<p>Nilikueleza kuwa wanadai huku kuwa ninadumu. Hawajui. Unaweza kusema hivi; sehemu yangu fulani iko huku na nyingine upande wa pili. Ni kitu kama kusema kuwa nimekufa na kuishi wakati huo huo.</p>	<p>simulizi fupi</p>	<p><b>UK. 80</b></p>
<p>Nyinyi ni kiungo chetu upande huo; tuepusheni na ukuba tuliotupiwa na wanaotulizia ndege wabaya.</p>	<p>simulizi fupi</p>	<p><b>UK. 80</b></p>
<p>Mimi huwa walipo wazungu na ndugu zangu. Mimi ndiye kimbilio lao na kificho chao; mwanzo na mwisho wao. Mimi ni kiini chao.</p>	<p>simulizi fupi</p>	<p><b>UK. 80-81</b></p>
<p>Unasikia? Waambie wanapita wao mimi ninaishi milele! Tumaini la kesho limefungwa kwenye mwili wangu. Wana wa kesho watanyonya maziwa yangu.</p>	<p>uzungumzi nafsiya</p>	<p><b>UK.81</b></p>
<p>Zamani alinionya mwalimu wangu kuwa nikitaka kuliwazia jambo gumu ninaloambiwa niyafunge macho. Unasikia, yafunge ili ufanye akili yako iwe pamoja. Katika hali ile unaweza kuwaza na kutafakari vizuri!</p>	<p>simulizi fupi</p>	<p><b>UK.81</b></p>

<p>Hadithi iliendelea:          Nilikuwa nimefika mbali na mipango yangu          ya kuwa kiongozi wa kudumu. Jina          nilishatafuta la kufaa: OMNIMZEE. ...          Uongozi unaenda sambamba na ugumu.</p>	<p>simulizi fupi,          lakabu</p>	<p><b>UK. 85</b></p>
<p>Mzee, wanasema huu ni upepo mwingine!.          Kuna maneno yanayodai kuwa umepita Baa          la Ini huko Njaamani na hata kuangusha          ukuta uliojengwa zamani kuweka mpaka kati          ya imani na ndoto.</p>	<p>simulizi fupi,          urejeleomatini,          utohozi, lakabu</p>	<p><b>UK. 87</b></p>
<p>Ni zimwi likujualo. Unasikia bwa'mdogo we,          hayaumani meno ya mbwa. ... kile kimbunga          hakikuwa kimeangusha ukuta tu bali majengo          kadha imara; makasri hata ya wafalme.</p>	<p>methali, simulizi          fupi, dayolojia</p>	<p><b>UK. 88</b></p>
<p>Vua kubwa lilishaanza kuanguka na makao          kadha ya maskini yalisombwa. Tangu siku          zile watu waliniheshimu kama Mleta Baraka,          yaani tangu mazingaombwe ya          chembechembe. Bado unakumbuka?.</p>	<p>dayolojia, lakabu</p>	<p><b>UK. 88</b></p>
<p>Mzee Mvumbua Usomi!</p>	<p>lakabu</p>	<p><b>UK. 91</b></p>
<p>Nazikumbuka hata sauti za watu          wakishangilia ufufuo mpya! Ehh, akapewa na          jina mpya: Musaleo! Musaleo! Musaleo! Ile          ya pili ilidakia, "Siku hizo aliweza          kutegemewa. Nakumbuka hata wazee          wakisisitiza kuwa mwanzo wa nazi kokochi.          Kisha?" ... "Kichwa cha kuku hakistahimili          kilemba. Akajawa na kiburi na kusema ndiye          anayeumiliki ukweli. Akasahau ukiujua huu,          huu huujui.</p>	<p>dayolojia. semi,          simulizi fupi</p>	<p><b>UK. 92</b></p>
<p>Ilipodaiwa kuwa ana chembechembe za          Ukolongwe katika mwili wake akaja juu!          Mabaya yaliyopo yanatokana na jana. Uhalisi          uligeuzwa, meno ya mbwa yakaanza          kuumana!"</p>	<p>simulizi fupi,          methali</p>	<p><b>UK. 93</b></p>
<p>Palikuwapo na wanaume wanne walioketi juu          ya jabali kubwa lililoinamiwa na mti ambao          sikuweza kuutambua. Katikati yao palikuwa          na moto uliowaka bila ya kuzimika ingawa          sikuona ishara zozote za kuni.</p>	<p>urejeleomatini</p>	<p><b>UK. 93</b></p>

Nchi hii haina tatizo la usalama, hiki ni kisiwa cha Amani katika bahari iliyochafuka!”	simulizi fupi	<b>UK. 99</b>
Lazima mtu uwe imara: usinywee tu, haitoshi kuishika fimbo tu. Lazima uitumie na mara hii sio kupasulia maji! Nyama za leo zinahitaji kuchangamkiwa!”	dayolojia, simulizi fupi, urejeleomatini	<b>UK.100</b>
Ilibidi kila mtu ajue Mzee ni Osagyefo. Musa. Jogoo anayewaandama Makoo Wote. Simba Mwangusha Falme na Mjukuu wa Solomon.	urejeleomatini, simulizi fupi	<b>UK.101</b>
Shujaa Mfumua-Ufalme wa Uingereza. Life Preident. Alpha na Omega. Kilele kilikuwa pale Profesa alipopendekeza apewe jina mpya kutokana na wasifu wake, kutowezekana. Jina alipendekeza yeye: Jini-Badiri-Boko Hasa!	urejeleomatini, simulizi fupi	<b>UK.101</b>
Coup d’etat. Ukabila. Ethnic Cleansing. Wazazi wakafa, wakabakia watoto waliolazishwa kushika bunduki. Shule wakasusia. Kwa kifupi, sanduku la Pandora lilifunguliwa upya. Lilibakia wazi maskini!	simulizi fupi, urejeleomatini	<b>UK.101</b>
Mbona wananiua mara ya pili. Wanangu wenyewe?	semi	<b>UK.102</b>
Uwanja wa Mafanikio.	semi	<b>UK.103</b>
Akili iko katika giza la kufunga macho? Profesa huyu huyu hapa alikuwa akifanya utafiti fulani aliopewa wakati huo. Profesa: Ehh! Nilisema ni heri neno linalotamkika; watu hawataki kujisumbuasumbua! Kasuku: hasa! Tuliwaza siku nzima. Mawaziri hawakuenda kazini siku hiyo wakiwazia jina hilo. Siku iliyofuatia tulipata pendekezo la Profesa: Dogmazee! Tutaitikia Dogmazee! Dogmazee! Dogmazee! Mara tatu. Wachache walitaka tuanzia vyuo vikuu. Mzee akaja juu: Kambare mkunje angali mbichi, mti hupindwa ukiwa mkinda.	semi dayolojia, semi/methali, uradidi	<b>UK.104</b> <b>UK.109</b>

Asali walijipakaa hasa na maziwa waliishia kunawia.	simulizi fupi	<b>UK.110</b>
Alichukizwa kuona watoto wanajizungukia tu. Isitoshe, walitoa picha mbaya kwa watalii.	simulizi fupi dayolojia	<b>UK.110</b> <b>UK.116</b>
“Walijitahidi kuizika historia! Jitihada za kuizika historia! Historia ndiyo inayozika!”		
Jivi na wenzake (wanasema walikuwa wengi). Imani yao ilikuwa dudu liumalo halipewi kidole. “ Vipi bwana, majuzi tu... tukubali tena?” waliuliza. Wengine walidai kuwa uhusiano wao na Jivi ulikuwa wa kidugu ati. “Lazima tuudumishe udugu kwa sababu mkataa wengi ni mchawi. Ndugu yetu huyu, na zimwi likujualo halikuli likakwisha!”	semi, simulizi fupi, dayolojia	<b>UK.118</b>
“Ucheshi ndio uboho uliobakia katika mifupa ya uhai wetu! Bado tunajua nafasi ya komedi katika maisha ya binadamu!”	dayolojia	<b>UK.120</b>
Kijiji hiki kina sura ya meli. Hiki ni kijiji kinachoelea majini. Tezi na omo ina ndumulakuwili. Jina lake Yanguis. Anasema uwezo wa kushusha winchi kufumbua msuko wa tanzia!” Kichaa aliketi chini. Wasomi walibaki wakiangaliana na kuambizana. Usimchezee jamaa yule, anamjua Aristotle sawasawa.” “Lazima alimsoma Euripides.” “Huyo lazima ana mwelekeo wa kirasimi!”	dayolojia, simulizi fupi, urejeleomatini	<b>UK.120</b>
Ni kitu kama Super Power na mimi siihitaji Super Power, mwenyewe ni hiyo yenyewe. Nilianza kuyapitisha majina yote akilini. Shai-Tani halikutamkika vizuri na ilielekea lilikuwa na maana mbaya mbaya hivi. Mjomba nalo nililiona halifai. Je, na Yanguis? Hili lilitamkika vizuri. Nilijaribu maharaja mbambali: Yang.. iii.i.ii! Yangwi.i.i! Yangi...i.iisi! lakini maana yake ni nini? Ahh, potelea mbali. Hakuna jina lisilomkuza mtu. Niliweza kutasawiri akilini jinsi hadhira itakavyolipokea jina langu hili.	simulizi fupi, uradidi	<b>UK.121</b>

Mzee Yanguis! Mzee Yanguis! Mzee Yanguis!

Zamani kuna wakati wanawake walikuwa kila kitu, viongozi mpaka hata miungu. Waliwatesa wanaume sana. Basi siku moja nao wakaamua kuwa lazima wajitoe katika hali hiyo ya kuteswa. Unasikia bwana? Ndio walikwenda mzengwe. Walipitisha muda wakisemezana na kuambizana. Neno hapa, kineno pale, wazo pale. Mwisho wakakubaliana. Hamna njia nyingine. Ehh, haipo nyingine ya kujitoe kwenye mikono hii isipokuwa kujitahidi kuwanyamazisha. Njia ya pekee ilikuwa moja tu: kuwatunga mimba wanawake wote. Hali ilivyokuwa hivi basi wakabiruliwa biru na wanaume wakachukua nafasi zao.

simulizi fupi,  
semi,  
urejeleomatini

**UK.123**

“Katika ulimwengu wa leo maana za maneno zimebadilika. Chukua maneno yafuatayo: kijiji, uzalendo, uhuru. Sote tunajua maana ya kijiji. Wanakoishi watu kwa ujirani na mapatano; ndugu, mama, baba, babu, na nyanya, mifugo na mizimu yao. Wote wanaheshimiana na kusaidiana, hamna kiongozi wala anayeongozwa. Lakini kwingine kijiji ni kitu kingine kabisa. Tena mara hii kinaongozwa na sio na babu bali na Mjomba!”

simulizi fupi,  
dayolojia

**UK.127**

Hatimaye Profesa aliyapeleka macho yake kidimbwini. Alianza, “Unaona yale maji yanapita, yamepita kwa karne na karne. Kidimbwi kiko pale pale. Kidimbwi kimebakia katika hali ile ile licha ya dhoruba za maji. Usikione vile, kimeona mengi. Unayaona maji yale kutulia lakini yanaweza kubadilika ghafla na kulipindua lile jahazi nahodha asiweze lolote. Wakati mwingine maji yapitayo huwa mekundu ajabu. Maji ya damu. Yafikapo kidimbwini hukoza rangi na wekundu ukatisha. Lile jahazi liko pale pale; siku hizo linaelea juu ya damu. Linaenda tezi. Linaenda omo. Halina nahodha. Alikuwako na akacheza na kuishia kuwa asusa ya maji

simulizi fupi,  
semi/methali

**UK.127**



yaliyo chini. Kama uanaingiliana na wazee lazima ulisikia kitu kama *ukangaapo tu chini ya gae.*”

Hakuna giza lisilochewa.	simulizi fupi	<b>UK.128</b>
Nilipotokeza ng’ambo ya pili nilijihisi mchangamfu. Lazima ilikuwa siri ya maji.	simulizi fupi	<b>UK.128</b>
Nilishindwa kuyafungua lakini sikutaka kuishi katika giza. Nilijitahidi kuyafungua.	simulizi fupi	<b>UK.130</b>
“Mtafuna polepole huishia kumeza.	semi, methali,	<b>UK.134</b>
Kinachodumu pamoja ni jabali tu.” Methali ambazo zamani hazikutilia maanani zimeishia kuwa liwazo kubwa.	simulizi fupi	<b>UK.134</b>
Alikuwa bado kituoni ilipopiga mvua ambayo haiishi siku hizi kuanza kuanguka mfululizo.	simulizi fupi	<b>UK.134</b>
Kila moja lilikuwa na kichwa chake: Mzee Azirai Matopeni- Kanyeshewa Mara ya Kwanza! Life President Atorokea Uarabuni. Jogoo Anayewaandama -Makoo –Wote Asafiri Ughaibuni. Yangwii-Mzee Ayoyomea Mwituni. Musee Achujwa na Demokrasia. Moja linalopendwa na wafuasi na wakereketwa wa kiongozi liliandika kwa kifupi tu: Yunga Mwamba Milimani, tena! Jengine lililopendwa na wasomi kutokana na lugha yake ngumu liliandika: Kisasili chayeyuka Kwenye Uhalisi. Gazeti moja maarufu lililochapishwa katika maeneo ya pwani na lililopendwa sana na wavuvi, wakwea minazi, wagama, ,mabaharia na makuli lilisema: Bahari Yachafuka, Nahodha Kinda na Meli Yake Wazama.	simulizi fupi	<b>UK.135</b>
Moja lenye mwelekeo wa kidini liliandika kwa kifupi: Mafuu ya Kufuru.		

harufu ngeni ilienea kila mahali kama eneo  
lililosombwa takataka linavyoachwa  
likivunda kwa harufu ya uozo. Wote  
waliyacheua yote hayo huku wakielezana  
kisa cha Musaleo: kisa ambacho mara hii  
kilipigwa mwanzi ulimwengu mzima!

---

simulizi fupi,  
tashbihi

**UK.136**

**D: Simulizi Fupi zenye Taashira katika Riwaya ya *Msichana wa Mbalamwezi***

<b>Riwaya</b>	<b>Simulizi Fupi</b>	<b>Marejeleo (Ukurasa)</b>
<i>Msichana wa Mbalamwezi</i>	Mapaka shume ya jijini. Lazima yaliwafuatia panya buku waliotokeza hapo ghalani mara kadha au labda makombo ya chakula kwenye jalala kubwa lililokuwa upande wa nyuma wa kontena lenyewe. Ghala la Mlo liliwavuta watu mfano wa ganda la muwa linavyowavuta chungu.	<b>UK. 5</b>
	Nje kulikuwa na mabehewa ya magari moshi yaliyobambuka rangi na kuchakaa na kujaa vumbi kama mimea ilivyokuwa kando ya barabara ya vumbi.	<b>UK. 5</b>
	Ndani ya hoteli hiyo kama mtu anayekagua chumba chake.	<b>UK. 6</b>
	Mgongoni pake palikuwa na picha ya rais wa nchi ambaye hata naye amepanda ghalani.	
	Niliwaangalia walivyoegemea kama wasafiri waliochushwa na machovu ya kukaa kwenye basi kuukuu linalolishindwa kuukwea mlima wa maisha.	<b>UK. 8</b>
	Nikakumbuka jinsi mhubiri wa kanisa alipotokeza ili kutugutusha kuwa alikuwa karibu. Halafu jinsi kwa sauti yake nzito mithili ya mtangazaji wa redio, alivyotukemea huku ameyafutua macho kwa kuigeuza ‘Nyumba ya Mungu kuwa pango la Wanyang’anyi’.	<b>UK. 8</b>
	Nilihisi kitetemeshi fulani mwilini kisha vimulimuli vya machoni vilivyonifanya nione taswira za vipepeo katika giza la macho yangu yaliyofungwa.	<b>UK.32</b>
	Kwenye giza la macho yangu, nilijaribu kutafuta kama ningeweza kupekuapekua na kupekenyua hapa na pale na kufichua yalijificha hayo maisha yaliyocheza	<b>UK. 33</b>

mwajificho nami na labda niyacheke kama  
tulivyofanya zamani nilipocheza mwajificho  
na vijana wenzangu.

Nilitamani kuyaona kwenye giza hilo, labda  
kwa kuona macho yake yanayoangaza gizani  
kama macho ya paka yaliyopigwa na  
mwanga wa kurunzi, na kuyauliza msururu  
wa maswali niliyokuwa nayo.

Nilishindwa kula na gizani nikawa bundi.

**UK. 35**

Ili kuukatiza mkondo huo wa mawazo,  
niliamua kulizima joto la hali iliyonizunguka  
kwa barafu ya kumbukumbu zangu.  
Kumbukumbu ni ganzi nzuri ya kupoza  
maumivu ya sasa.

**UK.38**

“YK...pole sana bwana, jikaze kabisa wala  
usife moyo. Haya ni maisha yetu  
bwana...ni...mtihani wa muda, ni kile  
kishawishi tunachoomba tusitiwe kila siku.

**UK. 41**

Mke wa Konzi, Tabitha, akaruka juu. Hawezi  
kuuvunja mgongo wake usiku na mchana  
kwa ajili ya mwanamume. Mwanamume  
ambaye lake ni kuja kukaa hotelini  
kudondokwa na udenda anapowaona  
wanawake wenye ngozi za nyanya kama  
kelbu anayeshabikia mzoga wa punda. Hajui  
kwanza anakwenda kinyume cha maagizo ya  
Muumba kwa kufanya hivyo?  
Alishautundika uta wake na podo la mishale  
ukutani vilikookotea vumbi, na kwanza kama  
kuna mtu anayeyajua hayo vizuri ni  
mwenyewe Tabitha.

**UK. 50 - 52**

‘Ikiwa wewe ni bafe, basi mimi ni bingwa wa  
kuitopoa sumu yake!’

“Jogoo gani wa kuwika; jogoo alishajifia  
zamani!” akasema Konzi siku hiyo.

“Basi huyo mfu anawika!”

haoni aibu, mtu mzima na ndevu zake tena  
nyingine zenye mvi.

“Hayo eehh...Hii miili yetu ni ya dongo  
towe...tukinyeshewa kidogo, hata na mvua

**UK. 57**

za rasharasha tunakuwa na utelezi.  
Tunanyumbuka nyambu nyambu kama  
nyumba zinazojengwa na watoto wakiwa  
mafugani! Kinachobakia ni kusombwa na  
maji ya mto wa maisha hadi kwenye bahari  
ya usahaulifu.”

Nilimwangalia na kushangaa kama aliweza  
kuubaini uchungu uliokuwa ukinisumbua  
hapa nilipokuwa. Akilini niliisikia sauti ya  
methali ya zamani niliyoisikia tangu nikiwa  
shule ya msingi; wanaume ni kuni  
zinazootana motoni (hawawezi kuoneana  
huruma). Labda huruma na mapenzi  
vimefumbatwa na ishara ya mwanamke.  
Ishara ya Amore. Ishara ya Msichana wa  
Mbalamwezi.

**UK. 61-62**

Iliendelea kuwaka bila ya kuzimwa na  
kunikumbusha mwanamume mmoja wa  
kijijini ambaye alipokuwa akitoka kwenye  
soko la karibu, alikotoka takriban saa nne au  
tano za usiku kila siku, alikuwa na mazoea ya  
kuiwasha kurunzi yake njia nzima kwa  
sababu ya kuliogopa giza – walivyosema  
watu.

**UK. 74**

Katika akili yangu nilianza kuisawiri picha na  
umbile la kifo. Labda kifo kilikuwa mgeni,  
yamkini mwenye wivu mwingi, anayetembea  
kwenye nchi ngeni (labda asikotakiwa wala  
kukaribishwa), anayejizungukia na furaha na  
matumaini makubwa ajitose ndani, bila ya  
hata kubisha, na kuyapopota matunda ya  
matumaini kwenye mti wa uhai. Au labda  
kilikuwa mwizi, mfano wa yule mzee wa  
kijijini aliyezunguka na chembechembe za  
mahindi alizofunga kwenye uzi mrefu na  
ambazo alizitupa karibu na palipokuwa na  
kuku, kisha kuku mmoja, kwa tamaa ya  
kutaka kuzilimbuka, akadona, naye kwa  
ujanja mkubwa, kama mvuvi anayeivuta  
ndoana, akavuta haraka haraka, kimya kimya  
hadi kuku anampofikia naye anambwakura  
ghafla na kizitimua mbio. Au kifo ni mtu  
anayejizungukia na kujihangaikia, kama

**UK. 75-76**

hambe aliyekosea makao, na ambaye mara anapoonana mwanya au mlango ulio wazi anajitoma ndani ghafla kama mtu anayeikimbia mvua. kwa maneno ya daktari asiyeikosea, daktari ambaye ametaalamika vizuri sana, nilikuwa bado na siku ishirini na tano, kuonana, ana kwa ana, kope kwa kope, bila ya kuyakapua macho yangu, na jamaa huyo anayekuja usiku wa manane kama mchawi.

Kwa kuwa ulikuwa usiku wa mbalamwezi, akawa Msichana wa Mbalamwezi.

**UK. 101**

kuwepo na hatari ya kuiharibu salamu iliyoko. Ni kama kuipasulia nyongo ilipo nyama; nyama ya ulimi.

**UK.115**

Au labda mapenzi si kiumbe; ni dhoruba dhahania ambayo inamjia mwanadamu ghafla kama chamchela. Ikamzoazoa kama usufi na kumpeperusha kwenye anga ya ndoto – ramsia ya ndoto na kwenda kumtua kwenye ulimwengu ajinabi, anaoshindwa kuelewa?

**UK. 131**

Labda palikuwa na mfanano fulani kati ya kifo cha mapenzi. Mapenzi yaliyopotea; kama yale ya Msichana wa Mbalamwezi; kama yale ya Diana, ni aina fulani ya kifo. Je, kuna uhusiano gani kati ya kifo kinachonijongelea na mapenzi yaliyonikimbia? Mapenzi na Kifo. Uhai na Kifo. Riale kwa ya pili?

**UK.132**

Jana yao ifariki – kabisaaa! Lazima unafsi wao ufe; ili umoja wao uzaliwe. Mbegu lazima ife ndipo mche uweze kuota. Kifo lazima kitangulie mapenzi au hata mapenzi yawe chanzo cha kifo kama ilivyotokea zamani. Yesu alikufa kwa kuwapenda wenye dhambi; kifo chake kikawa mwanzo wa mapenzi – bila kifo hakuna mapenzi. Hakunaaa!

**UK.132**

Nikahisi kama kijana aliyesimama kwenye kilele cha mlima kisha akasukumwa na

**UK. 139**

wenzake kuelekea upande wa chini; hana njia ya kukwepa, lazima akimbilie chini; anachoweza kufanya ni kujitahidi kuipunguza kasi yake ya kwenda chini lakini hana budi kukimbilia huko; anavutwa na kani ya uvutano. Yaelekea hata sasa hapa nilipo nilikuwa navutwa na kani ya uvutano; uvutano wa mauti.

Nilijaribu kuwazia niliyoshauriwa na maneno yale. Taswira ya mivinje inayopulizwa na upepo majira ya jioni ikanijia akilini; nikaweza hata kuisikia vizuri sana.

**UK. 142**

“Je. Kipepeo ameruka na kuondoka?” Sikumjibu. Nilimwangalia na kutabasamu; sikujua niseme la au ndiyo. Lakini ujumbe uliofumbatwa na maneno yake ulikuwa wazi. Ingawa laki lilikuwa swali, nilitambua kuwa alikuwa ananipa taarifa fulani kwa njia ya upole.

**UK. 146**

Je, naye ataweza kunitambua? Au labda hakuhitaji kunitambua wala mimi sikuhitaji kumtambua – alikuwa kila mahali; alikuwa moyoni na moyo unaweza kutambua unachokitafuta wakati wowote ule. Moyo si mtumwa wa macho; macho ni *mamluki* wa moyo ambao ndio *maliki*.

**UK. 157**

Niliyakumbuka maneno aliyowahi kuniambia: Kijana usijisumbue kwa mawazo yasiyofaa kwa kuiwazia kesho ambayo hujui ina siri gani; hata wanasayansi na ujuzi wao hawawezi kujua hiyo kesho au siku hizi mwanangu wanasayansi na utundu wao wamevumbua hadubini za kuona kesho? (Kimya) Usijikalifu akili yako kwa tanzia ya maisha... tafuta ramsia au futuhi iliyoko kwenye maisha yenyewe ili uicheke tanzia yenyewe. Hicho kicheko kitakuwa na uwezo wa kukutakasa na kukupa nguvu za kuendelea mbele na utakuwa na tamaa ya kuelekea huko mbele badala ya kukaa tu ubururwe na nguvu za wakati. Mwanangu, kila janga lina mwanga fulani kwenye

**UK.160-161**

vyumba vyake vya siri. Upande wa pili wa mauti, kama hujui, ni mapenzi. Matatizo na uchungu wa maisha upo ili kutufundisha jinsi ya kupenda zaidi! Mwanangu, huwezi kuijua na kuithamini furaha kabla ya kuyakabili matatizo!

Nilipania kuufuata ule ushauri wa Mzee Maftah; lazima unatokana na uzoefu wake wa maisha.

Niliweza kuielewa hiyo lugha ya kipekee ya mapenzi – lugha ya kibinafsi na isiyokuwa na sura wala umbile la maneno yasemwayo; lugha ya mtazamo wa macho. **Lugha ya kimya.**

**UK. 163**

Nilihisi nanga fulani iliyokuwa kwenye mabega yangu imeenguliwa ghafla na kubwatika chini.

**UK. 177**

Kwanza sikuweza kukiona chochote akilini isipokuwa giza jeusi tititi lililokuwa na taswira zilizochezacheza tamthili ya kivuli wakati wa mbalamwezi.

**UK. 185**

Tukio lenyewe lilinifanyia kuhisi kuwa ule wakati aliouzungumzia Mshenga Adomis Kiranga, daktari anayefahamu mambo mengi, asiyeanguka mitihani wala kukosea, utafika mapema zaidi kama mkimbiaji anayemaliza mbio kwa kutumia njia ya mkato.

**UK. 187**

...huweza kuteleza ulimi tu; si lazima awe na maradhi yoyote, ila ni sifa ya kawaida tu ya mwanadamu, kila mwanadamu. ...mwanasaikolojia aliyeitwa Sigmund Freud, aliyesema kuwa hiyo mitelezo ya kauli huwa ina ukweli mkubwa.

**UK. 192**

---



**E: Simulizi Fupi zenye Taashira katika Riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji***

<b>Riwaya</b>	<b>Simulizi Fupi/Taashira</b>	<b>Mbinu za Kimajaribio</b>	<b>Marejeleo (Ukurasa)</b>
<i>Mwandishi Msomaji Na Mchapishaji</i>	Jamaa huyo akasema alitoka kwao kutokana na msukumo wa jasira. Hiyo jasira ni jadi yake, akasema yeye anapenda kujusuru. Ni jasiri. Alijasiri njia nyingi peke yake. Ni jusuri.	simulizi fupi	<b>UK.24</b>
	Nchi ambayo ilikuwa kanzi ya maarifa muhimu yaliyomhusu kila mtu. Je, kwa kusema “kila mtu” anamaanisha hata na wao?	simulizi fupi	<b>UK. 24-25</b>
	Alipoulizwa nchi yenyewe ilikuwa wapi akasema ilikuwa huko Majuu. Majuu kama huko anakoishi Muumba wa Watu na vyote vilivyo ulimwenguni? Akawadangana macho pekupeku huku na kule (wanasema nini hawa?) kabla ya kusema: Mmesema.	simulizi fupi, lakabu	<b>UK. 25</b>
	Mjakuja akapendezwa na hewa ya huku	lakabu	<b>UK. 27</b>
	Ya kwao ina mazoea ya kununa na kugomba kama mwanadamu mwenyewe kila baada ya miezi michache; ya huku inatabasamu na kucheka kama wenyeji wenyewe.	simulizi fupi, tashhisi, tashbihi	<b>UK.27</b>
	Ni njia ya kupita chombo kirefu kinachokwenda kikipindapinda huku na kule. Kama nyoka?	simulizi fupi, tashbihi	<b>UK. 30</b>
	Mzee mmoja akakohoa na kusema kuwa zamani kuna mwanamke wa jamii fulani aliyetabiri haya...Akataja hata jina la mwanamke huyo! Syokimau. Nini? Alisema atakuja mtu ambaye atakuwa ameutia moto mfukoni...anaona joka kubwa likinyiririka kutoka baharini hadi ziwani. Aliongeza na mengine. Joka lenyewe linatema moto kama jinamizi.	simulizi fupi	<b>UK. 30 -31</b>
	Moto mfukoni? Joka kubwa kutoka baharini hadi ziwani? Hawajasoma Biolojia? Nyoka hawaishi majini! ... Lakini kwa kutotaka kuwaudhi akaamua kusema kuwa labda mwanamke huyo alikuwa na maana nyingine.	dayolojia, uradidi, simulizi fupi	<b>UK. 31</b>

Utukuni	lakabu	<b>UK. 32</b>
Wengi hawakumwelewa. Walidai kuwa mzuka wa ushairi ulimfanya kusema mambo yasiyoeleweka ingawa wanashuku yana maana.	simulizi fupi, lakabu	<b>UK. 42</b>
Turudi tena pale pahali pao pa makutano. Utukuni. Mfumo wao wa zamani wa kubadilishana bidhaa ukaingiliwa na hayo mafundisho mapya ya Faranga.		<b>UK. 44</b>
Mikoba, Konde, Payo na Mtumishi Askari Joma. Maburende Mwana-Mpotevu Maburende, Mwana-Mpotevu...Atafutwe fahali mzuri achinjwe. Wakubwa zake wakasema haistahili. Miaka yote hii alikuwa amewaacha na kuyoyomea wapi Mungu. Sijui. Harakati za kupambana na mjanja alizikosa. Iweje sasa amefika na kuandaliwa karamu?	lakabu  simulizi fupi, urejeleomatini, lakabu	<b>UK. 50</b>
Na kila wanapofanya hivyo lazima wajivue magwanda ya ngazi iliyotangulia na kuyaacha kabisa. Hata jina wanalibadilisha. Lazima sasa wawe na jina ambalo linaonyesha kuwa wametoka kwenye kipindi hicho cha Joelon.	simulizi fupi, semi	<b>UK. 52</b>
Mzee-Mpenda- Mashairi Silver Mikoba – Ndugu Mikoba Lord Konde – Bwana Konde Drivel Payo – Rama Payo Instrument Askari Joma – Mtumishi Askari Joma	lakabu	<b>UK. 55</b>
Ya kuazima haisetiri matako. Yakatafutwa majina ya mashujaa wengi. Mugasha, Liyongo.	methali	<b>UK. 55</b>
Baadaye ilitangazwa hata kwenye redio ya taifa. Hiki ni kipindi cha mwanzo mpya. Hiki ni kipindi cha kuzaliwa upya. Ya kale hayapo tena. Mtu hawezi kuzaliwa upya asipokuwa na jina jipya na kwamba hicho kinachozaliwa	simulizi fupi	<b>UK. 56-57</b>

upya kina uwezo mkubwa kuliko  
kilichokizaa.

Hawaoni hata nywele yake ni kubwa ni kubwa na ndefu ajabu. Hajainyoa kwa miaka mingi...Ni kama ya Shujaa Samsoni katika Biblia. Matenzawa	simulizi fupi, urejeleomatini, lakabu	<b>UK. 56-57</b>
Matenzawa atapokezwa kijiti cha kuendeleza mbio za maisha ya jamii yao, ya nchi yao. ...muda mfupi baadaye akahamia makao mengine yaliyokuwa mjini huko walikosema ndiko zilikotua ndege zilizopita angani.	simulizi fupi, semi	<b>UK. 58</b>
Ilikuwa hadithi bubu.	sinekidoki,	<b>UK. 66</b>
Lawalawa za Joelon. Hata tende alizokuwa wanakula tangu zamani wakaanza kuzisusia.	simulizi fupi	<b>UK. 67</b>
Msiache mbachao kwa msala upitao... kama wazee hawajui ni gwanda lililoangikwa mtini kuwawinga ndege lililopigwapigwa na upepo na kurarukiana na hata kuwafanya ndege wenyewe kuja kutua juu yake na kulinyia. Hawa ni ndege wa wakati.	simulizi fupi, methali	<b>UK. 67</b>
Kimbunga cha hali mpya kilimzoa kila mtu kama ubua na kumpeperusha pepetu kwenye anga za ndoto; anga za Alnacha.	simulizi fupi, urejeleomatini	<b>UK. 73</b>
...ardhi ambayo ilikuwa imefunika hazina kubwa kwenye utumbo wake.	semi	<b>UK. 76</b>
Hawazitumii kwao lakini ni zao la utafiti na anaweza kuwa mtu wa kwanza kufaidika kutokana na uvumbuzi huo.	kinaya, simulizi fupi	<b>UK. 75</b>
Akanyamazisha sauti za akina Marugurugu na wenzake. Ujumbe wa kufuatilia kujua kama msaada wao ulikuwa wa kufaa au la. Ilikuwa Barua ya Kumbukumbu. Ahadi ni deni	simulizi fupi, kinaya	<b>UK. 75</b>

...Sasa yeye anachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kuwa amefungua njia. Atafute ujanja wowote ule lakini sharti, vyovyote atakavyofanya, afanikishe kupasuliwa kwa huo utumbo wa ardhi na kukakatuliwa kwa majabali hayo ili kufichua yaliyokuwa ndani. ...Watu husema unaweza kutoka walipo ndovu ukashusha pumzi kumbe unaelekea waliko mbogo.	simulizi fupi, semi,	<b>UK. 75-76</b>
Hakuna anayejua taarifa yenyewe ilifikaje kijijini. Yamkini wanaposema kuwa msitu una masikio wana maana hii.	semi	<b>UK. 80</b>
Wakiwaa waliutumia kupangia vikao vyao maji ya madhila ya Mjakuja yalipotishia kuwafika shingoni. Miti inatiwa kitanzi.	semi	<b>UK. 80</b> <b>UK. 83</b>
“kanyiririka kutoka mlimani!”	semi	<b>UK. 87</b>
Na watakaporejelea miezi miwili au mitatu baada ya kuwauzia nafaka kwa bei ya kutupwa, sasa walilazimika kuzinunua kwa bei ya kusapwa.	semi	<b>UK. 88</b>
Pendekezo la Mshauri Mkuu Monaterium Mysterium (ambaye watu waliposhindwa kulitamka jina lake kubwa –walitumia jina linalokaribiana na hilo, kwa mantiki yao, akawa Bwana Mikoba Mikubwa).	simulizi fupi, lakabu	<b>UK. 100</b>
Amemkunjia mikono ya shati Msomaji anapopata maana ya matini ya fasihi anayodhani ndiyo ya pekee, anayaziba masikio yake ya fahamu na kwa njia hiyo anajinyima fursa ya kuupanua mwanda wake wa kifasiri.	simulizi fupi	<b>UK. 101</b>
Mbegusato ni mbegu za kisasa ambazo ni tokeo la utafiti. Ni zao la watafiti na wanasayansi maarufu wa ulimwenguni (hata wengine wameshinda tuzo muhimu za kiulimwengu kutokana na tafiti zao hizo ikiwemo ile ya Nobel). ...mbegusato ni inkinsari ya kishairi.. mkufu mrefu wa	simulizi fupi, uradidi	<b>UK. 105, 107</b>

njaa...Nanga ya dhiki.

Umri wake ushaanza kumwinamia magharibi;nguvu zake mwilini zilishaanza kusapwa na hiyo kasi ya maisha ya siku hizi. Kitu cha pekee ambacho hakikuelekea kuathiriwa na umri wake ni uwezo wa kuona. Akishindwa kuvitambua vilivyo karibu atasema kuwa anaweza kuviona vya mbali vizuri sana.	simulizi fupi	<b>UK. 107</b>
Sijui wanachomaanisha kwa kusema hivyo. Lakini ushairi unafungamana na hisia - tena hisia kali; ziwe za naima ya furaha au kilindi cha tanzia. Ushairi ni mapigo, mapigo ya kimaisha. Ni nini kilichomwoko Matenzawa? “kupiga mbizi majini”	simulizi fupi	<b>UK. 107</b>
“uhusiano uliopo kati ya maji na Matenzawa ni uhusiano wa Baraka; si uhusiano wa janga. Alichofanya Matenzawa tu ni kujizika majini wala si kuyakausha maji yenyewe!”	simulizi fupi, uzungumzi nafsia	<b>UK. 112</b>
Kuwa waliohusika hawakuwa tu akina pangu pakavu tia mchuzi bali kina Shaka-nanyangumi-wala samaki wengine.	simulizi fupi, semi	<b>UK. 120</b>
Ya kale hayanuki. Akaambiwa siku hizi yananuka, tena sana. Matenzawa akatamani hata kucheka.	simulizi fupi, methali	<b>UK. 124</b>
Kuwa wanawake na watoto wanaoatilika kwa baridi na upepo wanapata hifadhi kwa sasa. Asipofanya hivyo, atalaumiwa kwa kukiuka Sheria za Kimataifa kuhusu binadamu. Hata panya aumapo hufanya hivyo kwa kupuliza. Badaloni ilivyonufaika kutokana na Mahema ya Utandawazi.	simulizi fupi	<b>UK. 125</b>
Mwenzako akipatwa na janga, unajitolea kumsaidia. Ulimwengu umekuwa kijiji, Kijiji cha Utandawazi.		

<p>Ikaelezwa kuwa ndovu wengi waliopatikana wamekufa, walikufa kutokana na njaa lakini walio wengi ni kutokana na uzee. Akasisitiza neno hilo: Uzee. Rama Payo, kama kawaida yake, akazuka na maelezo yake. Wamefikia hatima ya maisha na kuamua kujifia tu. Mnadhani tembo hawana haki ya kufa? Rama Payo wakaifumbata kwelikinzani iliyoko kwenye suala zima la kufa kwa ndovu kwa kuyatumia maneno yake katika vichwa vya habari zao: Haki ya tembo, kilio cha waja!</p>	simulizi fupi	<b>UK. 129-131</b>
<p>Adrenalini ikamjaa mwili mzima..</p>	semi	<b>UK. 134</b>
<p>“Inabidi mtu unapongea na mwandishi ujue lipi la kusema usije kuwa mhusika kwenye hadithi yake na hasa mhusika asiyependeza kijamii.”</p>	uzumgumzi nafsiya	<b>UK. 142</b>
<p>Yaelekea ni mchonyoto wa aina hii uliomfanya Dakta Factas kuuchukua ule mpira, akaupa sura ya mwanadamu na kuufichulia mpira siri hiyo. Akamlisha yamini lakini, chochote akifanyacho asimfichue. Hataki kudhurika, si anajua jinsi mfumo wa kufuatilia habari ulivyo mkali nchini?</p>	sinekidoki/ taniaba, simulizi fupi	<b>UK. 143</b>
<p>“Utakuwa unachezea sega la nyuki...labda hata kumchezea mbogo.“Labda tupuuze. Kama si unafiki huu, ni nini? Inakuwaje sasa wakati amefariki ndipo wanajitia kushughulika naye? Je, dhamiri zao zinawalaumu kwa kumpuuza miaka yote hiyo?</p>	semi	<b>UK. 145</b>
<p>simulizi fupi</p>	simulizi fupi	<b>UK. 146</b>
<p>“Faranga imeniua! Faranga imeniua! Faranga imeniua!” alisema Matenzawa kwa sauti ya mkataa.</p>		<b>UK. 147</b>
<p>Hatimaye punda naye ameelekea kuchoshwa na masogi ya miaka.</p>		<b>UK. 148</b>

---

**F: Mbinu za Kimajaribio na Uwasilishaji wa Maudhui katika Riwaya Teule**

<b>Riwaya</b>	<b>Nukuu</b>	<b>Maudhui</b>	<b>Mbinu za Kimajaribio</b>	<b>Ukurasa</b>
<i>Musaleo!</i>	<p>Nani asiyeiba nchi hii? Alijiuliza. Nani ambaye anaweza kuaminiwa kwa kusema ukweli? Alishangaa. ...anayesema ukweli ni mimi tu, mimi Mzee!</p> <p>“Ninachoandika sasa hivi ndicho hamkipati hata kidogo! Kwa nini ukweli hauna maana nchi hii siku hizi? Wanasiasa wezi, nyie wezi; nani asiyeiba?</p>	<p>Wizi wa mali ya umma unaoendelezwa na viongozi hasa katika mataifa yanayoendelea.</p>	<p>Simulizi fupi, Uzungumzi nafsia</p>	<b>ML. UK. 33</b>
	<p>Jina la baba lilibadilishwa. Sasa nilikuwa mjukuu hasa wa Yunga Mwamba. Kisa chake? Kisasili, kinasema alikuwa mzazi wa kabila fulani la wachonga vinyago. Alikuwa mwanamume. Inasemekana aliishi kule juu milimani alikokuwa akijitumbuiza na magoma yake makubwa ajabu. Uzeeni alijiona mkiwa na kuamua kuzaa watoto aliowaamuru nao wazaane. Mwanamume kuzaa? Usiniulize, hiki ni kisasili! Nami nilishaanza kukwea ngazi za visasili. Mimi nilikuwa kisasili; kuwako kwangu kulikuwa kisasili kilichofumbata uhalisi; nilishaanza kuwa sehemu ya fasihi simulizi kama alivyosema profesa siku moja.</p>	<p>Utabaka.</p>	<p>Simulizi fupi, mwingilianotan zu, uhalisiajabu.</p>	<b>ML. UK. 2</b>
	<p>Kila hatua ina sifa zake. Sasa ilibidi nijengewe nyumba nzuri kwenye kiini cha nchi. Palikuwa mahali palipoteuliwa mbali na fujo nyingi. Niliweza kutulia huko na wenzangu wachache</p>	<p>Utabaka</p>	<p>Simulizi fupi, taashira</p>	<b>ML. UK. 9</b>

walioniarifu hali ilivyokuwa pamoja na mwelekeo wa matukio yote.

<p>“Njia nzuri ya kuhakikisha kuwa umejizika katika bongo zao ni kujitosa kwenye kiwiliwili cha utamaduni na kukwamia hapo kama ruba” ilibidi isemwe kuwa mimi ndiye yule kiongozi aliyesemwa kuwa atakuja kuikomboa jamii kutokana na pingu za maisha. Kuna ithibati ipi nyingine kuliko kule kuja na uganga wa kugeua chmbe chembe? Sasa ilibidi wakumbuke uwezo wangu; nilikuwa na uwezo wa kukomboa.</p>	<p>Dhuluma dhidi ya raia</p>	<p>Simulizi fupi, uzungumzi nafsia</p>	<p><b>ML. UK.12</b></p>
<p>“Nimekwambia sijui! Nakumbuka kuna wakati familia yake ilipolalamika kuhusu kusumbuliwa kwa simu kisha kupotea kwake...”          “Serikali ilisema nini?”          “Kwamba amehamia nchi nyingine na walishahakikishiwa na ubalozi wao nchini humo!”</p>	<p>Dhuluma</p>	<p>dayolojia</p>	<p><b>ML. UK. 25</b></p>
<p>Siku chache zilizotangulia Shirika la Umeme nchini lililalamika kuwa ukame ulishaanza kuzua matatizo makubwa. “Sasa hatuna uwezo wa kupata umeme wa kutosha kama zamani. Itabidi hata ugavi wake nao uathirike”.</p>	<p>Ukosefu wa huduma muhimu kwa raia</p>	<p>Simulizi fupi</p>	<p><b>ML. UK.28</b></p>
<p>Walikoishi wenye uwezo umeme haukukatwa hata siku moja: si mchana si usiku. (utabaka).</p>	<p>Utabaka, uufisadi</p>	<p>Simulizi fupi.</p>	<p><b>ML. UK.28</b></p>
<p><i>Kumbe hata hawa wanafanya kazi!</i> Alishangaa. Alikumbuka</p>	<p>Ukosefu wa huduma bora.</p>	<p>Simulizi fupi, dayolojia</p>	<p><b>ML. UK. 31-32, 96-97</b></p>



barabara za mtaani zilikuwa katika hali ya kusikitisha. Mara ya mwisho zilipokarabatiwa kiongozi wa nchi alikuwa akiitembelea Hospitali ya Wagonjwa wenye Akili Taahira iliyokuwa upande wa chini.

“Itachukua zaidi ya saa nne kutoka hapa hadi hospitalini. Barabara za jiji hili unazifahamu na lenyewe sasa siliamini.” Walikula lakini walilazimika kulipa. “Ehhh, hawa hawajui cha dharura wala utu. Wakitambua simu imetumiwa tutakatwa mishahara sisi!”

Lakini hata huko nako kulikuwa na masaibu yake. Hundi ilikuwako tayari lakini haikuwa na sahihi ya mkurugenzi wa kampuni. “Samahani lakini ndio hivyo, alikuwa hapa hata kaahidi kutia sahihi lakini keshandoka,” aliambiwa na aliyehusika.

“Sasa kuanzia leo, na wala si kuanzia leo ni tangu zamani za azali, kuna MIMI na WENGINE tu. Mimi ndimi msingi wa kila kitu. Mimi sio kama nyie!” (inasemwa alikua na rangi nyepesi na nywele zake zilikuwa mbuyembuye, ambazo hazikuiva).

Hiyo ni kauli ya ukweli, walisema wengine walimsamehe, “Ni mtoto huyu, hajui alisemalo, mwacheni tu!”...Miaka michache baadaye jamaa za Ukolongwe walifuatia. Ukolongwe alitumia nafasi yake kuwatafutia ardhi ya kulima.

Matumizi mabaya ya mamlaka. Raia kukosa kuhudumiwa ipasavyo katika afisi za serikali.

Ubinafsi.

Ukoloni uliowapelekea Waafrika kupoteza ardhi yao.

Ushuritishaji wa Waafrika kufanya

Simulizi fupi; dayolojia

Simulizi fupi; uzungumzi nafsia

Simulizi fupi; dayolojia.

**ML. UK.33**

**ML. UK. 35**

**ML. UK. 36**

Alishatambua wapi palikuwa na ardhi nzuri na wapi mbaya. ...Ukolongwe alitumia ujanja wake. Ardhi yote iliyokuwa na rutuba aliichukua na kuwakabidhi jamaa zake hao. ...Ardhi ambayo wenyeji hawakuwa wameitumia kutokana na mfumo wao ilichukuliwa na Ukolongwe na jamaa zake na kubatizwa ‘Ardhi haribifu’. Ndugu zake nao lazima walikuwa wazembe: walishindwa kuyalima mashamba makubwa waliyoibiwa na mwenzao. Walihitaji vibarua. walimwendea Ukolongwe. “Mzee hatuna njia ya kuilima migunda hii; tunahitaji wasaidizi. Wajua tena mikono yetu laini, imezoea kalamu bwana, sio kupambana na magugu ya huku magumu kama *natives* wenyewe!” walisema.

kazi katika migunda ya wazungu wakoloni.

Aliamua kuwafanya watu kadha aliowajua kwanza alipofika wakuu akawaita *Paramount Chiefs*. Huo ukawa mwanzo wa uchifu na uchafu na udufu wake! ...”Kwa njia hii tutaupunguza uzembe na uovu wa jamaa wa huku kwa sababu watakuwa na kazi ya kufanya badala ya kujizungukia majiani tu!” Wafanyikazi hao waliruhusiwa kukaa kwenye mashamba ya jamaa za Ukolongwe (ambayo kusema kweli yalikuwa yao wenyewe!) ili kuweza kufanya kazi vizuri. Kauli iliyotamkwa na mmoja wa jamaa hao walioishia kuitwa Waselelezi inakumbukwa mpaka leo. Alisema “Sasa tumeshaiba

Ukoloni, Ufisadi ubwanyenye.

Simulizi fupi, taashira

**ML. UK. 37**

ardhi yao, kilichobakia ni  
kuiiba na kuvimiliki viungo  
vyao. Hii ni hatua ya pili!”  
Ukolongwe na jamaa zake  
walitaka kuwadhiti  
wafanyakazi hao. Ili kulifanya  
hili walishurutika kuzuka na  
mbinu nyingine...

Upande wa ndani palikuwa na  
kipofu aliyeegemea ukuta.  
Mkongojo wake ulikuwa kando  
yake. Nilikiangalia kile kikebe  
chake cha kuombea mapeni.  
Nilifutika mkono wangu  
mfukoni kuchukua chochote.  
Sikuwa na sarafu kwa hiyo  
niliamua kuchukua noti ya  
shilingi hamsini na  
kuitumbukiza kwenye kikebe  
chake.

Inasemwa kuwa alipitisha amri  
fulani zilizowakataza watu  
kwenda huku na huku. Pili  
alikuwa na jamaa aliowapaka  
mafuta kwa mgongo wa chupa  
wakishi kuamini kuwa alikuwa  
rafiki yao wa kufa kuzikana.  
Hawa ndio waliopenyeza na  
kumfichulia ni akina nani  
waliokuwa wakiwachochea  
wenzi wao. Hali hata hivyo  
haikutulia alivyotarajia  
Ukolongwe.

Nilikuwa na matumaini ya kuwa  
kiongozi wa wakati mrefu sana.  
Mbinu za kuwanyamazisha  
wapinzani nilishajifunza na  
kulainisha. ...Silikumbuki jina  
lake lakini ni kitu kama  
Makiveli au Maa akia Veli.  
Vijana wa Mzee walipelekwa  
kwa mafunzo maalum ya  
kuweza sio tu kutambua

Hali ngumu ya  
maisha kwa raia  
wa kawaida.

Simulizi fupi.

**ML. UK.42**

Ukoloni: ukosefu  
wa uhuru.  
Uzalishaji wa  
tabia ya  
kujipendekeza.

Simulizi fupi.

**ML. UK.66**

Dhuluma, ukoloni  
mkongwe/  
mamboleo.

Simulizi fupi;  
urejeleomatini,  
dayolojia.

**ML. UK.73-74**

mienendo inayoishia kuwa  
kiyasi bali pia kuweza kuwazuga  
kiakili walioenda kombo.  
Walijifunza mbinu mpya za  
kutia hofu. Ulikuwa wakati huu  
ambao watu kadha walipoanza  
kupendekeza nijitangaze  
kiongozi wa maisha. “Mzee,  
umma wote uko nyuma  
yako” ... “Nyuma yangu  
wakifanya nini?” ... “Maana  
yangu ni kuwa wanakuamini  
wewe tu! Wewe ni kila kitu, bila  
wewe nchi hii haipo. Wewe ni  
jana, leo na kesho...”

Mimi nimezaliwa na kufa,  
nikazaliwa na kufa na kuzaliwa  
upya. Mara zote wananiua  
wameshindwa kuniondoa tamaa  
ya kuwako. Kila nikija huwa na  
sura mbalimbali. Hivi unionavyo  
mimi ni dadake Kinyonga na  
mamake wakati huo huo.  
Alipozaliwa nilikuwako. Hata  
Ukolongwe alipokuja huku  
alinikuta lakini kutokana na  
dhiki nilizozipata wakati wake  
niliishia kufa.

Ungeniona siku hizo mwili  
wangu ulitamanisha kutokana na  
nguvu za ujana. Mwili wangu  
ulijaa nguvu kutokana na kula  
chakula kizuri. Nilikuwa na  
uhuru wa kwenda kila mahali  
nilipotaka. Maziwa yangu  
yalikuwa ndiyo yanaanza kuota  
kifuani siku alipohamia huku.  
Lakini sitamsahau maisha yangu  
yote; aliishia kunishika kwa  
nguvu na kunibaka mara kadha.  
Tabia ya ubabe ndipo ilipoanzia.

Baadaye madereva walianza  
kulalamika kuwa walisumbuliwa

Dhuluma, ukosefu Simullizi fupi.  
wa maadili,  
ugeugeu,  
kujipendekeza.

Ubabedume.

Kutowajibika kwa  
viongozi, ukosefu  
wa usalama.

**ML. UK.79, 98,  
102**

na majambazi jioni maeneo hayo. Waziri wa masuala ya Usafiri na Ujenzi alijinyamazia.

Dhuluma kwa raia wasio na hatia.

Siku nne baadaye mke wangu, mpenzi wangu mwenyewe alipigwa risasi ya kifuani akitoka Supermarket. Polisi waliapa kufanya kila kitu... Hatutatulia hadi wahalifu wapatikane; mawe yote tutayabirua, waliapa. Lakini kuna majabali waliyasahau: Vijana wa Mzee. Niliachiwa watoto wadogo.

Vua kubwa lilishaanza kuanguka na makao kadha ya maskini yalisombwa. Kwangu hii ilikuwa nafasi nzuri. Mungu si Athumani. Nilipata nafasi nzuri ya kuonyesha ukarimu wangu. Tangu siku zile watu waliniheshimu kama Mleta Baraka, yaani tangu mazingaombwe ya chembechembe. Bado unakumbuka? Nilihonyoa pesa fulani kuwasaidia waliofikwa na majanga. Marafiki zangu wafanyabiashara nao walichangia kwa ukarimu wa kutosha kuzilinda biashara zao.

Umaskini, matumizi mabaya ya mamlaka.

Simulizi fupi, taashira

**ML. UK.88**

Mikono yake ilizoea kushikashika na kupakatapakata vitu vya wengine; huku kwetu tunasema ukimwona mtoto anafanya hivyo jua umezaa mwizi. Wazee wanosimulia kisa cha jitu hili wanasema kuanzia siku hiyo lilijulikana kama Jivi.

Matumizi mabaya ya mamlaka.

Simulizi fupi; taashira

**ML.UK.89-90**

Tabia lilijaa kiburi na lilijiona bora. Basi Jivi lilianza kujiendea huku na huku; likavuka kwake

Ubinafsi, utabaka.

**ML. UK.89-90**

na kuhamia kwa jirani. Kila lilichopata lilitwaa na kubugia kinywani. Lilipokatazwa lilitumia ile mikono mingi likabinya, likasongoa na likaua. Haukupita muda mrefu likawa limesababisha maafa, watu wakatoroka makwao. Mwili wake ulikuwa mkubwa sasa. Likashindwa na kutembea na kuishia kuagiza lifanyiwe kila kitu. Kazi yake ikawa kukaa tu kusimulia visa vya Mashimo ya Mfalme Suleimani, Robinson Kruso na kuimba wimbo wa Arya na mwingine wa Boramimi-Kitovu. Watu walipoliangalia wakasmea hili limezidi sasa. Likapewa jina jingine: Mwinyi.

Uigaji kikasuku wa tamaduni za kigeni.

“Sasa nasikia kuna tatizo hapa. Maabara ya hospitali haina vifaa vinavyopasa kufanyia uchunguzi wa aina hii. Vingine vimo katika chumba cha daktari mkuu na amekwenda likizo!” Anima: Amekwenda likizo na funguo? Daktari: Ndio, ehh! Kingunge: Sasa tufanye nini? Daktari: Njia tuliyo nayo ni Wazito Nursing Home lakini ni ya kibinafsi, wanataka pesa kabla ya kufanya lolote! Kitungule: Mpelekeni huko tutalipa!

Ukosefu wa huduma muhimu kwa raia katika sekta za serikali, kutowajibika kwa wafanyakazi wa serikali.

Simulizi fupi, dayolojia

**ML. UK.95-96**

Ilikuwa lazima mbinu mpya zibuniwe. Mashtaka bandia. Mapatano maalum na Idara ya Sheria. Sharia mpya zikabuniwa, *Detention Without Trial. Preventive Detention Act.* Huu wakati wa kuijenga nchi hatuwezi kuuharibu kwa kesi zisizofaa,” alisema Mzee.

Matumizi mabaya ya mamlaka, dhuluma.

Simulizi fupi

**ML. UK.100**

Usimwone simba kajikunyata ukamwita paka. Zilianza vuguvugu. Vuta n’kuvute ya upinzani. Wanafunzi wakalalmika kuwa elimu imekosa mwelekeo. Wanawake nao wakaanza kudai wanapuuzwa kwenye nyadhifa kuu.

“Umaskini. Uhuru. Maendeleo. Wanawake wanasema wamepuuzwa! Siku hizi wanaimba wimbo unaoitwa *Affirmative Action*, kwa kifupi wanasema hivi: Kila refu lina mwisho!” Zamani kuna wakati wanawake walikuwa kila kitu, viongozi mpaka hata miungu. Waliwatesa wanaume sana. Basi siku moja nao wakaamua kuwa lazima wajitoe katika hali hiyo ya kuteswa. Unasikia bwana? Ndio walikwenda mzengwe. Walipitisha muda wakisemezana na kuambizana. Neno hapa, kineno pale, wazo pale. Mwisho wakakubaliana. Hamna njia nyingine. Ehh, haipo nyingine ya kujitoa kwenye mikono hii isipokuwa kujitahidi kuwanyamazisha. Njia ya pekee ilikuwa moja tu: kuwatunga mimba wanawake wote. Hali ilivyokuwa hivi basi wakabiruliwa biru na wanaume wakachukua nafasi zao.

Siku nne baadaye mke wangu, mpenzi wangu mwenyewe alipigwa risasi ya kifuni akitoka Supermarket. Polisi waliapa kufanya kila kitu... Hatutatulia hadi wahalifu wapatikane; mawe yote tutayabirua, waliapa. Lakini

Umaskini, nafasi ya wanawake katika jamii.

Changamoto katika sekta ya elimu.

Tumaini jipya la jamii.

Mauaji ya kiholela ya raia wasio na hatia.

Simulizi fupi.

Simulizi fupi.

**ML. UK. 101  
122-123**

**ML. UK.102**

kuna majabali waliyasahau:  
Vijana wa Mzee. Niliachiwa  
watoto wadogo.

Tukio hilo lilinizindua na kunitia  
hamasa. Nilikuwa tayari  
kushirikiana na wenzangu kuliua  
*Sphinx*. Sijui unakumbuka kisa  
cha King Oedipus? Lakini kabla  
sijakifumbua kitendawili cha  
kitoto ilinjia simu. “Unajua siri  
ya Mashamba ya Mawe?”  
Nikoseje? Utahusika katika  
kukiandaa kitu kisha  
usikikumbuke? Sikuhitaji  
maelezo zaidi. Profesa: Ikawa  
kama kisa Joseph Guillotin  
aliyevumbua *guillotine* na  
kuishia kuuliwa nayo! Ngwena:  
Hasa! Ndiyo siri ya msumeno  
kukata huku na huku! Profesa:  
Ndiyo siri ya neno pia! Ngwena:  
Ni kweli.

Uzalendo.

Simulizi fupi,  
dayolojia,  
taashira,  
urejeleomatini.

**ML. UK.102**

Kutokana na mipango ya  
Kitungule na msaada mkubwa  
wa Kingunge waliishia kumpata  
daktari mmoja mzuri wa  
kibinafsi aliyejitolea kuifuatilia  
hali yake. “Nchi hii, kama mtu  
huna akili utakufa tu! Alisema  
Kitungule.

Utabaka.

**ML. UK.103**

Wengi wao walishajiunga na  
madaktari wa kiserikali kwenda  
kupita mbele ya jukwaa la  
kiongozi. Hii siku ya  
wafanyikazi na lazima wenyewe  
washiriki kwa moyo mkunjufu,  
alisema kiongozi mara kadha.

Taswira ya  
sherehe za kitaifa.

**ML. UK.103**

Umeshawahi kusikia kisa cha  
mnyama mwenye mkia kisha  
anjiuma mwenyewe kwenye  
mkia huo huo? Amenitaja  
juzijuzi Mamanchi. Ni hivi,

Waafrika  
walisahau  
tamaduni zao na  
kuiga tamaduni za  
wazungu.

**ML. UK.108**



nilipozaliwa nilikuwa na kipawa  
fulani maalum cha kuiga.  
Tulipokuwa vijana niliwapiku  
wenzangu kwa kuiga milio ya  
wanyama kama mbweha, fisi,  
duma, kiboko na kima. Niliweza  
pia kuwaiga ndege shorewanda,  
kitwitwi na hasa kabisa kasuku.  
Maeneo ya kwetu hapakuwako  
na kasuku lakini niliishia  
kumwiga tu. Unaweza kusema  
ni kitu kama imani: unaamini  
kitu ambacho hujakiona na  
unaishia kuwa stadi pia. Huo  
ulikuwa mwanzo wa kuitwa na  
wenzangu Kasuku. Jina asilia  
likapotea hata mimi nikaishia  
kulisahau hata leo silijui

Kazi yangu ilikuwa kuzunguka  
huku na huku nikisomba  
waliokwenda kinyume na  
Dogmazee, Intelligence Network  
ilikuwa nzuri.

Dhuluma.

**ML. UK.114**

Vyuoni. Shuleni. Mitaani.  
Hospitalini. Kwa kifupi kila  
mahali! Hata wapi choo  
kimetumiwa. Ilikuwa kazi  
muhimu kuhakikisha kila mtu  
anaogopa, na muhimu zaidi  
anaogopa kitu asichokiona. Huo  
ndio woga wa kisawasawa.

Unakumbuka kile kisa  
nilichokusimulia cha ardhi kuwa  
pande kubwa lilivunjika na  
kuwa Godi-Wana na Huraa-Asi  
kisha na mengine madogo  
madogo mpaka yakafikia  
matano? Sasa inasemwa  
maajabu ya kijiografia  
yalitokea siku moja.  
Utakumbuka kisa cha tetemeko  
la ardhi lililotokea miaka ya  
nyuma na kuna takriban watu

Dhuluma,  
umaskini,  
matumizi mabaya  
ya mamlaka,  
kujipendekeza.

**ML. UK.118**

elfu sita – shida za kuwa na nyumba dhaifu! Karibu nisahahu kukuhongera Mzee, ulilitumia tukio hilo kujizika hasa kwenye mioyo ya watu wako kwa ukarimu wako. Siri ya jiografia hiyo, Mzee!

Jina la wimbo mmoja ni *Globalisation*. Kuna hata mwingine aliyedai kuwa mabadiliko hayo yalisababishwa na upepo wa mbisho ulioitwa Ikti-Saad ya Masoko-Huria.

Chanzo cha mabadiliko ulimwenguni.

Simulizi fupi

**ML. UK.119**

Jamaa mwingine aliyetoka Iran au Irag-sio muhimu atokako, anasema huko jina walijualo ni Shai-Tani. Uhindini naskia wanasema Amrika. Huku kwetu nasikia wanamwita Mjomba kwa kuwa wanaamini ana roho nzuri. Inawezekana hata alijiita na kuwafanya wengine walidakie tu. Inaelekea sehemu hizi maneno yake yanasikilizwa sana na hata nyendo zake kuigwaigwa.”

Kuiga mienendo ya kigeni.

Simulizi fupi, taashira

**ML. UK.120-121**

“Shida iliyopo siku hizi ni kuwa wanaume wengi ni misenge tu; wengine hawana habari kabisa!”

Matatizo ya jinsia ya kiune

Simulizi fupi, taashira

**ML. UK.123**

Uvumi unatawala mahali ambapo taarifa hazitolewi hivi hivi. Magazeti nayo yalifuata mkondo huo. Yaelekea hayana mengi ya kusema au yameamua kusema kwa kubania mengine kama jamii yenyewe ilivyo. Lazima hata hii ilikuwa njia ya kuyasema hayo kwa kuyaacha mapengo ya habari. Yamkini walitaka wasomaji wachangie kwa kuyaziba mapengo yaliyoachwa na taarifa zao.

Jamii ya leo haisemi mambo yake yote hadharani ingawa inapendelea uvumi wa kila aina.

Simulizi fupi.

**ML. UK.135**

<i>Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji</i>	<p>Mzee Insafu Uvi na kamati ya kushughulikia malalamiko yote ya ardhi na kuandaa ripoti ya jinsi ya kuyatatua. Waliopembeza rizavu wakapata matumaini. Akatoa mapendekezo yake. Hakuna mtu wa kuyumbishwayumbishwa. Siku mbili kabla ya ripoti yake kuwasilishwa akapotea. Juhudi za kumtafuta ziliambulia patupu.</p>	Ubinafsi.	Simulizi fupi, taashira.	<b>MMM UK. 68</b>
	<p>Hata baada ya mwaka mwingine ripoti ya Mzee Insafu haikupatikana. Mashamba yakapotea hivyo. Shamba lililomilikiwa na Joelon halikurudishwa kwa wamiliki wa zamani.</p>	Dhuluma.		
	<p>Mtumishi Askari Joma- hakuna njia nyingine ya kuwadhibiti watu isipokuwa kuhakikisha wana hofu. Na hasa wakihofu wasichokijua. Hana haja ya kuwa na urafiki na kila mtu. Hilo haliwezekani.</p>	Dhuluma.	Simulizi fupi, taashira.	<b>MMM UK. 75</b>
	<p>Vikafuatia vikundi vya watu waliolalamikia masuala mbalimbali. Wanataka kuwa huku kudadisi anayoyafanya. Yuko hapo kwa niaba yao. Ahadi chungu nzima alizotoa zimeishia wapi? Amezisahahu wamkumbushe? Aliahidi kuutokomezwa ujinga, umaskini na njaa. Amefanikiwa? Inakuwaje marafiki zake wa karibu ndio wanaofaidika tu? Hali ikawa ngumu. Akasaka ushauri wa wenzake.</p>	Uongozi mbaya.	Simulizi fupi.	<b>MMM UK. 74</b>
	Akanyamazisha sauti za akina	Dhuluma	hasa Simulizi fupi.	<b>MMM UK. 75</b>

Marugurugu na wenzake.  
Mwenzake naye akamtumia  
ujumbe wa kuja kuangalia jinsi  
alivyokuwa amepiga hatua.  
Ujumbe wa kufuatilia kujua  
kama msaada wao ulikuwa wa  
kufaa au la. Ujumbe huu ndio  
ndio uliomfikishia barua  
iliyotokea kwao. Ilikuwa Barua  
ya Kumbukumbu.

kwa wazalendo.

Wachache waliothubutu kufanya  
hivyo wakasombwasombwa na  
kufikishwa mahakamani kwa  
mashtaka mbalimbali. Uvunjaji  
wa sharia. Kujizungukia  
ovyooovyoo. Kuepuka sharia na  
maagizo ya wajuao. Kwenda  
msituni bila idhini ya Idara ya  
Misitu.

Dhuluma.

Simulizi fupi.

**MMM. UK. 82**

mia beba, mia beba' –

Simulizi fupi

**MWM. UK. 7**

Hewa iliyoghoshi moshi wa  
rangi ya lami kutokana na  
magari yaliyopitisha miaka ya  
kuishi na viwanda visivyojua  
uchafuzi ni nini katika enzi hii  
ya msako mkubwa wa fedha.  
Hewa iliyosheheni harufu kali  
ya miili ya watu wanaomaliza  
siku nzima wakichap miguu na  
wengine kwa viatu vilivyoisha  
soli kuacha alama mchangani. –

Simulizi fupi

**MWM. UK. 7**

Kwenye uwanja huo wa  
kupumzika, palikuwa na viti  
kadha vya saruji vyenye rangi  
iliyobambukabambuka. Viti  
hivyo vilikuwa na mabakabaka  
meupe hapa na pale kutokana na  
vinyesi vya kongoti waliotua  
kwenye mierezi mirefu  
iliyokuwa pale. Wafanyakazi wa  
Halmashauri ya jiji walipaswa

**MWM. UK. 7**

kuvishughulikia viti hivyo lakini  
hakuna aliyeelekea kuvijali. –

**MWM. UK. 8**

Ile taswira ilinikumbusha jinsi  
nilivyosimama karibu na jengo  
la kanisa la kijijini. Lilikuwa  
kanisa lisilokuwa na madirisha  
yake na lenye paa la mabati  
yaliyokuwa na kutu na mashimo  
mengi kama tenga la kubebea  
nyama. –

**MWM. UK. 16**

Maneno hayo aliyoyatamka  
baina ya harufu kali ya sigara na  
moshi wenyewe; yaliyoonyesha  
meno yake yaliyokoza rangi ya  
hudhurungi, yakanipiga.  
Nilijaribu kuyapitisha akilini  
maneno hayo ya moshi wa  
sigara. Nikayatia kwenye mizani  
ya akili kujaribu kuona maana  
iliyofichwa. Nilishajifunza kuwa  
maana nzito huwa kwenye  
mapengo bali si kilichosemwa.  
Binadamu ni kiumbe  
anayependa mbinu ya mdokezo  
sana labda kwa kuwa kimsingi  
ni kiumbe mwenye woga  
uliokithiri.

**UK. 60**

Ninachojua ni kuwa alinidai  
fedha nilizomkopa mwezi jana  
kulipia deni langu la benki baada  
ya mishahara yetu  
kucheleweshwa kidogo.

**UK. 75-76**

kwa maneno ya daktari  
asiyekosea, daktari ambaye  
ametaalamika vizuri sana,  
nilikuwa bado na siku ishirini na  
tano, kuonana, ana kwa ana,  
kope kwa kope, bila ya  
kuyakupua macho yangu, na  
jamaa huyo anayekuja usiku wa  
manane kama mchawi.

Akatafuta genge la vijana kama  
wafanyavyo wanasiasa, akawapa  
fedha za kununulia pombe yao  
kwenye mtaa wa  
Madongokinama uiloko hapo  
karibu. Wakaibugia wakawa  
chordo chupa na kizibo chake na  
kwenda pale usiku na  
kuivurumishia nje mizigo ya  
mwenye nyumba.

---